# UTANGULIZI WA IBADA YA KIKRISTO

shepherds
GLOBAL CLASSROOM

Shepherds Global Classroom ipo kwa ajili ya kuujenga mwili wa Kristo kwa kutoa mtaala kwa ajili ya kuwaendeleza viongozi wa Kikristo duniani kote. Tunalenga kuongeza programu za mafunzo ya asili kwa kuweka chombo cha mtaala wa kozi 20 mikononi mwa viongozi wa kiroho wanaotoa mafunzo katika kila nchi duniani.

Kitabu hiki kinapatikana bure kwa njia ya kupakua kutoka katika https://www.shepherdsglobal.org/courses

Mwandishi Mkuu: Dr. Randall D. McElwain

Hakimiliki © 2023 Shepherds Global Classroom
Ilitafsiriwa kutoka Toleo la Nne la Kiingereza.

Haki zote zimehifadhiwa.

Nyenzo za wahusika wengine zilizotumika ni hakimiliki ya wamiliki husika ambazo zimeshirikishwa na kutumika humu chini ya leseni mbalimbali.

Tafsiri ya Maandiko "yaliyonukuliwa" kutoka chapisho la Kiingereza kwa ajili ya chapisho hili la Kiswahili yanatoka katika Biblia Takatifu ya Kiswahili, "Swahili Union Version Bible" (SUVB®)." Yametumika kwa kibali. Haki zote zimehifadhiwa.

**Taarifa kuhusu vibali:**

Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa na kutawanywa bure kikiwa kimechapishwa na katika mifumo ya kidigitali chini ya miongozo ifuatayo: (1) Maudhui yaliyoko kwenye kitabu hiki hayawezi kubadilishwa kwa namna yeyote ile; (2) Nakala zinazopatikana haziwezi zikauzwa kwa ajili ya kupata faida; (3) Taasisi za elimu zina uhuru wa kutumia na kukinakili kitabu hiki, hata kama wanalipisha ada za masomo ya ziada; na (4) Kitabu hiki hakiwezi kufanyiwa tafsiri pasipokuwepo na kibali na usimamizi wa Shepherds Global Classroom

# Yaliyomo


Muhtasari wa kozi ..... 5

(1) Kuelezea maana ya Ibada ..... 7

(2) Mungu na Muabuduji ..... 25

(3) Kuabudu katika Agano la Kale ..... 39

(4) Ibada katika Agano Jipya ..... 57

(5) Ibada Katika Historia Ya Kanisa ..... 75

(6) Muziki katika Ibada ..... 89

(7) Maandiko na Maombi katika Ibada ..... 111

(8) Kupanga na Kuongoza Ibada ..... 135

(9) Maswali Mengine ..... 157

(10) Mtindo wa Maisha wa Kuabudu ..... 177

Muhtasari wa Kupanga Huduma ya Ibada ..... 187

Fomu ya Tathmini ya Wimbo ..... 191

Vyanzo na Rejea Zinazopendekezwa ..... 193

Kumbukumbu za Mazoezi ..... 195

# Muhtasari wa kozi

Kozi hii inatambulisha kanuni za kuabudu.

Kama mnasoma kama kikundi, msome kwa kuachiana. Mnapaswa muwe mnasimama kwa muda ili mpate kujadiliana. Wewe kama kiongozi wa darasa, unawajibika kutunza mjadala usihame kwenye mada ya kujifunza. Ni vizuri kutunza muda kwa kila kipindi cha mjadala.

**Maswali ya mjadala** na **mazoezi ya darasani** yanaoneshwa kwa mshale ► .

Kila unapofikia swali, waruhusu wanafunzi kujadili jibu. Jaribu kuhakikisha kwamba wanafunzi wote katika darasa wanashiriki katika mjadala. Kama ni lazima, unaweza kuwaita wanafunzi kwa majina.

Katika kipindi chote cha somo, kuna mazoezi ya darasani na kazi za nyumbani zinazohusisha kutafuta nyimbo za tenzi na korasi zinazokidhi vigezo maalum. Lengo la mazoezi haya ni kukuandaa uweze kuchagua nyimbo za ibada kwa ajili ya ibada unazoongoza.

Ikiwa kuna vitabu vya tenzi vilivyochapishwa kwa lugha yako, unaweza kuvitumia. Tovuti ya https://worshipleaderapp.com/ na programu ya simu inayoitwa "Worship Leader" zinatoa nyimbo za Kikristo kwa lugha mbalimbali. Unaweza pia kuangalia kwenye tovuti nyingine zinazochapisha maneno ya nyimbo za ibada yaliyoandikwa kwa lugha yako.

**Maandiko** mengi yametumika katika kozi hii. Vifungu ambavyo vitasomwa darasani pia vimeoneshwa kwa alama ya mshale ► . Tafadhali wanafunzi waitazame mistari hii na kuchukua kumbu kumbu halafu wasome katika mzunguko wa kikundi.

Kila somo linaishia na **mazoezi**. **Mazoezi** yanapaswa kukamilika na kuwasilishwa kabla ya somo jingine.

Kila somo lina mtihani, na sehemu ya mtihani ni kukariri maandiko ya Biblia. Kwa kila mwisho wa kipindi, kiongozi anaweza kurudia maswali haya pamoja na wanafunzi. Darasa linalofuata linapaswa kuanza na **jaribio** katika maswali haya. Mjaribio yanapaswa kufanyika bila kuangalia kitabu, kumbu kumbu zilizoandikwa, Biblia, au wanafunzi kuulizana. Majibu ya zoezi yapo kwa kiongozi kupakua kutoka Shepherds Global Classroom.

Katika Somo la 1, wanafunzi wanapangiwa **mradi wa siku 30**. Baada ya mradi huu kukamilika, kila mwanafunzi anapaswa kuwasilisha ripoti ya ukurasa mmoja ikifupisha walichojifunza kutokana na mradi huo. Wanafunzi hawatawasilisha taarifa nzima ya mradi.

Ikiwa mwanafunzi anataka **kupata cheti kutoka Shepherds Global Classroom,** anapaswa kuhudhuria vipindi vya darasa na kukamilisha mazoezi yanayotolewa. Fomu inatolewa mwishoni mwa kozi kwa ajili ya kurekodi mazoezi yaliyokamilishwa.

# Somo la 1
# Kuelezea maana ya Ibada

## Malengo ya Somo

Mwisho wa somo hili, mwanafunzi anapaswa:

(1) Kuelewa maana ya Ibada katika kibiblia.

(2) Elewa kwamba ibada ya kweli inaathiri maeneo yote ya maisha yetu.

(3) Tambua aina ya ibada inayokubalika na Mungu.

(4) Thamini umuhimu wa ibada katika maisha ya Kikristo.

## Matayarisho kwa somo hili

*Kariri Yohana 4:23-24.*

## Utangulizi

Ni asubuhi ya Jumapili nchini Marekani. Wakristo waliopendeza hukusanyika kwa ajili ya ibada katika patakatifu pazuri. Wanaimba nyimbo za ibada wakisindikizwa na muziki pamoja na kwaya, wanaimba tenzi kuu zenye utukufu. Muziki unapigwa wakati sadaka zinakusanywa. Washirika wanaomba kimya kimya huku mchungaji akiwaongoza katika maombi. Wakati wa mahubiri yake, mchungaji ananukuu maneno ya waandishi tofauti kutoka kwenye maktaba yake kubwa. Baada ya mahubiri, kanisa wanashiriki meza ya Bwana kwa kutumia sahani yenye rangi ya fedha, mikate, na vikombe kwa kila mtu binafsi. Hii ni kuabudu.

Ni jumapili asubuhi huko China. Waumini 30 waliovaa mavazi ya kawaida hukusanyika katika chumba cha kupanga. Wanaimba nyimbo za sifa na za kitabuni wakiimba bila ala za muziki. Kiongozi anahubiri ukweli wa neno ambalo amelipata kwa siku za karibuni kwa kupitia usomaji wa Maandiko. Wakati wa kipindi cha maombi ya muda mrefu, washirika wa nyumba hii wanaomba kulingana na mahitaji ya kila mmoja. Baada ya maombi, washirika wa nyumba hii wanakula ushirika mtakatifu huku mkate na divai ikiwa kwenye kikombe cha plastiki. Watu wanapoondoka, wanaweka sadaka zao kimya kimya katika kikapu kilichopo mlangoni. Wenye mahitaji maalumu watapewa sadaka hii. Hii ni kuabudu.

Ni jumapili asubuhi kule Nigeria. Wakristo wanavaa mavazi ya kumeremeta wamekusanyika wakiwa na hamasa ya ibada. Timu ya kuimba na kuabudu ikiwa na magitaa, vinanda, na ngoma inaongoza ibada kwa nyimbo ambazo zinaoneshwa katika kioo kikubwa cha projecta. Kwaya hii inaimba wakati watu wanaenda kutoa sadaka katika sanduku la sadaka mbele ya kanisa. Ujumbe wa mahubiri unaendana na mahitaji yaliyopo ya watu wa Nigeria. Ibada inaisha kwa kubusiana mikono, kukumbatiana, na sherehe za furaha. Hii ni kuabudu.

Kuabudu kuna namna tofauti. Kwa kila nchi na kila utamaduni, kuabudu kuna tofautiana. Kuabudu ni zaidi ya ibada aina fulani. Kusema kweli kuabudu ni zaidi ya ibada yenyewe; kuabudu inahusisha maeneo yote ya maisha ya mkristo. Katika somo hili, tutaangalia maana ya kuabudu kibiblia.

► Soma Yohana 4:1-29. Jadili maana ya kuabudu katika roho na kweli.

## Vipengele vya Kuabudu vya Kibiblia

Kuabudu ni kutambua na kuheshimu thamani ya Mungu. Inamaanisha kumpa Mungu heshima anayostahili.

► Hapa chini kuna maana tatu za kuabudu. Kariri maana ambayo ina maana muhimu zaidi kwako.

- "Ibada ni mwitikio wa kuabudu wa mwanadamu kwa Mungu wa Milele." - Evelyn Underhill
- "Ibada ni kuinua moyo wetu kwa mwitikio wa hiari kwa Mungu." - Franklin Segler
- "Ibada ni mwitikio wa yote tuliyo kwa yote Mungu alivyo." - Warren Wiersbe

**Ibada ni utiifu wa heshima.**

Kwa lugha ya Kiebrania na Kiyunani neno "kuabudu" lililotafsiriwa katika Biblia lina dhana ya kuinama chini mbele ya Mungu.[1] Htii inaonesha kuwa kujisalimisha kwa heshima kunahusishwa katika kuabudu. Tendo la kuinama lina akisi heshima ya moyo. Kuanzia ngalau karne ya pili, Wakristo walipiga magoti wakati wakiomba.

Katika Ufunuo 4:10-11, Mtume Yonana aliona tukio la kuabudu mbinguni:

> Ndipo hao wazee ishirini na wanne huanguka mbele zake yeye aketiye juu ya kile kiti cha enzi, nao humsujudia yeye aliye hai hata milele na milele, nao huzitupa taji zao mbele ya kile kiti cha enzi, wakisema, Umestahili wewe, Bwana wetu na Mungu wetu, kuupokea utukufu na heshima na uweza; kwa kuwa wewe ndiwe uliyeviumba vitu vyote, na kwa sababu ya mapenzi yako vilikuwako, navyo vikaumbwa.

Wakati wa Rumi mfalme aliyeshindwa vita akiletwa kwa Kaisari, alitakiwa kutupa taji lake la kifame chini ya miguu ya Kaisari na kuinama kwa kujisalimisha. Yohana anaonesha kuwa Mungu, ambaye ana nguvu na anastahili kuliko Kaisari, anastahili heshima yenye kujisalimisha ya wanaoabudu.

Katika Agano la Kale, Mungu Mungu alikataa sadaka za walioasi. "Watu hawa hunikaribia na kuniheshimu kwa vinywa vyao, bali mioyo yao wamefarakana nami, na kicho chao walicho nacho kwangu ni maagizo ya wanadamu …" (Isaya 29:13). Kwa nje, wnaonekana

---

[1] Neno la kiebrania ni *shachah*, katika Agano la kale limetafsiriwa "kuabudu," "kuinama chini," "anguka chini," au "kuheshimu." Neno la kiyunani ni *proskuneo*, katika Agano jipya limetafsiriwa "kuabudu" au "inama chini."

kana kwamba ni watu wanaoabudu; walisema maneno sahihi na kufuata utaratibu wa ibada. Kwa ndani, mioyo yao ilikuwa mbali na Mungu. Kuabudu yenye kweli ni kujisalimisha kwa heshima kutoka moyoni.

Ukweli ule ule unaonekana katika Agano Jipya. Mwanamke Msamaria anahoji kuhusu mahali pa kuabudia, ni Yerusalem au Mlima wa Gerizim. Yesu akaonesha moyo, kuwa ni mahali pa kiroho pa kuabudia. "Mungu ni Roho, nao wamwabuduo yeye imewapasa kumwabudu katika roho na kweli" (Yohana 4:24). Kuabudu yenye ukweli inahitaji kujisalimisha kwa Mungu.


Kuabudu yenye ukweli inamheshimu yule anayeabudiwa. Katika baadhi ya makanisa, kuabudu kunashindwa kutambua heshima anayomstahili Mungu. Kama tutakavyoona maana nyingine baadaye, kuabudu kunajumuisha kusherehekea, lakini pia kuabudu ni kunamheshimu Mungu. Hii haina maana kuwa mtindo moja wa kuabudu ndio unaofaa. Walakini, maana hii ya kwanza inatukumbusha kwamba pale tunapoamua kuhusu vitendo vya vyetu vya kuabudu, tunapaswa kujiuliza, "Je, mimi ninaonesha heshima kwa Mungu ninayemwabudu?"

**Ibada ni huduma**

> Basi, ndugu zangu, nawasihi, kwa huruma zake Mungu, itoeni miili yenu iwe dhabihu iliyo hai, takatifu, ya kumpendeza Mungu, ndiyo ibada yenu yenye maana (Warumi 12:1).

Mstari huu unaunganisha kujisalimisha kwetu kwa heshima na maisha ya kila siku. Ni pale tu tunapojisalimisha kama dhabihu iliyohai ndipo huduma zetu, au kuabudu kwetu, kunakubalika na Mungu. Kukutana mara kwa mara kanisani ni muhimu; kanisa la kwanza walithamini kuabudu pamoja.[2] Walakini, kuabudu hakuishii pale mkusanyiko wa kanisa unapomalizika. Kuabudu ya ukweli huendelea katika nyanja zote za maisha.

**Ibada ni sifa.**




Neno sifa limetumika zaidi ya mara 130 katika kitabu cha Zaburi. Kuna maneno matatu ya kiebrania yanayotafsiriwa "kusifu." Neno la kwanza, *halal*, lina maana ya kusherehekea au kujivunia. Neno la pili, y*adah*, maana yake kusifu, kutoa shukrani, au kukiri. Neno la tatu, *zamar*, maana yake "kuimba" au "kuimba sifa."

Maneno haya, hususani *halal*, linaashiria furaha ya kuabudu. *Halal* ni neno ambalo Myahudi angelitumia kujivunia mtu fulani. Katika kuabudu, tunajivunia

[2] Kuabudu pamoja **imeamriwa** katika Maandiko kama Waebrania 10:25. **Inasadikika** kuna kuabudu kwa pamoja katika Matendo 2:46-47.


Mungu; katika kuabudu, tunasherehekea wema wake; katika kuabudu, tunafurahia ukuu wa Mungu.

Kuabudu kwa ukweli kunamheshimu Mungu; walakini, kuabudu kwa ukweli vile vile ni kumsherehekea Mungu! Katika kuabudu, tunafurahia wema wa Mungu. Katika somo la 6, tutajifunza kazi ya mziki katika ibada. Muziki ni muhimu kwa sababu unatengeneza njia kwa kusanyiko kuungana katika kusherehekea na kumsifu Mungu.

**Ibada ni ushirika.**

Kuabudu ni ushirika kati ya Mungu na mwanadamu. Kuabudu pia ni pamoja na ushirika kati ya wanaoabudu. Neno la Kigiriki (koinonia) lenye maana ya ushirika au kushirikiana mara nyingi hutumiwa katika muktadha wa kuabudu. Wakristo walijitolea kwa mafundisho ya mitume na ushirika (koinonia), kwa kuvunja mkate na maombi (Matendo 2:42). Kama waamini, tumekaribishwa katika ushirika (koinonia) wa Mwana wa Mungu, Yesu Kristo Bwana wetu (1 Wakorintho 1:9).

Kielelezo cha kufahamu kuabudu kama ushirika ni Utatu. Kwa njia ile ile ambayo Utatu unavyohusiana kati yao katika ushirika, sisi pia tunahusiana kati yetu na kwa Mungu katika kuabudu. Katika baraka inayohusisha kuabudu ya kidunia na Utatu wa milele, Paulo aliandika, " Neema ya Bwana Yesu Kristo, na pendo la Mungu, na ushirika wa Roho Mtakatifu ukae nanyi nyote” (2 Wakorintho 13:14). Tunapokuwa umoja na Kristo, tunashiriki kwa njia ya Roho katika ushirika wa Mwana na Baba. [3] Katika kuabudu, tunakutana na ushirika tajiri wa Utatu. Kuabudu kwetu duniani kumeigwa kulingana na ushirika kamili wa Utatu.




Kuabudu kwa namna ya Utatu ni uzoefu wa neema, si matendo. Kuabudu inawezekana kupitia kuhani wetu mkuu, Yesu Kristo. Yeye huchukua kuabudu yetu isiyostahili, anaitakasa, na kuileta mbele ya Baba bila doa wala mawaa. Kuabudu kwetu hukubaliwa na Baba kwa ajili ya Yesu, na sisi tunaungana na Yesu katika maisha yake katika Roho.

Tunaabudu si kwa sababu tujipatie kibali cha Mungu, bali kwa neema tumepewa heshima ya kushiriki katika ushirika na Mungu.

*Koinonia* yetu ambayo sio kamili leo (ushirika na Mungu katika kuabudu **na** ushirika na waamini wengine) ni kionjo cha kuabudu mbinguni. Kama waabudu, tunatafuta ushirika na waamini wenzetu kwa sababu kuabudu duniani ni mazoezi ya kuabudu milele.

---

[3] James B. Torrance, *Worship, Community, and the Triune God of Grace* (Downers Grove: InterVarsity Press, 1996), 20-21

**Ibada inajumuisha maisha yote.**

Neno lingine linalotumiwa kwa kuabudu katika Agano Jipya mara nyingi hufasiriwa kama "dini":[4]

> Mtu akidhani ya kuwa anayo dini, wala hauzuii ulimi wake kwa hatamu, hali akijidanganya moyo wake, dini yake mtu huyo haifai. **Dini** iliyo safi, isiyo na taka mbele za Mungu Baba ni hii, Kwenda kuwatazama yatima na wajane katika dhiki yao, na kujilinda na dunia pasipo mawaa (Yakobo 1:26-27).

Neno hili linaonesha kuwa kuabudu ni zaidi ya yanayotokea Jumapili. Kuabudu kwa kibiblia ni pamoja na maisha yote. Ibada ya kuabudu ni kielelezo kilichojikita katika kuabudu, lakini ibada ya kuabudu pekee haitoshi. Lazima kudumisha mtindo wa maisha ya kuabudu. Ibada yetu ya kikundi kila wiki lazima ionekane katika maisha yetu ya kila siku.

Kuabudu halisi huonekana katika kumtii Mungu kila siku. Yakobo anaonesha kwamba ikiwa ninaimba nyimbo za sifa Jumapili, lakini ninashindwa kudhibiti ulimi wangu Jumatatu, ibada yangu haijakamilika. Kuabudu safi na isiyo na taka pamoja na huduma ya vitendo (kutembelea mayatima na wajane) na utii wa kila siku (kujitunza mwenyewe usichafuke na ulimwengu).

Katika Isaya 6, Nabii aliona maono ya Mungu akiwa katika kiti chake cha enzi. Huduma ya Isaya kama Nabii ilibadilishwa kwa kuona hili. Isaya alimsikia Bwana akiuliza "Nimtume nani, naye ni nani atakayekwenda kwa ajili yetu? Ndipo niliposema, Mimi hapa, nitume mimi" (Isaya 6:8). Kuabudu ya kweli hubadilisha maisha yetu na kutufanya kuwa tayari na watumishi wa mungu wenye ufanisi.

► Soma Malaki 1:6-9, 1 Samweli 13:8-14, Walawi 10:1-3, na Matendo 5:1-11. Je, Maandiko haya yanafundisha nini kuhusu kuabudu?

## Je, Kwa nini Ibada ni Muhimu?

A.W. Tozer aliita Ibada "lulu iliyopotea" ya kanisa la kisasa. Alisema kwamba tunajua jinsi ya kuhubiri, jinsi ya kushuhudia, na jinsi ya kuwa na ushirika. Hata hivyo, licha ya nguvu zetu zote, mara nyingi tunashindwa katika kuabudu. Tunamtazama mhubiri akihubiri; tunasikiliza kwaya, kikundi cha sifa, au msanii akisoma; tunatoa sadaka. Lakini mara nyingi tunashindwa kuabudu kweli; tunaruhusu shughuli kuchukua nafasi ya Ibada ya kweli.

Kuabudu kunapaswa kuwa muhimu kwetu kwa kuwa ni muhimu kwa Mungu.

► Soma Kutoka 20:1-5 ili kuona umuhimu ambao Mungu anauweka katika Ibada.

Amri mbili za kwanza zinahusiana na kuabudu. Amri ya kwanza inatuambia **tunamwabudu nani**. "Usiwe na miungu mingine ila mimi" (Kutoka 20:3). Amri ya pili inatuambia

[4] Neno la Kiyunani kwa kawaida linarejelea kipengele cha nje cha kuabudu. Matendo ya Mitume 26:5, Wakolosai 2:18, and Yakobo 1:26-27.

**tunavyoabudu**. "Usijifanyie sanamu ya kuchonga..." (Kutoka 20:4). Kisha, katika mstari wa mwisho wa Kutoka 20, Mungu anarudi kwenye somo la kuabudu. Mistari hii inafundisha Israeli jinsi ya kujenga madhabahu yao na jinsi ya kukaribia madhabahu kwa njia ya heshima.

► Soma Kutoka 20:23-26. Kuabudu ni muhimu kwa Mungu!

Kuabudu ni jukumu muhimu katika Maandiko. Kitabu cha Kutoka na Walawi hutoa maelekezo maalum kwa ibada ya Israeli. Zaburi ni kitabu cha nyimbo kwa ajili ya kuabudu. Katika Injili, tunaona watu wakianguka chini kumwaabudu Yesu.

► Soma Mathayo 2:11, Mathayo 8:2, Mathayo 9:18, Mathayo 14:33, Mathayo 15:25, Mathayo 28:17.

Katika kitabu cha Matendo, kanisa linakusanyika kwa ajili ya ibada.[5] Katika barua zake, Paulo anazungumzia mazoea ya ibada katika kanisa (1 Wakorintho 11 na 1 Timotheo 2). Ufunuo unatupa fursa ya kuangalia mbinguni kupata mtazamo wa kuabudu ambao tayari unafanyika kwenye kiti cha enzi cha Mungu. Kuabudu duniani ni mazoezi kwa ajili ya kuabudu mbinguni (Ufunuo 4-5). Kuabudu ni muhimu kwa Mungu.

### Ibada ni Muhimu kwa sababu katika Kuabudu tunamwona Mungu

► Soma Isaya 6:1-8. Jadili uzoefu wa Isaya katika hekalu.

Isaya 6 inatoa kielelezo muhimu cha kuabudu. Inaonesha kuwa katika ibada tunamuona Mungu. Katika Hekalu, Isaya alimwona Bwana ameinuliwa.

Ukweli huu unarudiwa mara kwa mara katika Maandiko. Alipokuwa akiabudu siku ya Bwana, Yohana aliona maono yake ya mbinguni (Ufunuo 1:10). Paulo na Sila walipokuwa wakiabudu kwa maombi na wimbo, Mungu alifunua nguvu zake (Matendo 16:25-26). Daudi alivumilia mateso yaliyomsababisha kulia, "Mungu wangu, Mungu wangu, mbona umeniacha?" (Zaburi 22:1) Katikati ya mateso yake, Daudi alimwona Mungu kupitia kuabudu na sifa; " “Na Wewe U Mtakatifu, Uketiye juu ya sifa za Israeli” (Zaburi 22:3). Katika kuabudu, tunamuona Mungu.

### Ibada ni Muhimu kwa sababu katika Kuabudu Tunajiona na Kubadilishwa

Katika hekalu, Isaya aliona si tu Bwana aliyeinuliwa, alijiona mwenyewe pia. Alipomwona Mungu kwenye kiti chake cha enzi, Isaya alipiga kelele, "Ole wangu! Kwa maana nimepotea; kwa sababu mimi ni mtu mwenye midomo michafu..." (Isaya 6:5). Kuabudu ya kweli huturuhusu kujiona sisi wenyewe kama Mungu anavyotuona.

---

[5] Waumini wa kwanza walizidi kushiriki ibada katika Hekalu na sinagogi (Matendo 2:46-47, Matendo 3:1-11, Matendo 5:12, 21, 42). Aidha, walikusanyika nyumbani kwa sala, mafundisho, na ushirika, kama ilivyoonekana katika (Matendo 2:46-47, Matendo 4:31, Matendo 5:42).

Ndiyo maana jadi za liturujia zimekuwa zikijumuisha maombi ya kutubu. Maombi ya kutubu hayasemi, "tumeasi sheria ya Mungu na kutenda dhambi kwa makusudi." Maombi ya kutubu yanatambua kuwa, "Hata moyo wa mwanadamu uliye safi kabisa ni mchafu ukilinganishwa na utakatifu kamili wa Mungu mtakatifu. Tuna uhitaji wa daima wa neema ya Mungu."

Katika kuabudu, tunajiona kwa macho ya Mungu mtakatifu. Kusingekuwa kuabudu, mtazamo huu ungekuwa ni wa kutisha. Hata hivyo, kwa sababu tayari tumemwona Mungu, tunasafishwa, si kuhukumiwa. Kwa sababu tumemwona Mungu na neema yake, tunajiona kwa uaminifu, kukiri hitaji letu kwake, na kupokea neema yake katika maisha yetu.

Kuabudu huonesha sisi ni nani, lakini haituachi kama tulivyo. Katika mwanga wa utakatifu wa Mungu, Isaya alijiona kama mchafu. Hata hivyo, badala ya kusababisha kukata tamaa, kuabudu kulileta mabadiliko.

> Kisha mmoja wa maserafi wale akaruka akanikaribia; naye alikuwa na kaa la moto mkononi mwake, ambalo alikuwa amelitwaa kwa makoleo toka juu ya madhabahu; akanigusa kinywa changu kwa kaa hilo, akaniambia, Tazama, hili limekugusa midomo yako, na uovu wako umeondolewa, na dhambi yako imefunikwa (Isaya 6:6-7).

Isaya alibadilishwa kupitia kukutana kwake na Mungu mtakatifu.

Kuabudu ya kweli hubadilisha mwabudu—Isaya Hekaluni, mwanamke Msamaria kando ya kisima, na wanafunzi juu ya Mlima wa Yesu kubadilika sura. Kukutana na Mungu hubadilisha mwabudu.

### Ibada ni Muhimu kwa Sababu katika Kuabudu Tunauona Ulimwengu Wetu

Katika kuabudu, Isaya alimwona Mungu; alijiona mwenyewe; aliona mahitaji ya ulimwengu wake. "Nami ninakaa kati ya watu wenye midomo michafu" (Isaya 6:5). Kwa kuitikia, alisema, "Mimi hapa, nitume" (Isaya 6:8). Ni katika kuabudu ambapo tunajiandaa kwa huduma yenye ufanisi kwa ulimwengu wenye uhitaji.

> "Ingia Uabudu -
> Ondoka Utumike"
>
> - Alama juu ya mlango wa kanisa

Mapema, tuliona kwamba kuabudu halisi huathiri maisha yote. Baadhi ya makanisa yamegawa kuabudu na kuhubiri Injili. Wanasema, "Fikira kuu ya kanisa letu ni kuhubiri Injili. Makanisa mengine yanaweza kujikita katika kuabudu." Au wanaweza kusema, "Lengo letu ni kuabudu. Tutawaachia kuhubiri Injili na misheni wengine." Hii inaonesha kutokuelewa kuabudu. Katika kuabudu, tunamruhusu Mungu atuoneshe mahitaji ya ulimwengu wetu. Katika kuabudu halisi kutatokea kuhubiri Injili.

Kuabudu halisi ilifunua hitaji la Isaya—na alibadilishwa na kuabudu. Kuabudu halisi ilifunua hitaji la ulimwengu wa Isaya—na yeye alijitolea kwa kubadilisha ulimwengu huo. Katika kuabudu, tutapata hamu ya kutumikia ulimwengu wetu. Jibu muhimu kwa kuabudu halisi ni, "Hapa nipo! Unitume mimi."

Oswald Chambers aliwaonya wamisionari watarajiwa, "kama umekuwa huabudu katika matukio ya kila siku, unapojihusisha na kazi ya Mungu, sio tu hautakuwa wa maana wewe mwenyewe bali pia utakuwa kizuizi kwa wale walio karibu nawe."[6]

Chambers alitambua umuhimu wa kuabudu kama maandalizi ya huduma yenye ufanisi. Katika kuabudu, Mungu huonesha mahitaji ya ulimwengu unaotuzunguka na kutuandaa kukutana na mahitaji hayo.

**Ibada Ni Muhimu Kwa sababu Kukosa kuabudu kunatutenganisha na Mungu**

► Soma Warumi 1:18-25. Je, kuna uhusiano gani kati ya kuabudu kwa udanganyifu na dhambi?

Mwanzoni mwa Warumi, Paulo anaonyesha sababu kwa nini mwanadamu amehukumiwa mbele za Mungu. Anaonesha kwamba hali ya kupotoka mwanadamu ni matokeo ya kukataa kuabudu Mungu wa kweli. Tazama mchakato ambao Paulo anaelezea katika Warumi 1:21-25.

1. Hawakumwabudu Mungu. "Kwa sababu, walipomjua Mungu hawakumtukuza kama ndiye Mungu wala kumshukuru" (Warumi 1:21). "Waliibadili kweli ya Mungu kuwa uongo, wakakisujudia kiumbe na kukiabudu badala ya Muumba anayehimidiwa" (Warumi 1:25).
2. Matokeo yake "…bali walipotea katika uzushi wao, na mioyo yao yenye ujinga ikatiwa giza. Wakijinena kuwa wenye hekima walipumbazika; wakaubadili utukufu wa Mungu asiye na uharibifu kwa mfano wa sura ya binadamu aliye na uharibifu, na ya ndege, na ya wanyama, na ya vitambaavyo" (Warumi 1:21-23).
3. Katika hukumu "Mungu aliwaacha katika tamaa za mioyo yao, waufuate uchafu…" (Warumi 1:24).

Paulo anaonesha kwamba kuanguka kwa binadamu katika upumbavu, uharibifu, na tamaa ilikuwa ni matokeo ya watu kukataa kuabudu Mungu. Hawakuabudu Mungu; walikuwa wakiabudu na kutumikia kiumbe badala ya Muumba.

Kila mtu anaabudu. Wakristo wanamwabudu Mungu. Muislamu anamwabudu Allah. Mtu asiyeamini anaabudu hekima yake mwenyewe. Kila mtu anaabudu. Ikiwa tunakataa kuabudu Muumba, tutamwabudu kiumbe. Kuabudu ni muhimu. Kuabudu kweli ya Mungu wa kweli hutubadilisha kulingana na mfano wake. Kuabudu kwa mungu wa uongo hutubadilisha kulingana na mfano wa mungu huyo. Tunakuwa kama kile tunachokiabudu.

---

[6] Oswald Chambers, *My Utmost for His Highest*, (September 10 entry). Imepatikana kutoka tovuti ya https://utmost.org/missionary-weapons-1/ on July 21, 2020.

## Malengo Matatu ya Kuabudu

Marva Dawn anataja malengo halisi matatu ya kuabudu.[7] Katika ibada, tuna:

**(1) Katika Ibada, tunakutana na Mungu**

Ibada yoyote ambayo haituleti kwa Mungu inaupungufu wa kuwa ibada ya kweli. Hii haimaanishi kuwa kila ibada itakuwa ya kihisia au ya kusisimua. Hata haijalishi kuwa kila ibada itakuwa sawa na mada yake iliyotangazwa. Lakini katika kila ibada, tunapaswa kujikuta tukiwa mbele ya Mungu. Hii inaweza kuwa kupitia ukweli uliopatikana kutoka kwenye mahubiri; inaweza kuwa kupitia kusoma Neno la Mungu; inaweza kuwa kupitia wimbo unaomsifu Mungu; inaweza kuwa wakati wa sala ambapo tunapata nguvu mpya kwa safari yetu na Mungu. Kwa njia fulani, kila ibada inapaswa kutuleta katika kukutana na Mungu.

**(2) Katika Ibada, tunachonga tabia ya kikristo**

Katika ibada tunajiona wenyewe na tunabadilishwa. Katika ibada, tunajifunza ukweli ambao unachonga tabia yetu ya Kikristo. Tunapomwabudu Mungu, tabia yetu inarekebishwa zaidi na zaidi kufanana na sura yake. Tunakuwa kama kitu chochote tunachokiabudu.

**(3) Katika Ibada, tunajenga jumuiya ya kikristo**

Katika ibada, tunatazama ulimwengu unaotuzunguka na kujitolea kutumikia mahitaji ya ulimwengu huo. Tunapofanya hivi, kanisa linajengwa, na waamini wanakua katika kila njia kuwa kama yeye aliye kichwa, yaani, Kristo (Waefeso 4:15). Ibada ya kweli ni chombo cha kujenga jumuiya ya kweli ya Kikristo.

## Je, ni aina gani ya Ibada inakubalika kwa Mungu?

► Je, ni aina gani ya kuabudu unafikiri Mungu anaikubali?

Yesu alimwambia mwanamke Msamaria kwamba waabudu wa kweli wanamwabudu kwa roho na kweli (Yohana 4:23-24). Kuna ibada ya kweli ambayo ni ya kukubalika kwa Mungu; hii inamaanisha kwamba kuna ibada ya uongo ambayo si ya kukubalika.[8]

Viongozi wa kuabudisha mara nyingi hujitambulisha kwa kuuliza, "Je, kuabudu kwetu ilihamisha kanisa? Je, tulifanya kwa mtindo ambao watu wanafurahia?" Maandiko yanatuonesha kuwa maswali muhimu zaidi ni, "Je, ibada yetu ilimheshimu Mungu? Je, tulimwabudu Mungu kama anavyohitaji? Je, ibada yetu ni ya kukubalika kwake?"

---

[7] Marva Dawn, *Reaching Out Without Dumbing Down* (Grand Rapids: Eerdmans, 1995)
[8] Baadhi ya sehemu hizi zimechukuliwa kutoka kwa David Jeremiah. *Worship*. (CA: Turning Point Outreach, 1995), 20-24.

**Ibada Ambayo Mungu Huikataa**

***Mungu hakubali Ibada isiyo na uelewa***

Mwanamke Msamaria hakujua alichokuwa anakiabudu (Yohana 4:22). Kule Athene, Paulo aliona watu ambao waliabudu Mungu asiyejulikana (Matendo 17:23).

Katika somo la pili, tutajifunza asili ya Mungu ambaye tunamwabudu. Tunapokuwa hatumjui Mungu wa kweli, ibada yetu inakuwa haina uelewa; ni ibada ya Mungu asiyejulikana. Tunafuata desturi za liturujia,[9] lakini ibada yetu ni ya Mungu asiyejulikana. Ibada lazima ifunue asili ya Mungu kwa anayemwabudu. Lazima tuimbe nyimbo zinazotoa sifa za Mungu; lazima tusome maandiko yanayosema ukweli kuhusu Mungu; lazima tufundishe mahubiri yanayofunua asili ya Mungu. Hatupaswi kukubali ibada ya Mungu asiyejulikana.

***Mungu hakubali ibada ya sanam***

Sanamu ni kitu chochote kinachochukua nafasi ya Mungu na kuwa mamlaka ya juu katika eneo lolote la maisha. Katika baadhi ya maeneo ya ulimwengu, masanamu ni sanamu za miungu ya kipagani. Katika maeneo mengine ya dunia, masanamu ni kazi, akaunti za benki, nyumba, na burudani. Kitu chochote kinachochukua nafasi ya Mungu katika maisha yetu ni sanamu. Ikiwa tunakwenda kanisani jumapili lakini tunaruhusu vitu vingine viwe na mamlaka ya mwisho katika maisha yetu ya kila siku, tunatumikia sanamu.

***Mungu hakubali ibada isiyokuwa ya kiwango cha juu.***

► Toa mfano wa ibada ya kiwango cha chini.

Nabii Malaki alionya kwamba ibada ya Israeli ilikuwa inamkera Mungu. Walipinga, "Tumemkosea vipi Mungu?" Malaki akajibu,

> “Tena mtoapo sadaka aliye kipofu, si vibaya? Na mtoapo sadaka walio vilema na wagonjwa, si vibaya? Haya! Mtolee liwali wako; je! Atakuwa radhi nawe? Au atakukubali nafsi yako? Asema Bwana wa majeshi” (Malaki 1:8).

Hawangeweza kupeleka zawadi ya mnyama mlemavu kwa gavana wa jimbo lao, lakini walileta wanyama walemavu kama dhabihu kwa Mungu Mwenyezi wa dunia yote.

Baadhi ya watu wanaamini kwamba vipengele vya nje vya ibada si muhimu kwa sababu Mungu huangalia moyo. Ni kweli kwamba Mungu huangalia moyo. Hata hivyo, ni dhahiri katika Maandiko kwamba vipengele vya nje vya ibada ni muhimu kwa Mungu. Kitabu cha Kutoka na Mambo ya Walawi hutoa maelekezo ya kina kuhusu mahitaji ya Mungu kwa ibada. Maelekezo kuhusu Hema yalikuwa ya uhakika. Mungu alitoa maelekezo ya kina kuhusu

[9] Liturujia ni mpango unaotumiwa wakati wa ibada ya Pamoja. Liturujia inaweza kuwa imepangiliwa kwa mwongozo ulioandikwa. Unaweza pia usiwe na mwongozo ulioandikwa. Katika kozi hii neno “liturujia” linarejelea mpango wowote katika kuabudu. Baadhi ya watu hulaumu liturujia yote, wakidhani kuwa ibada iliyopangiliwa sio ibada ya kweli. Tutatumia neno “liturujia” katika dhana ya kiujumla. Ibada iliyopangiliwa inaweza kuwa isiwe na kitu, au inaweza kuwa na uwepo wa Mungu.

mavazi yaliyovaliwa na makuhani. Katika Kutoka 39-40, neno "kama Bwana alivyomwagiza Musa" linarudiwa mara 13 kuonyesha utii wa Israeli. Maelezo ya ibada yalikuwa na umuhimu kwa Mungu. Alikuwa anahitaji kitu bora kutoka kwa Israeli.

Tunaabudu kwa uduni tunapompa Mungu kitu kilicho chini ya ubora wetu. Kanuni hizi bado ni muhimu, ingawa hatuleti tena dhabihu za wanyama kwa Mungu. Maswali yaliyoulizwa katika kitabu cha Malaki ni kielelezo cha maswali ambayo tunapaswa kujiuliza kuhusu ibada yetu leo.

- **Wachungaji**: "Je, ningetayarisha mahubiri yangu kwa uangalifu zaidi ikiwa gavana angekuwepo kwenye ibada? Je, ninamletea Mungu dhabihu iliyo lemavu?"
- **Wanamuziki**: "Je, ningejifunza kwa uangalifu zaidi ikiwa mwanamuziki maarufu angekuwepo kwenye kanisani? Je, ninamletea Mungu dhabihu iliyo lemavu?"
- **Waumini**: "Je, ningesikiliza kwa uangalifu zaidi mahubiri haya ikiwa rais angekuwa anayatoa? Je, ninamletea Mungu dhabihu iliyo lemavu?"

#### ***Mungu hakubali kuabudu kwa kiburi***

Mungu haikubali dhabihu ambayo haina ubora. Hata hivyo, kuna hatari ambayo tunapaswa kuepuka. Mungu haikubali dhabihu ya moyo wenye kiburi na majivuno. Ingawa tunamletea Mungu kilichobora, tunapaswa kutambua kwamba hakuna chochote tunachomletea ambacho kweli kinamstahili Mungu. Dhabihu yetu bora ni ishara ndogo tu ya kile ambacho Mungu anastahili. Tunakaribia mbele za Mungu kwa unyenyekevu, kamwe si kwa mtazamo wa kiburi na thamani yetu wenyewe.

### **Ibada ambayo Mungu anaikubali**

Ikiwa hizi ni sifa za kuabudu ambayo Mungu hakubali, ni aina gani ya kuabudu ambayo Mungu anakubali?

#### ***Ibada inayokubalika inajikita katika Mungu.***

Kama ilivyo katika Isaya 6, Ufunuo 4 inafungua dirisha kuelekea mbinguni. Katika Ufunuo 4, tahadhari ya wanaomwabudu inaelekezwa kwa yule aliyeketi juu ya kiti cha enzi. Ibada ya kweli inazingatia Mungu. Ibada ya kweli inamweka Mungu kuwa yule anayestahili kuabudiwa.

#### ***Ibada inayokubalika inampa Mungu utukufu anaostahili.***

Zaburi 96:7-8 inaonesha kusudi la kuabudu:

> Mpeni Bwana, enyi jamaa za watu, Mpeni Bwana utukufu na nguvu.
> Mpeni Bwana utukufu wa jina lake, Leteni sadaka mkaziingie nyua zake.

Kuabudu humpa Mungu utukufu anaostahili. Bila kujali nyimbo tunazotunga, hisia tunazozua, au majibu tunayopokea kutoka kwa watazamaji, kuabudu ambako hakupeleki utukufu kwa Mungu imeshindwa kutimiza lengo lake.

Lengo la kuabudu siyo kupata baraka kwa ajili yangu mwenyewe; lengo la kuabudu ni kumheshimu na kumpa utukufu Mungu. Tunapomwabudu, mara nyingi tutabarikiwa - lakini baraka yetu siyo msukumo wa ibada. Msukumo wa ibada ni kumheshimu Mungu.

Kutambua lengo la ibada kunabadilisha swali tunalouliza mara nyingi kuhusu ibada. Badala ya kuuliza, "Je, nilifurahia ibada ya leo?" tutauliza, "Je, ibada ya leo ilimheshimu Mungu?" Tunapoelewa vizuri lengo la ibada, tutabadilisha mwelekeo wetu kutoka nafsi yetu kwenda kwa Mungu.

***Ibada inayokubalika ni ibada katika roho na kweli.***

Katika mazungumzo ya Yesu na mwanamke Msamaria katika Yohana 4, alimwambia kwamba wale wanaomwabudu Mungu lazima wamuabudu kwa roho na kweli (Yohana 4:24). Hii ndiyo namna sahihi ya kuabudu.

Kawaida tunapojadili mifumo ya ibada, tunazungumzia mitindo ya muziki, utaratibu wa liturujia, na masuala mengine ya muundo. Wengi wamekasirika kwa kutokuwepo taarifa za kina kuhusu walivyofanya ibada katika kanisa la Agano Jipya. Fikiria kuhusu mambo yote ambayo hatujui kuhusu ibada ya Agano Jipya:

- **Tunajua walikuwa wanaimba zaburi.** Hatujui tuni gani walizotumia; hatujui vyombo gani walivyotumia; hatujui nyimbo mpya walizoimba.
- **Tunajua walikuwa wakiomba.** Hatujui ikiwa wote walikuwa wakiomba kwa sauti, ikiwa walikuwa wanaomba kwa vikundi vidogo, au kama mtu binafsi aliongoza maombi. Hatujui ikiwa walitumia maombi yaliyoandikwa tu (zaburi) au maombi ya papo kwa papo.
- **Tunajua walikuwa wanahubiri**. Hatujui walihubiri kwa muda gani, ni mtindo gani wa kuhubiri walitumia, au ikiwa kila ibada ilikuwa na mahubiri.

Mbali na Agano Jipya na andiko moja lililoandikwa miongo kadhaa baadaye, tunazo taarifa chache kuhusu mfumo wa ibada ya kanisa la kwanza.[10]

Kwa wasomi, ukosefu huu wa taarifa ni kero. Hata hivyo, labda hii inaonesha kwamba masuala tunayoyaona kuwa muhimu zaidi siyo muhimu kwa Mungu! Yesu alipozungumza kuhusu mfumo wa ibada, Alielekeza katika masuala mawili: roho na kweli. Masuala haya ni muhimu zaidi katika ibada ya kweli.

---

[10] Maandiko ya *Didache* (Mafundisho) ni maandiko mafupi ya mwishoni mwa karne ya kwanza au mwanzoni mwa karne ya pili. Didache inajumuisha ya maadili ya kikristo, ibada za kanisa, na uongozi wa kanisa.

Ibada katika roho labda inahusiana na roho ya binadamu. Ibada haipaswi kuwa desturi isiyo na maana; inahusisha roho. Hii ni ibada halisi; inatoka moyoni.

| Kuabudu katika roho? |
| --- |
| Mwaka wa 1994, Kanisa la Vineyard huko Toronto liliripoti kuhusu uamsho ambapo watu walicheka, wakalia kama simba, na "kukandamiza" (kutapika kama mchakato wa kuondoa hisia). Wakati wa "kucheka takatifu," mara kwa mara watu walipoteza udhibiti wa hisia zao. Badala ya kuweka msisitizo kwenye kuruhusu Neno la Mungu kutenda kazi kwa kina mioyoni mwa watafutaji, "Baraka ya Toronto" ililenga tu jibu la kihisia. Je, hii ni ibada katika roho? Je, ni ibada halisi? |

Ibada katika kweli inalingana na mafundisho ya Biblia. Ni zaidi ya hisia nzuri au jibu la kihisia. Kama wachungaji na viongozi wa ibada, tunachunguza kila sehemu ya ibada yetu, tukijiuliza "Je, hii ni kweli?" Maneno tunayohubiri, nyimbo tunazotunga, na maombi tunayotoa lazima yawe ya uaminifu kwa Maandiko. Mungu haguswi na maneno matupu; anatafuta ibada katika roho na kweli (Yohana 4:24).

| Kuabudu katika kweli? |
| --- |
| Mchungaji Bill anaelewa umuhimu wa muziki katika ibada. Anathamini nyimbo za kitabuni, lakini pia anakaribisha nyimbo mpya. Wimbo ambao umekuwa maarufu katika makanisa mengi unafundisha kwamba waamini huendelea daima kuanguka katika dhambi za kukusudia na kisha hutafuta marejesho. Wimbo huo hautoi ahadi ya maisha ya Kikristo ya kushinda. Kusikiliza wimbo huo, Bill alisema, "Wimbo huu si wa kweli kulingana na Maandiko, lakini ni wimbo tu. Watu wanapenda muziki; maneno si muhimu." Je, hii ni ibada katika kweli? |

## Hatari za Ibada: Mbadala wa Ibada ya Kweli

Yesu aliongelea kuhusu ibada ya kweli. Kama kuna ibada ya kweli basi, kutakuwa na ibada ya uongo. Martin Luther mara nyingi alinukuu methali ya Kijerumani, "Popote ambapo Mungu anajenga kanisa, Shetani hujenga kanisa jirani." Shetani anapenda kututia moyo kuweka mawazo ya uongo badala ya ibada ya kweli. Mara nyingi tumekubali ibada ifuate mahitaji ya utamaduni badala ya kufuata mahitaji ya Mungu tunayemwabudu. Je, baadhi ya mbadala wa ibada ya kweli ni nini?

### Ibada ya chapuchapu

Hii ni ibada inayojikita katika urahisishaji binafsi, badala ya kumfurahisha Mungu. Mfano Kuna migahawa 35,000 ya McDonald's duniani. Wateja milioni 68 hula katika McDonald kila siku. Hii si kwa sababu McDonald inatoa chakula bora kilichopo. Si kwa sababu wanatoa lishe ambayo ni ya kipekee kwa afya. Ni kwa sababu McDonald inatoa urahisi, wepesi, na

mazingira ya kuvutia. Katika ibada za chapuchapu, shughuli kuu ni urahisi, wepesi, na burudani.

McDonald's na ibada chapuchapu hupima mafanikio kwa idadi. McDonald's hujivuna kuwa, "watu zaidi ya bilioni 300 wamehudumiwa." ibada ya chapuchapu hujivuna, "tuliongezeka kwa 17% kuliko mwaka uliopita." Idadi badala ya utakatifu huwa kigezo cha mafanikio.

Kuna mahitaji machache kwa wa ibada za chapuchapu. Ibada hizo zinatoa muziki mzuri, wazungumzaji wenye burudani, na vivutio vizuri - yote kwa gharama ndogo. Chapuchapu huvutia umati, lakini chakula cha kiroho mara nyingi hakina maana na hakisaidii afya ya kiroho. Ni vyema kutafuta kuvutia watu kwa Injili, lakini chapuchapu sio ibada ya kweli.

**Ibada ya Makumbusho**

Hali katika makumbusho ni kinyume cha McDonalds. Katika makumbusho, kuna mkazo mkubwa katika kuhifadhi utamaduni. Watu huonesha heshima wanapotazama maonesho. Zaidi ya hayo, makumbusho mengi hayasisitizi ushiriki na ahadi ya kibinafsi. Huwa hauombwi kuweka michoro yako kwenye ukuta wa Makumbusho ya Sanaa ya jengo la makumbusho!

Katika Ibada ya Makumbusho, shughuli kuu ni utamaduni na mfumo. Tunaimba nyimbo ambazo kanisa limekuwa likizimba daima. Tunajivunia uaminifu wetu kwa utamaduni. Lakini ni jambo linalowezekana watu kuhudhuria wiki baada ya wiki bila kukabiliana na mahitaji ya Mungu kwa ahadi ya kibinafsi. Ni jambo linalowezekana kuhudhuria kanisa kila Jumapili na kutazama maonyesho (hotuba, nyimbo, maombi) bila kufanyika mabadiliko ya maisha. Ni jambo zuri kuuthamini urithi wetu, lakini Ibada ya Makumbusho sio ibada ya kweli.

**Ibada ya Darasani**

Katika darasa, mwalimu ndiye anayesimamia. Mwalimu ndiye anayeamua kile ambacho darasa linajifunza. Mwalimu huendesha mihadhara; wanafunzi husikiliza na kuchukua maelezo. Ushiriki unadhibitiwa na mwalimu.

Katika Ibada ya Darasani, mchungaji ndiye mtu muhimu. Mahubiri ni kitovu cha ibada; kila kitu kingine ni kama maandalizi tu. Waumini wako hapo kusikiliza na kuchukua maelezo. Ibada imepunguzwa kuwa shughuli ya kiakili. Ni jambo zuri kutafuta kuwasiliana ukweli katika ibada yetu; tunapaswa kufafanua ukweli kwa waabudu wetu, lakini Ibada ya Darasani sio ibada ya kweli.

**Ibada ya Kweli**

Ibada ya kweli inazingatia Mungu. Ibada ya kweli inauliza, "Mungu anataka nini?" Ibada ya kweli husaidia kuona mwenyewe kupitia macho ya Mungu - na hilo ni gumu kwa mtu ambaye hataki kubadilishwa na Mungu. Ibada ya kweli ni kumhusu yeye. Ibada ya kweli inahusisha msalaba, sadaka, kujisalimisha. Ibada ya kweli hubadilisha mwabudu.

## Hitimisho: Ushuhuda wa Martha

Je, ibada ina umuhimu gani? Sikiliza ushuhuda wa Martha.

"Mimi ni mtu wa vitendo. Mtu lazima apige deki sakafu, apike chakula, na ajali mambo ya nyumbani. Hiyo ni nguvu yangu; nina karama ya huduma.

"Ninakumbuka siku Yesu alipotembelea nyumba yetu ndogo huko Bethania. Nilikuwa na wasiwasi kumkaribisha mwalimu muhimu hivyo katika nyumba yetu. Nilitaka kila kitu kiwe kamilifu. Baadaye Luka aliandika, 'Martha alikuwa akihangaika kwa utumishi mwingi ' (Luka 10:40) Nilikuwa ninajizatiti kufanya kila kitu kiwe kamili.

"Wakati nilikuwa nikijishughulisha nyumbani, Maria alikaa chumba kingine akimsikiliza Yesu. Sikufurahishwa; nilihitaji msaada! Zaidi ya hayo, yeye ni mwanamke; hahitaji kujifunza kutoka kwa Rabbi.

"Nikaingiwa na hasira kiasi kwamba niliingia ndani na kusema, Bwana, hujali kwamba dada yangu ameniacha nisaidie peke yangu? Mwambie basi anisaidie.' (Luka 10:40) Sitakuja nisahau jibu lake. Yesu alinitazama na kutikisa kichwa chake. Martha, Martha, unasumbuka na kufadhaika kwa ajili ya vitu vingi, lakini kinatakiwa kitu kimoja tu, na Mariamu amelichagua fungu lililo jema ….' (Luka 10:41-42).

"Ulikuwa ujumbe gani Mwalimu alikuwa akinipa? Hakumaanisha kwamba huduma si muhimu. Muda mfupi kabla ya kututembelea, Yesu alitoa mfano wa Msamaria Mwema - simulizi kuhusu huduma (Luka 10:25-37). Yesu hakumaanisha kwamba huduma si muhimu; alikuwa akinifundisha kwamba **huduma yangu inapaswa kutiririka kutoka katika abudu yangu.** Kitu muhimu ni ibada. Ikiwa ninaabudu, huduma itatiririka yenyewe; sitakuwa 'na wasiwasi na kuhangaika.' (Luka 10:41).

"Siku hiyo, nilijifunza somo katika maisha. Tangu siku hiyo, huduma yangu haijawahi tena kuwa kipaumbele kuliko ibada yangu. Tangu siku hiyo, nilichukua muda kushiriki na Maria miguuni mwa Yesu; nilitumia muda katika kumwabudu."

### Kujipima

Jitathmini mwenyewe, "Ninawezaje kuwa mwabudu bora zaidi?" Tafuta maeneo ambapo unaweza kufanya ibada yako ifanane zaidi na maana ya ibada ya Biblia.

## Mapitio ya Somo la 1

(1) Je, kuabudu ni nini?

- Ibada ni kujisalimisha kwa heshima (Ufunuo 4:10-11).
- Ibada ni huduma (Warumi 12:1).
- Ibada ni sifa (Zaburi).
- Ibada ni ushirika (Matendo 2:42).
- Ibada inajumuisha maisha yote (Yakobo 1:26-27).

(2) Je, kwanini Ibada ni muhimu?

- Katika Ibada tunamwona Mungu (Isaya 6:1-8).
- Katika Ibada tunajiona na kubadilika (Isaya 6:1-8).
- Katika Ibada tunatazama ulimwengu wetu (Isaya 6:1-8).
- Kushindwa kuabudu kutatutenga na Mungu (Warumi 1:18-25).

(3) Malengo ya Ibada:

- Katika Ibada, tunakutana na Mungu.
- Katika Ibada, tunajenga tabia ya Kikristo.
- Katika Ibada, tunajenga jumuiya ya Kikristo.

(4) Je, ni ibada gani inayokubalika na Mungu?

- Ibada inayokubalika inajikita katika Mungu (Ufunuo 4).
- Ibada inayokubalika inampa Mungu utukufu anaoustahili (Zaburi 96:7-8).
- Ibada inayokubalika ni katika roho na kweli (Yohana 4:23-24).

## Somo la 1 Mazoezi

(1) Je, Biblia inaelezeaje kuhusu Ibada? Andika jibu lako katika ukurasa moja ukizingatia mistari ifuatayo:

- Zaburi 111:1-2
- Zaburi 147:1
- Zaburi 150
- Isaya 6:1-8
- Ufunuo 4

Kama unajifunza ukiwa katika kikundi, jadiliana jibu lako na wengine katka darasa linalofuata.

(2) Mwanzoni mwa somo linalofuata, utafanya jaribio kufuatia somo hili. Kwa kujitayarisha soma maswali ya jaribio kwa uangalifu.

## Mradi wa kozi

### Mchakato wa Siku 30 wa Ibada [11]

Utashughulikia mradi huu kipindi chote cha kozi hii. Mwishoni mwa kozi, utaripoti kwamba umekamilisha mradi huu. Hutawasilisha jarida lako kwa kiongozi wa darasa.

Kila siku kwa siku 30, utatumia dakika chache kutafakari moja ya sifa za Mungu. Ni bora kufanya mradi huu asubuhi ili uweze kutafakari kuhusu sifa hiyo mchana mzima. Maana ya kutafakari ni kufikiria kwa kina kuhusu kitu fulani.

Uwe na kitabu cha kumbukumbu utakachokitumia kwa matukio ya kila siku. Anza kila siku kwa maombi ukimwomba Mungu ajifunue kwako. Kisha, fungua kitabu cha Zaburi na anza kusoma. Lengo la mradi huu ni kutafakari, sio kusoma kwa wingi. Unaweza kusoma aya moja au Zaburi nzima.

Unaposoma, tafuta sifa moja ya Mungu au Mungu kufananishwa na mtu au kitu kingine. Sifa ni sehemu ya tabia ya Mungu - huruma yake, utakatifu wake, utunzaji wake. Mifano ya kumfanisha Mungu na kitu kingine ni kama vile –yeye ni mchungaji, mwamba, kimbilio letu au ngao yetu.

Ukipata sifa au mfananisho wa Mungu ambao unakugusa, andika sifa hiyo juu ya ukurasa wa jarida lako. Chini ya yake, andika aya inayohusiana na sifa hiyo.

Fikiria kuhusu sifa hiyo na inamaanisha nini kuhusu Mungu. Baada ya kuomba, andika mawazo yako kuhusu Mungu na sifa hii. Hii si karatasi ya kisomi; ni jarida la kibinafsi la ibada. Kupitia siku nzima, tafakari kuhusu Mungu na tabia yake. Msifu kwa ajili ya yeye ni nani. Unapofanya hivi kwa siku 30, utakuwa na maarifa ya kina zaidi kumhusu Mungu.

---

[11] Mradi huu umechukuliwa kutoka kwa Louie Giglio, *The Air I Breathe: Worship as a Way of Life* (Sisters, OR: Multnomah Publishers, 2003).

**Jaribio Somo la 1**

(1) Ulipewa maana tatu za kuabudu mwanzoni mwa somo hili. Andika maana unayoikumbuka.

(2) Orodhesha vipengele vinne vya ibada ya kibiblia.

(3) Mwanamke Msamaria alipojadili kuhusu mahali pa kimwili pa ibada, Yesu alionyesha mahali pa ________ pa ibada.

(4) Katika Zaburi, neno ___________ mara nyingi linatumika kupendekeza furaha ya ibada.

(5) Kulingana na Yakobo, ibada safi na isiyo na doa inajumuisha nini vipengele viwili?

(6) Orodhesha sababu nne kwa nini ibada ni muhimu.

(7) Kulingana na somo hili, ni tabia zipi tatu za kuabudu ambazo ni za kukubalika kwa Mungu?

(8) Andika Yohana 4:23-24 kwa kumbukumbu.

# Somo la 2
# Mungu na Muabuduji

## Malengo ya Somo

Mwisho wa somo hili, mwanafunzi anapaswa:

(1) Kutambua taswira ya kibiblia ya Mungu na jukumu lake katika ibada yetu.

(2) Kuelewa matakwa ya Mungu kwa wanaomwabudu.

(3) Kutafuta kuthibitisha matakwa ya Mungu kwa wanaomwabudu.

(4) Kuthamini neema ya Mungu kwa kuruhusu mwanadamu kuingia katika uwepo wake kwa ajili ya ibada.

## Matayarisho kwa somo hili

*Kariri Ufunuo 5:9-14.*

## Utangulizi

Kikundi kidogo kiliketi kuzungumzia somo la Biblia la wiki. Swali la majadiliano lilikuwa, "Mungu yukoje na tunamwabudu vipi?"

Sara alianza kusema kwanza. "Nikifikiria kuhusu Mungu, nafikiria kama ni babu mwenye ndevu ndefu nyeupe. Yeye anatuona kama wajukuu. Inamsikitisha anapotuona tukifanya dhambi, lakini anatupenda na anaelewa kuwa tunajitahidi. Sioni kama Mungu anajali tunavyomwabudu, mradi tuoneshe kwamba tunampenda."

Anna akajibu. "Mimi nafikiria kuhusu Mungu kama ni baba mwenye madai sana. Haji karibu sana na watoto wake, lakini anatazama ili aone ikiwa tunatii. Katika kuabudu, tunahitaji kuonesha kwamba tunanyenyekea na tunatii. Sipendi nyimbo zinazomwambia Mungu kuwa yeye ni rafiki yetu; lazima tukumbuke kwamba yeye ni Bwana wetu wa mbinguni na sisi ni watumishi wake! Naenda kanisani ili kujua Mungu anatarajia nitende nini."

Abigaili hakuridhika na majibu yote ya watu hawa. "Mimi nafikiria kuhusu Mungu kama rafiki. Biblia inasema kwamba Mungu anapenda kutoa zawadi njema kwa watoto wake. Naenda kanisani ili kujua Mungu anataka kunifanyia nini. Ninamwomba na kumwambia ninahitaji nini. Nasikiliza mahubiri na muziki ili kujifunza jinsi Mungu atakavyonibariki maishani mwangu. Mungu anataka kutoa zawadi njema; naenda kanisani kupokea hizo zawadi."

Kila mmoja wa hawa wanamke kati yao ana dhana tofauti kuhusu Mungu. Kwa sababu hiyo, kila mmoja ana matarajio tofauti kuhusu kuabudu.

Sara anamtarajia Mungu babu mwenye huruma ambaye hajali sana kuhusu vipengele vya kuabudu kwetu. Kwake yeye ibada bora, ni ile ambayo kila mtu atamwabudu kwa namna ambayo inamfanya ajisikie anafarijika zaidi. Sara atashangaa kama ibada itafanyikia Hemani. Huko angeona kuwa kumbe Mungu anajali kila kipengele cha ibada.

Anna anamwona Mungu kama yuko mbali na mkali. Angekuwa na wasiwasi na uhusiano wa kina unaopatikana katika Zaburi na malalamiko ya kweli ya Ayubu kwa Mungu. Kwake ibada bora itaendeleza umbali kati ya mwabudu na Mungu. Maombi yatakuwa rasmi na yaliyopangiliwa. Muziki utakuwa mzuri, lakini usiogusa hisia. Anna hangependa ushirika wa karibu uliopatikana katika makanisa ya nyumbani katika karne ya kwanza.

Katika mawazo ya Abigaili, Mungu ni mtumishi ambaye yupo kwa ajili ya kutoa mahitaji ya binadamu. Anapoondoka katika ibada, swali lake ni, "Nilipata nini katika ibada?" Muziki lazima uwe na uguse hisia zake binafsi. Maombi lazima yaelekee mahitaji yake binafsi. Mahubiri lazima yawe na uhalisia wa vitendo na lazima yaseme mahitaji yake halisi. Abigail angeweza kuudhika na ibada ya Hekaluni. Ibada ya Hekalu ilikuwa inahusu kuleta dhabihu kwa Mungu, sio kuhusu Mungu kuleta zawadi kwa mwanadamu.

Kila mmoja wa wanawake hawa anatafuta ibada inayohusisha dhana yake kuhusu Mungu. Uelewa wetu kuhusu Mungu una athari kubwa kwa ibada yetu.

► Jadili dhana yako kuhusu Mungu. Jinsi gani dhana yako kuhusu Mungu inaathiri ibada yako? Katika somo hili tutaangalia maswali mawili.

**(1) Je, tunamwabudu nani?**

Kwa kuwa ibada ni kumpa Mungu heshima anayostahili, kadiri tunavyomjua Mungu, ndivyo tutakavyokuwa tumejitayarisha vizuri kwa ajili ya ibada ya kweli. Sura ya Mungu iliyopotoshwa husababisha ibada iliyopotoshwa.

Picha ya ibada ya sanamu kibiblia inaonesha kanuni hii. Baali alikuwa mungu wa uzazi, mungu wa mazoea yasiyodhibitiwa. Manabii wa Baali walikuwa wakimwabudu vipi? Kwa hisia na desturi zisizodhibitiwa. " Wakapiga kelele, wakajikata-kata kwa visu na vyembe kama ilivyo desturi yao, hata damu ikawachuruzika" (1 Wafalme 18:28).

**(2) Je, Mungu anahitaji nini kwa wanaoabudu?**

Kwa kuwa Mungu ni mtakatifu, tunawezaje kuingia mbele zake? Mungu anahitaji nini kutoka kwa wale wanaomwabudu?

Miungu wa uongo kama Baal na Moleki hawakuwa watakatifu; waabudu wao hawakuwa na haja ya kuwa watakatifu. Waabudu wa Baal walikuwa kama Baal, hawakuwa watakatifu kimaadili. Tunakuwa kama vile tunavyomwabudu.

Mungu wa kweli ni mtakatifu. Kwa sababu hii, anahitaji watu watakatifu. Waabudu wa Yehova walikuwa kama Yehova; walipaswa kuwa watu watakatifu wanaomwabudu Mungu mtakatifu.

## Je, tunamwabudu nani?

"Mungu, Wewe ni...
Mkuu kuliko wote, mwenye sifa kuu;
mwenye huruma zaidi na mwenye haki zaidi;
aliyefichika zaidi na yupo karibu zaidi;
mzuri zaidi na mwenye nguvu zaidi;
daima akifanya kazi, daima akistarehe;
akikusanya, lakini hana haja ya chochote;
akishikilia na kulinda;
anayeumba na kudumisha;
akutafutaye, ingawa anamiliki vitu vyote."
- Imetokana na Augustine

Fikiria unavutiwa na machweo mazuri ya jua.[12] Ghafla unaacha kuangalia machweo ili kupiga picha yako: "Mimi Nikiangalia Machweo." Hii inaitwa "selfie," picha yako mwenyewe. Umakini wako umehamia kutoka machweo kuja kwako mwenyewe. Mtu anayechukua selfie anavutiwa zaidi na uwepo wake kuliko na tukio analoliona.

Mungu anastahili ibada yetu bora. Lakini tunapojikita katika ubora wa ibada yetu badala ya katika Mungu tunayemwabudu, tunakuwa tunapiga picha ya kidini ya 'selfie' ("Mimi Nikiabudu Mungu"). Hatupaswi kamwe kuruhusu mahangaiko yetu kuhusu ubora wa ibada yetu ya kuabudu kuchukua nafasi ya umakini wetu kwa Mungu tunayemwabudu!

C.S. Lewis aliandika kuhusu sanamu ya kuwa na uangalifu zaidi kwa ibada ya kuabudu kuliko kwa Mungu. Hivi karibuni, D.A. Carson alionya kwamba tunaweza kushawishiwa "kuabudu ibada badala ya kumuabudu Mungu."[13]

Ibada haiwezi kuwa ibada ya kweli mpaka nimepoteza nafsi yangu katika kumwabudu Mungu. Katika ibada ya kweli, natoa umakini zaidi kwa Mungu kuliko kwa ubora wa jitihada zangu za kuabudu. Ibada ya kweli inajikita kwa Mungu, si katika ubora wa uzoefu wangu wa kuabudu.

Kama tulivyoona katika Somo la 1, amri ya kwanza inatuambia tunamwabudu nani. "Mimi ndimi Bwana, Mungu wako... Usiwe na miungu mingine ila mimi" (Kutoka 20:2-3). Kwa kuwa kuabudu inamaanisha kumpa Mungu heshima anayostahili, kujifunza kuabudu kunapaswa kuanza kwa kujiuliza Mungu ni nani? Kuna nyimbo nne katika kitabu cha Ufunuo hutoa jibu la sehemu kwa swali hili.

### Tunamwabudu Muumbaji (Ufunuo 4)

► Soma Ufunuo sura ya 4 kwa sauti. Chukua muda kufikiria mandhari ya kimbingu. Kitabu hiki kinatuambia nini kuhusu Mungu tunayemwabudu?

Na dirisha lake kuelekea mbinguni, Ufunuo 4 hutoa mtazamo wa Muumba tunayemwabudu.

---

[12] Sehemu kubwa ya haya yamechukuliwa kutoka kwa Warren Wiersbe, *Real Worship*, (Grand Rapids: Baker Books, 2000), Sura ya 5.
[13] Imechukuliwa kutoka kwa D.A. Carson, *Worship by the Book*, (Grand Rapids: Zondervan, 2002), 31.

***Muumbaji ni mwenye enzi.***

Mungu anaketi katika kiti cha enzi juu ya ulimwengu. Neno "kiti cha enzi" hutumiwa mara 14 katika sura hii. Yeye ni Bwana Mungu Mwenyezi; yeye ni mwenye enzi. Ibada lazima iutambue daima uweza wa Mungu. Katika ibada, tunaelezea utii wetu kwa Mungu mwenye enzi. Yeye ni Baba mwenye upendo, lakini yeye ni mwenye enzi.

***Muumbaji ni Mtakatifu.***

Mungu anaonekana kama Mungu mtakatifu katika maandiko yote.

- Mungu anawaambia Waisraeli, "Mimi Bwana, Mungu wenu, ni mtakatifu" (Walawi 19:2).
- Mungu anasifiwa, "Na Wewe U Mtakatifu, Uketiye juu ya sifa za Israeli" (Zaburi 22:3).
- Nabii Isaya anaona malaika wakiabudu karibu na kiti cha enzi, "Mtakatifu, mtakatifu, mtakatifu, ni Bwana wa majeshi; dunia yote imejaa utukufu wake" (Isaya 6:3).
- Mtume Yohana anaona mbinguni, ambapo wazee wanapaza sauti, "Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu, Bwana Mungu Mwenyezi, aliyekuwako na aliyeko na atakayekuja!" (Ufunuo 4:8).

Tunamuabudu Mungu mtakatifu.

***Muumbaji ni wa Milele.***

Yeye alikuwako na yupo na atakayekuja (Ufunuo 4:8).

Daudi alielekeza kwa mshangao wa uumbaji kama dirisha la utukufu wa Mungu. "Mbingu zauhubiri utukufu wa Mungu, Na anga laitangaza kazi ya mikono yake" (Zaburi 19:1). Sura ya kwanza ya Mwanzo inaanza na Mungu kama Muumbaji; kitabu cha mwisho cha Biblia kinatukumbusha tena kwamba Mungu ni Muumbaji na kwamba atatawala milele juu ya viumbe vyake.

Kusisitiza huku kunadhihirisha umakini sahihi wa kuabudu. Sisi tuliumbwa kumwaabudu Mungu Muumba. Ibada ni sahihi kumhusu yeye, si sisi. Tunapojizamisha katika kumwabudu Muumbaji, mbingu zinaendelea kutangaza utukufu wake.

**Tunamwabudu Mkombozi (Ufunuo 5)**

► Soma Ufunuo 5 kwa sauti. Je, Ni nini kinachotueleza kuhusu Mungu tunayemwabudu katika mandhari hii yenye utukufu?

Kama Wakristo, hatupaswi kamwe kupoteza hisia za kustaajabu tunapokumbuka kwamba Mfalme wa ulimwengu ametupatia ukombozi wetu. Katika Ufunuo 5, tunatazama jinsi Mwana-Kondoo wa Mungu, Mkombozi wa ulimwengu, anavyoabudiwa. Yesu anaitwa

"Mwana-Kondoo" mara 28 katika Kitabu cha Ufunuo. Hii ni mojawapo ya picha kuu katika Ufunuo.

***Tunamuabudu Mkombozi kwa sababu ya yeye ni nani.***

Yeye ni Simba wa kabila la Yuda. Yeye anatokana na Daudi. Yeye ni Mwana-Kondoo aliyechinjwa. Yeye ni Mwana-Kondoo mwenye pembe saba na macho saba (Ufunuo 5:6), ishara ya ukamilifu. Katika kuabudu, tunamtukuza Yesu kwa sababu ya yeye ni nani. `Ibada ni "karamu ya utukufu wa ukamilifu wa Kristo" (John Piper).

***Tunamuabudu Mkombozi kwa sababu ya mahali alipo.***

Katika Ufunuo 5:6, Yesu yuko katikati ya ibada ya mbinguni. Yeye yuko kati ya kiti cha enzi na viumbe hai wanne na kati ya wazee. Mwandishi wa Waebrania anatoa ahadi nzuri kwamba mtetezi wetu ameketi upande wa kulia wa kiti cha enzi cha Mungu (Waebrania 12:2).

***Tunamuabudu Mkombozi kwa sababu ya kile alichofanya.***

Katika hali ya kuzingatia thamani ya Mungu, baadhi ya walimu wamependekeza kimakosa kwamba tunapaswa kumuabudu Mungu tu kwa ajili ya yeye ni nani, si kwa ajili ya yale anayotufanyia. Yohana Mfunuliwa anaonesha kwamba ibada ya mbinguni inamtukuza Mwana-Kondoo kwa yale aliyoyafanya. " Astahili Mwana-kondoo aliyechinjwa..." (Ufunuo 5:12).

Huu mfano unaonekana katika Zaburi. Zaburi 134 inatuamuru kumbariki Bwana. Haitupi sababu; tunamtukuza kwa sababu yeye ni Mungu. Hii inafuatwa na Zaburi 135-136, ambazo zinamtukuza Mungu kwa sababu ya yale aliyoyafanya katika historia ya Israeli. Tabia ya Mungu, lakini pia matendo yake makuu, yanastahili sifa. Tunapaswa kumsifu Mungu kwa ajili ya yeye ni nani **na** kwa ajili ya yale aliyoyafanya.

### Tunamuabudu Mfalme (Ufunuo 11:15-18)

Ufunuo 11 hutoa mtazamo mwingine wa ibada ya mbinguni. Katika tukio hili, wazee wanamtukuza Mfalme ambaye amechukua kiti chake cha enzi kwa haki. Ingawa falme za dunia zinampinga, mwishowe lazima zitii mamlaka yake. "Ufalme wa dunia umekwisha kuwa ufalme wa Bwana wetu na wa Kristo wake, naye atamiliki hata milele na milele" (Ufunuo 11:15).

Katika wimbo huu, Mfalme anatukuzwa kwa hukumu yake ya haki juu ya ulimwengu. Wimbo huu hutukumbusha kwamba Mungu anatawala kwa nguvu kuu. Ingawa mataifa walikuwa na ghadhabu, Mungu aliwahukumu kwa haki.

Ibada ni kuabudu katika ukweli. Ibada ya kweli haipunguzi hukumu za kweli za Mungu. Tena, ibada ya Ufunuo inalingana na ibada ya Zaburi. Zaburi 96 ni wimbo mpya kwa Bwana. Katika wimbo huu, Mungu anatukuzwa miongoni mwa mataifa. Anahofiwa kuliko miungu

yote. Anatukuzwa kwa sababu atawahukumu watu kwa haki. Ibada ya kweli inajua kwamba lazima tumwogope Mungu; tunamtukuza kama Mfalme.

**Tunamuabudu Bwana Arusi Mshindi (Ufunuo 19:1-9)**

Katika darasa la masomo ya uchunguzi wa Biblia, mwalimu aliuliza, "Je, ni wangapi miongoni mwenu wanafurahia Kitabu cha Ufunuo?" Wanafunzi wachache sana waliinua mikono yao. Mwalimu alipouliza, "Kwa nini mnachukia kitabu cha Ufunuo?" mwanafunzi mmoja alijibu, "Unatisha!". Wanafunzi hawa wanapata woga kutokana na Ufunuo kwa sababu wanapuuzilia mbali sehemu bora za kitabu hicho. Wanazingatia hukumu zinazowapata wale wanaopinga Mungu. Hilo bila shaka ni ujumbe muhimu katika Ufunuo. Lakini kwa Wakristo, ujumbe mkuu wa Ufunuo ni ushindi wa mwisho wa Mungu wetu!

Ufunuo 19 unafafanua ujumbe huu. Sura hii inajumuisha maelezo ya ziwa la moto linalowaka kwa kiberiti (Ufunuo 19:20) na ndege wanaokula nyama ya wafalme, nyama ya makapteni, na nyama ya wanaume wenye nguvu... (Ufunuo 19:18). Hii ndiyo hatima ya wale wanaopinga Mfalme. Kwa wale wanaomtukuza Mfalme kwa unyenyekevu wenye heshima, Ufunuo 19 ni wimbo wa furaha. Kahaba mkuu ambaye aliufanya ulimwengu uharibike kwa uasherati wake (Ufunuo 19:2) anaharibiwa. Bwana Arusi mshindi anawashinda adui zake na kumpokea bibi arusi wake mtakatifu kwenye karamu ya arusi ya Mwana-Kondoo (Ufunuo 19:9).

Kama mwitikio wa ushindi huu mkubwa, Yohana alisikia " sauti ya makutano mengi, na kama sauti ya maji mengi, na kama sauti ya radi yenye nguvu, ikisema, Haleluya; kwa kuwa Bwana Mungu wetu, Mwenyezi, amemiliki. Na tufurahi, tukashangilie, tukampe utukufu wake; kwa kuwa arusi ya Mwana-Kondoo imekuja, na mkewe amejiweka tayari" (Ufunuo 19:6-7).

Katika ibada, tunamtukuza Bwana Arusi Mshindi. Ibada yetu inatarajia siku za usoni ambazo Yesu anaandaa kwa ajili ya bibi Arusi wake. Moja ya sababu kuu ya umuhimu wa ibada ni kwamba ibada inatupa nguvu ya kuishi maisha ya Kikristo yenye ushindi katika ulimwengu wenye upinzani. Katika ibada, tunakumbuka kwamba " wenyeji wetu uko mbinguni; kutoka huko tena tunamtazamia Mwokozi, Bwana Yesu Kristo; atakayeubadili mwili wetu wa unyonge, upate kufanana na mwili wake wa utukufu, kwa uweza ule ambao kwa huo aweza hata kuvitiisha vitu vyote viwe chini yake" (Wafilipi 3:20-21).

Nyimbo hizi nne kutoka kwenye Ufunuo zinatupatia taswira ya Mungu tunayemuabudu. Katika ibada, tunahamisha mawazo yetu wenyewe kutoka kwetu na kuyaelekeza kwa Mungu. Katika ibada, tunapiga magoti mbele ya Muumbaji; katika ibada, tunamtukuza Mkombozi; katika ibada, tunasherehekea Kristo Mfalme; katika ibada, tunatarajia umilele mbele za Bwana Arusi Mshindi.

Huyu ndiye Mungu tunayemuabudu. Hii inasababisha swali, "Nani anaweza kuabudu? Mungu anahitaji nini kutoka kwa wale wanaomwendea mbele ya uso wake?"

## Je, Mungu anahitaji nini kwa wanaoabudu?

Katika mazungumzo yake na mwanamke Msamaria,[14] Yesu alitoa kauli ya kushangaza. Baada ya kumwambia kwamba waabudu wa kweli watamuabudu Baba kwa roho na kweli, Yesu alisema kwamba Baba anatafuta watu kama hao wamuabudu (Yohana 4:23). Mungu anatafuta aina fulani ya mwabudu, yule anayeabudu kwa roho na kweli. Mungu anatafuta waabudu.

Je, ni tabia gani ambazo Mungu anatafuta kwa wale wanaomwabudu? Mtu yeyote anaweza kuhudhuria ibada; mtu yeyote anaweza kuimba nyimbo za sifa; mtu yeyote anaweza kuomba. Hata hivyo, Mungu ametoa mwongozo maalum kwa tabia za mwabudu wa kweli. Mahali pekee pa kuona hili ni Zaburi 15.

► Soma Zaburi 15. Je, inasemaje kuhusiana na Maisha ya mwabudu?

Zaburi 15 ni zaburi ya utaratibu wa ki-ibada. Inaelezea mazungumzo kati ya kuhani na mwabudu kwenye mlango wa Hekalu. Mwabudu anatafuta lango la kuingia katika Hekalu takatifu la Mungu. Katika kujibu swali la mwabudu " ni nani atakayekaa Katika hema yako?" kuhani anataja mahitaji ya kuingia. Mtindo huu huo hutumiwa katika Zaburi 24:3-6 na Mika 6:6-8. Zaburi 15 inagawanyika katika sehemu tatu:

1. Swali: Nani awezaye kuabudu?
2. Jibu: Maelezo ya mwenye kuabudu
3. Hitimisho: Ahadi kwa mwenye kuabudu

### Swali: Nani Anaweza Kuabudu? (Zaburi 15:1).

Mlangoni mwa Hekalu, mwabudu anauliza, 'Bwana, ni nani atakayekaa Katika hema yako? Ni nani atakayefanya maskani yake Katika kilima chako kitakatifu?' Maswali haya yanamaanisha sifa tatu za mwabudu.

#### *Mwabudu wa kweli anajua hofu ya Mungu.*

Zaburi hii inaonesha kwamba kuingia katika uwepo wa Mungu kamwe si jambo la kawaida. Mwabudu wa kweli anaelewa kwamba Mungu ni mtakatifu na sisi tumetengwa naye.

Katika Maandiko, kuna hisia ya hofu inayohusishwa na uwepo wa Mungu. Katika Mlima Sinai, watu walionywa kuwa mbali na mlima ambapo Mungu aliongea na Musa (Kutoka 19:7-25). Juu ya Mlima ambaye Yesu aligeuka sura, wanafunzi walikuwa na hofu sana (Mathayo 17:6).

---

[14] Kiasi kikubwa cha haya kimechukuliwa kutoka"The Worshipper's Approach to God" by Ronald E. Manahan, kinachopatikana katika Sura ya 2 ya *Authentic Worship*, kilicho haririwa na Herbert Bateman. (Grand Rapids: Kregel Books, 2002).

Kwa muumini, hofu ya Mungu si hofu inayomfanya mtu kutoroka kutoka kwa uwepo wa Mungu. Badala yake, ni heshima inayomfanya anayeabudu kumkaribia Mungu kwa unyenyekevu. Mwabudu haipaswi kuingia katika uwepo wa Mungu bila maandalizi.

***Mwabudu wa kweli anamwabudu kwa unyenyekevu.***

Mwabudu aliuliza, "Nani atakayeishi katika hema yako?" Wageni ni wageni wa kudumu katika nchi nyingine. Wao ni wageni, ambao hawana haki ambazo raia wanazo.

Zaburi 15 inahitaji mwabudu kutambua kwamba sisi ni wageni katika uwepo wa Mungu. Kwa sababu Mungu ni mtakatifu na nyumba yake ni takatifu, hatustahili kuwa hapo. Kwa hali yoyote katika maisha, lazima tuingie katika uwepo wa Mungu kwa nia ya unyenyekevu. Sisi ni wageni wake.

***Mwabudu wa kweli anasherehekea neema ya Mungu.***

Kwa sababu tunatambua utakatifu wa Mungu, tunasherehekea neema ya Mungu anapotukaribisha katika nyumba yake. Mwabudu aliyeuliza, "Nani atakayekaa katika kilima chako kitakatifu?" aliuliza swali hili kwa ujasiri kwamba wangealikwa katika nyumba ya Mungu. Mungu alikuwa ameanzisha uhusiano na Israeli; ibada ya Kiyahudi ilisherehekea uhusiano huu wa neema.

Zaburi 103 ni mwaliko wa kuabudu, "Ee nafsi yangu, umhimidi Bwana " Zaburi 103 ina kumbukumbu nzuri ya neema inayoturuhusu kuingia katika uwepo wa Mungu.[15]

"Kama vile baba awahurumiavyo watoto wake, Ndivyo BWANA anavyowahurumia wamchao. Kwa maana Yeye anatujua umbo letu, Na kukumbuka ya kuwa sisi tu mavumbi" (Zaburi 103:13-14). Mungu ambaye alitufanya kutoka mavumbini ametuita kwa neema ya kuabudu! Tunapoingia katika ibada, tunakumbuka neema ya Mungu. Ni neema inayouhusu mavumbi kuingia katika uwepo wa Muumba wa ulimwengu.

Kuabudu kweli kunahusisha hofu ya Mungu, unyenyekevu, na neema. Kila moja ya vipengele hivi vya ibada vilionekana katika ibada ya Hekaluni. Waabudu wa Kiyahudi waliliheshimu Hekalu kwa sababu ilikuwa ni nyumba ya Mungu mtakatifu.[16] Walijiandaa kwa makini kwa ajili ya ibada ili kuonesha unyenyekevu sahihi mbele ya Mungu. Pia walisherehekea katika ibada. Ibada ya Kiyahudi ilijaa kuimba, vyombo vya muziki, harufu nzuri, na hali ya kusherehekea neema ya Mungu kwa watu wake.

Leo, tunapaswa kuingia katika nyumba ya Mungu na hisia ya hofu ya Mungu. Lazima tukubali kutokuwa wa thamani mbele ya Mungu. Lakini ibada yetu pia inapaswa kusherehekea neema ya Mungu inayotukaribisha katika uwepo wake. Liturujia ya zamani

---

[15] Uchunguzi huu unatokana na Richard Averbeck, "Worshipping God in Spirit."

[16] Kwa wakati wa Yesu, heshima hii ilikuwa imepotea na mlango wa Hekalu ulikuwa umekuwa soko. Yesu aliwafukuza wabadilishaji wa fedha waliokuwa wamelidhalilisha Hekalu, na kulifanya kuwa 'pango la wanyang'anyi'. (Mathayo 21:12-13).

ya meza ya Bwana husema, "Hatuji kwa sababu tunastahili, bali kwa sababu tumekaribishwa." Hii ni ibada inayosherehekea neema ya Mungu.

**Jibu: Maelezo ya Mwabudu (Zaburi 15:2-5)**

Katika kujibu swali, "Nani awezaye kuingia katika nyumba ya Mungu?" kuhani alitoa maelezo kuhusu mwabudu. Mwabudu anatembea bila lawama mbele za Mungu. Yeye ni mwangalifu wa jinsi ya kuwatendea wengine. Anakataa wale wanaomkataa Mungu, lakini anaheshimu wale wanaomcha Mungu. Anajaribu kuiga tabia yake Mungu. Mtu ambaye kweli anamwabudu Mungu atakuwa kama Mungu zaidi na zaidi.

Jibu hili linatukumbusha kwamba ibada inagusa maisha yote. Kuingia katika uwepo wa Mungu kunahitaji utii kamili. Daudi hawezi kukumbuka mtu aliyewahi kusema, "Mimi ni mwana wa Mungu, lakini siishi chini ya sheria ya Mungu." Maandiko hayaruhusu mtu kusema, "Yesu ni mwokozi wangu, lakini yeye si Bwana wa maisha yangu." Kuingia katika uwepo wa Mungu kunahitaji kujitolea kwa mamlaka ya Mungu.

***Muabudu wa kweli anaishi maisha ya kimungu***

Zaburi 15:2 kwa kweli inatupa kanuni muhimu ya mwabudu. Wale wanaoingia mbele ya uwepo wa Mungu wanapaswa kutembea bila lawama; hii inamaanisha maisha yenye uadilifu katika maeneo yote. Wanapaswa daima kufanya yaliyo sawa. Wanapaswa kusema ukweli kutoka moyoni. Maneno haya yanafafanua maisha endelevu ya mwabudu. Maisha yote yanaguswa na ibada.

***Muabudu wa kweli anaishi katika uhusiano sahihi na jamii.***

Kama vile Daudi hawezi kumkumbuka mtu aliye wahi kusema, "Mimi ni mtoto wa Mungu, lakini siitii sheria ya Mungu," vivyo hivyo hawezi kumkumbuka mtu anayesema, "Mimi ni mwenye haki mbele za Mungu, lakini siwatendei jirani zangu kwa haki."

Mtu anayeingia mbele za Mungu ni mtu anayeishi katika uhusiano sahihi na jamii. Yeye:

- Hachongei watu kwa ulimi wake.
- Hawatendei mabaya jirani zake.
- Hasemi mabaya dhidi ya rafiki yake; hasambazi uvumi.
- Anapinga wale wanaomkataa Mungu.
- Anawaheshimu wale wanaomcha Mungu.
- Anashikamana na neno lake.
- Hakandamizi au kuwadhulumu maskini kwa mikopo isiyo ya haki.
- Hawatendei vibaya wasio na hatia kwa kupokea rushwa.

Mtu anayeishi katika hema la Mungu ni mtu mwenye haki, ndani na nje. Mwabudu wa kweli ni mtu wa uadilifu. Mwabudu wa kweli haruhusu desturi za ibada kuchukua nafasi ya maisha ya kila siku ya utii.

### Hitimisho: Ahadi kwa Mwabudu (Zaburi 15:5c)

Zaburi 15 inamalizia kwa ahadi kwa mwabudu; "Mtu atendaye mambo hayo hataondoshwa milele" (Zaburi 15:5). Mtu anayeishi kwa kutii amri za Mungu ameahidiwa ulinzi wa Mungu. Zaburi 15 inafanana na Zaburi 1 kwa maelezo yake ya uchaji Mungu na ahadi yake ya baraka za Mungu kwa mtu mcha Mungu.

Zaburi 15 inaonesha kile ambacho Mungu anahitaji kwa wale wanaomwabudu. Zaburi 15 inapaswa kusomwa kama amri ("Hivi ndivyo Mungu anavyotaka") na pia kama ahadi ("Hivi ndivyo Mungu atakavyowafanyia wale wanaomuomba"). Kwa kuzingatia Isaya 6, tunaelewa kuwa Mungu ndiye anayempa mwabudu uwezo wa kutii; Mungu ndiye anayetakasa midomo michafu; Mungu ndiye anayefanya mahitaji ya Zaburi 15 yawezekane. Ibada ya kweli inategemea neema ya Mungu. Inapatikana si kwa juhudi zetu dhaifu, bali kwa neema ya Mungu katika maisha ya wale wanaotafuta kumwabudu. Usisahau kamwe neema ya Mungu katika ibada; Baba anatafuta waabudu wa kweli, *na* Baba ndiye anayefanya ibada iwezekane.

### Kujipima

Jiulize, "Je, nina moyo na mikono ya mwabudu wa kweli?" Soma Zaburi 15 kama kipimo. Baada ya kila kifungu, jiulize "Je, hii inanielezea mimi? Je, niko tayari kwa ibada?"

Soma Zaburi 15 tena, kama sala ya kibinafsi. "Bwana, nipe uwezo wa kutembea bila lawama na kutenda yaliyo haki…. Nipe neema ya kuepuka majungu na kashfa…" Maliza kwa kusikia ahadi ya Mungu, "Atendaye mambo hayo hatatikisika kamwe."

### Hatari za Ibada: Unafiki

Yesu alizungumza na watu waliodhani kuwa wao ni wataalamu wa ibada. Waandishi na Mafarisayo walikuwa makini kutii kila undani wa ibada, amri za kibiblia na pia mapokeo ya Kiyahudi. Walikuwa wepesi wa kumlaumu yeyote aliyeshindwa kufuata kila undani wa taratibu zao. Hata hivyo, Yesu aliukosoa ibada yao kwa sababu walikuwa wanafiki.

Mafarisayo walilalamika kwamba wanafunzi wa Yesu hawakufuata taratibu za kiibada za kunawa mikono. Yesu alijibu, "Enyi wanafiki, ni vema alivyotabiri Isaya kwa habari zenu, akisema, Watu hawa huniheshimu kwa midomo; Ila mioyo yao iko mbali nami. Nao waniabudu bure, Wakifundisha mafundisho Yaliyo maagizo ya wanadamu. (Mathayo 15:7-9) Mafarisayo, kama waabudu wa uongo wa wakati wa Isaya, waliitwa wanafiki na Yesu kwa sababu ya makosa mawili:

1. Ibada yao ilikuwa ya nje, si kutoka moyoni (Mathayo 15:8).
2. Ibada yao ilitegemea mapokeo ya kibinadamu, si amri za Mungu (Mathayo 15:9).

Tunapaswa kuwa waangalifu kuepuka hatari ya ibada ya kinafiki. Ibada yetu lazima itoke moyoni, na ibada yetu lazima iongozwe na Mungu, si kwa mapokeo ambayo yameinuliwa kuwa sawa na Neno la Mungu.

## Hitimisho: Ushuhuda wa Mwabudu

Tukisoma Zaburi 15 bila kukumbuka nafasi ya neema katika maisha ya Kikristo, tunaweza kupata wazo potofu kwamba lazima tujitahidi kupata haki ya kuabudu. Hata hivyo, Zaburi 15 inaonesha kile ambacho Mungu anatufanyia, si kile tunachofanya, ili kupokea makaribisho katika nyumba yake.

Nani anaalikwa kuabudu? Sikiliza baadhi ya ushuhuda wa waabudu. Wanaonesha kuwa ibada si suala la kuwa unastahili; ibada ni kuhusu kuja kwa unyenyekevu mbele za Mungu na kubadilishwa na neema yake.

Farisayo anasema:

"Nina hakika unaweza kuelewa kwa nini nimekasirishwa na mafundisho ya Yesu. Mimi ni mtu mwema. Sivunji amri. Ninafunga na kutoa zaka. Ikiwa kuna mtu anayestahili kibali cha Mungu, ni mimi! Naenda nyumbani kwa Mungu kuonesha kuwa mimi ni mtu mwema. Inawezekanaje Mungu kukataa ibada yangu?"

Mtoza ushuru anasema:

"Kusema kweli, mimi nimeshangazwa kama Farisayo! Sikujua kama ningekubaliwa kuingia Hekaluni. Nilikaa mbali na watu wema kadiri niwezavyo. Nilitarajia mtu yeyote asinionee. Nilitafuta rehema ya Mungu ingawa sistahili rehema. Kwa mshangao wangu, nilienda nyumbani nikiwa nimetakaswa. Maisha yangu yalibadilishwa katika ibada."

Tajiri anasema:

"Natoa pesa nyingi kwa Hekalu. Nadhani Yesu anapaswa kuvutiwa na sadaka yangu. Hiyo ndiyo ibada yangu. Ninapoweka sadaka yangu kwenye kisanduku, kila mtu anajua 'Bw. Pesa' yupo. Natumaini Mungu ataona jinsi ninavyotoa nyingi!"

Mjane maskini anasema:

"Nilikua na aibu kuweka sadaka yangu kwenye kisanduku. Nilikuwa na sarafu mbili ndogo tu. Kila mtu alikuwa akitoa michango mikubwa; mimi nilikuwa kama sina chochote. Lakini ibada ni kuhusu kumpa Mungu kilicho bora zaidi. Haikuwa nyingi; lakini nilitoa vyote nilivyokuwa navyo. Nilitumaini hakuna atakayeona sadaka yangu ndogo, lakini mtu aliona. Yesu aliona nilichotoa! Na alisema kuwa nilitoa zaidi ya mtu yeyote. Sijui Yesu alimaanisha nini kwa kauli hiyo, lakini ninafuraha nilitoa bora yangu!"

## Majadiliano ya kikundi

► Kwa matumizi ya kivitendo ya somo hili, jadilini yafuatayo:

*Yohana amekuwa Mkristo kwa miaka kadhaa. Anajua kuwa kwenda kanisani, kusoma Biblia, na kuomba ni muhimu, lakini ni vigumu kwake kuhisi uwepo wa Mungu katika shughuli hizi. Inaonekana kuwa ni taratibu tu. Unawezaje kumsaidia Yohana kumwona Mungu katika ibada yake?*

## Mapitio ya Somo la 2

(1) Uelewa wetu wa Mungu ni muhimu kwa ibada kwa sababu taswira potofu ya Mungu itaongoza kwenye ibada potofu.

(2) Ibada lazima ilenge kwa Mungu, si kwa ubora wa uzoefu wetu wa ibada.

(3) Ufunuo unatupa picha ya ibada ya mbinguni:

- Ibada ya mbinguni ni ibada kwa Muumba ambaye ni mkuu, mtakatifu, na wa milele.
- Ibada ya mbinguni ni ibada kwa Mkombozi.
- Ibada ya mbinguni ni ibada kwa Mfalme.
- Ibada ya mbinguni ni ibada kwa Bwana Harusi Mshindi.

(4) Zaburi 15 ni zaburi ya ibada inayofupisha mahitaji ya Mungu kwa waabudu. Waabudu wa kweli:

- Wanajua hofu ya Mungu.
- Wanaabudu kwa unyenyekevu.
- Wanasherehekea neema ya Mungu.
- Wanaishi maisha ya ucha Mungu.
- Wanaishi katika uhusiano sahihi na jamii.
- Wanapokea ahadi ya Mungu ya ulinzi na baraka.

## Somo la 2 Mazoezi

(1) Zaburi 120-134 ni mkusanyiko wa nyimbo za wanaohiji wanaosafiri kuelekea Yerusalemu. Zaburi hizi zinafundisha kuhusu ibada katika hali mbalimbali. Soma zaburi hizi wakati unajibu maswali katika jedwali hapa chini.

| Zaburi | Swali la Kujibu |
|---|---|
| 120 | Mesheki na Kedari ziko wapi? Kwa nini ibada Yerusalemu ni muhimu kwa hija anayeishi Mesheki au Kedari? |
| 122 | Je, Zaburi hii inatufundisha nini kuhusu mtazamo wa kuabudu? |
| 123 | Je, mstari wa pili unafundisha nini kuhusu uhusiano wa mwabudu na Mungu? |
| 124 | Unajifunza nini kuhusu sifa katika hali ngumu kutoka kwa zaburi hii? |
| 126 | Je, kuabudu kunahusianaje na umisheni miongoni mwa mataifa? Angalia mstari wa pili. |
| 130 | Zaburi hii inafundisha nini kuhusu jukumu la maungamo katika ibada? |
| 131 | Je, mwandishi wa zaburi anajiandaa vipi kwa ibada? Ni hatua zipi za kivitendo unazoweza kuchukua kufuata mfano huu? |
| 133 | Zaburi 133, Yohana 17:20-23, na Waefeso 4:1-16 zote zinazungumzia umoja na zote zinahusiana na maisha ya kanisa kwa namna fulani. Je, umoja unahusianaje na ibada na maisha ya kanisa? |
| 134 | Je, Zaburi 134 inafaa vipi kama mwisho wa mfululizo huu wa zaburi za ibada? |

(2) Mwanzoni mwa somo linalofuata, utafanya mtihani unaotokana na somo hili. Soma maswali ya mtihani kwa makini ili kujiandaa.

**Jaribio Somo la 2**

(1) Orodhesha mambo matatu tunayojifunza kuhusu Mungu Muumba katika wimbo wa Ufunuo 4.

(2) Orodhesha sababu tatu za kumwabudu Mkombozi katika Ufunuo 5.

(3) Ujumbe mkuu wa Ufunuo kwa Wakristo ni nini?

(4) Zaburi 15 ni zaburi ya liturujia iliyogawanywa katika sehemu tatu. Orodhesha sehemu hizo tatu.

(5) Mtazamo wa muabudu anayeelewa kuwa yeye ni mgeni katika uwepo wa Mungu ni nini?

(6) Tabia mbili muhimu za mwabudu wa kweli kutoka Zaburi 15:2-5 ni zipi?

(7) Kwa nini Yesu aliwaita Mafarisayo wanafiki?

(8) Andika Ufunuo 5:9-14 kwa kumbukumbu.

# Somo la 3
# Kuabudu katika Agano la Kale

## Malengo ya Somo

Mwisho wa somo hili, mwanafunzi anapaswa:

(1) Kuthamini neema ya Mungu inayowezesha ibada.
(2) Kukaribia ibada kwa moyo wa utii.
(3) Kufahamu jukumu la matendo ya ibada.
(4) Kufanya sifa kama kipengele muhimu cha ibada.
(5) Kutambua umuhimu wa kuhubiri Neno la Mungu katika ibada.
(6) Kuepuka hatari ya kutokuwa na uwiano katika ibada.

## Matayarisho kwa somo hili

*Kariri Mika 6:6-8.*

## Utangulizi

Kikundi kimoja cha wachungaji hukutana kila mwezi kujadili masuala katika makanisa yao. Hivi karibuni wamejadili ibada. Kuna tofauti kubwa kati ya hawa wachungaji kuhusu suala la ibada. Ingawa wanashiriki imani za doktrini sawa, wanatofautiana sana katika mitindo ya ibada.

Yakobo ni mchungaji wa kanisa linalofuata desturi za zamani katika ibada. Enoki anahudumu katika kanisa linalokua ambalo hutumia mawazo mengi ya kisasa katika ibada. Gideoni bado anajaribu kupata aina ya ibada inayofaa zaidi kwa kanisa lake. Wachungaji hawa wamekuwa na mazungumzo mengi kuhusu ibada, lakini wanahisi kuchanganyikiwa katika juhudi zao za kukubaliana juu ya kanuni za msingi za ibada.

Leo, Jasoni anasema, "Labda tumekuwa tukiliangalia hili vibaya. Tunaendelea kujiuliza, ‘ni aina gani ya ibada tunayoifurahia? Tunataka kufanya ibada vipi?' Labda tunapaswa kujiuliza, 'Mungu anataka tuabudu vipi? Aina gani ya ibada anayoifurahia? Kama Mungu angebuni ibada, ingekuwa vipi?' Ikiwa tutajifunza jinsi ibada ilivyokuwa katika Biblia, hiyo inaweza kutupa mfano wa ibada leo."

► Ikiwa Mungu angebuni ibada, ingekuwa vipi? Eleza kile unachokijua kuhusu ibada kulingana na Biblia.

## Utangulizi: Mungu Anahitaji Ibada Sahihi

Katika Somo la 2, tuliona kutoka katika Ufunuo kwamba ibada ya kweli ni ibada kwa Mungu mtakatifu. Tuliona kutoka katika Zaburi 15 kwamba Mungu anahitaji wanaomwabudu wawe

watakatifu. Katika Somo la 3, tunajiuliza, "Mwabudu anawezaje kumkaribia Mungu mtakatifu?"

Baadhi ya watu husema kwamba Mungu hajali jinsi tunavyomwabudu; anajali tu kwamba moyo uko sawa. Ni kweli kwamba moyo ni msingi wa ibada. Hata hivyo, tuna ushuhuda wa kutosha kutoka katika Maandiko kwamba Mungu anajali sana jinsi anavyoabudiwa.

Aina ya ibada ni muhimu kwa sababu **ibada yetu inaathiri ufahamu wetu kumhusu Mungu**. Katika somo lililopita, tuliona kwamba picha iliyopotoshwa ya Mungu husababisha ibada iliyopotoshwa. Ni kweli pia kwamba ibada iliyopotoshwa hupotosha taswira yetu kuhusu Mungu. Wakati Israeli walipomwabudu Yehova kama vile Wakanani walivyoabudu miungu yao, ndipo walianza kuamini kwamba asili ya Mungu ilikuwa kama miungu ya Wakanani. Walianza kuamini kwamba Mungu alikuwa mkali na asiyeaminika, kama miungu ya Wakanani.[17]

Aina ya ibada ni muhimu kwa sababu **jinsi tunavyoabudu mara nyingi ni kielelezo cha kwa nini tunamwabudu.** Moyo wa upendo unafurahi kuleta ibada inayomheshimu Mungu; moyo wa utii kwa shingo upande unataka kufanya ibada kwa njia yangu badala ya njia ya Mungu.

Madarasa mengi ya vyuo vikuu huwa wanataka aina fulani ya dodoso la karatasi za utafiti. Wanahitaji ukurasa wa kwanza, rejea, na upana fulani wa ukurasa. Maelezo haya si sehemu muhimu zaidi ya utafiti; maudhui ndiyo muhimu zaidi. Hata hivyo, walimu wengi wameona kwamba mwanafunzi anayejali maelezo kiundani huwa mwangalifu kuhusu maudhui; anataka kufanya vizuri zaidi. Kwa upande mwingine, mwanafunzi anayeipuuza matakwa haya mara nyingi ni mkaidi kuhusu maudhui. Aina ya karatasi la dodoso mara nyingi linarefusha maudhui ya karatasi. Njia tunayoabudu mara nyingi inaakisi mtazamo wa mioyo yetu. Jinsi tunavyoabudu mara nyingi inahusiana na sababu yetu ya kuabudu. Kwa sababu hii, Mungu anajali jinsi tunavyoabudu.

- Kaini alileta sadaka kwa Bwana. Kaini alikuwa mkulima wa ardhi. Alileta matunda ya ardhi, lakini Bwana hakumtazama Kaini wala sadaka yake. Kukosekana kwa Kaini kumwabudu kwa usahihi kulionesha mtazamo wa moyo wake. Sadaka ya Kaini ilikuwa rahisi kwake mwenyewe, lakini Mungu hakukubali ibada yake (Mwanzo 4:1-5).
- Haruni alijenga ndama wa dhahabu kutumika katika ibada kwa Yehova. Alisema, "Kesho itakuwa sikukuu kwa BWANA" (Kutoka 32:1-5). Labda Haruni alijishawishi kwamba angeweza kumwabudu Mungu kwa njia inayopendeza watu, lakini Mungu hakukubali ibada yake.

[17] Katika Mika 6:6-7, "Viongozi wa kidini wanajaribu kumhonga Yehova kwa dhabihu za watoto. Wanadhani kwamba Yehova anatarajia dhabihu za watoto ambazo Moleki alidai.".

> "Kama ungekuwa kuhani wa Agano la Kale, na ukamtumikia Mungu kama unavyomtumikia sasa, itakuwa muda gani kabla Bwana hajakuua?"
>
> - Warren Wiersbe (kutokana na umuhimu wa ibada)

- Nadabu na Abihu walimuona Mungu wa Israeli katika Mlima Sinai (Kutoka 24:1-11). Walikuwa karibu na Mungu kuliko mtu yeyote isipokuwa Musa, lakini siku yao ya kwanza ya huduma ya ukuhani katika Maskani, walitoa moto usio halali mbele za Bwana. Kama jibu, moto kutoka kwa Bwana uliwaangamiza. Musa alieleza hukumu ya Mungu kwa Mungu baba yao mwenye huzuni; "Jambo hili ni hilo BWANA alilolinena, akisema, Nitatakaswa mimi katika hao wanikaribiao, nami nitatukuzwa mbele ya watu hao wote" (Mambo ya Walawi 10:1-7) Makuhani hawa walitoa uvumba kwa njia yao wenyewe, badala ya kufuata amri za Mungu. Mungu hakukubali ibada yao.

- Uzia alikuwa mfalme mkuu. Alichokifanya kilikuwa kizuri machoni pa Bwana. 2 Mambo ya Nyakati yanahitimisha utawala wake: "... kwa kuwa alisaidiwa mno ajabu, hata akapata nguvu" (2 Mambo ya Nyakati 26:15). Kwa kusikitisha, hii sio mwisho wa hadithi ya Uzia. "Lakini alipokuwa na nguvu, moyo wake ulitukuka, hata akafanya maovu, akamwasi BWANA, Mungu wake; kwani aliingia hekaluni mwa BWANA, ili afukize uvumba juu ya madhabahu ya kufukizia" (2 Mambo ya Nyakati 26:16). Alijaribu kumwabudu Mungu kwa njia yake mwenyewe na akapigwa na ukoma (2 Mambo ya Nyakati 26:1-21). Mungu hakukubali ibada yake.

- Wayahudi baada ya kuondoka uhamishoni walileta sadaka za vilema Hekaluni. Kukosekana kwao kuleta dhabihu sahihi kulionesha mtazamo wa kutokujali wa mioyo yao. Hawakumpenda kweli Mungu, kwa hivyo Mungu hakukubali ibada yao (Malaki 1:6-14).

Mungu hujali *jinsi* anavyoabudiwa. Mifano hii inaonesha kwamba, tukiachwa wenyewe, hatutamkaribia Mungu kwa njia inayomheshimu. Kile kinachoonekana kuwa sahihi kwetu kinaweza kutokuwa kinakubalika kwa Mungu. Lazima tuwe na mwongozo wake katika ibada yetu.

Kwa kuwa ibada maana yake ni kumpa heshima Mungu, ibada yetu lazima iwe inafuata tabia za Mungu badala ya tamaa zetu. Hatuwezi kujua wenyewe ni nini kinachompendeza Mungu; lazima tutazame Neno la Mungu ili kujifunza jinsi ya kuabudu kwa njia inayompendeza Mungu.

### Kuambatana na Mungu: Ibada kama Uhusiano wa Neema

Picha ya kwanza ya ibada katika Biblia inapatikana katika Bustani ya Edeni, "Wakasikia sauti ya BWANA Mungu, akitembea bustanini wakati wa jua kupunga..." (Mwanzo 3:8) Hii inaonyesha kusudi la Mungu kwa ibada: ushirika usiovunjika kati ya mwanadamu na Muumba wake. Kabla ya Kuanguka, ushirika kati ya mwanadamu na Mungu haukuzuiliwa na dhambi. Ibada katika Bustani ilikuwa rahisi na isiyopata utata.

Katika Bustani, tunaona kwamba Mungu anatamani ushirika na viumbe vyake. Hadi Kuanguka, mwanadamu alifurahia ushirika kamili na Mungu; ilikuwa tu baada ya dhambi kuharibu asili ya mwanadamu ndipo mwanadamu alijificha mwenyewe kutoka kwa Mungu.

Katika Agano la Kale, neno "alitembea pamoja na Mungu" hutumiwa kuonyesha kwamba ibada inajumuisha uhusiano na Mungu. Henoko alitembea na Mungu; Nuhu alitembea na Mungu; Ibrahimu aliagizwa kutembea na Mungu (Mwanzo 5:24, Mwanzo 6:9, Mwanzo 17:1). Kila mfano huu unaonesha mtu ambaye alijenga uhusiano kwa kutumia muda pamoja na Mungu. Ibada sahihi inategemea uhusiano sahihi na Mungu.

Mwanzo 3:8 inaonesha kwamba ibada ilikuwa msingi wa uhusiano. Pia inaonesha kwamba ibada inawezekana tu kwa sababu ya neema ya Mungu. Miungu wa kipagani walitarajia mwanadamu apate njia ya kufanya ibada ipasavyo ili kuwafurahisha miungu. Kinyume chake, Yehova kwa neema alitoa njia sahihi ya ibada. Mifano mitatu inaonyesha hili.

**Mungu Aliwezesha Ibada Kwa Adamu na Hawa**

Baada ya kuanguka, Mungu hakuwa na jukumu la kutafuta au hata kukubali ibada kutoka kwa Adamu na Hawa. Walikuwa wamevunja sheria ya Mungu; walikuwa wameharibu uumbaji wake; hawakustahili chochote ila hukumu.

Baada ya kutenda dhambi, Adamu na Hawa walijificha kutoka mbele za Bwana (Mwanzo 3:8). Hakukuwa na hatua nyingine kwa Adamu na Hawa; hawakutarajia chochote ila kifo. Majibu pekee waliyoyajua ilikuwa kujificha kutoka kwa Mtoaji wa Sheria, lakini kwa neema Bwana Mungu alimwita Adamu. Ibada inawezekana kwa neema ya Mungu. Tukiachwa wenyewe, hatuna njia ya kumkaribia Mungu mtakatifu. Ni kupitia neema yake pekee tunaitwa kwa ibada.

**Mungu aliwezesha Ibada kwa Abraham**

► Soma Mwanzo 18:1-8.

Katika Somo la 1, tuliona kwamba moja ya maneno ya Kiebrania kwa ibada (Shachah) lina maana ya "kusujudu" au "kuabudu." Neno hili linatumika kwa mara ya kwanza katika Mwanzo 18:2. Bwana na malaika wawili walionekana wakati Abramu alipokuwa ameketi mlangoni mwa hema yake. Abramu alikimbia kutoka mlangoni mwa hema ili kukutana nao na akainama mpaka nchi. Ibrahimu akainama—aliwaabudu.

Kumbuka kwamba Mungu alichukua hatua ya kwanza katika simulizi hii; alikuja kukutana na Ibrahimu. Mungu alifanya ibada iwezekane. Katika Agano la Kale kama ilivyo katika Agano Jipya, ibada inawezekana tu kwa neema. Dhabihu za Agano la Kale si njia ya kumtuliza Mungu mwenye hasira ambaye hataki uhusiano; bali zilipangwa na Mungu mwenyewe kama njia ya upatanisho kati ya Mungu na mwanadamu mwenye dhambi. Hata katika Agano la Kale, ibada inawezekana tu kupitia neema ya Mungu. Ndani yetu wenyewe, hatuna uwezo wa kuabudu ipasavyo.

**Mungu aliwezesha Ibada kwa Yakobo**

► Soma Mwanzo 28:10-22. Je, simulizi hii inafunua nini kuhusu jukumu la Mungu katika ibada?

Moja ya picha za kushangaza zaidi za ibada katika Biblia inapatikana katika Mwanzo 28:10-22. Hakuna kitu katika maisha ya nyuma ya Yakobo kinachoonesha sifa za mwabudu. Hapitani na sifa za Zaburi 15. Hamtafuti Mungu; kwa kweli, anakimbia matatizo aliyoyasababisha kwa matendo yake ya udanganyifu. Hakuna kitabu chochote kinachohusu ibada kinachosema, "Ibada inayokubalika inatoka kwa wadanganyifu wanaokimbia matokeo ya dhambi zao wenyewe."

Hata hivyo, Mungu alijidhihirisha kwa Yakobo licha ya kutostahili kwake. Neema ya Mungu hufanya ibada iwezekane hata kwa mtu asiye na sifa kama Yakobo. Warren Wiersbe aliandika, "kwa neema Mungu hutuingilia wakati hatutarajii – au hata hatustahili. **Wakati ibada inapoacha kuwa jambo la neema, inaacha kuwa suala la utukufu."**[18]

Ni kwa neema tu kwamba Mungu anatualika katika uwepo wake. Ibada yetu ni mwitikio wa neema yake. Hakuna kitu tunachofanya katika ibada kinachostahili kwake; isipokuwa ni neema yake tu inayotuwezesha kuabudu.

Simulizi ya Yakobo inaonesha moja ya tofauti kubwa kati ya ibada ya Yehova na ibada ya miungu ya uongo. Waabudu wa miungu ya uongo walijenga madhabahu kwa kujaribu kupata kibali cha mungu wao. Kwenye Mlima Karmeli, manabii wa baali "Wakaliitia jina la Baali tangu asubuhi hata adhuhuri, wakisema, Ee Baali, utusikie. Lakini hapakuwa na sauti, wala aliyejibu. Nao wakaruka-ruka juu ya madhabahu waliyoifanya" (1 Wafalme 18:26).

> Katika ibada ya uongo, mtu hujenga madhabahu ili kupata upendeleo wa sanamu (kazi).
>
> Katika ibada ya kweli, mtu hujenga madhabahu kusherehekea upendeleo wa Mungu (neema).

► Soma 1 Wafalme 18:20-39 ili kuona tofauti kati ya ibada ya kweli na ibada ya uongo.

Manabii wa baali walijaribu kumshawishi baali ajidhihirishe kwao. Mfano huu unaonekana mara kwa mara katika ibada ya sanamu. Madhabahu na dhabihu ni jaribio la kupata kibali cha sanamu.

Kinyume chake, Mungu kwa neema hujidhihirisha kwa watu wake katika ibada. Eliya alijenga madhabahu yake kwa kujiamini kabisa kwamba Mungu anayemtumikia angejibu maombi yake.

[18] Warren W. Wiersbe, *Real Worship*, (Grand Rapids: Baker Books, 2000), 72

> Ee Bwana, Mungu wa Ibrahimu, na wa Isaka, na wa Israeli, na ijulikane leo ya kuwa wewe ndiwe Mungu katika Israeli, na ya kuwa mimi ni mtumishi wako, na ya kuwa nimefanya mambo haya yote kwa neno lako (1 Wafalme 18:36).

Katika kitabu cha Mwanzo, mababa wa imani walijenga madhabahu si kwa ajili ya kuvuta umakini wa Mungu bali kama kumbukumbu za sehemu ambazo Mungu alijidhihirisha. Madhabahu haikupata kibali cha Mungu; ilisherehekea neema yake. Yakobo anatufundisha kwamba ibada inawezekana tu kwa neema. Hatupaswi kamwe kufikiria kwamba ibada yetu inatufanya tustahili kupata kibali cha Mungu; tunaabudu kwa sababu ya neema.

Je, ni kitu gani hutokea Mungu anapofanya ibada iwezekane? Yakobo alibadilishwa. Ilipita miaka 30 kabla ya mabadiliko haya kukamilika, lakini mabadiliko yalianza Betheli. Ibada (hata ibada isiyo kamilifu ya mtu asiye kamilifu kama Yakobo) inatubadilisha na kutufanyia yale ambayo hatuwezi kujifanyia wenyewe.

**Kujipima**

Hebu jiulize, "Je, ninabadilishwa na ibada, au ninapitia tu hatua zisizo na maana? Ni lini mara ya mwisho nilibadilisha matendo yangu, imani zangu, au mitazamo yangu kwa sababu ya kukutana na Mungu katika ibada?"

### Ibrahimu: Ibada inahitaji Utii

► Soma Mwanzo 22:1-19. Je, ni mahitaji gani ya ibada katika simulizi hii?

dhabihu ya Ibrahimu ya kumtoa mwanawe ilikuwa kitendo kikuu cha ibada. Katika simulizi hii, angalia mkazo juu ya utiifu wa Ibrahimu. Mungu alisema, “Umchukue mwanao… ukaende… ukamtoe sadaka…” Amri tatu. Ibrahimu “alimchukua mwanawe Isaka... akaondoka na kwenda... na akachukua kisu ili amchinje mwanawe.” Ibrahimu alitii kila amri.

Sadaka ya Ibrahimu ya Isaka inaonesha kwamba ibada ya kweli inahitaji utiifu kamili. Ibada ni zaidi ya hisia au mhemko; ibada ni zaidi ya kumsikiliza mwimbaji au mhubiri; ibada ni mwitikio hai kwa Mungu.

Rudi kwenye simulizi ya Ibrahimu katika Mwanzo 18. Mwanzoni mwa simulizi, tunaona ibada kama huduma ya utiifu. Ibrahimu aliona wageni watatu wakikaribia kambi yake. Aliinama mpaka chini. Aliabudu.

Kisha tunaona Ibrahimu akiwa na shughuli nyingi za kuhudumu. Alitoa maji ili kuosha miguu yao; alikimbilia ndani ya hema ili Sara aoke mikate; aliandaa chakula na kuwawekea. Akiwa katika nafasi ya mtumishi anayesubiri, alisimama karibu nao chini ya mti wakati walipokuwa wanakula. Hii yote ni lugha ya mtumishi anayetoa huduma bora kwa bwana wake. Mwabudu wa kweli ana mtazamo wa huduma ya hiari.

Umuhimu wa utiifu katika ibada unaonekana katika Agano la Kale lote. Sadaka ya Abeli ilikubaliwa kwa sababu ilikidhi mahitaji ya Mungu kwa sadaka. Abeli alileta mzaliwa wa kwanza wa kundi lake na sehemu zao za mafuta (Mwanzo 4:4). Abeli alileta kwa utiifu

kilicho bora zaidi. Kinyume chake, Kaini alitaka kutimiza wajibu wake kwa njia rahisi iwezekanavyo.

Umuhimu wa utiifu katika ibada unaonekana katika maisha ya Sauli. Wakati Sauli alipokosa kutii amri ya Mungu ya kuharibu wanyama wote wa Amaleki, alijaribu kujisamehe kwa kudai kwamba wanyama bora wamehifadhiwa kwa ajili ya sadaka. "Samweli akasema, je! Bwana huzipenda sadaka za kuteketezwa na dhabihu Sawasawa na kuitii sauti ya Bwana? Angalia, kutii ni bora kuliko dhabihu, Na kusikia ushauri kuliko mafuta ya beberu" (1 Samweli 15:22).

► Soma 1 Samuel 15:1-23.

Mungu hatakubali ibada kutoka kwa moyo wa uasi.

Ibada ya kweli inachochea uhusiano wa kina na Mungu. Angalia tena simulizi ya Ibrahimu. Mwanzo 18 inaanza na huduma ya Ibrahimu kwa Mungu; sura hiyo inaisha na uhusiano. Bwana aliuliza, "Je! Nimfiche Abrahamu jambo ambalo ninataka kulifanya...?" Baada ya kusikia nia ya Mungu, Ibrahimu alijadiliana kwa ujasiri na Mungu juu ya hatima ya Sodoma. Nini kilitokea? Tunaona kuwa mtumishi wa Mungu pia ni rafiki wa Mungu.

Ni katika ibada tunapomjua Mungu kwa kweli. Ni katika ibada tunapojifunza moyo wa Mungu hadi tunapoweza kuomba kwa ujasiri. Ni katika ibada ya utiifu ambapo uhusiano wetu na Mungu unakua kwa kina. Ibada inayokubalika inajumuisha utiifu (huduma) na uhusiano. Ibrahimu mwabudu ni mtumishi wa Mungu na pia ni rafiki wa Mungu.

## Ibada ya Kibiblia Siku Hizi

Je, umewahi kujiuliza kwa nini baadhi ya watu wanahudhuria ibada na kujionea uwepo wa Mungu wakati wengine wanahudhuria ibada hiyo hiyo na hawaoni chochote cha Mungu? Baadhi wanatoa sadaka na kubarikiwa; wengine wanatoa na hawana furaha. Hapo tofauti ni moyo mtiifu.

Haijalishi ibada yetu ni nzuri kiasi gani, haijalishi wanamuziki ni wenye vipaji kiasi gani, haijalishi mahubiri ni yenye nguvu kiasi gani, ikiwa ibada haitoki kwa moyo mtiifu, ni ibada ya Kaini. Ibada ya Kaini inasema, "Ninaweza kuleta sadaka yangu kwa njia yangu mwenyewe. Inatosha." Ibada ya kweli inatoka kwa moyo mtiifu.

### Kujipima

Jiulize, "Je, mimi ni mwabudu mtiifu? Je, ibada yangu inatoka kwa moyo wa Abeli au moyo wa Kaini?"

## Dhabihu: Ibada kama taratibu

Kabla ya Anguko, ibada ilifanyika katika uhusiano rahisi kati ya Mungu na mwanadamu. Baada ya dhambi kuharibu asili ya mwanadamu, mwanadamu alihitaji mchakato wa kuingia katika uwepo wa Mungu. Kwa neema, Mungu alitoa mfumo wa dhabihu. Dhabihu ziliwekwa na Mungu bustanini alipoua mnyama na kutumia ngozi yake kutengeneza mavazi kwa

Adamu na Eva. Kitabu cha Mambo ya Walawi kiliweka mfumo wa dhabihu kwa ajili ya ibada ya Israeli (Mambo ya Walawi 1-7 na 16).

Tunaposoma katika kitabu cha Kutoka na Mambo ya Walawi, inakuwa wazi kwamba maelezo ya ibada ni muhimu kwa Mungu. Kwa wale wanaosema kwamba "Mungu hajali jinsi tunavyoabudu mradi tu tuabudu," vitabu vya Kutoka na Mambo ya Walawi vinaonesha kwamba jinsi tunavyoabudu ni muhimu kwa Mungu! Mungu alitoa maagizo ya wazi kwa ajili ya ibada. Hii ni kama ufunuo wa Mungu kwa Adamu na Eva baada ya Anguko, ni ishara ya neema ya Mungu. Yehova alitoa maagizo ya wazi, "Hivi ndivyo mnavyopaswa kunikaribia." Hili lilikuwa tendo la neema.

Kwa Israeli, ibada ilianza kabla hawajaingia katika nyumba ya Mungu. Mchakato wa kujiandaa kwa ajili ya ibada ulionesha heshima yao kwa Mungu na nyumba yake. Nyimbo za Maandalio katika Zaburi zinaonesha kwamba hata safari ya kwenda Yerusalemu ilikuwa ibada (Zaburi 120-134). Taratibu za ibada hazikuwa tupu; kila kipengele cha dhabihu kilimkumbusha mwabudu umuhimu wa ibada ya kweli.

**Dhabihu Ziliwakilisha Kujisalimisha Kikamilifu kwa Mungu**

Baadhi ya Wakristo wamekosea kuelewa mfumo wa dhabihu wa Agano la Kale. Wanadhani ni mfumo ambao Waisraeli waliweza kukiuka sheria ya Mungu kwa hiari, halafu wakaleta dhabihu isiyo na maana, kisha mara moja wakarudi kwenye dhambi zilezile bila mabadiliko ya moyo.

Ni kweli kwamba hili lilitokea katika baadhi ya mazingira. Kwa kujibu hilo, Mungu alisema, "Mimi nazichukia sikukuu zenu, nazidharau, nami sitapendezwa na makutano yenu ya dini. Naam, ijapokuwa mnanitolea sadaka zenu za kuteketezwa na sadaka zenu za unga, sitazikubali" (Amosi 5:21-22).

Hata hivyo, hii ilikuwa ni kushindwa kwa mwanadamu, si kwa Mungu. Mfumo wa dhabihu ulishindwa wakati mwanadamu aliposhindwa kufanya kile ambacho Mungu aliamuru. Mpango wa Mungu ulikuwa ni dhabihu ambazo zinaakisi toba ya kweli ya moyo.

Taratibu zinazohusiana na sikukuu zilionesha Israeli umuhimu wa matendo ya ibada. Kila kila kitu kilionesha heshima ya Israeli kwa Yehova. Ibada ya Israeli haikuwa taratibu tupu; taratibu hizi zilionesha ukweli wa kujisalimisha na utiifu wao. Kwa kuweka mikono yake juu ya kichwa cha mnyama, mwabudu alijitambulisha na kifo cha sadaka. Kwa kufanya hivyo, alikuwa anakiri, "Huyu anapaswa kuwa mimi. Dhambi yangu inastahili kifo" (Rejea Mambo ya Walawi 1:4).

**Mungu Alitukuza Ibada ya Kweli kwa Uwepo Wake**

Kwa kujengwa kwa Hekalu, Ibada ya Israeli ilipangwa zaidi. Kama Maskani ilivyo, kila jambo katika Hekalu liliashiria utiifu wa heshima ya Israeli kwa Mungu (2 Mambo ya Nyakati 1-7). Uzito wa dhabihu na umakini wa ibada ya Hekalu uliwakumbusha Israeli ukuu wa Yehova na unyenyekevu ambao walipaswa kumkaribia.

Mipango makini ya taratibu za ibada kwa ajili ya Hekalu haikuzuia uwepo wa Mungu. Mojawapo ya ibada zilizoandaliwa zaidi katika historia, yaweza kuwa ni ile ya kuweka wakfu Hekalu. Daudi alikuwa amepanga Hekalu miaka mingi kabla. Baada ya Hekalu kukamilika, Sulemani aliongoza ibada nzuri ya kuweka wakfu jengo kama iliyoelezewa katika 2 Mambo ya Nyakati 5. Wanamuziki walipiga matoazi, vinubi, na vinanda. Makuhani 120 walipiga tarumbeta. Kwaya iliimba nyimbo za sifa. Walipoimba, "ndipo nyumba ikajawa na wingu, naam, nyumba ya BWANA, hata makuhani hawakuweza kusimama ili kufanya huduma yao, kwa sababu ya lile wingu; kwa kuwa nyumba ya Mungu imejaa utukufu wa BWANA" (2 Mambo ya Nyakati 5:13-14).

## Ibada ya Kibiblia Siku hizi

Baadhi ya watu wanapinga muundo na namna yeyote katika ibada. Wanaamini kwamba liturujia yoyote iliyoandaliwa inazuia ibada ya moyo. Hata hivyo, tunaona ibada ya Kibiblia ilikuwa na muundo.

Ikiwa tunajitahidi kumletea Mungu kilicho bora, ibada yake inastahili kupangwa kwa umakini. Tunapanga ibada si kwa ajili ya kuwashangaza wengine kwa uzuri wa ibada yetu, bali kumletea Mungu dhabihu bora ya ibada.

Katika Biblia ibada zote, ibada iliyo na muundo uliopangwa kwa umakini (kama kuweka wakfu Hekalu) na ibada isiyokuwa na muundo (kama mikutano ya makanisa ya nyumbani katika karne ya kwanza) zilibarikiwa na uwepo wa Mungu. Na pia, ibada yenye muundo uliopangwa kwa umakini (kama ibada ya Hekalu wakati wa Yeremia) na ibada isiyo na muundo (kama ibada yenye machafuko ya Korintho) inaweza kufanywa bila uwepo wa Mungu. Swala si kiwango cha muundo; swala ni utii kwa Mungu na njaa ya uwepo wa Mungu.

### Kujipima

Jiulize, "Je, ibada yangu ya pamoja na wengine (bila kujali ni ya kawaida au isiyo ya kawaida) inatoka kwa moyo mtiifu?"

## Zaburi: Ibada kama Sifa

Kitabu cha Zaburi ni kitabu cha ibada cha Israeli. Kilikuwa kitabu cha nyimbo za sifa; kilikuwa mkusanyiko wa maombi; kilikuwa mwongozo wa ibada sahihi; kilikuwa mwongozo wa maisha ya haki. Kitabu cha Zaburi kilikuwa muhimu katika ibada ya Israeli.

### Sifa katika Ibada

> "Hakikisha unaendelea kumfurahia Mungu kila wakati."
>
> - Richard Baxter

Kitabu cha Zaburi kinaonesha kwamba ibada ya kweli inajumuisha msisitizo mkubwa juu ya sifa. Isipokuwa Zaburi ya 88, kila zaburi ina kauli fulani ya sifa. Taratibu za Mambo ya Walawi zinatukumbusha uzito wa ibada ya Kibiblia; zaburi zinatukumbusha furaha ya ibada ya Kibiblia. Zaburi 120-134

zinaonesha furaha ya mahujaji Wayahudi walipokuwa wanakwenda Yerusalemu kwa ibada. Sifa ni kitovu cha ibada.

Sifa iliyopatikana katika kitabu cha Zaburi inaonesha furaha ya ibada ya kweli. Sifa inaonesha furaha yetu katika Mungu. Ibada ya kweli inajumuisha sherehe ya Mungu na matendo yake.

**Maombolezo katika Ibada**

Zaburi za maombolezo zinaonyesha upande mwingine wa ibada ya Kibiblia; ibada inaruhusu ukweli kamili kati ya mtoaji wa ibada na Mungu. Katika zaburi za maombolezo, mwandishi wa zaburi anaelezea kuchoshwa na udhalimu wa ulimwengu huu. Katika Zaburi 10:1, mwandishi wa zaburi aliuliza, "Ee Bwana, kwa nini wasimama mbali? Kwani kujificha nyakati za shida?" Kwa nini Mungu anaruhusu wafanya mabaya kufanya uasi na kiburi. Kwa sababu ibada inategemea uhusiano na Mungu, mtoaji wa ibada anaweza kusema kwa uaminifu na wazi.

Zaburi ya 10 inamalizika na tangazo la imani katika Mungu.

> "Bwana ndiye Mfalme milele na milele; Mataifa wamepotea kutoka nchi yake. Bwana, umeisikia tamaa ya wanyonge, Utaitengeneza mioyo yao, utalitega sikio lako. Ili kumhukumu yatima naye aliyeonewa, Binadamu aliye udongo asizidi kudhulumu" (Zaburi 10:16-18).

Tangazo hili linategemea imani katika Mungu. Ingawa watenda mabaya wanaendelea kutenda udhalimu, mwandishi wa zaburi anazungumza kwa ujasiri kwamba Mungu atafanya yaliyo haki.

Tunaona ukweli huo huo katika kitabu cha Ayubu. Ukweli kama huu unategemea uhusiano wa karibu na Mungu. Hii ni ibada ya kweli, ibada ambayo ni ya kukubaliwa na Mungu.

## Ibada ya kibiblia Siku hizi

Zaburi zinajumuisha aina mbili za nyimbo za sifa. Kanisa letu linapaswa kujumwisha vyote.

| | Nyimbo za Sifa ya kutangaza | Sifa za Maelezo |
|---|---|---|
| **Maana** | Sifa au agizo la kusifu lisiloelekezwa kwa mhusika maalum. | Sifa mahususi kwa tabia na matendo makuu ya Mungu |
| **Sentensi ya mfano** | "Haleluya. Mwimbieni BWANA wimbo mpya, Sifa zake katika kusanyiko la watauwa" (Zaburi 149:1). | "Yeye, BWANA, ndiye Mungu wetu; Duniani mwote mna hukumu zake." (Zaburi 105:7). |
| **Faida ya sifa ya aina hii** | Inamwalika mwabudu kumtukuza Mungu | Humfundisha mwabudu kweli za kina kuhusu asili ya Mungu. |
| **Kwa kawaida hupatikana katika mtindo huu wa wimbo** | Mapambio | Nyimbo za tenzi |
| **Mifano kutoka katika Zaburi** | Zaburi hizi zinaagiza sifa bila kutoa sababu mahususi**:** Zaburi 148-150 | Zaburi hizi zinaeleza sababu nyingi mahususi za kutoa sifa Zaburi 19, 105, na 136 |

► Tazama kila mojawapo ya Zaburi sita zilizoorodheshwa hapo juu. Linganisha aina za sifa zinazopatikana katika kila moja

► Tazama mkusanyiko wa tenzi na mapambio katika lugha yako. Tafuta mifano 2–3 ya kila aina ya sifa.

### Kujipima

Sifa za mwandishi wa zaburi zinaonesha furaha yake kwa Mungu. Jiulize, "Je, kweli ninamfurahia Mungu?"

## Manabii: Ibada kama Kutangaza

Sheria za dhabihu, Maskani, na Hekalu zinaonesha thamani ya utaratibu katika ibada. Hata hivyo, manabii wanaonesha kuwa taratibu ambazo haziendani na ibada ya moyo ni bure. Wakati watu wa Israeli walipoanza kufuata taratibu bila mioyo ya utii, manabii walileta ujumbe wa hukumu kutoka kwa Mungu. Walitangaza kwamba Mungu hakubali tena dhabihu za taifa lililoasi.

Manabii wanaonesha kwamba kutangaza la Neno la Mungu ni ibada. Katika huduma zetu, hatupaswi kutenganisha ibada na mahubiri. Tangazo la Neno ni ibada katika ukweli. Mahubiri yanathibitisha mamlaka ya Mungu juu yetu na hekima yake kwa maisha yetu. Hii ni ibada; inamheshimu Mungu.

### Ujumbe wa Manabii

#### *Taratibu bila ukweli si ibada.*

Amosi alitangaza kuwa Mungu alikuwa amekataa dhabihu za Israeli. Kwa nini? Kwa sababu maisha ya waabudu yalikuwa ya dhambi (Amosi 5:21-22). Isaya alitangaza kwamba sikukuu za Israeli zilikuwa mzigo wa kuchosha kwa Mungu. Kwa nini? Kwa sababu mikono yake ilikuwa imejaa damu.

Kabla ya kuabudu, waabudu wanaamriwa: "Jiosheni, jitakaseni; ondoeni uovu wa matendo yenu usiwe mbele za macho yangu; acheni kutenda mabaya; jifunzeni kutenda mema; takeni hukumu na haki; wasaidieni walioonewa; mpatieni yatima haki yake; mteteeni mjane" (Isaya 1:13-17).

Mungu hafurahii taratibu ambazo hazioneshi ukweli wa moyo.

#### *Ibada ya kweli inahitaji bora yetu.*

Ibrahimu alimtoa mwanawe kwa Mungu; alitoa bora yake. Habili alileta mzaliwa wa kwanza wa kundi lake; alitoa bora yake. Mambo ya Walawi yalihitaji wanyama bora kwa dhabihu. Daudi alikataa kutoa sadaka ambayo haikumgharimu chochote (2 Samweli 24:24). Katika kila mfano hapo juu, ibada inahitaji bora yetu.

Ujumbe huu unaendelea katika manabii. Malaki aliwaonya dhidi ya kuleta wanyama duni kwa dhabihu (Malaki 1:6-8). Hagai alionya juu ya hukumu kwa sababu watu walijali zaidi hali ya nyumba zao wenyewe kuliko nyumba ya Mungu (Hagai 1:8-11). Ibada ya kweli inahitaji bora yetu.

#### *Ibada ya Kweli Inahusisha Maisha yote.*

Amosi alitoa majibu ya kivitendo kwa uasi wa Israeli. Suluhisho halikuwa dhabihu zaidi; suluhisho lilikuwa maisha ya haki. "Lakini hukumu na itelemke kama maji, na haki kama maji makuu" (Amosi 5:24). Manabii hawakupinga ibada ya Hekalu na dhabihu.[19] Walipinga ibada isiyoambatana na maisha ya haki.

Katika Biblia nzima, tunaona kwamba ibada ya kweli inahusisha maisha yote. Katika Pentateuki, sheria kuhusu ibada ziko karibu na sheria kuhusu tabia ya kimaadili; hakuna

---

[19] "Baadhi ya wasomi wanasema kwamba manabii walikataa mfumo wa Hekalu. Hata hivyo, manabii wengi walihusishwa sana na Hekalu. Isaya alimuona Bwana ndani ya Hekalu. Ezekieli alitabiri Hekalu lililorejeshwa lililojaa utukufu wa Mungu. Hagai alimhimiza Zerubabeli kujenga upya Hekalu. Manabii hawakukataa dhabihu; walikataa matumizi mabaya ya dhabihu.".

utengano kati yao. Katika vitabu vya kihistoria, kutotii kwa Israeli katika maisha ya kila siku kunasababisha uharibifu wa mahali pa ibada ya Israeli, Hekalu. Manabii wanatangaza kwamba Mungu amekataa ibada ya Israeli kwa sababu ya kutotii kwake. Katika Agano Jipya, Yesu anakumbusha Mafarisayo kwamba desturi za ibada kama vile utunzaji wa Sabato hazina maana bila maisha ya rehema (Mathayo 12:7).

**Mfano wa Manabii: Mahubiri na Kutangazo ni Ibada**

Manabii wanaonesha kwamba kutangaza la Neno la Mungu ni ibada. Fikiria upuuzi wa Yeremia kusimama mbele ya Hekalu na kusema, “Nendeni Hekaluni kuimba Zaburi na kutoa dhabihu zenu. Hiyo itakuwa ibada. Mkimaliza, nitawahubiria ujumbe wa Mungu.” Hapana! Tangazo la Yeremia lilikuwa lenyewe ni kitendo cha ibada. Yeremia alihubiri kwamba Mungu alikuwa amekataa ibada ya Israeli kwa sababu ya maisha yao ya dhambi. Hii ilikuwa ibada. Ilitambua usafi wa Mungu mtakatifu; ilitambua thamani ya Mungu.

## Ibada ya Kibiblia Siku hizi

Baadhi ya makanisa hutenganisha ibada na mahubiri. Wanatangaza, “Tutaanza na muda wa ibada.” Baada ya ibada kukamilika, wanahama kwenda kwenye mahubiri. Hii ina hatari mbili.

1. Inamaanisha kwamba ibada inahusishwa na muziki tu. Mtazamo huu wa ibada unalenga tu hisia. Ibada ya kweli lazima iwe zaidi ya muziki na wimbo.
2. Inatenganisha tangazo kutoka kwa ibada. Kila kitu tunachofanya katika huduma ya kanisa kinapaswa kuwa ibada. Muziki, sala, maandiko, mahubiri, na hata sadaka ni sehemu ya ibada.

**Kujipima**

Jiulize, "Je, mahubiri yangu ni kitendo cha ibada? Ninapohubiri, je, ninaongea kama mjumbe wa Mungu anayemheshimu Mungu?"

## Hatari za Ibada: Kutokuwa na Kiasi katika Ibada

### (1) Hatari ya ibada ya kimazoea

Tunaposahau kwamba ibada ya kibiblia inahitaji utii, tunaweza kuanza kumchukulia Mungu kama rafiki wa kawaida ambaye hapewi heshima. Ibada ya kimazoea huhamasisha mtazamo huu. Hatupaswi kamwe kusahau kwamba Mungu ni Mungu wa ajabu anayehitaji utii kamili. Yeye ni " Mfalme wa milele, asiyeweza kuona uharibifu, asiyeonekana, Mungu peke yake" (1 Timotheo 1:17). Baadhi ya makanisa yanasahau ukuu wa Mungu; ibada inakuwa kama kunywa kikombe cha kahawa na rafiki wa zamani mnayekutana naye.

### (2) Hatari ya ibada inayozingatia desturi

Tunaposahau kwamba ibada ya kibiblia ni ibada kwa Mungu anayetamani kujenga uhusiano nasi, tunaweza kuanza kumchukulia Mungu kama mungu wa mbali. Mtazamo rasmi sana

wa ibada unaweza kuhamasisha mtazamo huu. Baadhi ya makanisa hayatoi nafasi kwa mwamini kupata urafiki na Mungu; mkazo wote uko kwenye ukuu na ukubwa wake.

Katika ibada, tunapaswa kupata uzoefu wa mamlaka ya Mungu juu ya uumbaji wake na urafiki wake wa karibu na watoto wake.

**Kujipima**

Fikiria ibada yako ya hivi karibuni. Jiulize, "Sehemu gani za ibada ziliwahimiza waabudu kumheshimu Mungu kwa ukuu wake? Je, walitoka kwenye ibada wakiwa na hisia za Mungu wetu mkuu?" Kisha jiulize, "Sehemu gani za ibada ziliwahimiza waabudu kupata urafiki wa karibu na Mungu? Je, walitoka kwenye ibada wakijua kwamba Mungu anawapenda sana?"

## Hitimisho: Ushuhuda wa Shahidi wa Kuzinduliwa kwa Hekalu

Je, ingekuwaje kama ungekuwa kwenye uzinduzi wa Hekalu? Labda inaweza kuelezwa hivi:

"Nilikuwepo kwenye uzinduzi wa Hekalu. Sitausahau siku hiyo. Tulikuwa tumeisubiri ibada hiyo kwa miaka mingi.

"Miaka? Ndiyo, miaka! Mfalme Daudi alikuwa ametengeneza mipango ya kujenga Hekalu na akampa Solomoni kabla ya kifo chake. Sasa Hekalu lilikuwa limekamilika, na ibada iliyosubiriwa kwa muda mrefu ya uzinduzi ilifanyika.

"Ilikuwa ni mazingira mazuri na ibada yenye msisimko. Fikiria...

- Dhabihu za maksai 22,000 na kondoo 120,000
- Kwaya ya mamia ya watu ikiiimba Zaburi za Daudi
- Bendi ya matoazi, vinubi, zeze, na tarumbeta 120
- Makuhani na Walawi wamevaa mavazi meupe mazuri
- Moja ya majengo mazuri zaidi yaliyowahi kujengwa
- Vyombo vya dhahabu na fedha kwa kila tendo la ibada

"Ilikuwa ni ibada nzuri, lakini uzuri wa mipangilio siyo jambo muhimu zaidi katika kumbukumbu yangu. Ninachokumbuka zaidi ni kwamba wanamuziki walipoanza kupiga na kuimba, 'utukufu wa Bwana ulijaza nyumba ya Mungu.' Uwepo wa Mungu ulijaza Hekalu hadi makuhani hawakuweza kufanya kazi zao. Ibada kwa Mungu ilitawaliwa na Mungu!

"Imepita miaka tangu ile ibada ya kukumbukwa. Sidai kwamba kila ibada niliyohudhuria tangu siku ile imekuwa na ishara zile zile za wazi za uwepo wa Mungu; ile ilikuwa siku maalum. Hata hivyo, katika kila ibada ninayohudhuria, natarajia uwepo wa Mungu.

"Wakati mwingine, uwepo wake ni wa kusisimua; wakati mwingine, ni kimya. Wakati mwingine, uwepo wake unauhisi kwenye uimbaji; wakati mwingine, anazungumza kupitia mahubiri. Wakati mwingine, hisia zangu huguswa; wakati mwingine, ukweli wake unazungumza kwa akili na nia yangu. Wakati mwingine, natoka nikiwa nimehamasishwa; wakati mwingine, natoka nikiwa nimehukumiwa.

"Bila kujali jinsi Mungu anavyochagua kuwepo, nauthamini uwepo wake. Huenda nisije kuona tena tukio la wazi la uwepo wa Mungu kama lile, lakini ninaweza kuingia kwenye uwepo wake kila wakati ninapoabudu."

### Majadiliano ya kikundi

► Kwa matumizi ya vitendo vya somo hili, jadili yafuatayo:

*Esther ni Mkristo mkweli na anapenda kuhudhuria ibada za kanisani kijijini kwake. Muziki wenye nguvu na ushirika vinatoa mabadiliko mazuri kutoka kwenye matatizo ya maisha ya kila siku. Anapenda hisia na mihemko anayopata anapomwabudu Mungu kwa moyo wake wote. Hata hivyo, Esther anakutana na ugumu wa kuweka bidii sawa kwenye ndoa yake na majukumu ya maisha ya kila siku kama anavyoweka kwenye ibada za Jumapili asubuhi. Ungewezaje kumshauri Esther?*

## Mapitio ya Somo la 3

(1) Mungu anajali jinsi tunavyoabudu kwa sababu:

- Namna ya ibada yetu inaathiri ufahamu wetu juu ya Mungu.
- Namna ya ibada yetu inaonesha sababu ya kuabudu kwetu.

(2) Ibada ni uhusiano - kutembea na Mungu.

- Mungu alitoa njia za ibada kwa Adamu na Eva.
- Mungu alichukua hatua ya kufanya ibada iwezekane kwa Abrahamu.
- Neema ya Mungu ilifanya ibada iwezekane kwa Yakobo.
- Tunapotembea na Mungu, maisha yetu yanabadilika.

(3) Ibada inaanza na utiifu.

- Ibada ni zaidi ya hisia au mihemko.
- Ibada ni mwitikio kwa amri za Mungu.
- Utiifu kwa Mungu unazidisha uhusiano wetu naye.

(4) Ibada inajumuisha desturi (dhabihu za Agano la Kale).

- Dhabihu zilionesha kujisalimisha kikamilifu kwa Mungu. (Warumi 12:1)
- Mungu aliheshimu ibada ya kweli kwa uwepo wake. (2 Mambo ya Nyakati 5)
- Taratibu za ibada za pamoja lazima zitoke kwa moyo mtiifu.

(5) Ibada inajumuisha sifa (Zaburi).

- Kitabu cha Zaburi kinaonesha kwamba ibada inajumuisha sifa.
- Kitabu cha Zaburi kinaonesha kwamba ibada inajumuisha maombolezo.

(6) Ibada inajumuisha kutangaza (Manabii).

- Ibada ni zaidi ya sifa; ni pia kutangaza ukweli. Mahubiri ni ibada.
- Manabii walifundisha kwamba taratibu za ibada bila ukweli siyo ibada.
- Manabii walifundisha kuwa ibada ya kweli inapaswa kuwa ya kiwango cha juu kabisa.
- Manabii walifundisha kwamba ibada ya kweli inajumuisha maisha yote.

## Somo la 3 Mazoezi

(1) Orodhesha kanuni tatu kuhusu ibada ambazo umejifunza kutoka kwenye somo hili la ibada za Agano la Kale. Andika ukurasa mmoja ukielezea njia za vitendo za kutumia kila kanuni katika ibada ya kanisa lako.

(2) Mwanzoni mwa somo lijalo, utafanya mtihani kulingana na somo hili. Soma maswali ya mtihani kwa uangalifu katika maandalizi.

**Jaribio Somo la 3**

(1) Kutoka kwenye somo hili, orodhesha mifano miwili ya kibiblia ya ibada iliyokataliwa na Mungu.

(2) Neno “alitembea pamoja na Mungu” linaonesha kwamba ibada inahusisha __________ na Mungu.

(3) Kutoka kwenye somo hili, taja watu watatu wasiofaa ambao Mungu kwa neema aliwawezesha kumwabudu.

(4) Sadaka ya Ibrahimu ya Isaka inaonyesha kuwa ibada ya kweli inahitaji__________ kamili.

(5) Tofauti ilikuwa nini kati ya ibada ya Abeli na ibada ya Kaini?

(6) Umuhimu wa muabudu kuweka mikono yake juu ya kichwa cha mnyama wa sadaka ulikuwa nini?

(7) Eleza maana ya sifa za kutangaza na sifa za maelezo.

(8) Manabii wanaonesha kwamba__________ la Neno la Mungu ni ibada.

(9) Orodhesha vipengele vitatu vya ujumbe wa manabii kuhusu ibada.

(10) Taja mambo mawili ya hatari ya kutokuwa na uwiano katika ibada.

(11) Andika Mika 6:6-8 kwa kumbukumbu.

# Somo la 4
# Ibada katika Agano Jipya

## Malengo ya Somo

Mwisho wa somo hili, mwanafunzi anapaswa:

(1) Kuelewa jinsi Yesu alivyotimiza ibada.

(2) Kutambua aina za ibada za uongo katika injili, Matendo na Ufunuo.

(3) Kutoa ahadi binafsi kwa ibada na uinjilisti.

(4) Kujua vipengele vya msingi vya ibada katika kanisa la kwanza katika nyaraka.

(5) Kupata uzoefu wa ibada inayolenga Mungu.

## Matayarisho kwa somo hili

*Kariri Warumi 12:1-2.*

## Utangulizi

> "Ibada ni shughuli kuu na ya kipekee isiyoweza kuepukika ya kanisa la Kikristo. Ni ibada pekee itakayoendelea…hadi mbinguni, wakati shughuli nyingine zote za Kanisa zitakuwa zimekoma."
>
> - W. Nicholls

Mchungaji James, Enoch, Gideon, na Jason walikutana tena kujadili walichojifunza kuhusu ibada kutoka Agano la Kale.

James, anayethamini ibada za tamaduni za zamani, alisema, "Nadhani Agano la Kale linathibitisha kuwa kanisa langu linafanya ibada kwa usahihi. Ibada katika Hekalu ilikuwa rasmi na iliyopangwa. Hicho ndicho tunajaribu kufanya."

Enoch alicheka, "Ndiyo, lakini ulisoma manabii walivyosema? Ibada rasmi ya Hekalu haikumaanisha chochote! Ibada inayompendeza Mungu ni ibada kutoka moyoni. Hicho ndicho tunachofanya katika ibada yetu ya kisasa; tunagusa mioyo ya kizazi kipya."

Kwa hasira, Gideon alisema, "Hatuko mbali zaidi kuliko tulipoanza kujifunza kuhusu ibada. Kwa nini Mungu asiseme tu, 'Hivi ndivyo mnavyopaswa kuniabudu'?"

Jason alisema. "Tusikate tamaa. Sisi ni Wakristo wa Agano Jipya; labda Agano Jipya litajibu maswali yetu. Hebu tujifunze ibada katika Agano Jipya na tuone linasema nini."

► Je, ibada ilibadilika vipi katika Agano Jipya? Ibada ya kanisa la kwanza ilikuwa tofauti vipi na ibada ya Hema na Hekalu? Fupisha unachojua tayari kuhusu ibada ya Agano Jipya.

## Injili: Ibada Inatimizwa katika Yesu Kristo

Jumla ya neno *ibada* katika Agano jipya, nusu yake iko katika vitabu vya injili. Injili zinaonesha kwamba Yesu ndiye utimilifu wa mwisho wa ibada. Anatimiza ibada kwa njia mbili.

### Katika Ubinadamu Wake, Yesu Alikuwa Mfano Mkuu wa Ibada

Yesu aliweka mfano wa ibada ya kweli. Yesu alimwambia mwanamke Msamaria kwamba Mungu anatafuta wale wanaomwabudu kwa roho na kweli (Yohana 4:24). Katika desturi zake za ibada (kusoma Biblia, kuomba, kuhudhuria sinagogi na Hekalu), Yesu alionesha maana ya kuabudu kwa roho na kweli.

#### *Yesu alipenda mahali pa ibada.*

Luka anaonesha upendo wa Yesu kwa mahali pa ibada. Hata akiwa mtoto, Yesu alitambua Hekalu kama nyumba ya Baba yake (Luka 2:41-49). Alikuwa na shauku kwa usafi wa ibada ya Hekalu; mara mbili aliwafukuza wale waliokuwa wakinyanyasa Hekalu.[20]

Mwanzoni mwa huduma yake kwa umma, Yesu alikwenda katika sinagogi huko Nazareti siku ya Sabato kama desturi yake (Luka 4:16). Katika huduma yake yote duniani, Yesu mara nyingi alitembelea masinagogi.

#### *Yesu alikataa kumwabudu yeyote au chochote isipokuwa Mungu.*

Katika jangwa, Yesu alikataa jaribu la ibada ya uongo.

► Soma Mathayo 4:9-10.

Jaribu la kuabudu kiumbe badala ya Muumba ni mada ya mara kwa mara katika maandiko. Ni mzizi wa sanamu katika Agano la Kale. Ufunuo unaonesha tofauti kati ya ibada ya joka na mnyama, na ibada ya Mungu na Mwana-Kondoo. Yesu alikataa kuabudu kiumbe.[21]

#### *Yesu alizoea kuomba.*

Maombi yalikuwa muhimu katika huduma yote ya Yesu. Mara kumi na tano, injili zinaripoti kwamba Yesu aliomba. Katika baadhi ya nyakati hizi, alitumia usiku kucha akiwa peke yake na Baba yake. Kabla ya kuchagua mitume kumi na wawili, alitumia usiku kucha katika maombi (Luka 6:12). Katika masaa yake ya mwisho na wanafunzi wake, Yesu aliwaombea wanafunzi na wote watakaokuja kuamini ndani yake (Yohana 17). Akikabili msalaba, alikwenda Gethsemane kuomba (Mathayo 26:36-42). Maombi yalikuwa muhimu katika ibada ya Yesu.

---

[20] Yohana 2:13-16 anazungumzia kutakaswa kwa kwanza. Mathayo 21:12-27, Marko 11:15-17, na Luka 19:45-46 wanatoa taarifa kwa kutakaswa pili wakati wa juma la mwisho la huduma yake duniani.

[21] Yesu hakuwa kama watu wanaotajwa katika Warumi 1:25.

***Yesu alielezea ibada ya kweli.***

Mbali na kuonesha ibada kupitia matendo yake mwenyewe, Yesu alifundisha mara kwa mara kuhusu ibada. Alifundisha mwanamke Msamaria kuhusu ibada ya kweli. Yesu aliwafundisha wanafunzi maombi ya mfano na alifundisha kuhusu maombi kupitia mifano (Luka 11:5-8, Luka 18:1-14).

► Soma Luka 11:1-4.

Maombi ya mfano ya Yesu yanaonesha kwamba maombi lazima yatoke katika moyo wa ibada. Maombi yanaanza, "Jina lako litukuzwe." Kutukuza ni kuheshimu kama takatifu. Katika maombi, tunamtambua Mungu kama mtakatifu.

***Yesu alikemea ibada ya uongo.***

Kama ibada ya kweli ni ibada katika roho na kweli, basi ibada ya uongo ni chochote kinachokosa haya. Yesu alikataa:

**(1) Ibada ya kinafiki**

Katika Mahubiri ya Mlimani, Yesu alionya kwamba inawezekana kufanya mambo sahihi kwa sababu zisizo nzuri. Kutoa kwa maskini, maombi, na kufunga ni vipengele vyote vya ibada. Yesu alionya dhidi ya wale wanaofanya matendo haya ili kuwavutia wengine; wao ni wanafiki (Mathayo 6:1-18). Waabuduo wa kweli hufanya matendo haya kwa nia ya kufanya ibada kwa Mungu.

Katika Mathayo 23, Yesu aliwalaani viongozi wa kidini ambao hufundisha mambo sahihi kuhusu ibada, lakini mioyo yao iko mbali na Mungu. Yesu alisema kwamba mafundisho yao yalikuwa sahihi, lakini mioyo yao ilikuwa mibaya; wao ni wanafiki.

**(2) Ibada ya kisheria**

Hatari moja ni ibada ya kinafiki; ibada inayokusudiwa kuwavutia watazamaji badala ya kumpendeza Mungu. Hatari nyingine ni sheria; ibada inayokusudiwa kupata kibali cha Mungu kupitia kutimiza masharti fulani. Tunapojaribu kupata kibali cha Mungu kwa matendo yetu ya ibada, tunapoteza ukweli wa ibada ya kweli. Ibada inakuwa kazi ambayo tunapata kibali cha Mungu badala ya jibu la furaha kwa wema wa Mungu.

Yesu aliwakera viongozi wa kidini wa Israeli alipozivunja desturi zao [22] Yesu hakuvunja sheria au hata roho ya sheria; alivunja desturi za kibinadamu zilizokuwa zimejengeka kupitia miaka ya uhalali wa Kifarisayo. Kwa Mafarisayo, desturi hizi zilikuwa muhimu kama sheria yenyewe. Waliamini kwamba kuzingatia sheria kunapata kibali kwa Mungu. Hii inafafanua sheria: jaribio la kupata kibali cha Mungu kwa kutimiza masharti. Yesu alikataa sheria kwa nguvu kama alivyokataa unafiki.

---

[22] Mathayo 12:1-14, Luka 13:10-17, na Yohana 5:8-18, kati ya wengine.

**Katika Uungu Wake, Yesu Anaabudiwa**

Baada ya kifo na ufufuo wake, **Yesu anakaa mkono wa kuume wa Baba na kwa haki anapokea ibada** (Ufunuo 5:12-14). Paulo aliandika kuhusu mabadiliko haya katika Wafilipi 2. Kwa sababu ya kujinyenyekeza kwa hiari ya Yesu, sasa anatukuzwa na kuabudiwa.

> Kwa hiyo tena Mungu alimwadhimisha mno, akamkirimia Jina lile lipitalo kila jina; ili kwa jina la Yesu kila goti lipigwe, la vitu vya mbinguni, na vya duniani, na vya chini ya nchi; na kila ulimi ukiri ya kuwa YESU KRISTO NI Bwana, kwa utukufu wa Mungu Baba (Wafilipi 2:9-11).

Katika Mathayo 18:20, Yesu alishuhudia kwamba anastahili kuabudiwa. Katika desturi ya Kiyahudi, wanachama wa kiume 10 walihitajika kabla ya sinagogi kukutana kwa maombi na ibada. Yesu aliwaambia wanafunzi wake, "Kwa kuwa wawili au watatu wamekusanyika kwa jina langu, hapo nipo kati yao." Katika Kanisa, **uwepo wa Yesu, si idadi ya watu waliohudhuria, ndio huamua ibada.**

Kwa kupitia makundi ya watu waliotazama miujiza yake, Yesu anaonesha kwamba anastahili kuabudiwa. Walipoona miujiza yake, **watu walimtukuza Mungu**, kitendo cha ibada. Watu waliouona uponyaji wake wote walishangaa (Marko 1:23-27).

Usiku wake wa mwisho na wanafunzi, Yesu alikula Pasaka. Wakati mlo huu ulifuata mpangilio wa kawaida wa mlo wa Pasaka ya Kiyahudi, Yesu aliupa maana mpya alipowaambia wanafunzi kwamba mkate "ndio mwili wangu unaotolewa kwa ajili yenu" na kikombe "ni agano jipya katika damu yangu" (Luka 22:19-20).

► Soma Luka 22:13-20.

Aliwaamuru wafanye hivi kwa ukumbusho wake. **Meza ya Bwana inamlenga Kristo, utimilifu kamili wa Pasaka.**

## Ibada ya Kibiblia Leo

Karipio la Yesu dhidi ya ibada ya uongo na mfano wake wa ibada ya kweli unaonesha kwamba ibada yetu lazima iwe ya dhati, siyo kwa ajili ya kuwavutia wengine. Ibada ya kweli lazima ilenge kumpendeza Baba, siyo kuwafurahisha wengine.

Jaribu hili ni la mara kwa mara kwa viongozi wa kanisa. Kwa sababu kuhubiri na kuongoza ibada kunafanywa hadharani, tunaweza kushawishika kufanya maonesho badala ya kuabudu. Tunapolenga kuwafurahisha watu badala ya kumheshimu Mungu, tunafanya maonesho badala ya kuabudu.

Je, nini jaribu la ibada ya uongo kwa kiongozi?

- Kuchagua andiko la mahubiri kwa sababu tunajua litapendwa na wasikilizaji
- Maombi yanayozungumzia zaidi wasikilizaji badala ya Mungu
- Sadaka inayotolewa kwa namna inayovutia umakini kwa mtoaji
- Muziki unaomletea utukufu mwimbaji badala ya Mungu


**Mafundisho na mfano wa Yesu yanatukumbusha kwamba ibada ya kweli ni ya Mungu pekee.** Ibada ni kuhusu yeye, siyo kuhusu sisi.

### Kujipima

Jiulize, "Je, nani anaheshimiwa katika uongozi wangu wa ibada? Je, ninahubiri, kuimba, kuomba, na kutoa kwa utukufu wa Mungu, au kwa ajili ya kutambuliwa kwangu? Je, kweli ninaabudu?"

## Matendo ya Mitume: Ibadan a Uinjilisti

Ibada inahusiana kwa karibu na uinjilisti. Wasioamini wanakuwa waabudu wanaposikia na kuipokea injili. Kitabu cha Matendo ya Mitume kinaonesha uhusiano kati ya ibada na uinjilisti.




Isaya 6:8 inaonesha kwamba ibada husababisha uinjilisti; jibu la Isaya kwa ibada lilikuwa "Mimi hapa! Nitume mimi." Tunapoabudu kiukweli, tunapata shauku ya uinjilisti. Katika ibada, tunamwona Mungu na tunayaona mahitaji ya dunia yetu kupitia macho ya Mungu. Ibada huumba wainjilisti.

Ibada huwahamasisha kanisa kwa uinjilisti. Kanisa linapowaongoza wasioamini kwa Kristo, waumini wapya wanakuwa waabudu. Waabudu hawa wapya kisha wanahamasishwa kwa uinjilisti.

Kitabu cha Matendo ya Mitume kinaonesha mchakato huu kwa vitendo. Baada ya Paulo kuhubiri huko Efeso, watu waligeuka kutoka kwa mungu Diana na ibada ya miungu iliyotengenezwa kwa mikono na kuelekea kwa ibada ya Mungu wa kweli (Matendo 19:26-27). Tunapomhubiri Kristo, waumini wapya wanavutwa katika ufalme; wanakuwa waabudu. Uinjilisti huumba waabudu.

### Ibada ya Kweli huhamasisha Uinjilisti

Matendo ya Mitume yanaanza na wanafunzi wakiabudu; walikuwa pamoja wakijitoa kwa maombi (Matendo 1:14). Matendo yanaisha na Paulo akihubiri huko Rumi; alikuwa " akihubiri habari za ufalme wa Mungu, na kuyafundisha mambo ya Bwana Yesu Kristo, kwa ujasiri mwingi, asikatazwe na mtu " (Matendo 28:31).

Ibada ya Wakristo wa mwanzo iliongoza kwa uinjilisti. Wito wa Paulo na Barnaba ulitokea katika mazingira ya ibada.

> Basi hawa walipokuwa wakimfanyia Bwana ibada na kufunga, Roho Mtakatifu akasema, “Nitengeeni Barnaba na Sauli kwa kazi ile niliyowaitia.” Ndipo wakiisha

> kufunga na kuomba, wakaweka mikono yao juu yao, wakawaacha waende zao (Matendo 13:2-3).

Ibada ya kweli inahamasisha uinjilisti.

**Uinjilisti Wa Ufanisi Huunda Waabudu**

Katika kitabu chote cha Matendo, wanafunzi walikuwa wakijishughulisha na ibada. Siku ya Pentekoste, watu 3,000 waliokolewa. Waumini hawa wapya wakawa waabudu; walijitoa kwa mafundisho ya mitume na ushirika, kwa kumega mkate na maombi (Matendo 2:42).

► Soma Matendo 2:42-46 kwa picha ya ibada katika kanisa la mwanzo.

Wakristo wa Kiyahudi waliendelea kuabudu katika Hekalu.[23] Zaidi ya hayo, Wakristo wa Kiyahudi na watu wa Mataifa waliokoka walikutana kwenye sinagogi kwa ibada. Katika miji mingi, Paulo alianza huduma yake katika sinagogi, akionesha kuwa Yesu ni utimilifu wa ahadi za Agano la Kale.[24] Ibada pia ilifanyika katika nyumba za faragha. Waumini walitembeleana nyumba kwa nyumba kwa ushirika na ibada (Matendo 2:46). Barua za Paulo zinajumuisha salamu kwa makanisa yanayokutana nyumbani.[25] Jitihada za uinjilisti za kanisa la mwanzo ziliunda kundi jipya la waabudu.

**Uinjilisti katika Areopago**

Ujumbe wa Paulo kwenye Areopago ni maandiko ya kawaida yanayoonesha uhusiano kati ya uinjilisti na ibada (Matendo 17:16-34). Huko Athene, Paulo alikabiliana na utamaduni uliojaa sanamu za miungu. Paulo alionesha tofauti kati ya ibada ya uongo ya sanamu na ibada ya kweli ya Yehova.

***Waathene walikuwa washika dini sana (Matendo 17:22).***

Watu wa Athene walikuwa waabudu, lakini hawakuabudu Mungu wa kweli. Ibada yenyewe haitoshi; ibada lazima ilenge kwenye kitu sahihi.

***Waathene waliabudu kwa ujinga (Matendo 17:23).***

Hawakujua nani wanayemwabudu. Paulo aliwatangazia Bwana ambaye walikuwa wakimtafuta. Aliwaambia kwamba Mungu ameumba mataifa yote kwa namna yao ili kumtafuta na kumpata. Hii ni kauli ni ya mtu papasa gizani. Njaa ya mwanadamu kwa Mungu ilitoa nafasi ya injili.

***Waathene waliabudu mungu asiyeweza kutosheleza.***

Yehova haabudiwi kwa mikono ya wanadamu, kana kwamba anahitaji chochote. Yeye ndiye anayewapa watu wote uhai, pumzi, na vitu vyote (Matendo 17:25). Ibada ya Waathene

[23] Matendo 2:46, Matendo 3:1, 11-26; Matendo 4:2, Matendo 5:12, 42
[24] Matendo 13:14-15, Matendo 14:1, Matendo 17:1, 10; Matendo 18:4, 19; Matendo 19:8
[25] Warumi 16:5, 1 Wakorintho 16:19, Wakolosai 4:15, Filemoni 1:2

ilikuwa ya uongo kwa sababu mungu wao asiyeweza kutosheleza. Mungu wa kweli anawapa wote uhai; hahitaji chochote. Tunamwabudu Mungu kwa sababu anastahili ibada yetu, si kwa sababu anahitaji ibada yetu.

Paulo alilinganisha sanamu na Mungu wa kweli.

1. **Mungu ni Muumbaji**. Alifanya ulimwengu na kila kitu ndani yake... Yeye ni Bwana wa mbingu na dunia (Matendo 17:24). Tofauti na sanamu zilizotengenezwa kwa mikono ya wanadamu, Mungu aliumba mwanadamu. Yeye si mungu mgeni; (Matendo 17:18) yeye ni muumbaji wa ulimwengu wote.

2. **Mungu yuko karibu.** Yeye hayuko mbali na kila mmoja wetu (Matendo 17:27). Ingawa Mungu ni mtukufu, ameuingia ulimwengu wetu na yuko karibu na kila mwabudu.

3. **Mungu atawahukumu wale wanaokataa kutubu** (Matendo 17:30-31). Ibada katika ukweli inatambua kwamba Mungu ni hakimu mwenye haki ambaye hatavumilia uasi. Katika ibada yetu, tunajisalimisha kwa enzi yake.

4. **Mungu alimfufua Yesu kutoka kwa wafu**, akionesha kwamba Yesu anastahili kuabudiwa (Matendo 17:31). Yesu alijinyenyekeza kwa hiari hadi kufa; sasa ameinuliwa na Baba, " ili kwa jina la Yesu kila goti lipigwe, la vitu vya mbinguni, na vya duniani, na vya chini ya nchi; na kila ulimi ukiri ya kuwa Yesu Kristo ni Bwana, kwa utukufu wa Mungu Baba" (Wafilipi 2:10-11).

Ujumbe wa Paulo huko Athene ulikabiliana na ibada ya uongo ya sanamu kwa injili ya ibada ya kweli ya Yehova. Uinjilisti wenye ufanisiwa kweli huunda waabudu.

### Hatari za Ibada: Ibada Bila Uinjilisti

Makanisa mengi hutenganisha ibada na misheni na uinjilisti. Makanisa mengine husema, "Tumejitolea kwa kufanya uinjilisti. Shauku yetu ni kuwafikia waliopotea." Makanisa haya hayazingatii sana ibada. Wanajiona kama makanisa ya uinjilisti. Makanisa mengine husema, "Tunaamini lengo kuu la kanisa ni ibada. Watu wengine wanaweza kufanya uinjilisti; lengo letu ni ibada."

Matendo yanaonesha kwamba kanisa lazima lijitolee kwa ibada **na** uinjilisti. Ibada ya kweli hutupa shauku kwa uinjilisti. Uinjilisti wa kweli huunda waabudu wapya.

Hatuwezi kutenganisha ibada na uinjilisti. Ibada ambayo haihamasishi uinjilisti ina uwezekano wa kuwa ibada ya kujitakia yenyewe ambayo hufanywa kwa ajili ya msukumo wetu wenyewe. Uinjilisti ambao hauongozi kwa ibada utatengeneza Wakristo wa juu juu ambao wanashindwa kumwona Mungu kweli.

Katika ibada ya kibiblia, tunapata shauku mpya kwa uinjilisti. Kama Isaya, mtazamo wetu wa Mungu utaambatana na mtazamo wa dunia yenye uhitaji. Kama Isaya, ahadi yetu ya ibada kwa Mungu itatuongoza kusema, "Mimi hapa! Nitume mimi."

**Kujipima**

Jiulize, "Je, ibada inanihamasisha kushiriki injili na wasioamini? Je, nina shauku ya kuwaleta waabudu wapya kwa Mungu?"

**Waraka: Ibada ya Kanisa la Kwanza**

Tofauti na Agano la Kale lenye maelekezo maalum kwa ajili ya ibada ya Kiyahudi, Agano Jipya halitoi maelekezo mengi kwa ajili ya ibada kanisani.[26] Hakuna maelezo kamili ya ibada katika Agano Jipya, lakini nyaraka zinaonesha baadhi ya vipengele vya ibada ya Kikristo vya kanisa la kwanza.

**Kusoma Maandiko**

Kusoma maandiko kulikuwa muhimu katika ibada ya Kikristo ya kwanza. Wakolosai 4:16 na 1 Wathesalonike 5:27 zinaagiza makanisa kusoma barua za Paulo kwa pamoja. Katika 1 Timotheo 4:13, Paulo anamkumbusha Timotheo kuzingatia usomaji wa maandiko wa pamoja.

Umuhimu wa kusoma maandiko unaoneshwa katika Wakolosai 3:16, "Neno la Kristo na likae kwa wingi ndani yenu… katika hekima yote." Mwandishi wa zaburi anamwelezea mtu aliye barikiwa; anafurahia na kutafakari sheria ya Bwana (Zaburi 1:2). Ibada yetu ya hadhara inaonesha thamani tunayoweka kwenye Maandiko.

**Kuhubiri Neno**

Pamoja na kusoma maandiko, kiongozi alikuwa na jukumu la kuhubiri Neno (2 Timotheo 4:1-4, Tito 2:15). Tangu wakati wa Ezra, waandishi walifafanua Maandiko kwa watu. Ezra na wenzake walisoma kutoka kitabu, kutoka Sheria ya Mungu, kwa uwazi, na wakafafanua maana, ili watu waelewe usomaji (Nehemia 8:8). Masinagogi ya Kiyahudi katika enzi ya Agano Jipya yaliendeleza desturi hii (Matendo 13:14-15). Kutoa ufafanuzi wa maandiko ni msingi wa mahubiri ya Kikristo ya kwanza.

Mahubiri katika Matendo yanaonyesha yaliyomo katika mahubiri ya Kikristo ya kwanza.[27] Mada muhimu katika mahubiri haya ni pamoja na:

- Yesu alitimiza unabii wa Agano la Kale.
- Yesu alifanya kazi kuu kwa nguvu za Mungu.
- Yesu alisulubiwa na kisha kufufuka kutoka kwa wafu.
- Yesu sasa ametukuzwa na kufanywa Bwana.
- Wote wanaosikia wanapaswa kutubu na kubatizwa.

[26] Sehemu kubwa imechukuliwa Franklin M. Segler na Randall Bradely, *Christian Worship: Its Theology and Practice.* (Nashville: B&H Publishing, 2006), Chapter 2.
[27] Mahubiri muhimu katika Matendo yanapatikana katika Acts 2, 7, 10, 17.

**Maombi ya pamoja**

Maombi ya Pamoja yalikuwa muhimu katika ibada za Kikristo za kwanza (1 Timotheo 2:1-3). Wanazuoni wengi wanaamini kwamba maombi yalijumuishwa katika barua za Paulo zilitumika katika ibada za pamoja. "Amina" ya mkusanyiko ilionesha kukubaliana kwao na maombi.[28]

**Kuimba**

Kuimba kulikuwa muhimu katika Hekalu na kuliendelea kuwa na nafasi katika ibada za Kikristo za kwanza. Pamoja na Zaburi ambazo Wakristo walileta kutoka kwenye ibada zao za Kiyahudi, nyimbo mpya zilimsifu Yesu kama Masiya. Hii inashauriwa na Waefeso 5:19 na Wakolosai 3:16. Wanazuoni wengi wa Biblia wanaamini kwamba Wafilipi 2:5-11 ilikuwa wimbo wa Kikristo wa kanisa la kwanza. Zaidi ya hayo, wimbo wa Maria katika Luka 1:46-55 na maombi ya Simeoni katika Luka 2:29-32 huenda zilikuwa zinaimbwa katika ibada.

**Sadaka**

Katika baadhi ya nyakati, sadaka ilikuwa sehemu ya ibada ya pamoja. 1 Wakorintho 16:2 na 2 Wakorintho 9:6-13 zinaelekeza kanisa la Korintho kukusanya sadaka kwa ajili ya Wakristo wanaoteseka huko Yerusalemu.

**Ubatizo na Meza ya Bwana**

Ubatizo na Meza ya Bwana zilikuwa sehemu ya ibada. Paulo aliandika kurekebisha matumizi mabaya katika sherehe za Meza ya Bwana za Wakorintho. Badala ya kuwa ukumbusho wa dhabihu ya Kristo, ilikuwa imekuwa karamu. Paulo alionya juu ya uzito wa Meza ya Bwana. Ushirika unakumbuka tukio takatifu zaidi kwa Mkristo; haupaswi kuchukuliwa kwa wepesi.[29]

Zaidi ya viashiria hivi vya vipengele vya ibada, tunajua kidogo sana kuhusu ibada za Kikristo za kwanza. Nyaraka hazielekezi utaratibu maalum wa ibada, mazingira ya ibada, au maelezo mengine kuhusu ibada za pamoja katika kanisa la kwanza. Kwa sababu ya aina mbalimbali za asili za kidini na kitamaduni zilizowakilishwa katika kanisa la kwanza, inawezekana kwamba ibada za pamoja zilionekana tofauti kutoka mahali hadi mahali. Wakristo wa Kiyahudi huenda waliendelea kuabudu kwa namna inayofanana na ibada za sinagogi. Wakristo wa Mataifa wasingekuwa na mazoea ya Kiyahudi na huenda waliabudu kwa namna tofauti. Hata hivyo, ni wazi kwamba kanisa la kwanza liliweka msisitizo mkubwa juu ya maandiko na kuhubiri na kufundisha Neno la Mungu.

## Ibada ya kibiblia Siku hizi

Katika makanisa mengi, kusoma maandiko pamoja kumekuwa nadra. Si jambo la kushangaza kuona makanisa ya kiinjili ambapo ni mistari michache tu ya maandiko

---

[28] 1 Wakorintho 14:16 inamsingi katika utendaji huu.
[29] Mathayo 28:18-20, Matendo 2:38-41, 1 Wakorintho 11:20-34

husomwa wakati wa ibada. Maandiko yanapaswa kuwa kipaumbele katika ibada yetu. Kupitia nyimbo zinazotokana na maandiko, usomaji wa Biblia, au ufafanuzi makini wa maandiko katika mahubiri, tunapaswa kujulikana kama "watu wa Kitabu." Biblia lazima iendelee kuwa na nafasi ya katikati katika ibada yetu.

**Kujipima**

Jiulize, "Je, ibada yangu inajumuisha kila kipengele kilichokuwa sehemu ya ibada ya kanisa la kwanza?"

## Ufunuo: Ibada kama Kumuabudu Mungu kwa Upendo wa Dhati

Ibada ni kiini cha ujumbe wa Ufunuo.

- Yohana alikuwa katika Roho siku ya Bwana aliposikia sauti ya Alfa na Omega (Ufunuo 1:10).
- Mojawapo ya mada kuu za Ufunuo ni tofauti kati ya wale wanaomwabudu Yehova kwenye kiti chake cha enzi na wale wanaomwabudu mnyama.
- Ufunuo unaahidi kwamba Mungu atashinda maadui zake, na mataifa yote yatakuja na kumwabudu mbele zake (Ufunuo 15:4).

Kuelewa ibada katika Ufunuo, ni muhimu kupitia hali ya kihistoria ya kitabu hiki. Wakristo wa karne ya kwanza walikabiliana na madai mawili yanayopingana. Kwa upande mmoja, walijua kwamba Yesu Kristo ni Bwana (Wafilipi 2:11). Imani kwa Kristo inahitaji kujitolea kwa mamlaka na ubwana wa Yesu Kristo. Kwa upande mwingine, Ruma ilihitaji kila mtu chini ya mamlaka ya himaya kushuhudia kwamba Kaisari alikuwa bwana na mungu wao.

> "Kamilisha uumbaji Wako mpya,
> Utu safi usio na doa utufanye tuwe;
> Tuweze kuona wokovu wako mkuu,
> Ulio timilika kikamilifu ndani Yako:
> Tukibadilishwa kutoka utukufu hadi utukufu,
> Hadi tupate nafasi yetu mbinguni,
> Tukiimba na kutupa taji zetu mbele Yako,
> Tukizama katika mshangao, upendo na sifa!"
>
> - Charles Wesley

Ilikuwa haiwezekani kwa Wakristo kutoa utii wa mwisho kwa yeyote isipokuwa Mungu. Mizizi ya mgogoro kati ya Roma na Wakristo wa karne ya kwanza ilikuwa, "Nani anastahili kuabudiwa?" Katika hali hii, Ufunuo unasema, "Yesu ni Bwana." Hata katika dunia isiyotambua mamlaka yake, Yesu ni Bwana. Anastahili kuabudiwa. Ufunuo unatoa picha ya ibada ya kweli.

### Ibada ya Kimbinguni Ikilinganishwa na Ibada Iliyoshindwa

Ufunuo unaanza na ujumbe kwa makanisa saba ya Asia Ndogo. Asia Ndogo ilikuwa mojawapo ya vituo vikali vya ibada ya mfalme. Kulikuwa na mahekalu ya kifalme katika kila

mojawapo ya miji iliyotajwa katika Ufunuo. Ibada ya mfalme ilikuwa ni karibu ya kila mahali katika Roma.

Ujumbe kwa makanisa saba unaonesha kushindwa kwa ibada katika makanisa kadhaa. Ingawa makanisa yote saba yanamwabudu Mungu, makanisa matano yanakaripiwa. Karipio hizi zinaonesha kwamba makanisa haya yalishindwa kumwabudu Mungu kwa namna inayokubalika.

1. **Ukosefu wa upendo unazuia ibada ya kweli.** Waefeso walifanya mambo mengi vizuri, lakini walikuwa wameacha upendo wao wa kwanza. Kuwa na mikono mitupu katika ibada kunaweza kuwa ishara kwamba tumepoteza upendo wetu kwa Mungu tunayemwabudu.

2. **Mafundisho ya uongo yanazuia ibada ya kweli.** Pergamo na Thiatira walivumilia mafundisho ya uongo. Hatari hii inaweza kuonekana katika makanisa yanayobadilishana ishara na maajabu kwa ukweli wa kibiblia.

3. **Matendo yaliyokufa yanazuia ibada ya kweli.** Mji wa Sardi ulikuwa umeshindwa mara mbili wakati walinzi waliolala walishindwa kuona adui anayekuja.[30] Yohana alionya kwamba kanisa la Sardi lilikuwa linalala kwa sababu lilitegemea kazi zake nzuri. Kukutana na Mungu katika ibada kungeamsha Sardi kutoka kwenye utepetevu wake.

4. **Ukosefu wa shauku unazuia ibada ya kweli.** Laodikia ilionesha roho ya uvuguvugu ambayo kanisa limeona mara nyingi katika nyakati za ustawi. Ukosefu wa shauku wa Walaodikia ulisababishwa na utajiri wao na kujitegemea. Ibada ya kweli inatukumbusha utegemezi wetu kwa Mungu.

### Ibada ya Mbinguni Inamlenga Mungu

Ufunuo 4-5 inaonesha kwamba ibada ya mbinguni inamlenga Mungu na utukufu wake. Waabudu wa mbinguni wanamwabudu Mfalme wa Milele na Mwanakondoo aliyefufuka.

Je, unaweza kumwazia malaika akimwambia Yohana, "Kuna kitu chochote tunaweza kubadilisha ili uwe na faraja zaidi katika ibada?" Bila shaka hapana! Ibada inamhusu Mungu, sio mimi. Ibada inambariki mwabudu lakini hilo siyo lengo kuu la ibada. Lengo la ibada ni kumheshimu Mungu. Waabudu waliomzunguka kiti cha enzi cha Mungu wanaimba wimbo wa kumsifu Mungu:

> Matendo yako, Ee Bwana Mungu Mwenyezi; Ni za haki, na za kweli, njia zako, Ee Mfalme wa mataifa. Ni nani asiyekucha, Ee Bwana, na kulitukuza jina lako? Kwa kuwa wewe peke yako u Mtakatifu; kwa maana mataifa yote watakuja na kusujudu

[30] Hii ilitokea Koresh aliposhambulia mwaka 547 K.K. na tena Antiochus III alishambulia mwaka 214 K.K.

> mbele zako; kwa kuwa matendo yako ya haki yamekwisha kufunuliwa (Ufunuo 15:3-4).

Ibada ya mbinguni hufanyika mbele za Mungu. Tangu wakati Adamu na Hawa walipofukuzwa kutoka bustanini, mwanadamu ametenganishwa na Mungu. Mbinguni, ibada itafanyika tena mbele za Mungu bila ushawishi wowote wa uovu.

> Tazama, maskani ya Mungu ni pamoja na wanadamu, naye atafanya maskani yake pamoja nao, nao watakuwa watu wake. Naye Mungu mwenyewe atakuwa pamoja nao. (Ufunuo 21:3).

**Ibada ya Mbinguni Inaonesha Ukweli Halisi**

Yohana alikuwa uhamishoni kwenye kisiwa cha Patmo, alipoandika Ufunuo. Wakristo kote katika Dola la Roma walikuwa wakiteseka kwa ajili ya imani yao. Kutoka mtazamo wa duniani, siku zijazo zilikuwa na giza. Hata hivyo, Ufunuo unaonesha mtazamo wa mbinguni juu ya matukio ya duniani.[31]

Duniani, tunaona upande mmoja tu wa historia. Tunajaribiwa kufikiri kwamba dunia inayotuzunguka ndiyo ukweli halisi. Ibada na mbingu zinaonekana kuwa mbali na mapambano ya dunia halisi. Mionekano ya ibada ya mbinguni inayoonekana katika Ufunuo 4, 5, na 15 inaonesha picha ya dunia halisi.

Kwa wafanyakazi wa Kikristo, Ufunuo ni ukumbusho muhimu kwamba mapambano ya dunia hii ni ya muda mfupi. Ibada siyo kimbilio la kila wiki kutoka kwenye ukweli; badala yake, ibada inaonesha ukweli kutoka mtazamo wa Mungu - na hili linabadilisha mtazamo wetu wa dunia yetu. Katika Ufunuo, Mungu anasema, "Mambo siyo kama yanavyoonekana kuwa. Mambo hayapo nje ya udhibiti, Shetani hajashinda, uovu haujashinda. Tazama kupitia mlango na upate kuona ukweli. Mungu yuko kwenye kiti chake cha enzi."[32]

## Ibada ya kibiblia siku hizi

"Amefufuka!" "Yeye ni Bwana!" Matamko haya ni muhimu kwa ibada. Ni ufufuo uliomtangaza Yesu kuwa Bwana (Warumi 1:4).

Kanisa la kwanza liliitambua kila Jumapili kama sherehe ya Ufufuo; kila Jumapili ilikuwa Pasaka. Wakristo hawakufunga siku ya Jumapili; Jumapili ilikuwa siku ya sherehe.

Leo, ibada yetu inapaswa kuwa wakati wa sherehe. Ndiyo, kuna uzito unaohusishwa na kuingia mbele za Mwenyezi, lakini pia kuna furaha tunaposherehekea Bwana aliyefufuka. Ibada yetu inapaswa kujumuisha fursa za kusherehekea.

Ibada inajumuisha nyimbo za sifa na shuhuda za neema ya Mungu katika maisha ya washiriki. Kanisa moja nchini Nigeria husherehekea wanapotoa sadaka. Washiriki

[31] Kwa mfano: 6:1-7:8 yapo duniani; 7:9-8:6 ni mbinguni. 8:7-11:14 ni duniani; 11:15-19 ni mbinguni.
[32] David Jeremiah. *Worship*. (CA: Turning Point Outreach, 1995), 72

huandamana kuzunguka kanisa sadaka inapo kusanywa. Waabudu hawa wanajua furaha ya Ufufuo. Ibada lazima ijumuishwe na fursa za kusherehekea ushindi tuliopata kupitia ushindi wa Kristo juu ya kifo.

### Kujipima

Jiulize, "Je, ibada yangu ni sherehe au ni wajibu tu? Je, ninafurahia kuingia kwenye ibada, au nahudhuria ibada kwa sababu tu ni wajibu wangu kama Mkristo?"

### Weka katika Vitendo

"Chukua muda kutafakari juu ya Mungu tunayemwabudu. Fikiria kile maandiko yanayotuambia kumhusu."[33]

| Mungu ni Nani katika Maandiko | |
|---|---|
| Katika Mwanzo | Yeye ni Muumba wa Ulimwengu. |
| Katika Kutoka | Yeye ni Mwanakondoo wa Pasaka. |
| Katika Mambo ya Walawi | Yeye ni Dhabihu Kamilifu |
| Katika Hesabu | Yeye ni Wingu |
| Katika Kumbukumbu la Torati | Yeye ni Nabii wa Kweli. |
| Katika Yoshua | Yeye ni Jemadari wa Jeshi la Bwana |
| Katika Ruthu | Yeye ni Mkombozi wa Ukoo. |
| Katika 1 na 2 Samweli | Yeye ni Nabii. |
| Katika Mambo ya Nyakati | Yeye ni Hekalu la Mbinguni |
| Katika Ayubu | Yeye ni Mpatanishi |
| Katika Zaburi | Yeye ni Mchungaji. |
| Katika Isaya | Yeye ni Mkuu wa Amani. |
| Katika Ezekiel | Yeye ni Mwana wa Adamu. |
| Katika Hosea | Yeye ni Mponyaji wa Wale Wanaorudi Nyuma. |
| Katika Hagai | Yeye ni Tamaa ya Mataifa Yote |
| Katika Malaki | Yeye ni Jua la Haki. |

[33] Jedwali lifuatalo limechukuliwa kutoka kutoka kwaVernon Whaley, *Called to Worship.* (Nashville: Thomas Nelson, 2009), 331-333.

| | |
|---|---|
| Katika Mathayo | Yeye ni Masiya Aliyeahidiwa. |
| Katika Marko | Yeye ni Mtumishi. |
| Katika Luka | Yeye ni Mwana wa Adamu. |
| Katika Yohana | Yeye ni Neno. |
| Katika Warumi | Yeye ni Yule Anayehesabia Haki. |
| Katika Wafilipi | Yeye ni Furaha Yetu. |
| Katika Wakolosai | Yeye ni Utimilifu wa Uungu. |
| Katika Waebrania | Yeye ni Kuhani Mkuu. |
| Katika 1 & 2 Petro | Yeye ni Mchungaji Mkuu wa Kondoo |
| Katika Ufunuo | Yeye ni Mwanakondoo Aliyechinjwa, Mfalme wa Wafalme, na Bwana wa Mabwana! |

**Hitimisho: Ushuhuda wa Mtume Yohana**

Jina langu ni Yohana. Maisha yangu yamebadilishwa na ibada. Tangu nilipokutana na Yesu wa Nazareti kwa mara ya kwanza, nimekuwa mwabudu.

Nilikuwepo kwenye Mlima wa Mabadiliko. Tulisikia sauti kutoka mbinguni, tukaona utukufu wake, na tukaanguka kifudifudi kwa hofu (Mathayo 17:6). Tuliabudu bila ukamilifu. Matendo yetu wakati wa Wiki ya Mateso yalionesha kwamba hatukuelewa kabisa yale tuliyoona mlimani.

Nilikuwepo mlimani Galilaya Yesu alipoonekana baada ya kufufuka. Tuliabudu, ingawa wengine walikuwa na mashaka (Mathayo 28:17). Tuliabudu kusiko na kamilifu. Tulijua kwamba amefufuka, lakini hatukuwa tumeelewa kikamilifu maana yake yote.

Nilikuwepo katika chumba cha juu tulipojitolea kwa maombi kwa moyo mmoja (Matendo ya Mitume 1:14). Tulipoabudu, Roho Mtakatifu alitujia. Ibada ikawa kichocheo cha uinjilisti; tulipeleka injili Yerusalemu, Yudea na Samaria, na hata mwisho wa dunia.

Nilipokuwa uhamishoni katika kisiwa cha Patmo, nilikuwa katika Roho siku ya Bwana niliposikia sauti kuu kama tarumbeta. Ilikuwa sauti ya Alfa na Omega, wa kwanza na wa mwisho (Ufunuo 1:10-11).

Nilikuwepo wakati Mungu alipofungua mlango mbinguni na kuniruhusu kuona ibada kuzunguka Kiti cha Enzi cha Mungu.

Nitakuwa milele katika Yerusalemu mpya, ikishuka kutoka kwa Mungu kutoka mbinguni (Ufunuo 21:2). Katika mji huo, ibada yetu hatimaye itakuwa kamilifu kwa sababu tutauona uso wa Yule tunayeabudu. Mbinguni, "maskani ya Mungu ni pamoja na wanadamu, naye

atafanya maskani yake pamoja nao, nao watakuwa watu wake. Naye Mungu mwenyewe atakuwa pamoja nao” (Ufunuo 21:3).

Mimi ni Yohana. Na nitatumia umilele wote kumwabudu Mungu wangu na Mkombozi wangu!

### Weka katika Vitendo

Kabla ya kumaliza somo hili, chukua muda kuabudu. Soma nyimbo za Ufunuo 4, 5, na 15 au Zaburi 19. Imba wimbo unaomsifu Mungu. Omba maombi ya kumsifu Mungu. Sikiliza Mungu anapozungumza nawe. Chukua muda wa kumwabudu Mungu hasa.

### Majadiliano ya kikundi

► Kwa matumizi ya vitendo vya somo hili, jadilini yafuatayo:

*Tim anachunga kanisa ambalo lina shauku kubwa ya uinjilisti. Waamini wapya wanabatizwa kila mwezi. Ni wakati wa kusisimua katika kanisa.*

*Hata hivyo, Tim anahofia kwamba kanisa halijaabudu hasa. Mahubiri mengi yanalenga wasioamini na waongofu wapya. Ni vigumu kutumia nyimbo kuu za kitabuni kwa sababu watu wapya hawazijui nyimbo hizo. Tim anaogopa kwamba kanisa lake litakuwa kubwa kwa ukubwa lakini lina kina kidogo kiroho. Anataka kujikita zaidi kwenye ibada. Jadili jinsi Tim anavyoweza kudumisha msisitizo wa uinjilisti huku pia akikuza kina cha ibada katika kanisa.*

**Mapitio ya Somo la 4**

(1) Injili zinaonesha kwamba ibada inakamilishwa katika Yesu Kristo:

- Yesu alitoa mfano wa ibada.
- Yesu alikataa majaribu ya ibada ya uongo.
- Yesu alionyesha umuhimu wa maombi.
- Yesu ataabudiwa milele.

(2) Matendo ya Mitume yanaonesha uhusiano kati ya ibada na uinjilisti.

- Ibada ya kweli inachochea uinjilisti.
- Uinjilisti wenye ufanisi huunda waabudu.
- Ibada ambayo haituongozi kwenye uinjilisti itakuwa ya kujishughulisha binafsi.

(3) Nyaraka zinaonesha vipengele muhimu vya ibada katika kanisa la kwanza. Ibada katika kanisa la kwanza ilijumuisha:

- Kusoma Maandiko
- Kuhubiri Neno
- Maombi ya pamoja
- Kuimba
- Sadaka
- Ubatizo
- Meza ya Bwana

(4) Ufunuo unaonesha kwamba ibada ni kumsifu Mungu.

- Ibada inabariki mwabudu, lakini hiyo si lengo kuu la ibada.
- Lengo kuu la ibada ni kumletea Mungu heshima.
- Ibada ya mbinguni inatukumbusha kwamba dunia tunayoiona haina ukweli wa mwisho.

**Somo la 4 Mazoezi**

(1) Orodhesha kanuni tatu za ibada kutoka somo hili. Kwa kila kanuni, andika aya moja ikijadili njia za vitendo za kutumia kanuni hiyo katika kanisa lako.

(2) Mwanzoni mwa somo lijalo, utapewa mtihani unaotokana na somo hili. Soma maswali ya mtihani kwa makini ili kujiandaa.

**Jaribio Somo la 4**

(1) Orodhesha njia tatu ambazo Yesu alionesha ibada ya kweli.

(2) Mafundisho na mfano wa Yesu yanatukumbusha nini kuhusu ibada ya kweli?

(3) Kauli mbili zinazofupisha uhusiano kati ya ibada na uinjilisti ni zipi?

(4) Ibada ya uongo ya Athene inaelezwaje katika Matendo 17?

(5) Mungu wa kweli anaelezwaje katika Matendo 17?

(6) Orodhesha vipengele vitano vya ibada ya kanisa la kwanza katika Nyaraka.

(7) Orodhesha mifano miwili ya vizuizi vya ibada vilivyopatikana miongoni mwa makanisa ya Asia Ndogo.

(8) Andika Warumi 12:1-2 kwa kukariri.

# Somo la 5
# Ibada Katika Historia Ya Kanisa

## Malengo ya Somo

Mwisho wa somo hili, mwanafunzi anapaswa:

(1) Kuheshimu tofauti kati ya mila mbalimbali za Ibada.

(2) Kuelewa tofauti kati ya kanuni zisizobadilika za ibada na kubadilisha desturi za ibada.

(3) Kutambua kwamba ibada huakisi imani zetu za kitheolojia na pia huathiri imani hizo.

(4) Kutumia masomo kutoka katika ibada ya mapokeo mbalimbali ya kanisa kuabudu leo.

## Matayarisho kwa somo hili

*Kariri Zaburi 100:1-5.*

## Utangulizi

James anathamini ibada ya kimapokeo. Katika mkutano wao wa kila mwezi Enoch, ambaye anaongoza ibada ya kisasa, aliuliza, "Kwa nini usijaribu jambo jipya katika ibada zako?"

"Sisi ni wa kibiblia," James alijibu. "Ikiwa Biblia haiamuru desturi fulani ya kuabudu, hatuko huru kuiongeza tu kwenye mazoea ya ibada ya kanisa la kwanza. Sisi ni nani kubadili ibada ya kibiblia? Katika kanisa letu, tunaimba zaburi pekee. Nyimbo hizo zilikuwa nyimbo za kanisa la kwanza; zinatufaa!"[34]

Enoch alijibu, "Inaonekana kwangu kana kamba unadhani historia ilikoma mwishoni mwa kitabu cha Ufunuo. Je, tunawezaje kujizuia na mtindo wa kuabudu ambao una miaka 2,000? Maadamu Biblia haijazuia desturi fulani, na desturi hiyo haigawanyi kanisa, tunapaswa kurekebisha ibada kulingana na mahitaji ya kizazi chetu. Katika kanisa langu, tunaimba nyimbo nyingi mpya. Kama Mungu angependa kuzuia nyimbo mpya, Biblia ingekataza waziwazi."[35]

Jibu la Jason lilikuwa la vitendo. "Tumejifunza yale ambayo Biblia inasema kuhusu ibada. Tunajua kanuni za ibada kutoka kwenye Maandiko. Tunahitaji kuona jinsi Wakristo wengine wametumia kanuni hizi katika kila kizazi. Je, ibada inaonekanaje katika historia ya kanisa?"

---

[34] Hii inaitwa "kanuni ya udhibiti" ya ibada. Iliyofundishwa na John Calvin, inakataza mazoea yoyote ya kuabudu ambayo hayajaanzishwa katika Maandiko. Hapo awali, hii ilizuia muziki wowote wa ala za muziki (kwakuwa ala za muziki hazijatajwa katika ibada ya Agano Jipya) au matumizi ya nyimbo zozote isipokuwa Zaburi. Baadhi ya makanisa yanayofuata kanuni hii leo yameongeza ala za muziki na nyimbo; lakini wanaendelea kuepuka mbinu mpya zaidi za kuabudu.

[35] Hii inaitwa "kanuni ya kawaida" ya ibada. Mbinu hii inafundisha kwamba ibada zozote ambazo hazijakatazwa katika Maandiko zinaruhusiwa, mradi tu hazivurugi amani na umoja wa Kanisa.

Jason anaelewa kanuni muhimu tunapojadili ibada. Ingawa kanuni za kibiblia za kuabudu hazibadiliki, kila uzoefu wa ibada katika Biblia ni tofauti. Maelezo yanatofautiana; vipengele muhimu vya ibada vinabaki vile vile. Tumeona kanuni muhimu za ibada katika masomo mawili yaliyopita, lakini maelezo yanabadilika. Zingatia:

- Ibrahimu alikuwa kwenye mlango wa hema lake alipokuwa akiabudu. Mtu anaweza kusoma hii na kusema, "Ibada ya kweli huanzia ukiwa nyumbani." Lakini …
- Isaya alikuwa Hekaluni alipomwona Bwana akiinuliwa. Mtu anaweza kusoma hii na kusema, "Ibada ya kweli hutokea ukiwa kanisani." Lakini …
- Ayubu alifunikwa na majipu kuanzia kichwani hadi miguuni aliposema, "Nilikuwa Nimesikia habari zako kwa kusikia kwa masikio, bali sasa jicho langu linakuona" (Ayubu 42:5). Mtu anaweza kusoma hii na kusema, "Aha! Ibada ya kweli hutokea ukiwa na huzuni."

Je, unaona hoja? Ibada hufanyika katika hali nyingi tofauti, kwa njia nyingi tofauti, na kufuata mifumo mingi tofauti. Mara nyingi tunachanganya mabadiliko ya hali ya ibada na kanuni zisizobadilika.

Katika somo hili, tutaona jinsi kanisa limetumia kanuni za ibada katika historia. Hilo litakupa ufahamu wa njia mbalimbali ambazo watu wa Mungu huabudu. Tunatumahi hii itakusaidia kuona kwamba hakuna mtindo mmoja wa ibada ambao lazima ufuatwe na watu wote katika hali zote. Badala yake, lazima tutafute mwongozo wa Roho wa Mungu ili kuamua jinsi ya kutumia kanuni za kibiblia za ibada kwa hali yetu.

Katika somo hili, tutaona pia jinsi ibada zetu huakisi imani zetu. Mazoea yetu ya ibada huathiriwa na imani yetu kuhusu Mungu na jinsi tunavyomfikia.

Ufahamu huu ni muhimu unapofanya maamuzi kuhusu ibada. Je, unaendesha ibada yako kwa njia inayowasilisha imani yako, au unaiga tu muundo wa kanisa lingine? Ikiwa unaiga kanisa lingine, lazima uhakikishe kwamba unashiriki imani ya kanisa hilo kuhusu Mungu na jinsi tunavyomfikia. Kuabudu kwetu kunaonyesha kile tunachoamini.

► Kabla ya kuendelea na somo hili, jadili huduma zako za ibada za sasa. Kama mtu hajui chochote kuhusu mafundisho yako, je, mtindo wako wa ibada ungezungumza nini kwao? Wangejifunza nini kuhusu mtazamo wako kwa Mungu, mtazamo wako kuhusu uhusiano wetu na Mungu, na mtazamo wako wa uinjilisti kama matokeo ya huduma yako ya ibada?

## Picha ya Ibada katika Karne ya Pili

Picha yetu ya kwanza ya ibada baada ya Agano Jipya inakuja katika barua kutoka A.D. 113. Pliny, gavana wa Bithinia, alielezea ibada ya Kikristo katika barua kwa Mfalme Trajan.[36] Aliandika kwamba Wakristo, "hukusanyika siku iliyotajwa kabla ya mapambazuko na

[36] Pliny, *Letters 10.96-97*, Imetolewa kutoka https://faculty.georgetown.edu/jod/texts/pliny.html mnamo Januari 26, 2023.

kuimba kwa kupokezana wimbo kwa Kristo kama kwa mungu, na kwamba waape… Usiibe, usidanganye, wala usizini …. Ni kawaida yao kuachana na kurudi baadaye kula chakula pamoja.”

Kulingana na Pliny, Wakristo walikutana kabla ya jua kuchomoza siku ya Jumapili ili kuimba nyimbo na kuahidi maadili mema, pengine kwa kuitikia usomaji wa Maandiko. Baadaye mchana, walikula chakula, ambacho huenda kilijumuisha meza ya Bwana.

Miaka arobaini baadaye, Justin mfia dini alitoa maelezo ya kina zaidi kuhusu ibada.[37] Justin aliandika ili kutetea ibada ya Kikristo kwa mfalme wa kirumi ambaye aliwatuhumu Wakristo kwa ukosefu wa maadili na ukosa uaminifu kwa mfalme. Justin alimhakikishia mfalme kwamba ibada ya Kikristo haikuwa tishio kwa Warumi. Kulingana na Justin, ibada ya Kikristo ilijumuisha mambo yafuatayo:

1. **Usomaji wa Maandiko.**
2. **Mahubiri kutoka kwa Kiongozi wa Kutaniko.**
3. **Maombi.** Watu binafsi waliomba kimya kimya; kisha kiongozi akaongoza maombi rasm, ambayo watu waliitikia, “Amina.” Mwisho wa maombi, waumini walisalimiana kwa busu takatifu kuashiria uwepo wa Roho Mtakatifu.
4. **Ibada ilihitimishwa kwa kushiriki meza ya Bwana.** Baada ya ibada, mashemasi wawili walichukua mikate na divai iliyobaki na kupeleka kwa Wakristo waliokuwa wagonjwa au waliokuwa gerezani wakingoja kuuawa.
5. **Mwishoni mwa ibada, wale waliokuwa na pesa au chakula walileta zawadi zao kwa kiongozi.** Sadaka zilipelekwa kwa “mayatima na wajane, walio na uhitaji kwa sababu ya ugonjwa au sababu nyingine yo yote, na wafungwa na wageni kati yao.”

Moja ya nguvu za ibada ya karne ya pili ilikuwa ushiriki wa waumini. Wote wawili Pliny na Justin Martyr wote walielezea ibada rahisi, itofauti kabisa na mila ya kitamaduni iliyoenea katika dini za siri za kipagani za Rumi. Ibada ilikuwa ya kina, huku vikundi vidogo vilipokusanyika katika nyumba za watu.

Nguvu nyingine ilikuwa uhusiano wa wazi kati ya ibada na maisha. Barua ya Pliny inataja kujitolea kwa Mkristo kuhusu tabia ya maadili; Justin Martyr anataja zawadi za kuwasaidia wahitaji. Ibada ilihusisha maisha yote.

► Ni mambo gani ya ibada katika karne ya pili yanaweza kunufaisha ibada yako? Je, unaona hatari yoyote katika ibada ya karne ya pili?

---

[37] Justin Martyr, (Translated by Marcus Dods), *The First Apology of Justin* (Chapter 67). Imechukuliwa kutoka https://en.wikisource.org/wiki/Ante-Nicene_Christian_Library/The_First_Apology_of_Justin_Martyr#Chapter_67 mnamo Januari 26, 2023

## Picha ya Ibada katika Zama za Kati

Kwa ajili ya picha ya pili ya ibada, nenda kwenye karne ya 12. Katika miaka iliyofuata, Ukristo ulikuwa dini rasmi ya Dola Takatifu ya Rumi. Baada ya Amri ya Konstantino ya Milan mwaka 313 B.K., waumini walianza kujenga majengo makubwa ya kanisa. Makanisa mengi makubwa ya Ulaya yalijengwa wakati wa miaka hii 1,000.

Katika zama za Kati, ibada ilizidi kuwa kubwa. Kwa upande mzuri, ibada ya kanisa kuu ilionyesha ukuu wa Mungu. Dirisha za vioo vya rangi zilionyesha matukio ya kibiblia kwa wale ambao hawakuweza kusoma. Kwaya ziliimba nyimbo nzuri. Ibada ilikuwa ya ajabu na nzuri.

### Udhaifu wa Ibada katika Zama za Kati

***Urembo ulikuwa muhimu zaidi kuliko hali ya kiroho.***

Matumizi wa mambo yenye kupendeza kwa ajili ya ibada ulitiliwa mkazo: uvumba, muziki wa fahari ulioimbwa na waimbaji waliofunzwa, kengele, na mavazi ya pekee kwa ajili ya makuhani. Sanaa ikawa muhimu zaidi kuliko ya kiroho.

***Watu hawakuweza kuelewa Ibada.***

Ibada hiyo ilikuwa katika Kilatini, lugha ambayo watu wachache waliielewa. Wachungaji wengi wa eneo hilo hawakuzoezwa sana kuhubiri mahubiri. Maombi yalikuwa ni sehemu ndogo ya vifungu kutoka vyanzo vingi tofauti na mara nyingi havikuwa vinaeleweka.

***Watu walikuwa watazamaji, si waabudu halisi.***

Kulikuwa na ushiriki mdogo wa watu. Waumini walikuwa kundi la watazamaji waliokuwa wakitazama tamthilia, yaani Misa. Makasisi walikuwa wakitekeleza matukio ya ibada huku hadhira ikitazama. Kitovu cha ibada kilikuwa Ushirika Mtakatifu badala ya Maandiko Matakatifu.

Kanisa Katoliki lilifundisha kwamba mkate na divai viligeuzwa kuwa mwili na damu halisi ya Kristo (Hili linaitwa fundisho la kugeuka kwa mkate na divai). Watu wengi wa kawaida walifanya meza ya Bwana tu wakati wa Pasaka pekee. Kuhani alikunywa divai na kushiriki mkate tu na waumini.

***Injili ilibadilishwa na taratibu.***

Ibada zetu hutengeneza imani zetu. Tunaona kanuni hii ikifanya kazi katika Zama za Kati; Ibada ya Kikatoliki ya Kirumi ilitengeneza theolojia yao. Mungu alionekana kuwa mbali na maisha ya wanadamu. Watu wa kawaida hawakuhisi wanaweza kumkaribia Mungu; badala yake, waliweza kuzungumza na Mungu kupitia kuhani pekee. Kuhani akawa mpatanishi kati ya Mungu na mwanadamu.

Nguvu ya ibada katika Zama za Kati ilikuwa katika hali yake ya ukuu na hofu mbele za Mungu. Kupitia usanifu wa majengo, muziki, maigizo, na sanaa nzuri, ibada ilidhihirisha utukufu wa Mungu.

Hata hivyo, udhaifu wa ibada katika Zama za Kati ulizidi nguvu zake. Mkristo wa kawaida alikuwa mtazamaji tu katika ibada. Kwa njia nyingi, ibada ya Zama za Kati ilikuwa ni mkengeuko wa kusikitisha kutoka kwa ibada ya Agano Jipya.

### Hatari za Ibada: Ibada Isiyo na Maana

Ni lazima tuchukue muda kufundisha waumini wetu kwa nini tunaabudu jinsi tunavyofanya, vinginevyo mapokeo yenye maana yanaweza kuonekana kuwa hayana maana kwa waabudu.

Muumini mmoja mpya alimuuliza mchungaji wake, "Kwa nini tunasema 'Amina' mwishoni mwa maombi? Je, 'Amina' ni neno la miujiza linalomfanya Mungu afanye tunachomwomba?" Mchungaji alitambua kwamba anapaswa kutoa melezo kuhusu ibada. Kitu rahisi kama "Amina" kinaweza kukosa maana ikiwa hatufundishi waumini wetu kuhusu ibada.

Sio lazima kuondoa ishara na siri kwenye ibada. Suluhisho ni kufundisha waumini maana ya mazoea yetu kuhusu ibada. Wanapaswa kujua kwa nini tunatumia lugha tunayotumia; wanapaswa kujua kwa nini uimbaji wa pamoja kanisani ni muhimu kwa waumini; wanapaswa kujua nini maana ya Maandiko.

► Ni mambo gani ya ibada katika Zama za Kati yanaweza kunufaisha ibada yako? Je, unaona hatari yoyote katika ibada ya Zama za Kati?

### Picha ya Ibada katika Matengenezo ya Kanisa

Wanamatengenezo walijua kuwa ibada yetu inaathiri theolojia yetu. Kwa sababu hii, walijua kwamba kweli za kitheolojia za matengenezo zingepotea kama ibada isingeakisi theolojia ya matengenezo.

Jambo kuu la kitheolojia la Wanamatengenezo lilikuwa ni ukuhani wa mwamini. Hii ina maana kwamba waumini wanamwabudu Mungu moja kwa moja; hatupitii kwa kuhani. Wanamatengenezo pia waliamini sana kwamba Neno la Mungu lazima lipatikane kwa kila mwamini.

Ibada katika Matengenezo ya Kanisa ilihusisha kila mwabudu. Ibada ilikuwa katika lugha ya watu, si Kilatini. Maandiko yalisomwa na kuhubiriwa ili waabudu wote waweze kuelewa Neno la Mungu katika lugha yao wenyewe. Wimbo wa waumini uliruhusu kila mwabudu kushiriki katika ibada. Martin Luther alikuwa mwandishi wa nyimbo, na nyimbo zake zinahesabiwa kuwa zilisaidia kueneza Matengenezo ya Kanisa.

Zaidi ya maeneo haya ya kawaida, kulikuwa na kutokubaliana kwingi kati ya Wanamatengenezo kuhusu ibada. Walutheri na Waanglikana walidumisha sehemu kubwa ya sherehe za Kanisa Katoliki la Roma. Luther aliamini kwamba, isipokuwa kama

yamekatazwa katika Maandiko au yalileta migogoro kanisani, desturi mpya ya kuabudu zinapaswa kuruhusiwa.

Kelvin na wafuasi wake walishikilia baadhi ya taratibu lakini walikataa desturi za ibada ambazo hazijazungumziwa haswa katika Maandiko. Kelvin alihimiza uimbaji wa waumini, lakini uimbaji wa zaburi pekee. Aliamini kwamba "Neno la Mungu pekee ndilo linalostahili kuimbwa katika sifa za Mungu."[38] Alirudi kwenye Ibada ya Ushirika ya waumini, akipendekeza kwamba Meza ya Bwana iandaliwe angalau mara moja kwa mwezi na ikiwezekana kila jumapili.

Waanabaptisti na Wapuritani walikataa sehemu kubwa ya taratibu na kurejea kwenye aina rahisi ya ibada. Wakati mwingine watu hawa waliabudu katika nyumba za kibinafsi na kujiona kuwa wao pekee ndio hufuata ibada ya karne ya kwanza kwa usahihi.

Nguvu ya ibada ya Matengenezo ilikuwa ni kurudi kwa ushiriki wa waumini. Ingawa kulikuwa na tofauti kati ya makanisa mbalimbali ya Matengenezo, Wanamatengenezo wote walitafuta kuiga ukuhani wa mwamini katika ibada.

► Ni mambo gani katika ibada ya matengenezo yanaweza kunufaisha ibada yako? Je, unaona hatari yoyote katika ibada ya Matengenezo ya Kanisa?

## Picha ya Ibada Katika Makanisa Huru

Kufuatia Matengenezo ya Kanisa, makanisa fulani yalikataa udhibiti wa serikali. Makanisa haya, yanayoitwa "makanisa huru" yalihusisha Anabaptisti, Wapuriti, Wasiofuata kanuni, Wanaojitenga, na Waasi. Wengi wao pia walikataa liturujia na taratibu zilizowekwa.

Vipengele vya ibada ya Makanisa huru:

**(1) Kuhubiri kulikuwa kwa sehemu kubwa.**

**(2) Ushiriki wa waumini ulikuwa muhimu.**

Asili ya ushiriki wa waumini ulitofautiana kutoka kanisa hadi kanisa.

- Katika baadhi ya makanisa, waumini waliimba nyimbo. Katika makanisa mengine, hakukuwa na uimbaji katika ibada ya pamoja.
- Katika baadhi ya makanisa washirika wa ibada waliomba kwa sauti. Katika makanisa mengine padri aliomba kwa niaba ya watu.

Kulikuwa na tofauti ndogo kati ya waumini wa kawaida na viongozi wa kidini. Makanisa mengi ya huru hayakuwa na nguo maalumu za viongozi wa kidini.

[38] Imenukuliwa kwa Donald P. Hustad, *Jubilate II* (Carol Stream: Hope Publishing Company, 1993), 194.

**(3) Ibada yote ilikuwa katika lugha ya watu.**

Muhtasari wa ibada mnamo 1608 ni pamoja na yafuatayo (ibada ilidumu kwa masaa manne):

- Maombi
- Usomaji wa Maandiko (Sura ya 1-2 zenye maelezo)
- Maombi
- Mahubiri (ya saa moja au zaidi)
- Michango inayozungumzwa na waumini wa kawaida
- Maombi
- Sadaka

Ibada haikutawaliwa tena na komunio na kuhani. Ibada za makanisa huru zilionekana zaidi kama ibada ya kanisa la Agano Jipya.

Kuna hatari katika njia hii ya ibada. Ijapokuwa makanisa huru yalifundisha ukuhani wa mwamini, katika vitendo mhubiri mara kwa mara alichukua nafasi ya padri kama kitovu cha ibada. Katika baadhi ya makanisa, kulikuwa na ushiriki mdogo wa waumini.

Labda moja ya hatari kubwa zaidi katika ibada ya makanisa huru ilikuwa hatari ya ubinafsi uliokithiri. Iwapo fundisho la ukuhani wa mwamini haliambatani na fundisho la umoja wa kanisa, kanisa linakuwa mkusanyo wa watu binafsi badala ya mwili wa Kristo uliounganishwa katika ibada. Hii inaonekana wakati ibada inahusu "Yesu na mimi" tu bila maana ya kanisa kama mwili.

► Ni vipengele vipi vya Ibada katika makanisa huru vinaweza kunufaisha ibada yako? Je, unaona hatari yoyote katika ibada ya makanisa huru?

## Picha ya Ibada katika Uamsho wa Wesley

John Wesley aliathiriwa na mapokeo ya ibada ya pamoja aliyopokea kutoka kwa kanisa la Anglikana na pia kwa msisitizo wa uzoefu wa binafsi wa kiroho aliopata kupitia mapokeo ya Anabaptisti. Wakati ibada ya Anglikana ilipokuwa inafuata Kanisa Katoliki la zama za kati katika ibada zisizo na maana, Wesley na wafuasi wake (walioitwa Wamethodisti) walihuisha uhalisia wa ibada ambao uliwaleta waabudu mbele ya Mungu.

Vipengele vikuu vya ibada ya wamethodist wa mwanzo:

1. **Kuhubiri.** Kuhubiri ya John Wesley yalichapishwa na kuwa msingi wa mafundisho kwa waabudu wa Methodisti.

2. **Ushirika wa mara kwa mara.** John Wesley alishiriki meza ya Bwana wastani wa mara tano kwa wiki. Aliwahimiza wafuasi wake kushiriki meza ya Bwana angalau mara moja kwa wiki.

3. **Kuimba nyimbo za dini.** Nyimbo za Charles Wesley zilieneza mafundisho ya Kimethodisti kupitia Visiwa vya Uingereza na Ulimwengu Mpya.

4. **Vikundi vidogo.** Mikutano ya darasa ilikuwa muhimu kwa ufuasi wa Kimethodisti.

5. **Ibada ya ushirika.** Wamethodisti walikutana pamoja mara kwa mara, na hata baada ya wachungaji wengi wa Kianglikana kuwakataa Wamethodisti, Wesley aliwahimiza wafuasi wake kuhudhuria ibada ya Kianglikana.

6. **Uinjilisti.** Maelfu ya waongofu wapya walimpokea Kristo wakati uamsho wa Kimethodisti ulipoenea kupitia Uingereza na kwingineko.

Ibada ya Kimethodisti ilijumuisha nyimbo ambazo zilimtukuza Mungu, uanafunzi uliojenga waumini waliokomaa, na kuhubiri ukweli uliotangaza kwa kanisa na kwa ulimwengu wenye uhitaji.

► Ni vipengele vipi vya ibada katika uamsho wa Wesley vinaweza kunufaisha ibada yako? Je, unaona hatari yoyote katika ibada ya uamsho wa Wesley?

**Umethodisti na Ibada ya Karne ya Kumi na Nane**

Umethodisti ulizuka kutokana na kushindwa katika ibada ya karne ya kumi na nane.

"Sakramenti zilipokuwa pembeni
mwa maisha ya kanisa,
umethodisti wa kwanza iliwaweka kwenye
kituo; wakati bidii ya kidini ilikuwa
inapuuzwa, umethodisti alifanya
hamasa kuwa muhimu; mbapo
dini ilikuwa imezuiwa kwenye
makanisa, Umethodisti uliipeleka
mashamba na mitaani."

- James White katika Robert Webber
*Karne Ishirini za Ibada ya Kikristo*

## Picha ya Ibada katika Amerika ya Kwanza

Waingereza walikaa kwanza kwenye pwani ya mashariki ya nchi ambayo sasa inaitwa Marekani. Mwishoni mwa miaka ya 1700 na zaidi, watu waliendelea kuhamia magharibi katika eneo lisilo na utulivu ili kupata ardhi na kujenga nyumba. Watu walikutana na changamoto nyingi kama vile makanisa, shule, na utekelezaji wa sheria ulivyoendelea polepole. Katika historia, eneo hili ambalo lilitatuliwa polepole linaitwa Frontier ya Amerika.

Kusudi la kujifunza kuhusu ibada katika historia ya awali ya Marekani sio kuunga hoja mtindo wa Marekani kuwa kielelezo cha ibada zote, lakini kuilinganisha na ibada zinazokua za makanisa machanga katika sehemu zingine. Changamoto zilezile zinakabiliwa na makanisa mapya yaliyoanzishwa katika nchi nyingi.

Vipengele vya ibada katika Marekani ya kwanza:

1. **Uhuru kutoka kwa madhehebu na aina rasmi za ibada**. Makanisa ya mpakani mwa Marekani yalikuwa huru dhidi ya udhibiti wa madhehebu. Yalikuwa na umakini mdogo kuhusu taratibu na maagizo maalum ya ibada (ingawa John Wesley alirekebisha mtindo wake wa kuabudu kwa matumizi katika makoloni). Majengo ya kanisa na huduma za ibada zilikuwa rahisi na wazi.

2. **Fursa adimu za meza ya Bwana.** Huko Uingereza, akina Wesley walikuwa wamesisitiza umuhimu wa ushirika wa kawaida. Katika mipaka ya Marekani,

upungufu wa mapadri waliowekwa rasmi ulionesha kwamba waumini walikuwa na nafasi ndogo ya kushiriki meza ya Bwana.

3. **Kuhubiri kwa Neno**. Kuhubiri kuliendelea kuwa mkazo wa kimsingi katika ibada. Hata wahubiri ambao hawajazoezwa walisoma mahubiri ya akina Wesley na wahudumu wengine. Kitovu cha kanisa kilikuwa mimbari, si meza ya Bwana. Mkazo mkubwa ulikuwa juu ya kuhubiri Neno.

4. **Kuimba kwa uchangamfu.** Kuimba kulikuwa kuchangamsha. Makanisa ya Marekani yaliimba nyimbo za Charles Wesley pamoja na nyimbo rahisi za ushuhuda kwa mtindo ambao ulikuwa rahisi kwa waumini wasio na elimu kujifunza.

5. **Maombi, uinjilisti, na uamsho.** Maombi hayakuwa rasmi na mara nyingi yaliongozwa na watu wa kawaida. Uinjilisti ulikuwa muhimu, na vipindi vya uamsho huko Marekani vilipelekea maelfu kuokoka. Mahubiri kwa kawaida yalifuatiwa na mwaliko kwa watu ambao hawajaokoka kujitokeza na kuomba sala ya toba. Msisitizo kuhusu utakatifu wa Kikristo ulienea Marekani kote, mwaliko uliwaita wasioamini kuokoka na waumini kujitakasa.

Kama ilivyo kwa mapokeo mengine, kulikuwa na uimara na hatari katika ibada hii. Uimara ulijumuisha ushiriki wamtu binafsi na shauku. Hatari ilijumuisha msisitizo kuhusu uzoefu wa kibinafsi na mkazo mdogo juu ya mafundisho. Ilikuwa rahisi kwa mafundisho ya uongo kuenea katika maeneo ya mipakani kwa sababu kulikuwa na uwajibikaji mdogo.

► Ni vipengele vipi vya ibada kwenye mpaka wa Marekani vinaweza kunufaisha ibada yako? Je, unaona hatari yoyote katika ibada ya kanisa la mpaka wa Marekani?

### Hatari za Ibada: Kuchanganya Mabadiliko ya Mitindo na Kanuni Zisizobadilika

Mara nyingi tunajaribiwa kuchanganya mitindo ya ibada inayobadilika na kanuni zisizobadilika za ibada ya kibiblia. Fikiria:

- Katika makanisa mengine, waabudu hupiga magoti kuonesha unyenyekevu wanaposali. Katika makanisa mengine, waabudu huinua mikono mitakatifu wanapoomba.

- Katika makanisa mengine, kinanda hupigwa kwa upole wakati wa maombi. Katika makanisa mengine, kuna ukimya wakati mchungaji anaongoza maombi. Katika makanisa mengine, kila mtu huomba kwa sauti.

- Katika makanisa mengine, nyimbo huoneshwa kwenye skrini. Katika makanisa mengine, watu huimba kutoka kwenye kitabu cha nyimbo.

- Katika makanisa mengine, mchungaji husoma maandiko mwanzoni mwa mahubiri yake. Katika makanisa mengine, mshirika husoma maandiko kabla ya mchungaji kuhubiri. Katika makanisa mengine, kuna usomaji wa maandiko mawili au matatu.

Hakuna moja kati ya haya lililo kosa; ni masuala ya mitindo, si kanuni. Hatupaswi kufikiria kwamba njia yetu ndiyo njia pekee ya kibiblia. Ibada ya kweli si suala la mtindo; ni uwepo wa Mungu.

Kuna kanuni fulani ambazo hazibadiliki. Tumeziona kanuni hizi katika masomo ya ibada katika Biblia. Kanuni hizi si za hiari. Kama Wakristo, kanuni hizi hutuelekeza katika njia yetu ya kumkaribia Mungu.

Katika masomo machache yajayo, tutatazama mitindo ya ibada. Kanuni hazibadiliki; mitindo hubadilika katika maeneo na nyakati tofauti. Kwa sababu hii, tunapaswa kuwa na uvumilivu kwa wale wanaoabudu tofauti na sisi. Hii haimaanishi kwamba mitindo si muhimu; bali inamaanisha kwamba kuna urahisi zaidi wa kubadilika kuhusu mitindo kuliko kuhusu kanuni.

Oswald Chambers aliandika kuhusu kumpa Mungu nafasi katika maisha yetu. Hii inahusu ibada:

> Kama watumishi wa Mungu, lazima tujifunze kumpa nafasi… Tunapanga, lakini tunasahau kumpa Mungu nafasi ya kuingia kama anavyochagua. Je, tutashangaa ikiwa Mungu atakuja kwenye mkutano wetu au kwenye mahubiri yetu kwa njia ambayo hatukuwahi kutarajia? Usimtafute Mungu aje kwa njia fulani, bali mtafute. Njia ya kumpa nafasi ni kumtarajia aje, lakini si kwa njia fulani...
>
> Weka maisha yako katika hali ya kuwasiliana na Mungu mara kwa mara ili nguvu zake za kushangaza ziweze kuvunja mipaka wakati wowote. Ishi katika hali ya kutarajia kila wakati, na mpe Mungu nafasi ya kuja kama anavyoamua.[39]

## Hitimisho: Taswira ya Ibada siku Hizi

Ibada inaonekanaje katika karne ya 21? Ni swali ambalo haliwezi kujibiwa kwa urahisi. Ibada katika karne ya 21 inachukua maumbo mengi tofauti. Makanisa mengine yanathamini desturi na mapokeo; makanisa mengine yanakataa desturi kwa ajili ya uhuru wa kibinafsi katika ibada.

► Ibada inaonekanaje katika kanisa lako? Ikiwa unasoma katika kikundi, jadilini tofauti na ufanano kati ya ibada katika makanisa yanayowakilishwa katika kikundi chenu.

Kwa wakati huu katika kozi hii, lengo la maelezo haya si tathmini. Swali si, "Je, tuko sahihi au tumekosea?" Swali ni rahisi, "Tunafanya nini katika ibada yetu?"

Sababu ya maelezo haya ni kuweka msingi kwa masomo yanayofuata. Mara baada ya kuwa na maelezo ya kile mnachofanya kwa sasa katika ibada, mnaweza kuanza kujiuliza, "Kwa nini tunafanya tunachofanya?" na "Tunawezaje kufanya vizuri zaidi?"

---

[39] Oswald Chambers, *My Utmost for His Highest* (January 25 entry). Imepakuliwa kutoka https://utmost.org/leave-room-for-god/ on July 22, 2020.

Maamuzi kuhusu ibada yanaakisi imani za kitheolojia. Vipengele katika ibada yetu vinaonesha tunachoamini kuhusu Mungu na jinsi tunavyohusiana naye; vipengele katika ibada yetu vinaonesha tunachoamini kuhusu kanisa na jinsi tunavyohusiana na kila mmoja; vipengele katika ibada yetu vinaonesha tunachoamini kuhusu waliopotea na jinsi ibada inavyoweza kuwafikia.

Hebu tuchukue mfano mmoja – kuimba kwa mkusanyiko.

- Kutokuwepo kwa kuimba kwa mkusanyiko katika Kanisa Katoliki la Roma kulionesha imani kwamba watu wa kawaida hawakuweza kuelewa maandiko (ikiwa ni pamoja na maandiko yaliyokuwa yakiimbwa). Kama vile mtu wa kawaida hakuruhusiwa kusoma maandiko mwenyewe, mtu wa kawaida hakuruhusiwa kuimba nyimbo za ibada. Ibada ilifanywa na kasisi.

- Mkazo wa kuimba kwa mkusanyiko wakati wa Matengenezo ulionesha imani ya Luther kwamba kila Mkristo anaweza kuabudu kama sehemu ya mwili wa Kristo.

- Kukataa kwa Calvin kuruhusu nyimbo zaidi ya zaburi kulionesha imani yake kwamba ni Neno la Mungu pekee ndilo lililokubalika katika ibada.

- Mkazo wa Wamethodisti katika kuimba kwa mkusanyiko na kufundisha mafundisho kupitia nyimbo ulionesha imani ya Wesleys kwamba kila muumini anapaswa kuimba na kwamba kile tunachoimba kinaathiri kile tunachoamini.

- Urahisi wa kuimba kwa waimbaji wa mipakani ulionesha imani ya Wamethodisti kwamba wokovu ulikuwa kwa watu wote. Kwa sababu ya imani hiyo, walihusisha kila mtu katika kuimba kwa shauku.

Tunapoendelea na kozi hii, tutakuwa tukitazama vipengele vingi vya ibada. Swali lako la kwanza kuhusu ibada huenda likawa, "Je, ninapenda?" Hilo si swali muhimu. La muhimu zaidi ni, "Ibada yangu inasema nini kuhusu kile ninachoamini? Je, inaonesha uelewa sahihi wa Mungu na uhusiano wa mwanadamu naye?"

Ibada yetu inaumba kile tunachoamini, lakini pia ni kweli kinyume chake: imani zetu zinaumba jinsi tunavyoabudu.

**Mapitio ya Somo la 5**

(1) Katika kanisa la kwanza:

- Ibada ilikuwa isiyo rasmi na ya yenye uhusiano.
- Ibada ilisisitiza ushiriki wa waumini wa kawaida.
- Ibada ilihusisha maisha yote.

(2) Katika ibada za Enzi za Kati:

- Uzuri ulikuwa muhimu zaidi kuliko uadilifu wa kiroho.
- Watu hawakuweza kuelewa huduma.
- Watu walikuwa watazamaji, sio waabudu wanaoshiriki.
- Injili ilibadilishwa na desturi.

(3) Katika Matengenezo:

- Ibada ilionesha ukuhani wa muumini.
- Ibada ilikuwa katika lugha ya watu.
- Luther, Calvin, na Wapuritani walitofautiana kuhusu jukumu la desturi katika ibada.

(4) Katika Makanisa Huru baada ya Matengenezo:

- Kuhubiri kulikuwa msingi.
- Ushiriki wa waumini ulikuwa muhimu.
- Mafundisho ya ukuhani wa muumini yalikuwa muhimu.
- Ibada yote ilikuwa katika lugha ya watu.
- Ubinafsi uliopitiliza ulikuwa hatari.

(5) Ibada za mapema za Wamethodisti zilitambulishwa na:

- Msisitizo kwenye kuhubiri.
- Msisitizo kwenye Ushirika wa mara kwa mara.
- Msisitizo kwenye kuimba nyimbo za kiroho.
- Msisitizo kwenye vikundi vidogo.
- Msisitizo kwenye ibada ya pamoja.
- Msisitizo kwenye uinjilisti.

(6) Ibada katika Amerika Mwanzoni:

- Ilikuza ushiriki binafsi na shauku ya uinjilisti.
- Wakati mwingine ilisisitiza uzoefu binafsi kwa gharama ya uadilifu wa mafundisho.

(7) Ibada yetu leo inaakisi imani zetu kuhusu Mungu na jinsi tunavyohusiana naye.

## Somo la 5 Mazoezi

(1) Katika karne ya pili, Justin Mfia dini aliandika kuhusu ibada ya kanisa kwa mtu ambaye hakuwahi kuona ibada ya Kikristo. Andika aya 2-3 ambazo utaelezea ibada kwa mtu ambaye hajawahi kuhudhuria kanisa la kikristo. Fikiria kwa makini ni nini cha muhimu kuhusu ibada. Je, unawezaje kuelezea ibada zako kwa namna ambayo utawasilisha kile kilicho cha muhimu katika ibada?

Kama unajifunza ukiwa katika kikundi, jadiliana kuhusu majibu ya kila mtu katika kikundi chenu katika darasa litakalofuata.

(2) Kuanzia mwanzo wa somo lijalo, utafanya mtihani uliojikita kwenye somo hili. Jifunze maswali ya mtihani kwa umakini katika maandalizi.

## Jaribio Somo la 5

(1) Orodhesha vipengele vitatu vya ibada ya karne ya pili vilivyoelezewa na Justin Martyr.

(2) Orodhesha udhaifu tatu wa ibada katika Zama za Kati.

(3) Shida kuu mbili za Matengenezo zinazohusiana na ukuhani wa waamini zilikuwa zipi?

(4) Tambua kikundi/vikundi katika Matengenezo vinavyolingana vyema na kila maelezo.

- Waruhusu matendo yoyote ya ibada ambayo hayajakatazwa katika maandiko: ________________
- Wasiruhusu matendo ya ibada ambayo hayajadiliwa katika maandiko: ________________
- Walikataa sherehe nyingi. Wakati mwingine waliabudu katika nyumba za kibinafsi: ________________

(5) Orodhesha sifa tatu za ibada ya kanisa huru.

(6) Orodhesha mambo matatu yaliyosisitizwa katika ibada za kwanza za Wamethodisti.

(7) Orodhesha sifa tatu za ibada katika Marekani ya kwanza.

(8) Andika Zaburi 100:1-5 kwa kukumbuka.

# Somo la 6
# Muziki katika Ibada

## Malengo ya Somo

Mwisho wa somo hili, mwanafunzi anapaswa:

(1) Kutambua sababu za kibiblia, kitheolojia na kivitendo za muziki katika ibada.

(2) Kuelewa kwamba muziki unazungumza na akili, moyo, mwili na hisia.

(3) Kujitolea kwa kanuni za kibiblia zinazoongoza uchaguzi wa muziki katika ibada.

(4) Kutumia kanuni za kibiblia kujibu maswali ya vitendo yanayohusiana na muziki katika ibada.

## Matayarisho kwa somo hili

*Kariri Wakolosai 3:15-17.*

## Utangulizi

Mathayo anataka kujiuzulu wadhifa wake wa uchungaji katika kanisa lake. Alifika katika Kanisa la Lakeside First akiwa na msisimko na matumaini makubwa. Anapenda kusoma na kuandaa mahubiri. Anafurahia kutembelea watu na kuleta faraja kwa wale wanaoumia. Anafurahi kupata fursa ya kuhubiri injili kwa wasioamini. Washirika wa kanisa lake wanapenda mahubiri yake. Washirika wapya wanaongezeka. Mathayo anapaswa kufurahi kama mchungaji. Lakini kuna kitu hakiko sawa. Na hii inatokana na mgogoro kuhusu muziki.

Kila Jumatatu asubuhi, Yosia hupiga simu kwenye ofisi ya kanisa. "Mchungaji, muziki wa jana ulikuwa mbaya! Sikuuelewa wimbo wa mwisho. Kibodi ilikuwa na sauti kubwa sana. Siwezi kustahimili. Inabidi ufanye kitu kuhusu muziki katika kanisa hili!

Mathayo hukutana na Thomasi kiongozi wake wa muziki kila jumanne. Thomas ana malalamiko tofauti. "Mchungaji mbona bado tunaimba nyimbo nyingi za kizamani? Wanakwaya wamechoshwa na nyimbo hizi. Jumapili, tuliimba nyimbo mbili za zamani na wimbo mmoja tu mpya. Kwa nini hatuwezi kuondokana na nyimbo hizi za vitabuni? Makanisa yote makubwa yamebadilika. Tafadhali niruhusu nibadilishe muziki!"

Kufikia Jumanne usiku, Mathayo anahisi kuacha kazi yake kwakuwa sehemu ya Kanisa la Lakeside First inapenda nyimbo za zamani; wanalalamika kila wimbo mpya unapoanzishwa. Sehemu nyingine ya Kanisa inachukia nyimbo za zamani; wanataka kuimba nyimbo za kusifu na kuabudu pekee. Mathayo hawezi kupata suluhu.

► Je, ushauri gani unaweza kumpa Mchungaji Mathayo? Je, mziki wa kanisa utahudumiaje kila kundi katika kanisa lake?

## Sababu Muhimu za Mziki katika Ibada

Katika mahojiano kuhusu mziki kanisani, mchungaji alisema, “hatuhitaj mziki katika ibada. Kama nitahubiri neno la Mungu kwa ufanisi, uimbaji sio lazima.” Mchungaji huyu hakuona thamani yeyote ya mziki katika ibada.

► Ungemjibu vipi huyu mchungaji? Je, kwa nini mziki ni muhimu katika ibada zetu?

Wakristo ni watu wa kuimba. Waislamu wanapokutana hawaimbi. Wabudha wakikutana hawaimbi. Wahindu wakikusanyika hawaimbi. Wakristo wakikusanyika huimba. Sio kila mkristo anahubiri, anaongoza maombi, au kusoma Maandiko katika ibada. Wakrsito wote wanapaswa kuimba. Hapa chini kuna sababu chache ambazo zinaonesha kuwa mziki ni muhimu katika ibada ya kikristo.

### Sababu za kibiblia za umuhimu wa mziki katika Ibada

Mziki ni muhimu katika Ibada kwa sababu ni muhimu katika Biblia. Kuna takribani rejea 600 za uimbaji na muziki katika Maandiko. Vitabu arobaini na nne vya Biblia hurejelea muziki.

Nyimbo za kibiblia zinahusu matukio mbali mbali:

- Waisraeli walimsifu Mungu kwa ushindi dhidi ya jeshi la Farao (Kutoka 15).
- Waisraeli walimsifu Mungu baada ya ushindi wa Debora dhidi ya Yabini (Waamuzi 5).
- Waimbaji waliabudu wakati wa kuwekwa wakfu kwa hekalu. (2 Nyakati 5:11-14).
- Waimbaji waliongoza ibada katika ujenzi wa Hekalu (Ezra 3:10-12).
- Kitabu cha Zaburi ni mkusanyo wa nyimbo za ibada ya Kiyahudi na Kikristo.
- Yesu na wanafunzi wake waliimba nyimbo wakati wa karamu ya mwisho (Mathayo 26:30).
- Paulo na Sila waliimba nyimbo za sifa gerezani (Matendo 16:22-25).
- Yohana aliona kuwa uimbaji ni sehemu ya ibada mbinguni (Ufunuo 4 and 5).

### Sababu za Kitheolojia za Muziki katika Ibada

Waabudu wa Kiyahudi waliimba walipokuwa wakiabudu. Wakristo wakwanza waliimba huku wakitoa shukrani za mioyo yao kwa Bwana (Wakolosai 3:16). Muziki ulikuwa ni sehemu muhimu ya ibada za kikristo.

Kwa bahati mbaya, wakati wa Enzi za Kati, nafasi ya muziki katika ibada ilibadilika. Makanisa yaliruhusu waumini kuimba nyimbo za sifa kwa nadra sana. Badala yake, waumini walitazama na kusikiliza wakati vikundi vya waimbaji waliobobea vikiimba nyimbo ngumu za sifa.

Martin Luther alirudisha muziki wa ibada kwa waumini. Muziki wa kusanyiko unaeleza kanuni ya kitheolojia ya **ukuhani wa mwamini**. Kanuni hii ilifundisha kwamba kila Mkristo anaweza kumwendea Mungu moja kwa moja; hatuhitaji kuhani kuwa mpatanishi kati yetu na Mungu. Hii ina maana kwamba kila muumini ana haki na wajibu wa:

- Kuomba moja kwa moja kwa Mungu.
- Kusikiliza Mungu akinena kupitia Neno lake.
- Kuimba katika ibada.

Martini Luther aliona uhusiano kati ya usomaji wa Maandiko na uimbaji. Alisema, "Acha Mungu aseme moja kwa moja na watu wake kupitia maandiko, na watu wake waitikie kwa nyimbo za shukrani za sifa."[40]

Kanuni ya pili ya kitheolojia inayoonyeshwa na muziki ni umoja wa kanisa. Marejeleo mengi ya kibiblia ya uimbaji ni uimbaji wa kusanyiko, uimbaji wa watu wote. Paulo aliwaamuru Wakristo wa kwanza kufundishana na kuonyana kwa wimbo (Wakolosai 3:16). Kanisa linapoimba pamoja, tunadhihirisha umoja wa kanisa.

### Hatari za Ibada: Kupotea kwa wimbo wa Kanisa

Wimbo mkubwa wa Isaac Watts unasema,

> "Wasiimbe wale ambao hawakumjua Mungu wetu,
> Lakini watoto wa Mfalme wa mbinguni na watangaze furaha yao duniani!".[41]

Martin Luther alisema, "Ikiwa yeyote hataimba na kuzungumza juu ya yale ambayo Kristo ametufanyia, anaonyesha kwamba haamini kabisa.[42] Fursa ya wimbo wa kanisa uliopotea katika Enzi za Kati ilirudishwa na Wanamatengenezo. Waliamini kuwa kuabudu kwa nyimbo ni mali ya watu. Cha kusikitisha ni kwamba katika makanisa mengi fursa hii inapotea tena.

Usemi wa kimuziki wa ukuhani wa mwamini unaharibika kutokana na muziki ambao haufahamiki kwa mwimbaji wa kawaida. Hii hutokea wakati kwaya zilizofunzwa zinaimba muziki ambao ni mgumu sana kwa watu wengi. Inatokea wakati timu za sifa huimba nyimbo mpya ambazo watu wachache wanaweza kujifunza. Hatupaswi kamwe kuruhusu vikundi vidogo kuchukua nafasi ya nyimbo za kanisa.

Usemi wa muziki wa umoja wa kanisa uko hatarini katika makanisa ambayo yanagawanya kusanyiko katika huduma tofauti kulingana na mitindo tofauti ya ibada au tofauti za vizazi. Ni vigumu kuona kanisa kama mwili mmoja wakati washirika wa muda mrefu wa kanisa hawazingatii washiriki wachanga.

---

[40] Imenukuliwa kwa David Jeremiah, *Worship* (CA: Turning Point Outreach, 1995

[41] Imetafsiriwa kutoka Kiingereza kwa kitabu hiki kutoka kwa Isaac Watts, "We're Marching to Zion." Accessed January 12, 2023. https://library.timelesstruths.org/music/Were_Marching_to_Zion/

[42] Imenukuliwa kwa Ronald Allen and Gordon Borror, *Worship: Rediscovering the Missing Jewel* (Colorado Springs: Multnomah Publishers, 1982), 165.

Hebu fikiria maelekezo ya Paulo kwa kanisa la Efeso yaliyotafsiriwa upya kwa baadhi ya makanisa ya kisasa.

- Wale wanaoimba zaburi watakutana Jumapili saa 2:30 asubuhi.
- Wale wanaoimba Nyimbo za vitabu watakutana Jumapili saa 5:00 asubuhi.
- Wale wanaoimba nyimbo za kiroho watakutana Jumamosi saa 1:00 Jioni.

Hapana! Paulo alikuwa anazungumza na washirika *wote* wa kanisa alipowasihi wajazwe na Roho, wakisemezana kwa zaburi na tenzi na nyimbo za kiroho, huku wakiimba na kumshangilia Bwana (Waefeso 5:18-19).

Katika vitendo, hii ina maana kwamba kila sehemu ya mwili wa Kristo inasalimisha baadhi ya mapendekezo yake kwa ajili ya umoja wa mwili. Kijana anaimba wimbo wa kitabu kwa tuni ambayo haisisimui sana. Na kwa sababu yeye ni sehemu ya mwili wa Kristo, kanisa pia wanaimba wimbo huo wa kitabu. Mzee pia anaanzisha wimbo mpya wa sifa ambao haufurahishi. Na Kwa sababu yeye ni sehemu ya mwili wa Kristo, na kanisa wanaimba wimbo mpya.

Mwanamuziki aliyefunzwa katika kanisa dogo la kijijini anaimba nyimbo ambazo hazina changamoto kimuziki. Kwa nini? Kwa sababu yeye ni sehemu ya mwili wa Kristo, na mwili wa Kristo unajumuisha washirika ambao hawafahamu muziki mzuri. Mshirika wa kanisa ambaye hana taaluma ya muziki anaweza kusema "Amina" mwishoni mwa wimbo unaoimbwa kwa mtindo ambao hauthamini kabisa. Kwa nini? Kwa sababu yeye ni sehemu ya mwili, na mwili unajumuisha washirika wanaoimba muziki zaidi ya uthamini wake.

Kanuni hii huenda mbali zaidi ya muziki. Mchungaji anayarahisisha mahubiri yake ili yaweze kueleweka kwa watoto na washirika wapya. Waumini wapya hujifunza ili kuelewa kifungu cha mahubiri ambacho kinafaikia uelewa wao mdogo wa Biblia.

Vijana huketi katika ibada ambayo inaonekana kuwa ndefu sana. Kwa nini? Kwa sababu wao ni sehemu ya kanisa na wanajua kwamba baadhi ya vipengele vya ibada vinaweza kuwa juu ya ufahamu wao. Wazee wanamkaribisha mtoto mchanga ambaye analia kwa sauti katika ibada. Kwa nini? Kwa sababu wao ni sehemu ya mwili wa Kristo, na wanafurahi kwamba mwili wa Kristo unajumuisha watoto, wenye kelele.

Je, hii ni sehemu ya ibada? Kabisa! Theolojia ya kibiblia ya ibada inajumuisha kuthamini umoja wa kanisa. Hii inamaanisha kuacha vipaumbele binafsi kwa ajili ya mwili wa Kristo. Inamaanisha kuimba wimbo ambao haupendi. Kwa viongozi, ina maana ya kuchagua nyimbo zinazohudumia sehemu zote za mwili wa Kristo, si tu nyimbo zinazopendwa. Nyimbo za ibada lazima zihudumie kanisa zima, si kwa vikundi vichache tu.

► Fikiria juu ya muziki ulioutumia katika ibada wiki nne zilizopita. Je, uliimba wimbo ambao unahudumia kila mmoja ibadani? Kama kiongozi, je, umewahi kuchagua kwa hiari nyimbo ambazo hupendi, lakini zinahudumia kanisa? Je, muziki wako unaonyesha ukuhani wa mwamini na umoja wa kanisa kwa kuhimiza ushiriki wa kila mwamini ibadani?

## Sababu Muziki ni Muhimu katika Kuabudu (Inaendelea)

### Sababu za Kivitendo za Muziki katika Ibada

Pamoja na sababu za kibiblia na kitheolojia, kuna sababu za kivitendo za kuthamini muziki katika kuabudu. Nguvu ya muziki inatokana na uwezo wake wa kuhudumia vipengele vyote vya utu wetu.

***Muziki huzungumza na akili.***

Walimu wa shule wanajua kwamba kuweka sheria ya sarufi kwa tuni rahisi huwarahisishia watoto kukariri. Kuimba maandiko hurahisisha kujifunza. Baadhi ya watu wanaosema, "Siwezi kukariri Biblia" tayari wanajua mistari mingi ya maandiko; wanaziimba kwa nyimbo za sifa. Baadhi ya nyimbo bora za sifa ni mistari ya maandiko iliyowekwa kwa nyimbo za kukumbukwa.

Kanuni mbili zinazoonyesha uhusiano wa muziki na akili ni muhimu.

**(1) Muziki unapaswa uzungumze na akili, sio hisia peke yake.**

Muziki ni hisia; hiyo ni sehemu ya nguvu zake. Hakuna kitu kibaya na nguvu ya kihisia ya muziki, lakini muziki lazima pia uzungumze na akili zetu.

Baadhi ya waabudu hufikiri kwamba wanaweza kuzima akili wanapoimba. Sauti ya gitaa ni kubwa, mdundo ni mkubwa, muziki ni hisia, hivyo wanadhani wanaabudu. Hatupaswi kamwe kusahau kwamba Paulo alisema, "Mtaimba kwa roho, tena nitaimba kwa akili pia" (1 Wakorintho 14:15).

Ikiwa muziki wetu huzungumza na hisia bila kuzungumza na akili, tunakuwa katika hatari ya ibada ya uongo. Hakuna kibaya kuhusu muziki unaozungumza na hisia; Hatari ni muziki ambao unaozungumza na hisia bila kuzungumza na akili. Wachungaji wenye busara watahakikisha kwamba muziki wa kuabudu haupitwi na akili.

**(2) Ujumbe tunaoimba lazima uwe wa kweli.**

Muziki huzungumza na akili, kwa hivyo nyimbo ni zana yenye nguvu ya kufundisha mafundisho.

> Sababu za waumini kuimba: kuchochea ibada yao kwa Mungu, kuimarisha imani yao, kuhamasisha tumaini lao, na kuongeza upendo wao kwa Mungu na kwa watu wengine.
>
> - Umetoholewa kutoka kwa John Wesley

Katika karne ya 18, Mungu aliwatumia ndugu wawili, Charles na John Wesley, kutangaza kweli za kibiblia ambazo watu wengi walihitaji kusikia: Watu wote wanaweza kuokolewa kutoka dhambini, na kila mtu anaweza kuwa na uhakika binafsi wa wokovu. Ndugu hawa walieneza kweli hii kwa njia mbili: John alihubiri kweli hiyo kupitia mahubiri, wakati Charles aliandika nyimbo za tenzi zilizofundisha kweli hiyo. Tenzi zake zilikuwa rahisi kuimbwa na mtu yeyote kwa sababu muziki haukuwa mgumu. Wale waliomsikia na kuimba nyimbo za Charles waliweza

kuelewa na kukumbuka kweli za Mungu, hata kama hawakuweza kusoma. Nyimbo zetu leo pia zinapaswa kufundisha kweli thabiti za kibiblia kwa waimbaji na wasikilizaji.

Wachungaji, mkiruhusu nyimbo zisizo za kibiblia, mnadhoofisha ufanisi wa huduma yenu. Watu watakumbuka wimbo muda mrefu baada ya kusahau muhtasari wa mahubiri yako. Tumia muda kupanga muziki kwa ajili ya ibada. Hakikisha nyimbo zinaunga mkono ukweli wa mahubiri.

**Kujipima**

Je, nyimbo zako za kuabudu ziko sambamba na mafundisho ya Biblia? Makanisa mengi huimba nyimbo ambazo ama zinafundisha makosa **au** hazifundishi chochote (maneno ni tupu). Je, nyimbo zako zinafundisha ukweli wa ushindi dhidi ya dhambi? Je, nyimbo zako zinafundisha kwamba wokovu unapatikana kwa wote? Je, nyimbo zenu zinafundisha kwamba Mungu anakusudia kumpa kila muumini moyo safi?

***Muziki huzungumza na moyo***

Jonathan Edwards alisema kwamba tunaamriwa kumwimbia Mungu sifa kwa sababu kuimba "huchochea hisia zetu." "[43] Ingawa kuzingatia hisia kwa ajili yake mwenyewe ni hatari, hisia ni jibu la kawaida na linalostahili kwa muziki. Kuimba huleta mwitikio wa kihisia kuhusu ukweli. Muziki huzungumza na akili na moyo.

Wakristo wengine wa magharibi wanaogopa muziki ambao unazungumza kwa undani na hisia, lakini wahusika wa kibiblia ambao waliingia kwenye uwepo wa Mungu walihisi mwitikio wa kihisia. Muziki bora wa kuabudu huzungumza na akili na hudai jibu kutoka moyoni:

► Tazama mkusanyiko wa tenzi na mapambio katika lugha yako. Tafuta mfano wa wimbo ulioandikwa kama sala binafsi ya kujitoa kwa Mungu.

***Muziki huzungumza na mwili.***

Tazama mtoto akiwa kwenye tamasha; ikiwa muziki una mdundo, wataanza kucheza. Muziki huzungumza na mwili.

Muziki unaozungumza na mwili pekee ni wa kimwili. Hata hivyo, Biblia inapozungumza juu ya ibada, mara nyingi inazungumza kuhusu nafasi ya kimwili ya waabudu: mikono iliyoinuliwa, magoti yaliyopigwa, miili ya kusujudu, na harakati za kimwili. Mkao wetu na ishara za kimwili wakati mwingine huwasiliana kwa nguvu zaidi kuliko maneno yetu.

Katika Zaburi 149:3, Israeli inaitwa "walisifu jina lake kwa kucheza, Kwa matari na kinubi wamwimbie" Ingawa baadhi ya tamaduni za kisasa hucheza tu katika suala la mwendo wa kimwili; Biblia inatumia neno *dansi* kufafanua harakati zozote za kimwili katika ibada. Mtunga-zaburi alitambua kwamba hata mwili unahusika katika sifa.

---

[43] Imetoholewa kutoka Bob Kauflin, *Worship Matters* (Wheaton: Crossway Books, 2008), 98

Hii sio dansi ya kimwili mwili inayofanyika katika vilabu vya usiku, lakini pia sio ya kukaa kwa utulivu kwenye viti vilivyo rasmi. dansi ya Kibiblia ilihusisha kiwango fulani cha miondoko wakati wa nyimbo za ibada. Tunapoinua mikono yetu wakati wa kusifu au kufanya miondoko fulani inayoendana na muziki, Hii inalingana na neno *dansi* la kibiblia.

Ingawa maana ya ishara za kimwili hutofautiana kutoka tamaduni hadi tamaduni na kizazi hadi kizazi, hatupaswi kamwe kuruhusu ibada takatifu ya Mungu iwe na kielelezo cha mazoea machafu ya utamaduni unaotuzunguka.

► Pitia Kutoka 32 kuhusu ibada takatifu inayojulikana kama "sikukuu kwa Bwana" (32:5) na sanamu za ibada ya Wamisri (32:4) na mazoea ya aibu ya utamaduni wa kipagani (32:25). Ibada yetu lazima iathiri utamaduni unaotuzunguka kupitia uinjilisti. Utamaduni unaotuzunguka haupaswi kuamua mazoea yetu ya kuabudu.

Wachungaji na viongozi wenye hekima watapata muziki unaoepuka kuchafua ibada, lakini ambao pia unazungumza na watu wote, na kuruhusu kusanyiko kuabudu kwa nyimbo katika kweli.

**Kujipima**

Je, muziki wako wa kuabudu unahudumia mwili wa Kristo kwa namna sahihi ya ibada? Je, watu wako wanasifu na kuabudu bila kuharibu maana ya ibada kwa mazoea ya kimwili?

***Muziki huongea na moyo wa ndani***

Muziki mara nyingi hujibu matakwa ya mtu. Paulo aliwaamuru wakolosai kuonyana kila mmoja kwa zaburi, nyimbo na tenzi za rohoni (wakolosai 3:16). Kuonya ni kusahihisha kosa. Karipio linauliza jibu; masahihisho hutaka mtu afanye mabadiliko katika tabia yake. Paulo alitarajia muziki uwe sababu ya mabadiliko. Muziki huigusa nafsi na kuamsha utashi kutoa mwitikio.

► Tazama mkusanyiko wa tenzi na mapambio katika lugha yako. Tafuta mfano wa wimbo ulioandikwa kama sala binafsi ya kujitoa kwa Mungu.

Muziki katika kuabudu ni muhimu kwasababu unazungumza na mtu mzima, kwasababu hii, muziki ni wa thamani na hatari. Ni wa thamani kwasababu unaweza kuwasilisha ukweli kwa njia yenye nguvu. Ni hatari kwasababu inaweza kufanya mafundisho ya uongo yavutie. Warren Wiersbe alionya, "Nina hakika kwamba watu wanapokutanika kuabudu hujifunza theolojia zaidi (nzuri na mbaya) kutoka katika nyimbo wanazoimba kuliko kutoka katika mahubiri wanayosikia…. [Muziki] unaweza kuwa chombo kizuri katika mikono ya Roho au silaha ya kutisha mikononi mwa Adui. **Waumini wasio na ufahamu wa kina wanaweza**

**kuingia katika mafundisho ya uongo kwa njia ya nyimbo kabla hata hawajagundua kinachoendelea."[44]**

Muziki una nguvu; utumie kwa busara.

### Kujipima

Fikiria nyimbo ambazo umeimba katika wiki nne zilizopita. Je, uliimba nyimbo zilizozungumza na nafsi nzima?

- Taja wimbo ambao ulitoa mafundisho kwa washirika wakati wa kuabudu.
- Taja wimbo ambao uligusa hisia za washirika wakati wa kuabudu.
- Taja wimbo ambao ulitoa changamoto kuhusu kujitoa kwa kina mbele za Mungu wakati wa kuabudu.

## Kanuni za Kuchagua Muziki kwa ajili ya Ibada

Tulianza somo hili kwa hadithi ya mgongano juu ya muziki wa kuabudu. Ikiwa wewe ni mchungaji ambaye unakabiliwa na aina hii ya migogoro, tambua kwamba hili si tatizo jipya! Katika kila kizazi, kanisa limejitahidi kuamua aina ya muziki unaofaa kwa ibada. Kwa makanisa mengi, muziki umekuwa chanzo cha migogoro badala ya kuwa njia ya ibada ya kweli.

Muziki ni muhimu katika ibada za kuabudu. Katika makanisa mengi, nusu ya ibada inahusisha muziki: muziki wakati wa kufungua ibada, kanisa nzima kuimba wakati wa sifa, nyimbo maalum, muziki wakati wa kumaliza ibada, na muziki laini wakati wa maombi. Kwa sababu muziki ni muhimu katika kuabudu, migogoro kuhusu muziki inakua zaidi.

Watu wana mapendekezo tofauti kuhusu mitindo ya muziki. Watu wengi hawataki kuvumilia mitindo ya muziki ambayo hawafurahii.

Migogoro inatokana na tofauti za maoni kuhusu maadili ya mitindo ya muziki. Hapa kuna mitazamo mitatu ya kawaida:

1. Watu wengine wanaamini kwamba mitindo fulani ya muziki ni mibaya. Wanachagua kutumia mitindo ya muziki ambayo wanaamini kuwa safi.

2. Wengine wanaamini kwamba mitindo ya muziki haiwezi kuwa mizuri au mibaya, na hivyo kila mtindo unakubalika. Watu hawa kwa kawaida wanataka kutumia mitindo ya muziki ya kitamaduni kwa ajili ya kuabudu.

3. Wengine wanaamini kwamba mitindo ya muziki haiegemei maadili ilhali ina husisha hisia na tamaduni ambayo huathiri manufaa yao katika kuabudu. Watu hawa

[44] Warren Wiersbe, *Real Worship* (Grand Rapids: Baker Books, 2000), 136. Msisitizo umeongezwa

hutathmini kila mtindo ili kuona ikiwa utasaidia washirika kuabudu kwa njia inayomletea Mungu heshima.

Katika sehemu hii, tutaangalia kanuni za kibiblia zinazohusu muziki katika kuabudu kwetu.

**Maneno ya muziki wa ibada lazima yaweze kuwasilisha ukweli kwa uwazi.**

Lengo kuu la Maandiko ni juu ya maudhui ya ujumbe wa wimbo, sio mtindo wa muziki.

Bila kujali mtindo wa muziki, nyimbo zilizo na ujumbe wa uongo (au hazina ujumbe) hazifai katika kuabudu. Warren Wiersbe huonya kwamba maneno mengi katika wimbo "hayaeleweki na hayana hisia, sio ya kitheolojia."[45] jaribio moja la ujumbe wetu wa muziki ni, "Je, mtu asiyeamini, Mhindu, au Mwislamu anaweza kuimba maandishi haya bila kubadilisha maneno?" Ikiwa unaweza kubadilisha jina la Buddha bila kubadilisha ujumbe wa wimbo, huo wimbo haufai katika kuabudu. Kama wimbo hauzungumzi ukweli kwa uwazi, tunapaswa kuuliza umuhimu wake katika kuabudu. Nyimbo zetu zinapaswa kuwasilisha Imani yetu. Kama hazifanyi hivyo, nyimbo zetu hazitawaelekeza watu wanaoabudu kwa Mungu.

**Sheria Ya Miaka Ishirini**

"Ikiwa mtu angekua akiimba nyimbo zetu kwa miaka ishirini, angemjua Mungu vizuri kiasi gani? Je, wangejua kwamba Mungu ni mtakatifu, mwenye hekima, muweza yote, na mwenye enzi kuu? Je, wangeelewa utukufu na umuhimu wa injili?"

- Bob Kauflin
in *Worship Matters*

Sikiliza wimbo kutoka katika Maandiko:

Haleluya.

Msifuni BWANA kutoka mbinguni;

Msifuni katika mahali palipo juu.

Msifuni, enyi malaika wake wote;

Msifuni, majeshi yake yote.

Msifuni, jua na mwezi;

Msifuni, nyota zote zenye mwanga.

Msifuni, enyi mbingu za mbingu,

Nanyi maji mlioko juu ya mbingu.

Na vilisifu jina la BWANA,

---

[45] Warren Wiersbe, *Real Worship* (Grand Rapids: Baker Books, 2000), 137

Kwa maana aliamuru, vikaumbwa.

Amevithibitisha hata milele na milele… (Zaburi 148).

Linganisha hii na wimbo maarufu wa hivi karibuni:

"Ni sahihi kucheza unapocheza kwa jina la Yesu
Ni sahihi kucheza unapocheza kwa ajili ya Bwana…"[46]

Wimbo gani unatangaza Neno la Mungu? Paulo alionya juu ya ibada zisizoeleweka. Alisema, "Mtaimba kwa roho, tena nitaimba kwa akili pia" (1 Wakorintho 14:15). Tunaposoma nyimbo zinazopatikana katika Maandiko, tunagundua kwamba zinafundisha kwa uwazi. Maandishi ya muziki wa kuabudu yanapaswa kuzungumza kweli za kibiblia.

**Fomu Ya Tathmini Ya Wimbo**[47]

| | Dhaifu | Wastani | Bora |
|---|---|---|---|
| Je, maandiko haya ni ya kweli kwa mujibu wa mafundisho ya imani? | | | |
| Je, maneno ya wimbo yana muktadha wa kikristo | | | |
| Je, watu waliokusanyika kuabudu wataelewa ujumbe wa wimbo? | | | |
| Je, mtindo wa muziki unalingana na maneno? | | | |
| Je, tuni ya wimbo ni rahisi kwa wanaoabudu kuimba? | | | |

**Kujipima**

Je, nyimbo zako za kuabudu ni za kibiblia kweli? Je, mshirika mpya atamjua Mungu sawasawa na Biblia kupitia nyimbo za kanisa lako?

---

[46] James Roberson, "Everybody Dance!" Accessed January 10, 2023. https://genius.com/James-roberson-everybody-dance-lyrics

[47] Imechukuliwa kutoka kwa Constance M. Cherry, *The Worship Architect.* (Grand Rapids: Baker Academic, 2010), 202-203.

## Mitindo ya Muziki wa ibada Inaweza Kutofautiana

Mungu ni Mungu wa aina mbalimbali. Alivuvia injili nne katika Agano Jipya, sio moja. Alizungumza kwa namna pekee na kila mwandishi. Aliumba maelfu ya aina mbalimbali za Samaki, sio mmoja. Aliumba jicho la mwanadamu lenye uwezo wa kujua tofauti za rangi milioni 8. Uumbaji huonyesha utukufu wa Mungu katika aina yake na uzuri wake. Aliumba watu wa pekee, si aina moja tu ya utu. Mungu anaonyesha utofauti usio na kikomo.

Muziki wetu unapaswa kuakisi aina mbalimbali za ubunifu wa Mungu tunayemwabu. Katika Wakolosai 3:16 Paulo anaorodhesha aina tatu za nyimbo ambazo zinapaswa kutumika kwa ajili ya kuabudu: zaburi, nyimbo, na tenzi za rohoni (Tazama pia Waefeso 5:19). Paulo hakutoa maana ya aina hizi tatu. Waandishi wengi wamefafanua aina hizi tatu kama.

- *Zaburi* huenda zinarejelea kitabu cha zaburi.
- *Nyimbo* pengine ni nyimbo zilizotungwa na binadamu. Waandishi wengi huweka neno hili kuwa ni nyimbo zinazomuimbia Mungu au kuhusu Mungu. Hii inaweza kuhusisha nyimbo za biblia tofauti na kitabu cha zaburi.
- *Tenzi za rohoni* ni ngumu zaidi kufafanua. Waandishi wengine hufafanua hizi kama nyimbo zisizo rasmi; wengine huzingatia tenzi za rohoni kuwa ni nyimbo kuhusu Maisha ya Kikristo na nyimbo kuhusu ushuhuda binafsi.

Bila kujali ufafanuzi, mistari hii inaonyesha kwamba kanisa liliimba aina mbalimbali za muziki tangu siku zake za kwanza.

Warren Wiersbe anazungumzia kanuni ya uhalisia. Anaandika, "Maelezo ya kuabudu lazima yawe ya kweli, yakifichua tofauti za kitamaduni za watu."[48] Ibada halisi huzungumzia Neno la Mungu katika lugha ya kila tamaduni. Katika kila kizazi, wakristo wameandika nyimbo ambazo zinamsifu Mungu katika mtindo wa muziki wa tamaduni zao. Hatupaswi kudhania kwamba muziki wa tamaduni yetu ni muziki pekee mtakatifu na halisi. Badala yake, isipokuwa mtindo unapingana na kanuni ya wazi ya Maandiko, tunapaswa kuruhusu kila tamaduni na kila kizazi kumsifu Mungu katika lugha zao.

### Kujipima

Je, muziki wa kanisa lako unaonyesha aina mbalimbali za ubunifu wa Mungu wetu?

## Sio Kila Mtindo Unafaa kwa Kila Hali

Ingawa watu wengi wamejaribu kufafanua kuhusu mtindo wa muziki kibiblia, Biblia haijaamuru aina fulani ya mtindo wa muziki. Baada ya kusoma Falsafa ya mtindo wa muziki,

---

[48] Warren Wiersbe, *Real Worship* (Grand Rapids: Baker Books, 2000), 139

Francis Schaeffer aliandika, "Wacha niseme kwa uthabiti kwamba hakuna kitu kama mtindo wa kimungu…"[49]

Sauti za muziki haziwasilishi maudhui ya maadili. Muziki wa noti zilizopangwa pamoja si wa kiroho wala si wa kidunia. Je, hii inamaanisha kwamba kila mtindo wa muziki unafaa kwa ajili ya ibada? Hapana. Mitindo mingine inahusishwa sana na utamaduni wenye dhambi ambao hautawasilisha ujumbe wa kimungu katika ibada.

Wanamuziki na wamishonari wamepata kitu kimoja: watu huitikia sauti za muziki kwa njia tofauti. Ikiwa watu wawili wanasikiliza muziki uleule, mtu mmoja anaweza kuanza kulia kwa sababu ya jinsi anavyoathiriwa na wimbo huo. Na huenda mtu mwingine asihisi chochote katika kuitikia muziki.[50]

Kipimo kikuu cha muziki wa ibada hakiwezi kuwa, "Je, ninaupenda?" au "Je, unanivutia?" Kipimo kikuu ni utukufu wa Mungu. Hii ina maana kwamba ni lazima tutathmini mtindo gani wa muziki unawasilishwa ndani ya muktadha wetu wa kitamaduni. Ni lazima tuulize, "**Katika muktadha wangu wa kitamaduni, je mtindo huu wa muziki unamtukuza Mungu?"**

Ijapokuwa vitu vyote ni halali, bali si vitu vyote vijengavyo (1 Wakorintho 10:23). Ikiwa lengo la muziki wa kuabudu ni kuwajenga waumini, mtindo tunaotumia lazima usizuie kusudi hili. Muziki huohuo unaweza kuwa msaada wa kuabudu katika utamaduni mmoja, na pia kizuizi katika utamaduni mwingine. Kiongozi makini wa ibada atachagua muziki unaofaa kwa watu anaowaongoza.

Tunawezaje kujua kama mtindo fulani wa muziki unafaa? Kama kiongozi, unawajibika kusaidia watu wako kujibu swali hili katika mazingira yako ya kitamaduni. Kinachofaa katika utamaduni mmoja huenda kisifae katika utamaduni mwingine. Kwa sababu ya uhusiano wa kidini wa mtindo fulani au kwa sababu mtindo fulani umehusishwa na mazoea ya dhambi ya utamaduni unaozunguka, mtindo wa muziki hauwezi kufaa kwa ajili ya ibada. Lazima utathmini muziki kulingana na kufaa kwake katika hali yako.

Paulo alituamuru tujaribu mambo yote na kushika sana lililo jema (1 Wathesalonike 5:21). Bila kupima na kuthibitisha hatupaswi kukubali kitu chochote. Hii ni pamoja na muziki tunaoimba.

### Kujipima

Je, unaimba nyimbo zisizoendana na utamaduni wako? Je, muziki unawasilisha mtindo wa kimwili au wa kilimwengu **katika utamaduni wako?** Je, ujumbe wa muziki unapingana na ujumbe wa maneno?

---

[49] Francis Schaeffer, *Art and the Bible* (Downers Grove: InterVarsity Press, 1973), 51
[50] Gerardo Marti, *Worship across the Racial Divide: Religious Music and the Multiracial Congregation*. (England: Oxford University Press, 2012)

**Panapaswa kuwa na usawa katika muziki wetu wa ibada.**

Kitabu cha Zaburi kinaonyesha kuwa Mungu anathamini utofauti katika ibada. Kitabu cha Zaburi kina sifa, maombolezo, vilio vya kuomba msaada, na shukrani kwa ajili ya ukombozi. Zaburi zinazungumza na mahitaji ya ibada ya waabudu wote.

Alama moja ya ukomavu katika kanisa ni utofauti (1 Wakorintho 12:4-6). Mwili wa Kristo unajumuisha tamaduni tofauti, lugha tofauti, haiba tofauti, na karama tofauti. Ibada yetu, pamoja na muziki wetu, vinapaswa kuzungumza na washirika wote katika mwili wa Kristo. Kwa kweli, ibada yetu inapaswa kuzungumza zaidi ya kanisa lenyewe ili kutoa injili kwa wasioamini. Nyimbo katika Biblia huzungumza na hadhira tatu.[51]

***Muziki unapaswa kutangaza sifa kwa Mungu: "Mwimbieni na kumshangilia Bwana" (Waefeso 5:19).***

► Soma Zaburi 92:1-4.

Zaburi ya 92 inaonyesha kwamba tunamwimbia Bwana. Muziki unapaswa kueleza sifa kwa Mungu. Kuanzia kwenye wimbo wa sifa katika Kutoka 15 hadi nyimbo za mbinguni katika Ufunuo, nyimbo za kibiblia zinamsifu Mungu kwa ukuu wake. Kusudi kuu la muziki katika Biblia ni sifa. Zaburi za maombolezo, maombi, au sifa mara nyingi huelekezwa kwa Mungu. Ukiimba Zaburi zote, utaimba kuhusu:


- “Nilimlilia Bwana kwa sauti kuu…”
- “Niitikie ninapoita, Ee Mungu wa haki yangu!”
- “Nitamshukuru Bwana kwa moyo wangu wote.”
- “Nitamwimbia Bwana.”
- “Nakupenda, Ee Bwana.”

---

[51] Imechukuliwa kutoka kwa Herbert Bateman, editor. *Authentic Worship* (Grand Rapids: Kregel Publications, 2002), 150-155.

***Muziki unapaswa kutangaza ukweli kwa kanisa: "Mkifundishana na kuonyana" (Wakolosai 3:16).***

Viongozi wengi wa ibada wamesema, "Hatupaswi kuwaimbia watu wengine; tunamwimbia Mungu pekee." Hata hivyo, zaburi nyingi huimbia Israeli. Ingawa ni kweli kwamba nyimbo nyingi za Biblia humwimbia Mungu, Pia ni kweli kwamba nyimbo nyingi za Biblia huzungumza na kanisa.




Waefeso 5:19 inawaagiza waamini wasemezane **wao kwa wao** kwa zaburi, tenzi na nyimbo za kiroho. Wakolosai 3:16 huzungumza zaidi kuhusu kusudi la uimbaji wetu: "Neno la Kristo na likae kwa wingi ndani yenu katika hekima yote, **mkifundishana na kuonyana** kwa zaburi, na nyimbo, na tenzi za rohoni; huku mkimwimbia Mungu kwa neema mioyoni mwenu."

Paulo anaonyesha kwamba neno la Kristo linatangazwa kupitia uimbaji wa kanisa. Tunapoimba, tunasema kweli ya Mungu kwa waabudu wenzetu. Kupitia wimbo, kanisa linafundishana. Kupitia wimbo, waamini wanajengwa na mwili wa Kristo unajengwa.

***Muziki unapaswa kutangaza injili kwa ulimwengu: "Wahubirini mataifa habari za utukufu wake…" (Zaburi 96:3).***

Mtunga Zaburi anatuita kuimba kama ushuhuda kwa mataifa:

> Mwimbieni BWANA wimbo mpya, Mwimbieni BWANA, nchi yote. Mwimbieni BWANA, libarikini jina lake, Tangazeni wokovu wake siku kwa siku. Wahubirini mataifa habari za utukufu wake, Na watu wote habari za maajabu yake (Zaburi 96:1-3).

► Soma 1 Wafalme 8:41-43.

Mungu anaposifiwa, injili inatangazwa kwa mataifa. Wakati wa kuwekwa wakfu kwa Hekalu, Sulemani aliomba kwamba hata watu wa mataifa wangeabudu kwenye Hekalu; aliomba kwamba jina la Bwana lijulikane kwa watu wote wa dunia. Tunapoabudu, injili inatangazwa kwa ulimwengu unaotazama.

Muziki wetu wa kuabudu unapaswa kuzungumza na Mungu na kuhusu Mungu; muziki wetu wa kuabudu unapaswa kuzungumza na kanisa; muziki wetu wa kuabudu unapaswa kutangaza injili kwa ulimwengu.

Tunaposahau mojawapo ya wasikilizaji hawa, ibada yetu inashindwa kufikia kusudi kamili la Mungu kwa kanisa. Tunaposahau kwamba Mungu ndiye msikilizaji mkuu wa ibada, ibada yetu inashindwa kusema na Mungu kimsingi. Tunaposahau kuwa kanisa ni wasikilizaji wa ibada, tunashindwa kufundishana na kukumbushana kwa muziki wetu. Tunaposahau

kwamba ibada inapaswa kutangaza injili kwa ulimwengu, tunashindwa kuhubiri na kutimiza Agizo Kuu.

**Kujipima**

Je, katika nyimbo zako unazungumza na Mungu, kanisa, na wasioamini? Sio kila wimbo unazungumza na kila mmoja kati ya haya; lakini katika ibada yote, tunapaswa kuzungumza na kila mmoja wa wasikilizaji hawa.

**Kuiweka katika Vitendo**

Tumeona kwa nini muziki ni muhimu katika ibada. Tumechunguza kanuni za kibiblia za muziki katika ibada. Tutamaliza somo hili kwa kuangalia mawazo ya kivitendo kuhusu muziki katika ibada. Unaweza kuyachukua haya ili kuendana na kanisa lako na mpangilio wa kanisa.

Kwa kujibu kanuni zilizoorodheshwa hapo juu, mwanafunzi aliuliza, "Ikiwa mitindo ya muziki wa kuabudu inatofautiana na ikiwa mitindo ya muziki kwa asili si nzuri au mbaya, je, kuna miongozo yoyote inayoweza kutusaidia katika kuchagua muziki wa kanisa letu?"

Ndiyo, kuna miongozo yenye kutumika ambayo inaweza kutusaidia. Lazima uamue jinsi ya kutumia hiyo katika eneo lako mahususi, lakini baadhi ya kanuni za kimsingi zinapaswa kuongoza maamuzi yetu kuhusu muziki wa kanisa.

**Muziki Muhimu Zaidi Wa Kanisa Ni Uimbaji Wa Waumini Wote.**

Kwa kuwa muziki wa kanisa unaonyesha umoja wa kanisa na ukuhani wa waumini, muziki wetu muhimu zaidi ni uimbaji wa washirika wote. Ingawa kwaya, waimbaji binafsi, kikundi cha sifa, na vikundi vya ala na muziki mingine ni vya thamani, muziki wa kanisa nzima ni muziki muhimu zaidi katika ibada ya Kikristo. Kuna baadhi ya hatua zinazofaa tunazoweza kuchukua ili kusitawisha uimbaji wa waumini wote.

Kumbuka:

1. **Upigaji wa muziki haupaswi kuwa wa kifahari wenye sauti kali hivyo ukaondoa umakini kutoka kwa uimbaji.** Katika Agano Jipya, uimbaji ni muziki wa msingi wa kanisa. Wapiga kinanda, wapiga gitaa, wapiga ngoma sio muziki wa msingi wa kanisa. Acha kanisa liimbe**.**

2. **Baadhi ya nyimbo huimbwa vizuri bila vyombo za muziki.** Nyimbo za sala mara nyingi huweza kuwasilishwa vizuri kwa kuimba kimya kimya bila vyombo vya muziki. Hii huwawezesha waumini kuzingatia ujumbe wa wimbo bila vurugu yoyote.

3. **Muziki haupaswi kuwa mgumu sana au mpya hivi kiasi kwamba waumini wasiweze kushiriki.** Nyimbo mpya ni nzuri, lakini tunapaswa kuwaruhusu waumini muda wa kujifunza wimbo mpya vizuri kabla ya kuongeza nyimbo mpya zaidi. Matumizi ya mara kwa mara ya nyimbo mpya yanakuwa mengi hadi hatuwezi

kuelewa ujumbe vizuri. Mbinu nzuri ni kuongeza nyimbo mpya huku tukiendelea kuwa na zile tunazozoea.

4. **Wachungaji wanapaswa kuimba pamoja na waumini.** Ikiwa kuimba kwa pamoja ni ibada, basi lazima uabudu. Mchungaji anapofanya mambo mengine wakati wa uimbaji wa wote, matendo yake yanasema, "Ni mahubiri yangu pekee ndiyo muhimu katika ibada." Wachungaji wanapaswa kuwa kielelezo cha ibada kwa waumini wengine**.**

### Muziki Lazima Uhudumie Maandiko

Kwa kuwa muziki wa ibada unakusudiwa kutangaza sifa kwa Mungu, kusema ukweli kwa waumini, na kutangaza injili kwa ulimwengu, maandiko ndiyo kiini muhimu zaidi. Bila kujali mtindo wa muziki, ikiwa muziki unazuia mawasiliano ya maandiko, hatusemezane kwa zaburi, nyimbo, na nyimbo za kiroho.

Hii haimaanishi kuwa muziki wa ala sio muhimu. Vyombo vinaweza kutusaidia kuzingatia akili, hisia, na mapenzi yetu kwenye ibada. Muziki wa ala unaweza kuwa na thamani katika ibada, lakini katika uimbaji wa pamoja, lengo kuu linapaswa kuwa maandiko.

#### *Kiongozi Lazima Awasaidie Waumini Kuzingatia Maana Ya Maandiko.*

Viongozi wanaweza kufanya maandiko kuwa na maana zaidi kwa jinsi wanavyoongoza. Mifano miwili itaonyesha jinsi kiongozi anavyoathiri ujumbe wa wimbo.

Yohana hakufikiria kwa makini kuhusu ujumbe wa nyimbo za ibada za waumini. Wiki iliyopita, Yohana aliongoza nyimbo mbili kuhusu utatu. Beti za wimbo wa kwanza kila mmoja unajikita kwenye mambo tofauti: ubeti wa 1 ni sala kwa Baba; ubeti wa 2 ni sala kwa Mwana; ubeti wa 3 ni sala kwa Roho Mtakatifu; na ubeti wa 4 ni sala kwa utatu.

Kabla ya kuimba, Yohana alisema, "Tutaimba ubeti wa 1, 2, na 4."

Nini kibaya na kuacha ubeti wa 3? Ni wimbo kuhusu Utatu; ujumbe unahisiwa kupunguzwa ikiwa utaacha ubeti.

Katika wimbo wa pili, beti zote tatu ni ibada na sifa kwa mtu maalum katika Utatu. Yohana alisema, "Tuimbe beti mbili." Tena, Yohana alisahau kwamba wimbo wa Utatu lazima ujumuishe watu wote watatu. Kuacha ubeti wa wimbo bila kuzingatia maandiko kunazuia ibada ya waumini.

Daudi anajua kwamba uimbaji wa waumini wote ni muhimu katika ibada. Siku ya Jumapili, aliongoza wimbo usiojulikana. Alianza kwa kusema, "Wimbo huu ni mpya kwetu. Sikiliza Zaburi ya 150, zaburi ambayo wimbo huu umeegemezwa." Kwa maneno machache, Daudi alisaidia waumini kuzingatia maana ya wimbo mpya.

Baadaye katika ibada, Daudi aliongoza wimbo unaoelezea ukuu wa Mungu kama mfalme. Kabla hawajaimba, Daudi alisoma 1 Timotheo 1:17; "Sasa kwa Mfalme wa milele, asiyeweza kuona uharibifu, asiyeonekana, Mungu peke yake, na iwe heshima na utukufu milele na

milele. Amina." Wimbo ambao waumini walikuwa wameimba mara nyingi ulifanywa kuwa mpya waabudu waliposikia andiko lililoongooza wimbo huo. Kuunganisha wimbo na msingi wake wa kibiblia kunahamasisha ibada ya waumini.

► Tazama mkusanyiko wa tenzi na mapambio katika lugha yako. Chagua wimbo na kifungu cha Andiko ambacho kinautambulisha.

***Ikiwa unatumia kinasa picha (projekta), mtu anayesimamia kinasa picha ni sehemu ya uongozi wa ibada.***

Maneno kwenye skrini yanaweza kuwasaidia waabudu kuzingatia maandiko au yanaweza kuwachanganya. Mtu anayesimamia uonyeshaji anapaswa kuwa mwangalifu katika uongozi wake. Ipuka matatizo yafuatayo:

- Kuandika neno kimakosa
- Kuweka kimakosa alama za kusomea mf nukta na koma.
- Kugawa mistari ya wimbo katikati ya vifungu badala ya kuigawa kati ya vifungu
- Kuweka slaidi katika mpangilio usio sahihi
- Kutobadilisha slaidi kwa wakati unaofaa

Matatizo haya yote huvuruga ibada. Wakati kuna makosa, watu huanza kuyafikiria badala ya kuzingatia ibada. Kuonekana kwa maneno kwenye skrini huathiri uimbaji wa waumini.

Katika muziki wa ibada, muziki huhudumia waabudu. Kwa kuwa hii ni kweli, viongozi wa ibada lazima wasaidie waumini kuimba kwa maana. Hakuna chochote kati ya hii **inaunda** ibada; Ibada hutoka moyoni. Hata hivyo, kuondoa vikwazo kunawatia moyo waabudu kuzingatia lengo la kweli la ibada, ambalo ni Mungu.

### Hatua za Kivitendo za Kuboresha Wimbo wa Waumini Wote

1. **Fundisha umuhimu wa kuabudu katika wimbo**. Kama vile Wakristo lazima wafundishwe umuhimu wa maombi na nidhamu zingine za kiroho, vivyo hivyo lazima wajifunze jinsi Mungu anawavyokusudia kuimba.

2. **Hakikisha waumini wanajua kwanini wanaimba wimbo.** Ikiwa ni maombi, wakumbushe. Ikiwa ni wimbo wa kujisalimisha kwa Bwana, eleza hiyo. Ikiwa inaakisi ujumbe uliohubiriwa, weka wazi hilo. Watu wataimba kwa shauku zaidi ikiwa wanajua kwanini wanaimba wimbo.

3. **Chagua nyimbo za waumini wote badala ya nyimbo za maonyesho**. Nyimbo za kushiriki wote huwa na melodi rahisi zinazoweza kukumbukwa na na kuimbwa kwa urahisi. Ikiwa unataka watu wote kuimba, fikiria, "Je! Watoto wanaweza kuimba wimbo huu wanapokuwa njiani kurudi nyumbani?"

4. **Punguza sauti nyingi za muziki**. Usiruhusu gitaa, kinanda, ngoma, au kwaya kuzidi sauti ya waumini wote. Sauti kubwa katika chumba inapaswa kuwa sauti za waumini.

5. **Tafuta usawa kati ya nyimbo mpya na nyimbo za zamani.**

6. **Tumia nyimbo ambazo zinaakisi uzoefu mpana wa kikristo**. Ikiwa muziki wote ni wa furaha, hautawakilisha waumini ambao wanapitia wakati mgumu. Kama zaburi, nyimbo zetu za ibada zinapaswa kuwa na maneno kwa wakristo wenye furaha, wakristo wenye huzuni, na wakristo wanaopitia wakati mgumu.

7. **Mchungaji na viongozi wa kanisa wanapaswa kuwa mfano wa kuimba kwa shauku hata kama hawana ujuzi mzuri wa kuimba**. Kuimba nje ya toni ni bora kuliko kutokuimba kabisa. Mchungaji ambaye anatazama maelezo ya mahubiri yake wakati wa kuimba anasema, "kuimba katika ibada si muhimu sana."

8. **Wakumbushe waumini kuwa wao ndio chombo kikuu katika ibada ya pamoja.** Ikiwa watu hawaimbi kwa shauku, muziki wa waumini unafeli katika lengo lake. aumini lazima wafundishwe kuwa ni haki yao na jukumu lao kuimba kama tendo cha ibada.

## Hitimisho: Ushuhuda wa Gloria

Je, Mungu huzungumza kupitia muziki wa ibada? Sikiliza ushuhuda wa Mchungaji kutokea Taiwani.

Wakati Gloria alipoingia kanisani kwetu, alikuwa hajawahi kusikia injili. Hakuwa akitafuta mahubiri; Hakuwa na nia ya kuwa Mkristo. Gloria hakuwa akimtafuta Mungu, lakini Mungu alikuwa akimtafuta Gloria!

Gloria alitembelea kanisa letu ili kuboresha lugha yake ya Kiingereza. Alikuwa amesikia kwamba kanisa letu lilikuwa linatoa kozi za Kiingereza bure, kwa hivyo alikuja kujifunza Kiingereza. Katika ziara yake ya kwanza, Gloria alifika kwa kuchelewa. Alipoingia patakatifu, kanisa lilikuwa likiimba wimbo rahisi kulingana na Zaburi 42: 1, "Kama ayala aioneavyo shauku mito ya maji. Vivyo hivyo nafsi yangu inakuonea shauku, Ee Mungu."

Mwaka mmoja baadaye wakati wa ubatizo wake, Gloria alitoa ushuhuda huu:

"Sikumbuki chochote kuhusu ibada ile isipokuwa wimbo ambao mlikuwa mnaimba nilipokuwa nimeketi. Niliposikiliza wimbo huo, nilianza kulia. Kwa miaka 30, nimekuwa na kiu ya Mungu kama ayala anavyotamani maji, lakini sikuwahi kujua kile nilichokuwa nikihitaji. Nilijaribu elimu; Nilijaribu pesa; Nilijaribu burudani; Nilijaribu kila kitu - na bado nilikuwa tupu. Niliamua kujaribu kujifunza Kiingereza, kwa hivyo nilikuja kanisani kwenu.

"Badala ya Kiingereza, nilipata maji niliyohitaji. Nilipokuwa nikiketi katika ibada, nililia nilipogundua kuwa Mungu ndiye utimilifu wa kiu ya moyo wangu. Yeye ndiye mtoaji wa furaha ya kweli. Siku hiyo, niliamua kumpa Mungu moyo wangu. Leo hii, yeye ndiye mboni ya jicho langu. "

## Mapitio ya Somo la 6

(1) Muziki ni muhimu katika ibada yetu

- Kwasababu muziki ulikuwa muhimu katika ibada ndani ya biblia.
- Kwasababu inaelezea kanuni ya kitheolojia ya ukuhani wa mwamini.
- Kwasababu inaelezea kanuni ya kitheolojia ya umoja wa kanisa.

(2) Muziki

- Huzungumza na akili, hivyo ujumbe tunaouimba ni laizma uwe wa kweli.
- Huzungumza na moyo na hugusa hisia.
- Huzungumza na mwili na haupaswi kuigwa kwa mazoea machafu.
- Huzungumza na nia na huuliza mwitikio.
- Huzungumza na mtu mzima. Hii inafanya kuwa ya thamani wakati inafundisha ukweli na hatari wakati inafundisha uzushi.

(3) Misingi ya Maneno kwa muziki wa ibada ni pamoja na:

- Maneno ya muziki wa ibada lazima yawe wazi katika kuwasilisha ukweli.
- Mitindo ya muziki wa ibada inaweza kutofautiana*. Paulo anarejelea zaburi, nyimbo, na tenzi za rohoni. Tangu siku zake za mwanzo, kanisa liliimba aina mbalimbali za muziki.*
- Sio kila mtindo unafaa kwa kila mazingira. *Tunapaswa kujiuliza, "katika muktadha wa tamaduni yangu, je, mtindo huu wa muziki unampa Mungu utukufu?"*

(4) muziki unapaswa kuzungumza na wasikilizaji watatu:

- Muziki unapaswa kutangaza sifa kwa Mungu.
- Muziki unapaswa kutangaza kweli kwa kanisa.
- Muziki unapawwa kuhubiri injili kwa ulimwengu.

(5) Kanuni za muziki wa kanisa ni pamoja na:

- Muziki muhimu zaidi wa kanisa ni wimbo wa pamoja.
- Muziki ni lazima uhudumie maandiko.

## Somo la 6 Mazoezi

(1) Ili kufahamu aina ya muziki unaopatikana kwa ibada, tengeneza orodha ya nyimbo 4 au zaidi ambazo zinashughulikia kila mada zifuatazo. Orodha yako itatumika wakati unapanga ibada katika somo la baadaye. Tafuta nyimbo ambazo zinazungumza na akili, moyo, na nia.

- Nyimbo 4 kuhusu asili ya Mungu
- Nyimbo 4 kuhusu Yesu, kifo chake na kufufuka kwake
- Nyimbo 4 kuhusu Roho Mtakatifu na kanisa
- Nymbo 4 ambazo zinawaalika watu wa Mungu kuwa na maisha matakatifu
- Nyimbo 4 kuhusu injili na umisheni

Ikiwa unasoma katika kikundi, shirikisha orodha zako na kisha ujadili, "Je! Ni nyimbo ngapi ambazo tumeimba katika mwaka uliopita? Je! Tunatangaza injili nzima katika uimbaji wetu?

(2) Mwanzoni mwa somo linalofuata, utachukua mtihani kulingana na somo hili. Soma maswali ya mtihani kwa uangalifu katika maandalizi.

## Jaribio Somo la 6

(1) Orodhesha nyimbo 3 kutoka kwenye Biblia.

(2) Imani gani iliyowafanya baraza la Laodikea kupiga marufuku uimbaji wa waumini?

(3) Orodhesha kanuni mbili za kitheolojia ambazo zinapaswa kuonyeshwa katika muziki wetu wa ibada.

(4) Orodhesha sababu nne za Kivitendo za muziki katika ibada.

(5) Taja kanuni nne amabzo zinapaswa kuongoza uchaguzi wetu wa muziki wa ibada.

(6) Ni aina gani tatu za nyimbo zilizoorodheshwa na Paulo katika Wakolosai 3:16?

(7) Ni kipimo gani cha mwisho kwa muziki wetu wa ibada?

(8) Kulingana na nyimbo kwenye biblia, orodhesha njia tatu ambazo muziki unapaswa kuzungumza na wasikilizaji tofauti.

(9) Je! Wakolosai 3:16 hufundisha nini juu ya madhumuni ya muziki wa ibada?

(10) Andika Wakolosai 3: 15-17 kutoka kwenye kumbukumbu.

# Somo la 7
# Maandiko na Maombi katika Ibada

## Malengo Ya Somo

Mwisho wa somo hili, mwanafunzi anapaswa:

(1) Kuthamini umuhimu wa maandiko katika ibada.
(2) Kujua hatua za vitendo za kutumia maandiko katika ibada.
(3) Kutambua mahubiri kama sehemu ya ibada.
(4) Kuthamini umuhimu wa maombi katika ibada.
(5) Kuongoza kanisa katika maombi ya pamoja yenye maana.
(6) Kuelewa kwamba ukusanyaji wa sadaka ni kitendo cha ibada.
(7) Kutazama meza ya Bwana kama sherehe ya kufurahia na ukumbusho mzuri.

## Matayarisho kwa somo hili

*Kariri Mathayo 6:5-8.*

## Utangulizi

Kanisa la XYZ linajulikana kwa muda wanaoutumia katika ibada. Huduma zao zinafuata muundo huu:

| **Taratibu za Huduma ya Kanisa la XYZ** | |
|---|---|
| Utangulizi na matangazo | |
| Muda wa ibada (nyimbo za sifa) | dakika 30 |
| Sadaka/muziki maalumu/maombi | dakika 15 |
| Mahubiri | dakika 30 |
| Muda wa ibada (nyimbo za sifa) | dakika 15 |

Watu katika kanisa la XYZ wanapenda muziki. Wageni wanapongeza ibada yenye nguvu sana ingawa, Mchungaji Bill amekuwa na wasiwasi kuhusu matokeo ya muda mrefu ya huduma yake. Waongofu wapya hivi karibuni wanahamia kwenye makanisa mengine.

Jambo baya zaidi, utafiti wa washirika wa muda mrefu uligundua kwamba kanisa "halitengenezi wanafunzi imara wa Yesu Kristo. Idadi, ndiyo; wanafunzi, hapana."[52]

Bill anaamini kwamba sehemu ya tatizo ni uelewa wa kanisa kuhusu ibada. Katika Kanisa la XYZ, *ibada* inalingana na *muziki* tu. Mchungaji Bill anaanza kuuliza, "Je, ibada ya kweli inajumuisha zaidi ya muziki? Je, tunatenganisha Neno la Mungu na maombi kutoka kwenye ibada? Je, hii inapunguza matokeo ya mahubiri?"

► Tafadhali jibu wasiwasi wa Mchungaji Bill. Je, kuna tofauti kati ya ibada na mahubiri? Kanisa la XYZ linawezaje kuunganisha sehemu zote za ibada katika akili za waabudu?

## Umuhimu wa Maandiko katika Ibada

Kama wainjilisti tunafundisha kwamba mafundisho na ibada zetu zinaongozwa na maandiko. Tunaamini kwamba Biblia inapaswa kuwa na nafasi kuu katika ibada yetu. Mungu huzungumza na watu wake katika usomaji wa Neno. Tangu nyakati za Agano la Kale, maandiko yamekuwa muhimu katika ibada.

Kwa kusikitisha, ingawa tunasema kwamba Biblia ndiyo mzizi wa ibada yetu, makanisa mengi yanajumuisha maandiko machache katika ibada zao. Inawezekana kuhudhuria ibada katika baadhi ya makanisa na kusikia si zaidi ya mistari michache ya maandiko. Hii ni mbali na mfano wa kibiblia wa ibada.

**Kusoma Neno lilikuwa muhimu katika ibada za kibiblia.**

► Soma Kutoka 24:1-12.

Katika Kutoka 24:7, Musa akakitwaa kitabu cha agano, na kukisoma masikioni mwa watu. Watu waliahidi kuzifuata amri za Mungu: "Hayo yote aliyoyanena Bwana tutayatenda, nasi tutatii." Kufuatia haya, Mungu aliandika muhtasari wa agano (Amri Kumi) kwenye mbao za mawe. Israil walikuwa watu wa Kitabu. Agano lililoandikwa lilikuwa kiini cha ibada ya Israeli.

Neno la Mungu lilikuwa katikati ya Hema na Hekalu. Sikukuu za kila mwaka zilikuwa matukio muhimu zaidi katika mwaka wa Kiyahudi. Katika Pasaka, Sikukuu ya Malimbuko, na Sikukuu ya Vibanda sehemu za Neno la Mungu zilisomwa hadharani. Kila baada ya miaka saba, taifa lilikusanyika ili kusikiliza sheria ikisomwa, na agano lilifanywa upya.[53]

Katika Agano Jipya, Paulo aliwaamuru Wakristo kusoma maandiko hadharani. Hii ilijumuisha Agano la Kale, barua za Paulo, na maandishi mengine yaliyoainishwa kama maandiko.[54] Alimwagiza mtumishi kijana kujishughulisha na usomaji wa hadhara wa maandiko, kuonya, na kufundisha (1 Timotheo 4:13). Neno la Mungu lilikuwa kiini katika ibada ya Agano Jipya.

---

[52] Hii imenukuliwa katika utafiti uliofanywa na moja ya makanisa makubwa zaidi Marekani. Waligundua kuwa wengi wa waongofu wapya hawajawahi kufikia hatua ya kuwa wanafunzi wa kweli.
[53] Timothy J. Ralston, "Scripture in Worship" in *Authentic Worship.* Edited by Herbert Bateman. (Grand Rapids: Kregel, 2002), 201
[54] 1 Timotheo 4:13, 1 Thesalonike 5:27, Wakolosai 4:16, 2 Petro 3:16

**Kuhubiri Neno lilikuwa muhimu katika ibada za kibiblia.**

► Soma Nehemia 8:1-18.

Baada ya kurudi kutoka uhamishoni, Ezra aliwasomea watu Sheria. Watu wakakusanyika ili kusikiliza Ezra alipokuwa akisoma torati mbele ya wanaume na wanawake, na wale walioweza kuelewa; na masikio ya watu wote yakakisikiliza kitabu cha torati (Nehemia 8:3). Kwa kuitikia, watu walisema "Amina" na wakaanguka kifudifudi katika ibada. Ezra na wenzake waliposoma, walifafanua andiko hilo na kuwafanya wasikilizaji waelewe usomaji huo. Huu ni mfano wa kibiblia wa kuhubiri, kueleza, na kutumia Neno la Mungu kwa mahitaji ya watu. Mahubiri ya kweli ya kibiblia huchochea ibada katika mwitikio wa Neno.

Yesu alikuja kwenye sinagogi siku ya Sabato kama ilivyokuwa desturi yake na kusoma kitabu cha nabii Isaya. Alipomaliza, Yesu alihubiri mahubiri ambayo alionyesha kwamba amekuja kutimiza ahadi ya Isaya (Luka 4:16-29).

Katika mahubiri yake siku ya Pentekoste, Petro alionyesha kwamba ahadi za Agano la Kale zilitimizwa katika huduma ya Yesu na ujio wa Roho Mtakatifu. Alimalizia maelezo yake ya maandiko kwa kuwaalika watu kutubu na kubatizwa (Matendo 2:14-41). Mahubiri ya Biblia yalitaka mwitikio kutoka kwa wasikilizaji. Mahubiri huzungumza na akili, lakini lazima pia yazungumze na moyo. Mahubiri lazima yahitaji mwitikio wa msikilizaji sawasawa na mapenzi yake. Yesu alipofungua maandiko njiani kuelekea Emau, mioyo ya wasikilizaji iliwaka ndani yao (Luka 24:32).

**Kuhusu Mahubiri ya Biblia**

"Baraka ya ufafanuzi wa kweli wa Biblia ni moyo uliowaka, si kichwa kilichojaa."

- Warren Wiersbe

Kuhubiri kulikuwa muhimu katika kuenea kwa kanisa la kwanza. Katika Matendo ya Mitume, neno la Mungu linatajwa zaidi ya mara 20. Mitume walihubiri neno la Bwana; walisema neno la Mungu kwa ujasiri; walifundisha neno la Mungu. Na matokeo yake, watu wengi walipokea neno la Mungu; neno la Mungu likakua na kuongezeka; neno la Mungu likaenea; na mataifa wakalitukuza neno la Bwana. Neno la Mungu lilikuwa msingi wa ujumbe wa mitume.

Ingawa kuhubiri sio njia pekee ambayo maandiko huzungumza, ndiyo njia kuu ya kuleta Neno la Mungu kwa watu wa Mungu. Ili kutimiza kusudi hili, mchungaji hapaswi kusahau kamwe kwamba Neno la Mungu lazima liwe kiini. Mahubiri ya Biblia lazima yaanzie katika Neno la Mungu, yafafanue Neno la Mungu, na yatoe itikio la kibinafsi kwa Neno la Mungu.

**Kuhubiri Neno lilikuwa muhimu katika historia ya kanisa.**

Mahubiri yalikuwa muhimu katika ibada karne za mwanzo za kanisa. Katika karne ya pili, Justin Martyr aliandika kwamba Wakristo walikusanyika Jumapili ili kusoma Nyaraka na Manabii na kusikiliza zikifafanuliwa. Kufikia karne ya tatu, sehemu za kila sehemu kuu ya Biblia zilisomwa wakati wa ibada.

Katika kipindi cha karne za kati, kanisa Katoliki lilipunguza jukumu la kuhubiri, lakini Wanamatengenezo walirudisha kuhubiri katika nafasi kuu katika ibada. Lengo la kurudisha

mahubiri halikuwa burudani, ajenda ya kibinafsi ya mhubiri, au mahitaji ya kitamaduni ya jamii. Kusudi la kuhubiri lilikuwa ufafanuzi makini wa Neno la Mungu; kufafanua maandiko kwa njia ambayo iliwagusa wasikilizaji na kutaka jibu la kubadilisha maisha.

## Kufanya Maandiko kuwa Kitovu cha Ibada

Ikiwa Neno la Mungu linapaswa kuwa kiini katika ibada yetu, je, tunawekaje kanuni hii katika vitendo? Hatua za kivitendo za kufanya maandiko kuwa muhimu katika ibada zetu ni pamoja na:

### Maandiko Yanapaswa Kujumuishwa Katika Sehemu Zote za Ibada

Hatupaswi kusubiri hadi mahubiri ili kusikia maandiko katika ibada. Hakuna njia bora ya kuanza ibada kuliko kwa Neno la Mungu.

Chunguza namna mbili za ufunguzi wa ibada. Je ni mwaliko gani unafaa kuingia katika uwepo wa Mungu?

1. "Asante kwa kuja kanisani leo. Mvua ilifanya usafiri kuwa mgumu kwa baadhi yenu, lakini nina furaha mmekuja. Hebu tuelekeze mawazo yetu kwa Mungu na ibada. Je, unaweza kusimama tunapoimba, 'Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu?'"
2. "'Nalifurahia waliponiambia, na twende nyumbani kwa BWANA!' Karibu katika nyumba ya Mungu! Katika Hekalu, Isaya alimwona Bwana juu na akiwa ameinuliwa. Alisikia malaika wakiimba 'Mtakatifu, mtakatifu, mtakatifu ni Bwana wa majeshi; dunia yote imejaa utukufu wake.' Ungana nami katika sifa tunapoimba 'Mtakatifu, Mtakatifu, Mtakatifu.'"

Kiongozi wa kwanza alitukumbusha ugumu wa safari; kiongozi wa pili alitukumbusha furaha ya ibada. Kiongozi wa kwanza alianza kwa maneno ya kawaida; kiongozi wa pili alianza na Neno la Mungu. Kiongozi wa kwanza alitangaza wimbo wa kawaida; kiongozi wa pili alitukumbusha kwamba malaika huimba wimbo huu kwa kumsifu Mungu. Ni kanisa gani litaimba kwa shauku zaidi?

Baada ya mashambulizi ya kigaidi ya Septemba 11, 2001 nchini Marekani, waumini walikusanyika katika makanisa yao siku ya Jumapili kwa ajili ya ibada kama kawaida. Linganisha ufunguzi wa ibada kutoka kwa makanisa haya mawili:

1. "Asante kwa kuungana nasi leo. Hii imekuwa wiki ya huzuni katika taifa letu. Wengi wetu tunahuzunika. Asante kwa kuja kuabudu hata katika wakati huu wa giza. Tutaanza kwa kuimba 'Msalaba uliochakaa.'"
2. "Mungu kwetu sisi ni kimbilio na nguvu, Msaada utakaoonekana tele wakati wa mateso. Katika nyakati hizi ngumu, hatupaswi kusahau kwamba yeye ndiye tumaini letu; Yeye ndiye kimbilio letu. Jiunge pamoja tunapokumbuka kwamba 'Ngome Yenye Nguvu Ni Mungu Wetu, ngome isiyoshindwa kamwe.'"

Kiongozi wa kwanza aliwakumbusha waumini juu ya huzuni yao; kiongozi wa pili aliwakumbusha kuwa Mungu ndiye tumaini lao. Maandiko na utenzi kulingana na andiko hilo ulitoa msingi thabiti katika juma ambalo uthabiti wa watu ulikuwa ukijaribiwa.

Maandiko yanaweza kutumika katika sehemu nyingoi za Ibada:

- Maneno ya ufunguzi wa Ibada
- Mwaliko wa kutoa sadaka
- Maneno ya wimbo
- Maombi

Ibada yetu inapaswa kujazwa na Neno la Mungu. ibada ni majibu kuhusu ufunuo wa Mungu juu yake mwenyewe katika Neno lake. Maandiko yanapaswa kuwa msingi wa sehemu zote za ibada.

**Usomaji wa Maandiko Unapaswa Kupokea Nafasi Kuu Katika Ibada**

Je, umewahi kumsikia mchungaji akisema, "Tuna muda mfupi leo na nina mahubiri marefu, kwa hivyo nitaruka usomaji wa vifungu vya biblia?" Ni lipi lililo la maana zaidi, Neno la Mungu au maneno yetu? Ni lazima tutoe muda kwa maandiko katika ibada.

Kwa sababu usomaji wa maandiko ni ibada, tunapaswa kuzingatia jinsi tunavyosoma. Inapaswa kusomwa kwa uwazi na kwa usahihi. Msomaji (awe mchungaji au mtu wa kawaida) anapaswa kufanya mazoezi kabla ya ibada. Katika karne tatu za kwanza za kanisa, nafasi ya msomaji wa maandiko ilikuwa amana takatifu. Wasomaji waliweka vitabu walivyopangiwa nyumbani na kufanya mazoezi ya usomaji. Waliposoma katika ibada, walikuwa tayari kusoma kwa uwazi na kwa kueleza.[55]

Kumbuka, hili ni Neno la Mungu linalosomwa katika nyumba ya Mungu kwa watu wa Mungu kama tendo la ibada. Ikiwa nyimbo za ibada zinastahili mazoezi, Neno la Mungu linastahili mazoezi pia. Si jambo la kujivunia uwezo wetu; ni jambo la kuhakikisha kwamba Neno la Mungu linawasilishwa kwa wasikilizaji. Hili ni Neno la Mungu; ni muhimu!

Tunapaswa kufanya usomaji uwe na maana. Kutumia aina tofauti za usomaji kutafanya andiko kuwa safi katika masikio ya wasikilizaji.

**(1) Wakati fulani andiko linaweza kusomwa na kiongozi huku waumini wakimsikiliza Mungu akisema**. Aina hii ya usomaji inafaa kwa sehemu kubwa ya vitabu vya musa na vitabu vingi vya unabii.

**(2) Wakati mwingine kiongozi na waumini wanaweza kubadilishana usomaji.** Zaburi nyingi zinafaa kwa aina hii ya usomaji wa kuitikia.

---

[55] Keith Drury, *The Wonder of Worship,* (Fishers, IN: Wesleyan Publishing House, 2002), 35

► Soma Zaburi 136. Mpe kiongozi wa darasa kuanza kila mstari; darasa linapaswa kujibu kwa nusu ya pili ya kila mstari, "kwa maana fadhili zake ni za milele."

Heri zinafaa kwa usomaji wa kuitikia (Mathayo 5:1-10):

*Kiongozi*: Heri walio maskini wa roho,
*Waumini*: Maana ufalme wa mbinguni ni wao.
*kiongozi*: Heri wenye huzuni,
*Waumini*: Maana hao watafarijika.

**(3) Maandiko mengine yanaweza kusomwa na waumini kwa umoja.** Kama wimbo wa pamoja, kusoma maandiko kama mwili kunaonyesha umoja wa kanisa. Kanisa lote linaungana katika kunena Neno la Mungu. Maombi kama vile kwenye Zaburi 124 yanafaa kwa usomaji wa pamoja.

Simulizi ya Nehemia kuhusu kusomwa kwa sharia na Ezra kunaonyesha matokeo ya kuwa na maandiko kama kitovu katika ibada yetu.

► Soma Nehemia 8 tena ikiwa unataka kupitia upya simulizi hii.

Angalia maelezo ya usomaji.

- Ezra akakifungua kitabu mbele ya macho ya watu wote. Kulikuwa na muunganisho wa kuona na Neno.
- Alisimama juu ya watu wote. Msomaji angeweza kuonekana wazi na kusikika.
- Alipoanza kusoma, watu wote wakasimama. Kulikuwa na mwitikio wa kimwili kwa Neno.
- Alipokuwa akisoma, watu wote wakajibu, "Amina, Amina," wakainua mikono yao, wakainamisha vichwa vyao, wakamsujudia BWANA kifudifudi. Walionyesha utii wao kwa Neno la Mungu.
- Walawi wakaisoma sheria ya Mungu kwa uwazi, wakatoa maana, hata watu wakaelewa usomaji huo. Walitoa umakini kwenye kuelewa Neno la Mungu. Hili ndilo lengo la mahubiri leo.
- Watu walilia, waliposikia maneno ya sheria. Nehemia aliwaamuru wafurahi, "kwa kuwa furaha ya BWANA ni nguvu zenu." Neno la Mungu lilichochea toba na shangwe.

Ingawa si kila jambo la tukio hili maalum litarudiwa katika ibada zetu, simulizi hii inaonyesha nguvu ya Maandiko. Ni lazima tuweke Maandiko kuwa kitovu cha ibada zetu.

### Kujipima

Je, waumini wako wanatambua umuhimu wa kusoma Biblia katika ibada? Eleza baadhi ya tabia na mwitikio ambao unauona unapotazama kuzunguka kanisa wakati wa usomaji wa maandiko.

Kwa wastani wa kila Jumapili, ni vifungu vingapi tofauti vya Maandiko husikilizwa na waumini wako? Je, waabudu wanajua kwa nini kila kifungu kimejumuishwa?

**Mahubiri Ya Neno Yanapaswa Kuwa Kitovu Kikuu Katika Ibada Zetu**

Kama vile mitindo ya muziki inavyobadilika katika kila kizazi, mitindo ya kuhubiri inabadilika ili kukidhi mahitaji ya kila kizazi. Maandiko hayafafanui mtindo mmoja wa muziki kama mtindo wa kibiblia wa muziki wa Ibada; Maandiko hayafafanui njia moja ya kuhubiri kama mtindo wa kibiblia wa kuhubiri.

Mtindo unaweza kubadilika kutoka kizazi hadi kizazi na kutoka utamaduni hadi utamaduni; maudhui lazima yasibadilike. maandiko hayafafanui mtindo wa muziki, lakini yanafafanua maudhui. Vivyo hivyo, mitindo ya kuhubiri inaweza kubadilika kutoka kizazi hadi kizazi, lakini maudhui lazima yasibadilike.

Mahubiri katika maandiko yanaonyesha kwamba kuhubiri Neno la Mungu ni jukumu kuu la mhubiri anayesimama mbele ya kanisa. Shabaha kuhusu Neno la Mungu lazima Ibaki kuwa kiini katika mahubiri ya kisasa. Kubadilisha teknolojia na mitindo ya kujifunza kunaweza kuathiri mtindo wa kuhubiri; maudhui lazima yabaki na mizizi katika maandiko.

**Mahubiri kama Ibada: Matokeo ya Kivitendo**

Je, ni matokeo gani ya vitendo ya kuona mahubiri kama ibada? Hilo litaathirije namna yetu ya kuhubiri?

> "Ikiwa kuhubiri si tendo la ibada, basi huenda kanisa likaishia kumwabudu mhubiri badala ya kumwabudu Mungu."
>
> - Warren Wiersbe

> "Kuhubiri, kama si ibada, ni unajisi…. Mahubiri ya kweli ni tendo la Mungu, na si utendaji tu wa mwanadamu."
>
> - Adapted from J.I. Packer

***Kuhubiri kunahitaji Maandalizi Mazuri.***

Ikiwa kuhubiri ni ibada, tunawajibika kujiandaa kwa uangalifu. Ni lazima tutoe kilicho bora kwenye madhabahu ya Mungu. Daudi hangempa kitu kisichomgharimu; hatupaswi kuleta mahubiri ambayo hatujayatayarisha kama zawadi yetu kwa Mungu. Tunapaswa kuyaandaa kwa umakini mahubiri yetu kabla ya ibada (2 Samweli 24:24).

***Kuhubiri kunahitaji Mwitikio kutoka kwa Waumini***

Ikiwa kuhubiri ni ibada, Itahitaji mwitikio kutoka kwa waumini. Katika ibada tunamuona Mungu, Tunajiona sisi wenyewe, na tunaona uhitaji wa dunia yetu (Isaya 6:1-8; angalia somo la 1.). Mahubiri yetu yanapaswa kumfunua Mungu kwa msikilizaji, mahubiri yetu yanapaswa kumfanya msikilizaji kugeuka katika njia zake, na mahubiri yetu yanapaswa kuhamasisha kanisa kufikia ulimwengu uliopotea. Kuhubiri kama ibada kutaleta hatia kwa wenye dhambi na kutawatia moyo waumini katika uinjilisti.

***Kuhubiri kunahitaji mwitikio kutoka kwa mhubiri.***

Ikiwa kuhubiri ni ibada, tutatambua kwamba kuhubiri kunahitaji mwitikio kutoka kwetu. Tukijiandaa kuhubiri kama tendo la ibada ya Kujidhabihu, tutamwona Mungu;

tutahukumiwa kwa maeneo ya uhitaji katika maisha yetu wenyewe; na tutaona mahitaji ya ulimwengu unaotuzunguka. Kwa kujibu, tutalia pamoja na Isaya, "Mimi hapa; nitume mimi." Mahubiri ya kweli yatambadilisha mhubiri. Hatupaswi kuleta ujumbe wa Mungu kwa waumini wetu hadi Mungu azungumze nasi kibinafsi na sisi tumeitikia.

Yesu hakuwakemea waandishi (wahubiri) wa siku zake kwa mahubiri mabaya; aliwakemea kwa kushindwa kuishi yale wanayohubiri. Walijua maandiko na jinsi ya kueleza maandiko, lakini hawakubadilishwa na maandiko. Yesu alisema, "Hunena lakini hawatendi" (Mathayo 23:3). Ikiwa kuhubiri ni ibada, sisi kama wachungaji tutabadilishwa na kweli tunazohubiri. Naye, Mungu atazungumza kupitia sisi ili kubadilisha mioyo na maisha ya watu tunaowahubiria.

***Mhubiri lazima awezeshwe na Roho Mtakatifu.***

Ikiwa kuhubiri ni ibada, mhubiri lazima awezeshwe na Roho Mtakatifu. Kama vile maeneo mengine yote ya ibada yanamtegemea Roho Mtakatifu kwa nguvu za kweli, mhubiri lazima awe ametiwa mafuta na Roho wa Mungu ili awe na ufanisi.

► Soma 2 wakorintho 3:3-18.

Tunajidhabihu katika maandalizi ya mahubiri; hata hivyo, baada ya maandalizi yetu kukamilika, nguvu katika kuhubiri huja kupitia Roho Mtakatifu. Bila nguvu za Roho Mtakatifu, tunaweza kuzungumza kwa akili, tunaweza kuvutia waumini, na tunaweza kuwa na maudhui mazuri, lakini hatutabadilisha maisha yao.

**Kujipima**

Je, mahubiri yako ni tendo la ibada kibiblia? Ikiwa mtu anakusikiliza ukihubiri mara kwa mara, je, atasikia ukweli wa kibiblia unaofaa?

## Hatari za Ibada: Kupotea Kwa Neno

Biblia imepoteza nafasi yake katika maisha ya kila siku ya watu wengi wanaojiita waumini. Cha kusikitisha ni kwamba pia imepoteza nafasi yake katika ibada ya kila wiki ya makanisa mengi. Ambapo kanisa la kwanza liliimba zaburi, baadhi ya makanisa leo huimba nyimbo zenye maudhui machache ya kibiblia au hayana kabisa. Ambapo kanisa la kwanza lilisoma vifungu virefu vya Maandiko, leo baadhi ya makanisa husoma vifungu vichache pekee kabla ya hotuba. Kwenye ibada nyingi, nyimbo na mahubiri yasiyotoa kipaumbele kikubwa kwa Neno la Mungu yamekuwa mbadala wa Nafasi ya Maandiko.

Baadhi ya viongozi katika vuguvugu la kisasa la kuabudu wanasisitiza kwamba usomaji wa hadhara wa maandiko haugusi tena mahitaji ya kisasa. Hivi majuzi mchungaji mmoja mashuhuri aliwaomba wafanyakazi wa kanisa lake kutathmini mahubiri yake. Walimwambia kwamba anatumia Biblia nyingi kupita kiasi! "Ni vizuri kwako kujenga mahubiri yako kwenye Biblia, lakini unapaswa haraka kuelekea kwenye jambo linalohusiana vinginevyo tutakoma kusikiliza." Wafanyakazi hawa wa kanisa hawakufikiria kwamba Biblia ilikuwa muhimu kwa watu leo!

Kama viongozi wa ibada, lazima tudumishe umuhimu wa maandiko katika ibada. Katika ibada, tunazungumza na Mungu kupitia maombi na nyimbo za sifa. Katika ibada, tunamsikia Mungu akisema nasi kwa kusoma na kuhubiri Neno. Bila kujali mtindo wetu wa kuabudu, hatupaswi kamwe kupoteza umuhimu wa Neno la Mungu katika ibada.

► Pitia Nehemia 8. Tengeneza orodha ya kila kifungu cha maneno kinachoonyesha thamani ambayo watu waliweka katika usomaji wa Sheria. Linganisha hili na usomaji wa maandiko katika ibada yako leo. Jadili hatua moja ya vitendo ambayo inaweza kuongeza matokeo ya maandiko katika ibada yako.

## Umuhimu Wa Maombi Katika Ibada

Katherini[56] ni Mkristo aliyejitolea. Hata alipokuwa shuleni, alijitenga na Mungu kila asubuhi. Kabla ya kifungua kinywa, alitumia wakati katika Biblia na Maombi.

Lakini kwa kuwa sasa yeye ni mama wa watoto wanne, maombi na usomaji wa Biblia unazidi kuwa mgumu. Mtoto mmoja ni mtoto mchanga na humwamsha Katherini wakati wa usiku. Katherini hujikuta kwamba mara nyingi anapata shida kuamka kitandani asubuhi kabla watoto hawajaamka. usiku, anakuwa amechoka sana hivyo hawezi kuzingatia maombi na kusoma Biblia.

Katherine ana furaha Jumapili inapofika. Kila Jumapili, yeye hutiwa nguvu kiroho wakati wa ibada, lakini katikati ya wiki huvunjika moyo. Anahisi kwamba maisha yake ya ibada yamekuwa kushindwa kabisa.

► Tafadhali mpe Katherine ushauri wa vitendo kwa maisha yake ya ibada.

Tulianza somo hili kwa kujifunza Maandiko katika ibada. Tutaendelea na somo la maombi katika ibada. Katika Maandiko, Mungu anazungumza nasi; katika maombi, tunamjibu Mungu. Maandiko na maombi yanapaswa kujaza ibada yetu.

### Maombi ya Hadhara na ya Kibinafsi katika Ibada ya Biblia

Tumeona kwamba kitabu cha Zaburi kilikuwa kitabu cha nyimbo za ibada ya Kiyahudi. Pia kilikuwa "kitabu cha maombi" kwa ajili ya ibada ya Kiyahudi. Zaburi zilihusisha maombi ya ibada ya hadharani na maombi ya faragha. Maombi ya hadharani na ya faraghani ilikuwa muhimu kwa ibada ya Kiyahudi.

Nyumbani, wayahudi waaminifu waliomba mara tatu kwa siku (Danieli 6:10).[57] . Zaburi nyingi ni maombi ya faragha. Haya yanaweza kutambuliwa kwa matumizi ya **mimi** badala ya **sisi** katika maombi. Mifano ya zaburi za maombi ya faragha ni pamoja na:

- Zaburi 18 – wimbo wa shukrani

---

[56] Habari ya Katherini imenukuliwa kutoka kwenye kitabu cha Keith Drury, *The Wonder of Worship,* (Fishers, IN: Wesleyan Publishing House, 2002), 17.
[57] Kufuatisha desturi ya Danieli ilikuwa kawaida kwa wayahudi waaminifu.

- Zaburi 32 – Maombi ya furaha kwa ajili ya msamaha[58]
- Zaburi 38 – Maombi ya Toba
- Zaburi 41 – Maombi ya Rehema
- Zburi 51 – Maombi ya Toba
- Zaburi 88 – Maombolezo wakati wa mateso
- Zaburi 116 – Wimbo wa shukrani kwa utunzaji wa Mungu

Hekaluni, waabudu wa Kiyahudi waliungana pamoja katika maombi ya hadhara. Wakati wa kuwekwa wakfu kwa Hekalu, Sulemani aliongoza maombi ya kitaifa kwa ajili ya kibali cha Mungu kwa watu (2 Mambo ya Nyakati 6). Isaya alileta ujumbe wa Mungu kwa Yuda; "Kwa maana nyumba yangu itaitwa nyumba ya sala kwa mataifa yote" (Isaya 56:7). Baada ya Uhamisho, ibada ya sinagogi ilikazia usomaji wa Sheria na maombi. Ibada katika sinagogi zilianza kwa mfululizo wa maombi.

Utaratibu wa maombi wa Kiebrania uliendelea katika kanisa la kwanza. Wakristo wa karne ya kwanza waliomba mara tatu kwa siku nyumbani. Wakristo walipokutana pamoja kwa ajili ya ibada, walisali kama mwili mmoja. Sala ya Bwana ilikuwa sehemu ya kila ibada. Maombi mengine yalitolewa katika kila ibada.

**Maombi Katika Ibada Leo**

Ikiwa maombi yalikuwa muhimu katika ibada ya kibiblia, maombi yanapaswa kuwa muhimu katika ibada yetu leo. Maombi ya hadhara na ya faragha ni muhimu.

> "Wakristo wengi zaidi wanaamini katika ibada za kibinafsi kuliko kuwa nazo."
>
> - Keith Drury

**Maombi ya faragha** hutuunganisha na Mzabibu na hutoa lishe kwa maisha yetu ya kiroho. Ukosefu wa maombi ya kibinafsi unaweza kuelezea ukosefu wa nguvu za kiroho katika makanisa mengi. Ikiwa Yesu alihitaji nyakati za maombi ya faragha wakati wa huduma yake hapa duniani, je, ni kwa kiasi gani tunategemea maombi ili kupata lishe ya kiroho na nguvu katika huduma.

**Maombi ya hadhara** ni kipengele muhimu cha ibada. Makanisa mengine hayazingatii sana maombi. Mchungaji mmoja alitetea ukosefu wa maombi ya hadharani katika kanisa lake kwa kusema, "Huwezi kuwavutia watu macho yao yakiwa yamefumbwa."[59] Aliamini kuwa kufurahisha watazamaji ni muhimu zaidi kuliko kumpendeza Mungu.

Maombi ya ushirika husahihisha wazo potofu kwamba Ukristo unanihusu mimi tu na uhusiano wangu na Mungu; sisi ni sehemu ya mwili wa Kristo. Tunaposikia mahitaji ya maombi na kujiunga katika maombi ya pamoja, tunatambua ugonjwa wa Mkristo mwenzetu, maumivu ya kihisia, na hali za maisha. Maombi ya pamoja yanatukumbusha

---

[58] Yawezekana Zaburi hii iliandikwa mara tu baada ya toba ya Daudi katika Zaburi ya 51.
[59] Imenukuliwa kwa Keith Drury, *The Wonder of Worship,* (Fishers, IN: Wesleyan Publishing House, 2002), 28.

kwamba washirika wa kanisa ni mwili mmoja. Maombi ya ushirika hutukumbusha kwamba Mungu anajali kanisa kama mwili wake.

Kama vile maandiko yanavyopaswa kutumika katika ibada yote, maombi yanapaswa kutolewa katika ibada nzima. Kuanzia maombi ya ufunguzi ambayo yanakaribisha uwepo wa Mungu katika ibada, hadi wakati uliolengwa wa maombi kwa ajili ya mahitaji ya watu, hadi maombi ya kufunga ya baraka ambapo washirika wanakuwa wakioondoka kuhudumia ulimwenguni, maombi yanapaswa kuzingatia ibada yetu.

## Kufanya Maombi Kuwa Kitovu Cha Ibada

Je, ni baadhi ya njia zipi za kivitendo ambazo tunaweza kufanya maombi kuwa sehemu ya maana zaidi katika ibada ya hadharani? Hapa kuna mapendekezo sita ya kivitendo.

### Sitawisha Maisha Yako ya Maombi ya Kibinafsi

Hakuna aliye tayari kuwaongoza wengine katika ibada hadi aanze kuabudu. Hakuna aliye tayari kuongoza Maombi ya hadhara mpaka awe ameomba kwanza faraghani. Ni pale tu tunapokuza maisha ya maombi ya faragha ndipo tunapowezeshwa kuongoza katika maombi ya hadhara. Kama kiongozi wa ibada, jitolee kuwa na nidhamu ya maombi ya faragha ya kila siku.

> "Jambo kuu katika maisha ya Kikristo ni uzoefu wa kila siku wa ibada na kumwabudu Mungu kama kitovu cha maisha yetu binafsi."
>
> - Dennis Kinlaw

### Jifunze Jinsi ya Kuomba

Wanafunzi wa Yesu waliuliza, "Tufundishe sisi kusali" (Luka 11:1). Ili kujibu, Yesu alifundisha sala ya kielelezo inayoitwa Sala ya Bwana. Sala unaweza kujifunza.

Kwa kiwango fulani, maombi ni ya asili kwa kila mtoto wa Mungu; hata hivyo, unaweza kujifunza sala. Mtoto mdogo anajifunza kuzungumza bila kuchukua masomo ya kuzungumza. Hata hivyo, mtoto anapokua, hujifunza zaidi kuhusu lugha, msamiati, na usemi unaofaa. Vivyo hivyo, kwa kawaida Mkristo mchanga hutamani kuzungumza na Mungu, lakini kadiri tunavyokomaa katika imani, uelewaji wetu na uthamini wetu wa sala huimarishwa.

Vitabu kuhusu maombi vinaweza kuongeza uelewa wako wa maombi. Vitabu vichache kuhusu maombi ambavyo vinaweza kumnufaisha kila Mkristo ni:

- *Power Through Prayer* (*Nguvu kupitia Maombi*) E.M. Bounds
- *With Christ in the School of Prayer* (*Pamoja na Kristo katika Shule ya Maombi*) by Andrew Murray
- *Mighty Prevailing Prayer (Maombi yenye Nguvu Inayotawala)* by Wesley Duewel

**Omba Maneno ya Maandiko**

Hakuna mahali pazuri pa kujifunza maombi kuliko katika maandiko. Shule ya kwanza ya maombi ni Biblia. Zaburi na maombi mengine ya kibiblia yanatufundisha kuomba kwa ufanisi. Kupitia historia ya kanisa, Wakristo wakuu wamejaza maombi yao na maandiko. Baadhi ya maombi makubwa katika Biblia ni pamoja na:

- ***Maombi ya Kutukuza.*** Kutoka 15:1-18, 1 Samweli 2:1-10, 1 Mambo ya Nyakati 29:11-20, Luka 1:46-55, Luka 1:68-79, 1Timotheo 6:15-16, na Ufunuo 4:8 -5:14.
- ***Mombi ya Kuungama***. Ezra 9:5-15, Zaburi 51, na Danieli 9:4-19.
- ***Maombi ya Kuombea wengine***. Mwanzo 18:23-33, Kutoka 32:11-14, Waefeso 1:15-23, na Wafilipi 1:9-11.

**Zingatia Kuhusu Ushirika na Mungu**

Mara nyingi, maombi yetu yanajikita tu kwenye kuomba vitu kutoka kwa Mungu. Watu wengine humpa Mungu orodha ya mahitaji yao ya maombi, wanamshukuru kwa kujibu maombi ya jana, na kusema "Amina." Maombi ya kweli lazima yawe zaidi ya orodha ya kupeleka mahitaji; maombi ni ushirika na Mungu.

Sala ya Bwana hutoa kielelezo cha maombi (Mathayo 6:9-13). Sala ya Bwana ilijumuisha:

- **Kutukuza**: "Baba yetu uliye mbinguni, Jina lako litukuzwe."
- **Utii: "**Ufalme wako uje, Mapenzi yako yatimizwe, hapa duniani kama huko mbinguni."
- **Ombi:** "Utupe leo riziki yetu.**"**
- **Kuungama:** "Utusamehe deni zetu, kama sisi nasi tuwasamehevyo wadeni wetu."
- **Maombi ya Mwongozo:** "Na usitutie majaribuni, lakini utuokoe na yule mwovu."
- **Sifa:** "Kwa kuwa ufalme ni wako, na nguvu, na utukufu, hata milele. Amina."

Wengi wa wakristo wanafuata mfano wa sehemu nne ambao unajumuisha kila moja ya vipengele katika maombi ya mfano wa Yesu: kutukuza, ungamo, kushukuru na Dua.

***Kutukuza***

Maombi hayapaswi kamwe kuacha kutukuza na kusifu. Kwa kuanza na sifa, tunahakikisha kwamba maombi yetu siyo tu orodha ya maombi ya msaada. Zaburi hutoa mfano wa maombi ambayo msingi wake ni sifa. Hata zaburi za maombolezo zinajumuisha sifa. Ikiwa maombi ni ibada ya kweli, itajumuisha kusifu na kumwabudu Mungu.

### *Kuungama*

Isaya 6 inaonyesha kwamba tunapomwona Mungu (kutukuza), tutajiona wenyewe. Tunapojiona katika nuru ya usafi kamili wa Mungu, tunaelewa hitaji letu la kuungama. Hakuna Mkristo, hata awe amekomaa kiasi gani, hata awe ametembea na Mungu kwa kiasi gani, hapaswi kufikia mahali ambapo atasema, "Sina haja ya kutubu. Ukamilifu wangu ni wa hakika." Yesu aliwaambia wanafunzi wake, "Msalipo, semeni … utusamehe dhambi zetu, kwa kuwa sisi nasi tunamsamehe kila tumwiaye." (Luka 11:4). Ibada ya kweli inahusisha kuungama.

### *Shukrani*

Kutukuza humsifu Mungu kwa jinsi alivyo; shukrani inamsifu Mungu kwa kile anachofanya katika ulimwengu wetu. Shukrani inatambua kwamba kila kutoa kuliko kwema, na kila kitolewacho kilicho kamili hutoka juu (Yakobo 1:17). Katika kushukuru, tunamshukuru Mungu kwa yale ambayo ametutendea katika maisha yetu. Hadithi ya wakoma 10 inaonyesha umuhimu wa kushukuru (Luka 17:12-19).

### *Dua*

Katika Sala ya Bwana, Yesu alionyesha kwamba Mungu anathamini maombi ya watoto wake. Mungu si kama mtawala wa kidunia ambaye ana shughuli nyingi sana kiasi kwamba atahangaishwa na mahitaji ya raia wa kawaida. Badala yake, Mungu ndiye Baba mkamilifu ambaye hufurahia kuwapa watoto wake zawadi nzuri. Katika Sala ya Bwana, tunatiwa moyo kuomba kwa ajili ya mahitaji ya kawaida ("tupe mkate wetu wa kila siku") na kwa ajili ya mwongozo wa kiroho ("usitutie majaribuni").

Katika Sala ya Bwana, tunajifunza kuwasilisha mapenzi yetu kwa Mungu tunapoomba. Tukiwa kama watoto wenye imani, tunajifunza kwamba mapenzi yake ni makamilifu; "hapana" yake ni kwa faida yetu. Maombi sio zana ya kichawi ya kumlazimisha Mungu kufanya mapenzi yetu. Maombi ni nidhamu ya kiroho ambayo hutuletea utii kwa furaha kwa mapenzi ya Mungu.

### Sawazisha Vipaumbele Vyako na vya Mungu.

Mara nyingi maombi huonyesha lililo muhimu zaidi kwetu. Ni nini kinachochochea maombi yetu ya dhati, mahitaji ya kimwili au mahitaji ya kiroho?

Katika maombi yake kwa ajili ya Wakristo wa Thesalonike, Paulo alisema, "twawaombea ninyi sikuzote, ili Mungu wetu awahesabu kuwa mmekustahili kuitwa kwenu, akatimiza kila haja ya wema na kila kazi ya imani kwa nguvu; jina la Bwana wetu Yesu litukuzwe ndani yenu, nanyi ndani yake…" (2 Wathesalonike 1:11-12) Dhumuni kuu la Paulo lilikuwa kwamba Mungu angetimiza kusudi lake katika maisha yao. Wakristo hawa walikuwa wakiteswa, lakini maombi ya Paulo haikuwa ili Mungu awaokoe kutokana na mateso. Badala yake, aliomba kwamba jina la Bwana Yesu litukuzwe ndani yao.

Kama vile maombi yetu yanavyoonyesha vipaumbele vyetu, shukrani zetu zinaonyesha vipaumbele vyetu. Ikiwa shukrani zetu ni kwa ajili ya baraka za kimwili, baraka za kimwili zinaweza kuwa kile tunachothamini zaidi. Ikiwa sehemu kubwa ya shukrani zetu ni kwa ajili ya msaada wa Mungu katika maisha yetu ya kiroho, kukua kiroho ndiko tunakothamini zaidi.

Katika maombi yake kwa ajili ya Wathesalonike, Paulo alitoa shukrani kwa Mungu kwa sababu imani yao ilikuwa ikiongezeka sana, na upendo wao kati yao ulikuwa ukiongezeka (2 Wathesalonike 1:3). Shukrani zake kuu zaidi hazikuwa kwa baraka za muda; shukrani zake kuu zaidi zilikuwa kwa ukuaji wao wa kiroho. Ni nini kinakupa sababu kuu ya shukrani, baraka za kifedha au ushahidi wa ukuaji wa kiroho katika maisha yako?

**Zungumza na Mungu, si kwa waumini.**

Kupitia maandiko, Mungu anazungumza na waumini. Katika maombi, waumini huzungumza na Mungu. Muda wa maombi ya hadhara sio fursa kwa kiongozi kuwaambia watu (kupitia maombi) anachotaka kuwaambia! Maombi huzungumza na Mungu.

Yesu aliwaambia wanafunzi wake jinsi ya kusali katika roho ya ibada ya kweli:

> Tena msalipo, msiwe kama wanafiki; kwa maana wao wapenda kusali hali wamesimama katika masinagogi na katika pembe za njia, ili waonekane na watu. Amin, nawaambia, Wamekwisha kupata thawabu yao. Bali wewe usalipo, ingia katika chumba chako cha ndani, na ukiisha kufunga mlango wako, usali mbele za Baba yako aliye sirini; na Baba yako aonaye sirini atakujazi. Nanyi mkiwa katika kusali, msipayuke-payuke, kama watu wa mataifa; maana wao hudhani ya kuwa watasikiwa kwa sababu ya maneno yao kuwa mengi. Basi msifanane na hao; maana Baba yenu anajua mnayohitaji kabla ninyi hamjamwomba (Mathayo 6:5-8).

Maombi ya kweli hayajaribu kumvutia Mungu au watu; yanazungumza kwa urahisi na uwazi kwa Baba yetu wa mbinguni.

► Utafanya nini ili kukua katika maisha yako ya kibinafsi ya maombi? Je, utafanyaje maombi kuwa sehemu ya maana zaidi katika ibada ya hadhara ndani ya kanisa lako?

## Sadaka Kama Mwitikio wa Neno la Mungu

Maombi ni mwitikio wa asili kwa Neno la Mungu. Kwa sababu hii, tunapaswa kufuata usomaji wa maandiko na mahubiri na kufanya maombi. Katika maombi, tunaitikia kweli ambayo tumepokea kutoka kwa Neno la Mungu; tunajitoa kwa utii.

Sadaka pia ni mwitikio kwa Neno la Mungu. Katika Agano la Kale, dhabihu (sadaka) ilikuwa mwitikio wa anayeabudu kwa Sheria (Neno la Mungu). Katika Agano Jipya, sadaka inaashiria kujisalimisha kwa Mungu wa maisha yetu yote.

Sadaka ni sehemu ya ibada. Mtunga-zaburi aliwahamasiha waabudu kuleta sadaka, na kuingia katika nyua zake (Zaburi 96:8). Mwandishi wa Waebrania aliunganisha ibada na kutoa; "lakini msisahahu kutenda mema na kushirikiana; maana sadaka kama hizi ndizo

zimpendezazo Mungu" (Waebrania 13:16). Paulo aliwaambia Wafilipi kwamba zawadi yao kwake ilikuwa ni sadaka yenye harufu nzuri, dhabihu inayokubalika na kumpendeza Mungu (Wafilipi 4:18).

### Theolojia Ya Utoaji Ibadani

Waenda kanisani wengi huona kuwa sadaka kama njia ya kulipa bili za kanisa. Hii inafanya sadaka kuwa shughuli ya kifedha badala ya tendo la kiroho la ibada. Uwakili wa Kikristo unapaswa kueleweka kama sehemu ya ibada. Kila moja ya kanuni zifuatazo inapaswa kuwa sehemu ya theolojia yetu ya utoaji.

#### *Utoaji ibadani huchochewa na neema, sio woga*

Utoaji kama kitendo cha ibada huchochewa na shukrani kwa Neema ya Mungu. Paulo aliwasihi Wakorintho kutoa msaada kwa wakristo wenye uhitaji huko Yerusalemu. Hakuwatishia, "Ni lazima utoe kwasababu ipo siku utahitaji msaada." Badala yake, Alihitimisha msisitizo wake na sifa, "Mungu ashukuriwe kwa sababu ya kipawa chake" (2 Wakorintho 9:15). Utoaji wao ungechochewa sana na shukrani kwa kipawa cha Mungu chenye neema. Ikiwa sadaka ni ibada ya kweli, hutoka kwenye moyo wa utayari.

#### *Utoaji ibadani huchochewa na upendo, sio thawabu*

Ibada ya kweli huchochewa na **upendo kwa Mungu**, sio tamaa ya kupata thawabu. Kipawa cha fedha ni ishara ya zawadi yetu sisi wenyewe kwa Mungu. Paulo aliwasifu Wakristo wa Makedonia kwa sababu "walijitoa nafsi zao kwa Bwana; na kwetu pia, kwa mapenzi ya Mungu" (2 Wakorintho 8:5). Karama zao zilikuwa ishara ya upendo wao kwa Mungu na kwa mitume walioleta injili katika eneo lao.

Kama vile muziki au shughuli nyingine yoyote ya ibada inaweza kufanywa kwa sababu zisizofaa, utoaji unaweza kuchochewa na tamaa ya kupata thawabu badala ya kumpenda Mungu. Wainjilisti wengine huahidi kwamba Mungu atalipa zawadi za pesa kwa baraka za kifedha. Kwa kupindisha maandiko kutoka katika muktadha wake wa kibiblia, wanaahidi thawabu mara mia kwa zawadi kwa Mungu. Utoaji huo hauwezi kuwa tendo la ibada ya upendo, bali utakuwa kama kununua tikiti ya bahati nasibu ambayo mtoaji anatarajia kushinda! Hakuna mahali popote ambapo Biblia husifu utoaji wa namna hii.

Badala yake, Biblia inapongeza utoaji wa Maria. Alipomtia Yesu mafuta, hakukuwa na thawabu yoyote mbele yake. Alimwaga akiba yake bila kufikiria kurudi. Hata wanafunzi walikasirika kwa sababu ya uharibifu wake. Ni Yesu pekee aliyeona na kusifu zawadi yake, zawadi ambayo ilichochewa na upendo pekee (Mathayo 26:6-13).

Utoaji ibadani hauchochewi tu na upendo kwa Mungu, bali **upendo kwa wengine**. Yohana aliwakumbusha wasomaji wake kwamba upendo wa kweli ni zaidi ya maneno; ni vitendo. Upendo wa Wafilipi kwa Paulo ulionekana katika utoaji wao. Upendo wa muumini kwa wengine unaonekana katika kutoa.

> Lakini mtu akiwa na riziki ya dunia, kisha akamwona ndugu yake ni mhitaji, akamzuilia huruma zake, je! Upendo wa Mungu wakaaje ndani yake huyo? Watoto wadogo, tusipende kwa neno, wala kwa ulimi, bali kwa tendo na kweli (1 Yohana 3:17-18).

***Utoaji wa ibadani huchochewa na ukarimu, sio ubakhili.***

Paulo alitoa changamoto kwa kanisa la Korintho kwa kutoa kwa ukarimu aliposema, "Mkitajirishwa katika vitu vyote mpate kuwa na ukarimu wote, umpatiao Mungu shukrani kwa kazi yetu." Ukarimu wao ulikuwa udhihirisho wa shukrani zao kwa Mungu. " maana utumishi wa huduma hii hauwatimizii watakatifu riziki walizopungukiwa tu, bali huzidi sana kuwa na faida kwa shukrani nyingi apewazo Mungu" (2 Wakorintho 9:11-12). Ili kutoa iwe ibada ya kweli, ni lazima kuwe na ukarimu.

***Utoaji wa ibadani huchochewa na unyenyekevu, sio kiburi.***

► Soma Mathayo 6:1-4.

Katika Mahubiri ya Mlimani, Yesu alionya kuhusu nia mbaya za kutoa. Wengine hutoa ili kupokea sifa kutoka kwa wengine; malipo yao ni sifa. " Wamekwisha kupata thawabu yao." Wengine hutoa kwa utulivu, huku wakijisifu kwa unyenyekevu wao; malipo yao ni kujitosheleza. Yesu akasema, "hata mkono wako wa kushoto usijue ufanyalo mkono wako wa kuume." Usijipongeze kwa ukarimu wako. Badala yake, mruhusu Baba yenu aliye mbinguni awaone na kuwapa thawabu kama apendavyo.

**Hadithi ya Kutoa kwa Furaha**

Yohana Wesley alikuwa amemaliza kununua picha za kupamba chumba chake wakati mjakazi alipokuja kwenye mlango wake. Ilikuwa siku ya baridi na aligundua kuwa alikuwa amevaa gauni jepesi tu. Aliingiza mkono mfukoni ili kumpa pesa ya kununua koti, na akakuta amebakiza pesa kidogo. Alilia, "Nimepamba kuta zangu kwa pesa ambazo zingeweza kumkinga kiumbe huyu maskini kutokana na baridi!"

Yohana alianza kupunguza matumizi yake ili apate pesa za kuwapa maskini. Katika jarida lake, alirekodi kwamba mwaka mmoja mapato yake yalikuwa milioni 5, na gharama zake za maisha milioni 4, hivyo alikuwa na milioni 1 kwa ajili alitoa. Mwaka uliofuata, mapato yake yaliongezeka maradufu, lakini bado aliishi kwa shilling milioni 4 na alitoa milioni 6. Katika mwaka wa tatu, mapato yake yalipanda hadi milioni 15; tena aliishi kwa milkoni 4, akitoa milioni 11 kwa wahitaji. Mwaka wa nne, alitengeneza milioni 20, akaishi tena kwa milioni 4, na akatoa milioni 16 kwa masikini.

Yohana alihubiri kwamba Wakristo hawapaswi kutoa zaka tu, bali watoe ziada. Aliamini kwamba kwa kuongeza mapato, utoaji wetu unapaswa kuongezeka. Alifanya mazoezi haya katika maisha yake yote. Hata mapato yake yalipoongezeka hadi mamilioni ya pesa, aliishi kwa urahisi na kutoa pesa za ziada. Mwaka mmoja mapato yake yalikuwa zaidi ya milioni

50; alitoa zote isipokuwa milioni 5.[60] Alisema kuwa hakuwahi kuweka zaidi ya milioni 20. Alitoa zaidi ya milioni 100 alizopata katika maisha yake.[61]

Hoja ya hadithi hii sio amri ya kisheria ya umaskini! Jambo kuu ni kumtii Mungu kwa furaha na kwa hiari. Mungu hawapi kila mtu mapato sawa na Yohana; Mungu halazimishi kila mtu kutoa kwa kiwango sawa na Yohana. Kipimo sio, "Je, mimi natoa kama mtu mwingine?" kipimo ni, "Je, ninamtii Mungu kwa furaha?" Mungu anatutaka tuabudu kwa kutoa dhabihu.

**Mazoezi Ya Kutoa**

Kwasababu utoaji ni kitendo cha ibada, sadaka zinapaswa kukusanywa kwa njia ambayo inahamasisha roho ya ibada. Zingatia mawazo ya kivitendo yafuatayo.

***Mkazo kuhusu sadaka unapaswa kuwa ni Ibada, na sio mahitaji.***

Labda sababu ambayo Wakristo wengi wanaona sadaka kimsingi ni njia ya kulipa gharama za kanisa ni kwamba msisitizo katika utoaji ni kulipa gharama! Hii inakuwa mbaya zaidi wakati shida ya kifedha inapotufanya kusema, "Kanisa litafungwa" au "Hatuwezi kutuma mmishonari" ikiwa sadaka za ukarimu hazijatolewa. Wakati mwingine mchungaji huomba msamaha kwa ajili ya kuomba sadaka; "ningependa tusiwe tunahitaji kuomba sadaka kwenu." Badala yake, sadaka inapaswa kuwa kielelezo cha shukrani yenye furaha.

Wakati wa kutoa sadaka, mkazo unapaswa kuwa ibada. Utoaji wa sadaka unaweza kutambulishwa kwa andiko linalowakumbusha waabudu kusudi la kutoa sadaka. Maandiko kama vile 2 Wakorintho 8:9 na 9:7, Kutoka 25:2, Matendo 20:35, na hata Yohana 3:16 yanaelekeza kwenye motisha ya kweli ya kutoa.

***Sadaka inapaswa kuwa sehemu ya Ibada yenyewe***

Katika tamaduni zingine, ni jambo la kawaida kuhimiza watu kutoa sadaka zao mbali na ibada yenyewe. Ingawa hii inaweza kuchochewa na tamaa ya kuepuka maonyesho au kuokoa muda katika ibada, inapelekea kutenganisha sadaka na ibada. Kuchukua sadaka kama sehemu ya ibada huwasaidia waabudu kuelewa utaoji kama tendo la ibada.

Kwa kuwa sadaka ni mwitikio wetu kwa Mungu, unaweza kufikiria kuchukua sadaka baada ya mahubiri kuliko kabla ya mahubiri. Hii inaonyesha, "Tunamtolea Mungu kwa kuitikia Neno lake."

***Wazazi wanapaswa kuwaanzishia watoto wao tendo la kutoa ibadani.***

Kama vile tunavyowafundisha watoto wetu kuimba, kusali, na kusikiliza maandiko yanayosomwa na kuhubiriwa, tunapaswa kuwafundisha watoto wetu kutoa kwa furaha.

---

[60] Kwa kulinganisha na hali ya leo, hii ni sawa na kupata Tsh 538,577,934 na kuitoa yote isipokuwa Tsh 13,464,448. Inakadiriwa Wesley alipata na kutoa kiasi cha Tsh 8,078,669,010 kwa thamani ya fedha za leo katika Maisha yake yote.
[61] Habari hii imenukuliwa kutoka kwa Charles Edward White, "Four Lessons on Money from One of the World's Richest Preachers" Christian History 19 (Summer 1988): 24. Inapatikana kupitia https://christianhistoryinstitute.org/uploaded/50cf76d05900d6.14390582.pdf Julai 22, 2020.

Watoto wetu wanapojifunza kwamba kutoa ni tendo la kusifu la shangwe, wao pia wanakuwa waabudu.

***Muziki wakati wa sadaka unapaswa kuwa ibada.***

Ikiwa sadaka ni ibada, muziki wakati wa sadaka unapaswa kuwa ibada. Muziki huu unaweza kuwa wa kutumia vyombo vya muziki au sauti; unaweza kuongozwa na muimbaji binafsi au kanisa zima; unaweza kuwa wa utulivu na wa kutafakari au furaha na shangwe; bila kujali mtindo, unapaswa kuwa sehemu ya ibada. Wale wanaohudumu wakati wa sadaka wanapaswa kuomba mwongozo wa Roho kama vile kiongozi wa ibada anavyoomba mwongozo wa Roho. Hakuna sehemu ya ibada inayopaswa kuchukuliwa kirahisi.

***Sadaka inapaswa kuambatana na maombi ya kujitolea.***

Kwa kuwa sadaka ni zawadi kwa Mungu, sadaka inapaswa kuambatana na maombi ya kujitakasa. Hilo huwakumbusha waabudu kusudi la kutoa na hutoa uthibitisho unaoonekana wa kutoa kama ibada.

***Viongozi wa kanisa wanapaswa kuwa mawakili wazuri wa karama za watu.***

Katika sadaka, waabudu wanakabidhi zawadi zao kwa uwakili wa viongozi wa kanisa. Viongozi wa kanisa lazima wawe watunzaji wazuri wa zawadi hizo. Hesabu kwa waumini kuhusu matumizi ya fedha huonyesha kwamba sadaka zinatumika kwa ajili ya kazi ya Mungu. Hii inachochea utoaji na kupunguza jaribu la kukosa uaminifu kwa uongozi wa kanisa. Katika ulimwengu ambao viongozi wa Kikristo wanatazamwa kwa shaka, tunapaswa kufanya kila linalowezekana kuonyesha kwamba sisi wenyewe hatuna hatia.

Sadaka ni zaidi ya njia ya kulipa bili; ni ibada. Kupitia Neno lake, Mungu anajifunua kwa waabudu. Tunaitika kwa kutoa zawadi za sadaka kutoka kwenye mioyo yenye furaha. Hii ndiyo ibada ya kweli.

**Kujipima**

Je, watu katika kanisa lako wanahisi kwamba wanaabudu wanapotoa sadaka, au wanalipa tu gharama za kanisa? Ni hatua gani zinazofaa unazoweza kuchukua ili kufanya sadaka iwe tendo la ibada?

## Meza Ya Bwana

► Jadili jinsi mnavyoadhimisha ibada ya ushirika katika kanisa lako. Je, unaadhimisha Meza ya Bwana mara ngapi? Unapofanya ushirika, je, ni sehemu muhimu ya ibada?

Kama vile Mungu anavyofunuliwa katika Neno **lililoandikwa** (usomaji wa maandiko) na katika neno **linalonenwa** (kuhubiriwa kwa Neno lake), anafunuliwa katika neno

**lililoonyeshwa** la Meza ya Bwana.[62] Meza ya Bwana ni ukumbusho wa kifo cha upatanisho cha Yesu na sherehe ya ufufuo wake. Karamu ya Mwisho ilihusiana na Pasaka, lakini pia ilizindua agano jipya.

► Soma Mathayo 26:17-30 na 1 Wakorintho 11:17-34.

Marejeleo ya Agano Jipya kuhusu Meza ya Bwana yanajumuisha maelezo katika injili na maagizo ya Paulo kwa kanisa la Korintho.

Maswali matatu mara nyingi huulizwa kuhusiana na kuadhimisha Meza ya Bwana.

- Je, nini maana ya Meza ya Bwana?
- Je, ni mara ngapi Meza ya Bwana inapaswa kuadhimishwa?
- Je, ni kwa jinsi gani Meza ya Bwana inapaswa kuadhimishwa?


> “Meza ya Bwana ni miadi ya Bwana na watu wake. Wale wanaoshika miadi hii pamoja na Kristo wanaweza kutarajia kwa uhakika kwamba watakuja kukutana naye.”
>
> - Franklin Segler na Randall Bradley

**Nini maana ya Meza ya Bwana**

Kuadhimisha Meza ya Bwana ni sehemu yenye maana katika ibada.[63] Paulo aliandika kwa kanisa huko korintho, akionyesha hilo katika Meza ya Bwana.

1. Tunatazama nyuma kwenye kifo cha Kristo ("unatangaza kifo cha Bwana").
2. Tunatazamia kurudi kwa Kristo ("mpaka atakapokuja").

Tunapoadhimisha Meza ya Bwana, tunakumbuka dhabihu yake, na tunatazamia kurudi kwake kwa ahadi. Vifaa vinawakilisha mwili na damu ya Kristo na vinatukumbusha ushiriki wetu katika kifo cha Bwana. “Kikombe cha baraka tukibarikicho, je, si ushirika katika damu ya Kristo? Mkate tuumegao, je, si ushirika wa mwili wa Kristo?” (1 Wakorintho 10:16) Meza ya Bwana ni ishara yenye nguvu ya kuendelea kuwepo kwa Bwana aliyesulubiwa na kufufuka.



**Je, Meza ya Bwana Inapaswa Kuadhimishwa Mara ngapi?**

Maandiko wala historia ya kanisa haitoi jibu la uhakika kwa swali hili. Katika kanisa la kwanza, inaonekana kwamba Meza ya Bwana ilichukuliwa kila Jumapili. Leo, baadhi ya

[62] Franklin M. Segler and Randall Bradley, *Christian Worship: Its Theology and Practice* (Nashville: B&H Publishing, 2006), 178

[63] Picha: "The Lord's Supper" impigwa na Allison Estabrook on Oct. 14, 2022, Umetolewa kutoka https://www.flickr.com/photos/sgc-library/52476662295 kwa ruhusa ya CC BY 4.0.

makanisa husherehekea Ushirika kila juma wakati wengine huiadhimisha mara moja au mbili tu kwa mwaka.

Maadamu Meza ya Bwana ni sehemu takatifu ya ibada, kuadhimisha mara kwa mara hakupunguzi maana ya Meza ya Bwana kama vile usomaji wa Biblia wa kila juma hakupunguzi umuhimu wa maandiko katika ibada.

**Je, ni kwa jinsi gani Meza ya Bwana inapaswa kuadhimishwa?**

Paulo aliwaonya Wakorintho kuhusu kula na kunywa "isivyostahili" (1 Wakorintho 11:27 ).[64] Hatua kadhaa zinazofaa zaweza kutusaidia kuadhimisha Meza ya Bwana kwa njia inayostahili umuhimu wake kwa wakristo.

***Ushirika Mtakatifu unapaswa kuwa sehemu kuu ya ibada, sio nyongeza.***

Wakati wa kawaida wa Meza ya Bwana ni baada ya mahubiri. Katika hali hii, mahubiri yanapaswa kutuongoza kuelewa kwa kina Zaidi kuhusu Meza ya Bwana. Hii inaweza kufanywa kupitia mahubiri yanayolenga moja kwa moja Meza ya Bwana, au kupitia mahubiri kuhusu mada inayohusiana (ukombozi, upatanisho, neema, ufuasi). Kwa makanisa yanayoadhimisha Meza ya Bwana mara kwa mara, haifai kulenga mada ya kila ibada kwenye Ushirika. Hata hivyo, inapaswa kuwepo uhusiano wa wazi kati ya maadhimisho ya Ushirika na ibada iliyotangulia.

***Ushirika Mtakatifu ni tukio kuu na la furaha.***

Ushirika ni wakati wa kujichunguza na kusherehekea neema ya Mungu kwa furaha. Maadhimisho haya yanaakisiwa katika ukumbusho kwamba Meza ya Bwana huliwa kwa kukumbuka kifo cha Bwana. Furaha ya maadhimisho hayo inaonekana katika ahadi ya kurudi kwa Bwana.

Wakati fulani, kusherehekea ufufuo na kutazamia kurudi kwa Kristo kunaweza kuwa mkazo mkuu katika Ushirika. Wakati mwingine, sherehe kuu ya kifo cha Yesu na umuhimu wa kujichunguza mwenyewe kunaweza kuwa mkazo mkuu. Vipengele vyote viwili ni sehemu ya maadhimisho haya.

Tunafurahi katika Ushirika Mtakatifu kwa sababu Meza ya Bwana inawezekana kwa neema ya Mungu. Katika Meza ya Bwana, tunakumbushwa kwamba neema pekee hutoa wokovu wetu. Tunatambua maadhimisho ya Ushirika kwa sababu tunakumbuka kwamba kushiriki kwetu katika Meza ya Bwana kunawakilisha kujitolea binafsi kuikimbia dhambi. Katika Meza ya Bwana, kila mwabudu lazima ajichunguze mwenyewe.

---

[64] Katika KJV "kunywa isivyostahili" wakati mwingine inatafsiriwa kurejelea mtu asiye stahili meza ya Bwana. Walakini, katika "kwa namna isiyostahili" inaonekana kuwa ni tafsiri bora. Hakuna mtu anayestahili dhabihu ya Yesu. Tatizo la kusahihisha katika Korinto ilikuwa sio kutokustahili mwabuduji, lakini kutokuheshimu, namna isivyostahili ilikuwa ni njia isiyostahili ambayo walikuwa wakishiriki mlo huu mtakatifu.

***Ushirika unapaswa kuonyesha umoja wa kanisa.***

Inasikitisha kwamba Ushirika, agizo ambalo lilikusudiwa kuakisi umoja wa kanisa, wakati mwingine imekuwa sababu ya mgawanyiko. Tofauti za jinsi Meza ya Bwana inavyotolewa (vikombe vya mtu binafsi, kikombe cha kawaida, kuchovya mkate ndani ya kikombe) na tofauti za nani anaweza kushiriki (wote wanaojiita waumini, wale tu ambao wamebatizwa, washiriki wa kanisa la mahali pekee) zimeongoza kuleta mgawanyiko kati ya makanisa.

Paulo alikumbusha kanisa la Korintho kwamba waliposhiriki mkate mmoja, lazima wawe mwili mmoja. "Kwa kuwa mkate ni mmoja, sisi tulio wengi tu mwili mmoja; kwa maana sisi sote twapokea sehemu ya ule mkate mmoja" (1 Wakorintho 10:17).

Tunapaswa kukumbuka kwamba katika Ibada ya Ushirika, kuabudu ni ya msingi huku taratibu zikiwa za pili. Ni lazima kanisa lidumishe taratibu ambazo ni aminifu kwa injili na 1 Wakorintho. Hata hivyo, bila kujali njia ambayo Meza ya Bwana inaandaliwa, haipaswi kuleta mgawanyiko. Katika Meza ya Bwana, tunasherehekea umoja wa kanisa.

## Hitimisho: Ushawishi Mkubwa wa Ibada

Je, ibada ni muhimu? Hapa kuna ushuhuda kutoka 1945 unaoonyesha kile kinachoweza kutokea wakati mtu wa kawaida anaabudu kwa njia ya maombi.

Wakati wa Vita vya pili ya Dunia, mwanafunzi wa Kijapani-mmarekani aliyekuwa wa Imani ya kibbudha na kubadilika kuwa mkristo, katika Chuo Kikuu cha Baylor alikua chombo cha uamsho. Reiji Hoshizaki alifanya kazi kama mlinzi wa nyumba ili kulipa ada ya shule. Wakati alipokuwa akisafisha madarasa, alianza kuomba kando ya kila dawati.

Siku moja, baada ya wiki kadhaa za maombi, Reiji alikuwa ameketi darasani alipovamiwa na mzigo kwa ajili ya wanafunzi wenzake hivyo alipiga magoti na kuanza kulia na kuomba. Wanafunzi waliuliza, "Reiji ana shida gani?" Hakuna kibaya kilichokuwa kimemtokea Reiji; kiti chake kimekuwa madhabahu yake.

Kupitia maombezi ya Reiji, uamsho ulienea katika Chuo Kikuu cha Baylor na kisha kwenda jimbo la Texas. Makumi ya wainjilisti wanafunzi waliondoka chuo cha Baylor kwenda kuchukua uamsho katika kusini-magharibi mwa Marekani. Maombi ni sehemu muhimu ya ibada. Tunapoabudu, ulimwengu wetu unabadilishwa na nguvu za Mungu.

## Mapitio ya Somo la 7

(1) Tunaweza kufanya Maandiko kuwa kitovu cha ibada kwa kuingiza Maandiko katika sehemu zote za ibada yetu.

(2) Kwa kuwa maandiko ni muhimu katika ibada, tunapaswa kuhakikisha kwamba yanasomwa kwa ufasaha, kwa uwazi, na kwa njia mbalimbali ambazo zitafanya usomaji kuwa safi.

(3) Kwa kuwa Mahubiri ni sehemu ya ibada:

- Kuhubiri kunahitaji maandalizi mazuri.
- Kuhubiri kunahitaji mwitikio kutoka kwa waumini.
- Kuhubiri kunahitaji mwitikio kutoka kwa mhubiri.
- Mhubiri lazima awezeshwe na Roho Mtakatifu.

(4) Njia za vitendo za kufanya maombi kuwa sehemu ya maana katika ibada ya pamoja:

- Sitawisha maisha yako ya maombi ya kibinafsi.
- Jifunze jinsi ya kuomba.
- Omba maneno ya maandiko.
- Zingatia kuimarisha ushirika na Mungu.
- Sawazisha vipaumbele vyako na vya Mungu.
- Zungumza na Mungu, si kwa waumini.

(5) Kwa kuwa sadaka ni sehemu ya ibada:

- Utoaji unapaswa kuchochewa na neema, si na hofu.
- Kutoa kunapaswa kuchochewa na upendo, si thawabu.
- Kutoa kunapaswa kuwa kwa ukarimu, sio ubahili.
- Utoaji unapaswa kuchochewa na unyenyekevu, sio kiburi.
- Jinsi tunavyokusanya sadaka inapaswa kuchangia roho ya ibada.

(6) Meza ya Bwana

- Inatazama nyuma kwenye kifo cha Kristo.
- Inatazamia kurudi kwa Kristo.
- Inapaswa kuzingatiwa kwa njia inayofaa.
- Inapaswa kuzingatiwa kwa njia ya heshima na ya furaha.
- Inapaswa kuzingatiwa kwa namna inayoakisi umoja wa kanisa.

## Somo la 7 Mazoezi

(1) Katika Somo la 6, ulichagua nyimbo zinazohusiana na mada tano tofauti. Kwa kila moja ya mada hizi tano, tafuta marejeo 3-4 ya maandiko yanayozungumzia mada hiyo. Orodha zako zitatumika katika somo la baadaye unapopanga ibada.

- 3-4 mistari kuhusu asili ya Mungu
- 3-4 mistari kuhusu Yesu na kifo chake na kufufuka kwake
- 3-4 mistari Roho Mtakatifu na kanisa
- 3-4 mistari inayowaita watu kujitolea, maisha matakatifu
- 3-4 mistari kuhusu uinjilisti na umisheni

(2) Mwanzoni mwa somo linalofuata, utafanya mtihani kulingana na somo hili. Jifunze maswali ya mtihani kwa uangalifu katika maandalizi.

## Jaribio Somo la 7

(1) Orodhesha mifano mitatu inayoonesha umuhimu wa Maandiko katika ibada.

(2) Taja sehemu tatu za ibada ambayo maandiko yanaweza kutumika.

(3) Orodhesha athari nne za kivitendo za kanuni ya kwamba *kuhubiri ni ibada.*

(4) Orodhesha mapendekezo matatu yanayofaa ya kufanya maombi kuwa sehemu ya maana ya ibada ya pamoja.

(5) Orodhesha kanuni nne za kitheolojia za utoaji wa sadaka ibadani.

(6) Orodhesha mawazo manne ya kivitendo yanayoonyesha utoaji ni tendo la ibada.

(7) Orodhesha vipengele viwili vya Meza ya Bwana vinavyotambuliwa katika 1 Wakorintho.

(8) Andika Mathayo 6:5-8 kutoka kwenye kumbukumbu yako.

# Somo la 8
# Kupanga na Kuongoza Ibada

## Malengo ya Somo

Mwisho wa somo hili, mwanafunzi anapaswa:

(1) Kutambua umuhimu wa kuwa tayari kiroho kwa uongozi wa ibada.

(2) Kuelewa jukumu la muundo na mada katika huduma za ibada.

(3) Kupanga huduma za ibada zenye uwiano zinazozungumza na mwili wote wa Kristo.

(4) Kuthamini sifa zinazohitajika kwa kiongozi wa ibada.

(5) Kutofautisha uongozi na uendeshaji wa ibada.

(6) Kutumia hatua za vitendo kwa uongozi bora wa ibada.

## Matayarisho kwa somo hili

*Kariri 2 Nyakati 5:13-14.*

## Utangulizi

► Je, unatoa muda gani wa kupanga kwa huduma ya ibada ya kila juma? Je, unalinganisha nyimbo na mahubiri? Je, aina hii ya upangaji ni muhimu au kupanga mapema kunazuia uhuru wa Roho Mtakatifu katika ibada?

Fikiria kuhusu mwanamke anayetayarisha chakula kwa ajili ya wageni maalum. Wageni wanapowasili kwa chakula cha jioni, mhudumu anasema, "Siamini katika kutumia muda mwingi kupika chakula. Hapa kuna mkate uliobaki, nyama na mboga. Mnaweza kuweka pamoja vile mnavyotaka." Je, wewe ungefanya hivi kwa wageni maalum? Bila shaka hapana! Unataka kutoa kilicho bora kwako kwa ajili ya wageni wako.

Hebu fikiria mchungaji anayeleta ibada kama zawadi yake kwa Mungu. Anasema, "Siamini katika kutumia muda mwingi kupanga ibada. Ninataka kumpa Roho Mtakatifu uhuru wa kuzungumza kupitia mimi, kwa hivyo sitapanga chochote. Namuacha Roho aniongoze."

Viongozi wengine wanaamini kwamba Roho Mtakatifu hawezi kufanya kazi kupitia mahubiri yaliyotayarishwa vyema au huduma iliyopangwa vizuri. Hata hivyo, Biblia inaonyesha umuhimu wa kupanga kwa ajili ya ibada. Kuanzia kwenye maandalizi makini ya wanamuziki kwa ajili ya ibada hadi maelekezo ya Paulo kuhusu ibada kwa kanisa la Korintho, maandiko yanaonyesha kwamba kupanga ni muhimu kwa kuongoza katika huduma. Hatupaswi kuleta sadaka isiyotugharimu chochote. Kwa kuwa ibada ni dhabihu yetu kwa Mungu, Mungu anastahili toleo letu bora zaidi.

Katika somo hili tutaangalia vipengele viwili vya uongozi wa ibada. Kwanza, tutajifunza umuhimu wa kupanga kwa ajili ya ibada. Kisha, tutaangalia uongozi bora katika huduma ya kuabudu.

## Maandalizi ya Huduma ya Ibada

► Soma Kutoka 28-29. Ona maandalizi makini ya wale walioongoza katika ibada ya Israeli. Je, unajiandaa vipi kiroho, kiakili, na kihisia ili kuongoza ibada?

### Kuandaa Kiongozi wa Ibada

Kupanga na kuandaa ibada ni muhimu; **kuandaa kiongozi** wa ibada ni muhimu zaidi. Hatuwezi kuwaongoza watu mahali ambapo hatujafika. Kwa sababu hii, ni lazima tutayarishe mioyo yetu kabla ya kujaribu kuwaongoza wengine katika ibada.

Katika Somo la 2, tuliona matakwa ya Mungu kwa waabudu. Mungu huwaita waabudu wake wawe na mikono safi na mioyo safi. Kabla ya kuanza kutayarisha ibada, tunapaswa kujitayarisha kama viongozi wa ibada. Ni lazima tuwe tayari kiroho kuongoza ibada.

> "Mtu anayeongoza wengine mbele ya Mfalme lazima awe amesafiri mbali hadi katika nchi ya Mfalme na mara nyingi akatazama uso wake."
>
> - Charles Spurgeon

Anza kupanga ibada kwa maombi na usomaji wa Maandiko. Tumia muda katika Neno la Mungu kwa maendeleo yako ya kiroho. Hatari ya mara kwa mara kwa viongozi wa ibada ni kuruhusu maandalizi ya huduma kuchukua nafasi ya maendeleo ya kibinafsi ya kiroho. Tunaweza kujifunza Biblia ili kutayarisha mahubiri kwa wengine huku tukikosa kuruhusu Neno la Mungu lizungumze na mahitaji yetu wenyewe ya kiroho.

Kabla ya kuchagua Maandiko na nyimbo zinazozungumza Neno la Mungu na kanisa, chukua muda kuruhusu Neno la Mungu na Roho ya Mungu kusema nawe kibinafsi. Kisha unapoanza kupanga kwa ajili ya huduma ya Jumapili, mwombe Mungu akuongoze kwa Maandiko, mada ya mahubiri, na wimboi ambao utazungumza na mahitaji ya watu.

### Kujipima

Je, unawezaje kusitawisha mtindo mzuri wa ibada ya faragha maishani mwako? Je, unakumbana na vikwazo gani? Je, unashughulikiaje vikwazo hivyo?

### Kupanga Huduma Ya Ibada[65]

Fred Bock alieleza matayarisho ya mchungaji ambaye anatumika chini yake, Lloyd John Ogilvie. Dk. Ogilvie alipanga mahubiri yake kwa mwaka mzima. Mara nyingi, mada ya mahubiri iliyochaguliwa katika Januari ilikuwa inafaa kabisa kwa mahitaji ya kanisa ilipohubiriwa Julai. Kwa nini? "Mungu wetu ni Mungu wa jana, leo na kesho. Anajua mahitaji

---

[65] Mengi ya yaliyomo kwenye ibada ya kupanga yanatoka kwa "The Nuts and Bolts of Worship Planning" inayopatikana http://worship.calvin.edu/resources/resource-library/the-nuts-and-bolts-of-worship-planning accessed July 22, 2020.

yetu mapema, muda mrefu kabla ya sisi kufanya hivyo. …Na tunapotayarishwa na kupangwa, hii hutufanya kuwa chombo kinachotumika zaidi na rahisi kwa Roho Mtakatifu."[66] Roho Mtakatifu anajua ni nani atakuwa katika ibada yako; anaweza kukuongoza kwa nyimbo na maandiko ambayo yatazungumza na mahitaji yao.

Labda hupaswi kupanga mwaka kwa wakati, lakini kupanga ibada ni muhimu. Kupanga kwa uangalifu hutuweka huru kuzingatia kuabudu wakati wa ibada badala ya kuwa na wasiwasi, "Nini kitakachofuata?" Tusipopanga, huwa tunarudi nyuma kwa yale tuliyofanya wiki iliyopita. Mipango hutuweka huru kuwa wabunifu.

***Anza na muundo.***

Wengi wetu tunapenda utaratibu katika maisha. Tunapendelea kula kifungua kinywa asubuhi na chakula cha jioni usiku. Kwa kawaida tunasoma vitabu kuanzia sura ya 1 hadi mwisho badala ya kusoma kurasa ovyo. Hakuna msafiri anayetaka kupanda ndege ya kimataifa na kumsikia rubani akisema, "Hatujaamua njia ya kuitumia leo. Tutaondoka tu na kuona nini kitatokea." Tunapenda muundo.

Muundo katika ibada hauzuii uhuru wetu wa kumfuata Roho Mtakatifu anapobadilisha mipango yetu! Muundo unatoa mwongozo wa kuabudu, huku ukiendelea kuwa tayari kwa uongozi wa Roho Mtakatifu ikiwa atapita muundo wetu. Wakati wa kuwekwa wakfu kwa Hekalu, kulikuwa na muundo uliopangwa, lakini uwepo wa Mungu ulibadilisha utaratibu wa ibada (2 Mambo ya Nyakati 5:13-14).

> "Utoaji bila utaratibu inaweza kuwa fujo, na utaratibu bila utoaji unaweza kukosa uhai."
>
> - Franklin Segler na Randall Bradley

Katika Kiambatanisho A kuna muhtasari ambao baadhi ya viongozi hutumia kupanga ibada. Unaweza kuona ina manufaa kurekebisha mojawapo ya haya kwa ibada zako. Hizi sio muundo mgumu lakini zinaweza kutoa muundo ambao unaweza kubadilika kulingana na mahitaji yako.

Baadhi ya miundo ya kawaida ya kupanga ibada ni pamoja na:[67]

**(1) Muundo unaozingatia mahubiri**

- Kutangaza ukweli: nyimbo za ibada, maandiko, mahubiri
- Kuitikia ukweli: mwaliko, sadaka, wimbo wa kufunga

**(2) Muundo unaotegemea utendaji wa watu wa Mungu katika ibada**

- Watu wa Mungu hukusanyika: mwito wa kuabudu, nyimbo za sifa, maombi

---

[66] Lois and Fred Bock, *Creating Four-Part Harmony*, (Carol Stream: Hope Publishing, 1989), 43

[67] Miundo ninayojumuisha hapa ni ya huduma nzima. Baadhi ya viongozi wa ibada hutumia miundo kwa ajili ya sehemu ya muziki ya ibada pekee. Sijajumuisha hizi kwa sababu hutenganisha ibada na huduma nzima. Katika Biblia, ibada inajumuisha huduma zote, si ibada maalum ya muziki iliyotengwa na mahubiri.

- Watu wa Mungu husikia Neno: usomaji wa maandiko na mahubiri
- Watu wa Mungu huitikia Neno: wimbo wa mwaliko, sadaka
- Watu wa Mungu wanaondoka: wimbo wa kufunga, baraka

**(3) Muundo unaoonesha mazungumzo kati ya Mungu na watu wake (kulingana na Isaya 6)**

- Mungu anajifunua mwenyewe (mstari wa 1): wito wa kuabudu
- Watu wa Mungu wanajibu kwa sifa na kukiri (mstari wa 3-5): nyimbo na maombi
- Mungu anazungumza na watu wake (mstari wa 6-8): maandiko na mahubiri
- Watu wa Mungu wanajibu kwa kuweka azimio/kujitoa (mstari wa 8): nyimbo na sadaka
- Mungu anawatuma watu wake (mstari wa 9): baraka

**(4) Muundo unaotegemea Zaburi ya 95**

- Ingieni kwa shukrani za furaha (mistari wa 1-5): mwito wa kuabudu, nyimbo za sifa
- Endelea katika ibada ya uchaji (mistari wa 6-7): nyimbo za utakaso, maombi
- Sikia sauti ya Mungu (mistari wa 7-11): maandiko na mahubiri

***Wasilisha ujumbe uliounganishwa.***

Ibada huzungumza na Mungu, lakini pia huzungumza na kanisa. Katika ibada, tunaleta Neno la Mungu kwa waabudu. Unapopanga ibada, inafaa kuuliza, "Mungu anataka kuwaletea watu wake ujumbe gani katika ibada hii?"

Je, umewahi kuhudhuria ibada kama hii?

| Mtiririko wa Ibada | Mada/Dhima |
|---|---|
| Wimbo wa pamoja 1 | Faida za maombi |
| Wimbo wa pamoja 2 | Sifa kwa Mungu |
| Wimbo wa pamoja 3 | Tumaini letu la mbinguni |
| Wimbo binafsi/kwaya | Kumwalika Roho Mtakatifu maishani mwetu |
| Mahubiri | "Wito wa Yona kwenda Ninawi" – changamoto kwa uinjilisti |
| Wimbo wa pamoja 4 | Sifa kwa Mungu |

Ni ujumbe gani waabudu wataupata? Wameimba kuhusu maombi, kumsifu Mungu, mbingu, na Roho Mtakatifu, kisha wamesikia mahubiri kuhusu somo tofauti kabisa. Katika juma linalofuata, je, watu watakumbuka changamoto ya uinjilisti? Pengine; lakini muundo wa huduma haukuimarisha mada hii.

Sasa fikiria ibada iliyopangwa kwa mada ya uinjilisti:

| Mtiririko wa Ibada | Mada/Dhima |
|---|---|
| Wimbo wa pamoja 1 | Sifa kwa Mungu |
| Wimbo wa pamoja 2 | Sifa na uinjilisti |
| Wimbo wa pamoja 3 | Mhutasari wa ujumbe wa kiinjilisti |
| Wimbo wa pamoja 4 | Uhitaji wa Uinjilisti |
| Mahubiri | "Wito wa Yona kwenda Ninawi" – changamoto kwa uinjilisti |
| Wimbo binafsi/kwaya | Wito wa uinjilisti |
| Wimbo wa pamoja 5 | Mwitikio juu ya wito |

Kwa sababu viongozi wamepanga ibada ya kuwasilisha mada moja, watu wanaweza kusikia sauti ya Mungu kwa wiki nzima, wakiwakumbusha juu ya wito wa uinjilisti. Wanapokutana na watu wenye maisha ya shida au upweke, wanaweza kukumbuka kwamba "watu wanamhitaji Bwana." Wakiwa kazini siku ya Jumanne, wanaweza kufurahi wakikumbuka kuwa Yesu anaokoa. Na kwa sababu "Yesu ametuokoa," tunapaswa kushirikisha furaha hii na wengine.

Je, Mungu anaweza kufanya kazi kupitia ibada isiyo na mada kuu? Bila shaka! Hata hivyo, tunawasaidia waumini wetu kuzingatia ujumbe tukichukua muda kupanga ibada kwa uangalifu. Je, hii ni muhimu kila wakati? Hapana. Ibada wakati mwingine itakuwa na mada nyingi ambazo Mungu hutumia kuzungumza na mahitaji mbalimbali katika kanisa. Hatupaswi kamwe kuingia katika mtego wa kufikiri kwamba Mungu anafanya kazi kupitia mfumo mmoja tu. Hata hivyo, mada iliyounganishwa mara nyingi huwasaidia waabudu kuzingatia ujumbe wa ibada.

***Dumisha usawa katika ibada.***

Sote tuna vitu tuvipendavyo: vyakula tuvipendavyo, muziki tunaopenda, vitabu tupendavyo, michezo tuipendayo, na vitabu vya Biblia tuvipendavyo. Katika kupanga ibada, ni muhimu kwamba kiongozi ajumuishe zaidi ya nyimbo anazopenda, maandiko, na mada za mahubiri. Ibada iliyosawazishwa itazungumza injili yote kwa kanisa zima.

**(1) Ibada yenye usawa inaonyesha ukuu wa Mungu na uwepo wa Mungu pamoja nasi.**

Mungu ni Mungu aliyetukuka anayetawala juu ya dunia yote; Mungu pia ni Mungu aliyepo ambaye anakaa kati ya watu wake. Tunaona usawa huu katika Maandiko yote.

Baada ya kuvuka Bahari ya Shamu, watu wa Israeli waliimba juu ya uwezo wa Mungu; "Ee Bwana, katika miungu ni nani aliye kama wewe? Ni nani aliye kama wewe, mtukufu katika

utakatifu, mwenye kuogopwa katika sifa zako, mfanya maajabu?" Waliimba juu a vile Mungu amewatunza; "Wewe kwa rehema zako umewaongoza watu uliowakomboa, Kwa uweza wako uliwaelekeza hata makao yako matakatifu" (Kutoka 15:11-13).

Isaya alimwona Bwana ameketi katika kiti cha enzi, kilicho juu sana na kuinuliwa. Alikuwa mkuu na mbali sana juu ya dunia. Bwana aliinuliwa, lakini alizungumza kibinafsi kumtuma Isaya "Enenda, ukawaambie watu hawa..." (Isaya 6:1-13).

Mtunga-zaburi alimsifu Mungu aliyetukuka; "wewe Mungu, Bwana wetu jinsi lilivyo tukufu jina lako duniani mwote! Wewe Umeuweka utukufu wako mbinguni." Mungu huyu aliyeinuliwa amejinyenyekeza ili kuwa karibu na wanadamu; "Mtu ni kitu gani hata umkumbuke, na binadamu hata umwangalie?" (Zaburi 8).

Katika ibada, tunatilia maanani ukuu wa Mungu na uwepo wa Mungu pamoja nasi. Ibada yetu inaposahau ukuu wa Mungu, anakuwa rafiki wa kawaida ambaye hahitaji tena utii na ibada. Ibada yetu inaposahau jinsi Mungu anavyohusika nasi sasa, tunamwabudu kama Mungu aliye mbali ambaye hajali chochote katika mambo yetu. Katika kupanga ibada, tunapaswa kuzingatia vipengele vyote viwili vya uhusiano wa Mungu na wanadamu. Ni lazima tuwakumbushe waabudu kwamba tunamcha Mungu; lazima pia tukumbuke kwamba tunapendezwa na Mungu. Katika maombi, tunamsifu Mungu kwa matendo yake makuu, pia tunapeleka kwake mahitaji yetu ya ndani ya kibnafsi.

► Tazama mkusanyiko wa tenzi na mapambio katika lugha yako. Tafuta mfano wa wimbo ambao unonyesha ukuu wa Mungu. Tafuta wimbo mwingine unaozungumzia kuhusu Yeye kuwa na uhusiano wa karibu nasi.

**(2) Ibada yenye usawa ni ya pamoja na ya kibinafsi.**

Kitabu cha Zaburi hujumuisha sifa za pamoja na sifa za mtu binafsi. Zaburi zingine zinazungumza juu ya sifa "zetu"; baadhi ya zaburi huzungumza juu ya sifa "yangu". Hekaluni, waabudu wa Kiebrania waliabudu pamoja; nyumbani, walisali wakiwa mtu mmoja-mmoja. Yesu mara nyingi aliienda kwenye sinagogi kwa ajili ya ibada ya pamoja; pia aliienda mahali pasipokuwa na watu ili kukaa peke yake na Baba yake (Luka 4:16 na Marko 1:35). Ibada ya Biblia ilikuwa ya pamoja na ya kibinafsi. Katika ibada, ni lazima tutoe nafasi kwa waamini kuabudu kama kanisa na nafasi kwa waabudu mmoja-mmoja kuonyesha ujitoaji wao binafsi kwa Mungu.

**Kuiweka katika vitendo**

Ibada ambayo ni ya pamoja na ya kibinafsi itaathiri maeneo yote ya huduma. Kwa Pamoja tutaimba nyimbo kwa kusanyiko lote, kwa Pamoja tutaimba nyimbo za ibada binafsi. Tutasali kwa "Baba yetu uliye mbinguni"; tutakuwa na nyakati za maombi ya kikundi kuruhusu kila mshirika kuomba kibinafsi ndani ya mwili wa Kristo.

Zaidi ya wakati wowote katika historia, ibada ya pamoja ni changamoto. Katika enzi ya simu za mkononi, kompyuta ya mkononi, ujumbe wa maandishi, na upatikanaji wa mtandao mara kwa mara, tunaweza kukaa katika ibada huku tukiwa tumejitenga kihisia na kiroho. Uaminifu kwa ibada ya pamoja unahitaji sisi kujitenga na vikwazo na kuabudu kwa pamoja kama mwili wa Kristo.

► Tazama mkusanyiko wa tenzi na mapambio katika lugha yako. Tafuta mfano wa wimbo ambao umeandikwa katika mtazamo wa kijumuia. Unaweza kujumuisha viwakilishi kama "yetu," "sisi," au maneno kama "watu wote." Kisha, tafuta mfano wa wimbo ambao umeandikwa katika mtazamo wa mtu binafsi. Unaweza kujumuisha viwakilishi kama "yangu," "mimi".

**(3) Ibada yenye usawa inajumuisha yaliyojulikana na mapya.**

Uwiano huu ni wa vitendo badala ya kitheolojia, lakini ni muhimu ikiwa tunataka kushirikisha kikamilifu waumini katika ibada. Katika kupanga kwa ajili ya ibada, tunapaswa kusawazisha yaliyozoeleka na mapya.

Wingi wa mambo mapya husababisha waumini kuwa watazamaji badala ya kuwa waabudu; hawawezi kushiriki kwa sababu hawajui nyimbo. C.S. Isaka alilalamika wakati fulani kwamba wachungaji wengi husahau kwamba "Yesu alimwambia Petro "Lisha kondoo zangu," sio 'kuwafundisha mbwa wangu mbinu mpya.'" Mambo mapya kupita kiasi hufanya iwe vigumu kuzingatia ibada.

Mengi ya yale yanayofahamika husababisha utaratibu usio na maana. İbada ambayo imekuwa ya kutabirika kabisa inasababisha waumini kupoteza mwelekeo na kujitenga na ibada.

Upangaji wa ibada unapaswa kujumuisha yote yanayofahamika na mapya. Kwa mfano, kiongozi mmoja wa ibada alichagua kuongoza kusanyiko kwa tenzi mpya kuhusu upatanisho. Wimbo huu unaonesha wazi gharama ya upatanisho. Baada ya wimbo ule kuwa umeimbwa, aliongoza wimbo wa zamani, unaofahamika zaidi ualikao kusanyiko kuitikia sadaka ya Yesu.

Usawa wa yale yanayofahamika na mapya hutia moyo waumini kuabudu kwa bidii.

**Kuiweka katika Vitendo**

Ibada inayosawazisha ile inayofahamika na mpya itajumuisha nyimbo za zamani na mpya. Itajumuisha usomaji wa Maandiko unaofahamika na usiojulikana sana. Kabla ya kusoma kifungu tunachokifahamu kama vile Yohana 3:1-21 ambamo Yesu anafundisha kuhusu kuzaliwa upya, tunaweza kusoma kifungu kisichojulikana sana kama vile Ezekieli 36:16-38 ambapo Mungu anaahidi kuwaosha Waisraeli kwa maji na kuwapa moyo mpya. Maandiko haya mawili yanahusiana kwa karibu katika mada. Kuzisoma pamoja kutaongeza uelewa wa waumini kuhusu mafundisho ya Yesu katika Yohana 3.

Ikiwa unatanguliza wimbo mpya, zunguka wimbo huo mpya kwa nyimbo zinazofahamika. Tunapofungua ibada kwa wimbo usioufahamu, ibada huanza kwa njia isiyoeleweka. Ni jambo la hekima kufungua kwa wimbo unaojulikana kisha kutambulisha wimbo huo mpya.

Kanisa moja nchini Taiwan lilikuwa na mbinu ya ubunifu ya kutambulisha nyimbo. Wengi wa washirika wao walikuwa waamini wapya na hawakujua nyimbo nyingi zilizoimbwa. Kanisa hili lilikuwa na mazoezi kabla ya kila ibada. Dakika ishirini kabla ya ibada, watu waliimba nyimbo ambazo zingekuwa sehemu ya ibada. Mpiga kinanda alicheza wimbo huo ili kila mtu aweze kujifunza wimbo huo. Kwa kuwa hayo yalikuwa mazoezi, kiongozi angeweza kuacha na kurudia fungu la maneno hadi waumini wajifunze vizuri. Kufikia 10:00, watu waliimba hata nyimbo mpya kwa ujasiri.

► Tazama mkusanyiko wa tenzi na mapambio katika lugha yako. Tafuta nyimbo mbili zenye dhima moja au nyimbo mbili zenye dhima zinazohusiana. Kunatakiwa kuwe na mahusiano dhahiri kati ya nyimbo hizo. Moja uwe wenye kufahamika, mwingine uwe usiofahamika. Kama ungetakiwa kutumia nyimbo hizi mbili kwenye ibada ya kuabudu, ni wimbo upi ungeimba kwanza? Ungebadili vipi kuendea wimbo wa pili?

***Panga kama timu.***

Mhubiri anatoa ushauri huu unaofaa; “Afadhali kuwa Wawili kuliko mmoja; maana watapata ijara njema kwa kazi yao” (Mhubiri 4:9). Upangaji wa ibada unapaswa kuwa shughuli ya pamoja. Kila mtu anayehusika katika uongozi wa ibada anapaswa kuwa na jukumu katika kupanga.

Mchungaji, kiongozi wa sifa, na viongozi wengine wa kanisa wanapokutana pamoja kutafuta mapenzi ya Mungu kwa ajili ya ibada, karama za kila mtu huunganishwa pamoja. Kwa kufanya kazi kama timu, nguvu za kila mshiriki wa uongozi wa kanisa huchangia katika ibada.

***Panga kwa muda mrefu.***

Hakuna Ibada moja inayojumuisha ujumbe mzima wa Biblia, lakini baada ya muda tunapaswa kuwasilisha vipengele vyote vya injili kwa waabudu wetu. Kila mmoja wetu ana mada anazopenda; lazima tujitutumue kuhubiri na kuimba mada ambazo hatuzipendi.

Baadhi ya wachungaji na viongozi wa ibada hutumia kalenda inayopanga mada za kufundisha kupitia Biblia katika miaka mitatu.[68] Wengine hupanga kila wiki lakini wako makini kufanyia kazi ujumbe mzima wa maandiko kwa muda fulani.

Hata kama hutafuata kalenda ya mafundisho, ufahamu wa majira ya msingi ya mwaka wa Kikristo utakuongoza kupitia vipengele muhimu vya injili. Majira muhimu katika mwaka wa Kikristo ni:

- **Majilio** (Jumapili nne kuelekea Krismasi): Kuzingatia ujio wa kwanza na wa pili wa Kristo.
- **Krismasi:** Mkazo juu ya kufanyika mwili na kuzaliwa kwa Kristo.
- **Kwaresima** (Jumapili sita zinazoelekea Pasaka): Kuzingatia mateso na kifo cha Yesu, pamoja na mahitaji ya ufuasi kwa kila mwamini.
- **Pasaka:** Kuzingatia ufufuo na kupaa kwa Kristo.
- **Pentekoste:** Kuzingatia Roho Mtakatifu na kanisa.

Iwe unafuata mlolongo rasmi au mpango wa kila wiki, hakikisha kuwa kanisa lako linasikia injili yote kama sehemu ya ibada.

***Panga kwa amani.***

Ibada sio kuhusu sisi; ibada ni dhabihu yetu kwa Mungu. Upangaji wetu wa ibada ni sehemu ya sadaka hiyo. Tunapanga ibada bila shinikizo linaloongozwa na hatia ya kufikiri, "Je, hii ni nzuri vya kutosha?" Tunamwabudu Mungu wa neema. Sadaka yetu inakubaliwa si kwa sababu ni nzuri ya kutosha, lakini kwa sababu Mungu anakubali sadaka ya hiari ya watoto wake.

Hii ni muhimu katika kuzuia shinikizo kwamba "Lazima tuendane na kanisa la XYZ." Katika ulimwengu wa kisasa wa teknolojia na vyombo vya habari vingi, viongozi wengi wa makanisa wanapata shinikizo la mara kwa mara la kutaka kufanana na makanisa mengine. Wachungaji wanashindana kuwa na teknolojia ya kisasa. Waongozaji wa muziki hushindana kuimba nyimbo mpya zaidi. Waabudu hugeuka kuwa wanunuzi wanaotafuta kanisa linalotoa vivutio vipya zaidi.

Usikubali kuingia kwenye jaribu la kutaka kumvutia Mungu kwa sadaka yako. Usiruhusu zana za ibada, kama vile muziki na teknolojia kuchukua nafasi ya ibada halisi. Mletee kilicho bora zaidi ukijua kwamba Mungu wa neema hufurahia harufu nzuri ya sadaka yako. Mpe kilicho bora zaidi, kisha atakubali sadaka yako. Ibada si mashindano na makanisa mengine; ni zawadi kwa Mungu.

[68] Inapatikana mtandaoni kwa http://lectionary.library.vanderbilt.edu/calendar.php July 22, 2020.

## Kuongoza Huduma za Ibada/Ibada ya Kuabudu


### Swali muhimu zaidi: *Hadhira ni nani?*

► Je, waumini wana jukumu gani katika ibada? Je, jukumu la viongozi wa ibada ni nini? Nini jukumu la Mungu?

Watu wengi huona ibada kama tamasha. Kusanyiko linasikiliza mchungaji na wanamuziki wakiimba. Patakatifu ni ukumbi wa tamasha.


Barry Liesch alielezea mtazamo huu wa ibada kama mchezo wa mpira:[69]

- Viongozi wa ibada ni wachezaji wanaofanya ibada.
- Waamini ni watazamaji katika viwanja wakitazama mchezo.
- Mungu ndiye kocha anayewaambia viongozi wa ibada nini cha kufanya.




Picha ya kibiblia ya ibada ni tofauti sana. Katika ibada ya kibiblia, mkutano huabudu wakati viongozi wa ibada hufanya kama makocha wanaoongoza ibada:

- Kiongozi wa ibada ndiye kocha anayeongoza kanisa.
- Waabudu ni wachezaji wanaofanya ibada.
- Mungu ndiye hadhira inayopokea ibada zetu.





Katika mchezo wa kuigiza, hutawahi kumwona muongozaji. Muongozaji anajua kila mstari wa mchezo na anaelekeza kila mwigizaji wakati wa kuingia. Hatakama anafanya kazi yake vizuri, watazamaji hawatambui kamwe. Hilo ndilo jukumu la viongozi wa ibada. Kazi yetu si kuabudu kwa ajili ya watu; kazi yetu ni kuongoza watu katika kuabudu. Waumini wanaabudu, pamoja na mchungaji na kiongozi wa uimbaji, katika uwepo wa Mungu. Lengo letu katika ibada ni kumpendeza Mungu. Katika kielelezo cha kibiblia cha ibada, Mungu ndiye hadhira ya ibada yetu.

---

[69] Barry Liesch, *The New Worship*, 2nd edition (Grand Rapids: Baker Books, 2001), 123

Hata hivyo, Mungu ni zaidi ya hadhira; Mungu hututia nguvu yote tunayofanya katika ibada. Na, kiongozi wa ibada ni zaidi ya kocha au muongozaji. Kiongozi wa ibada ni muongozaji na mwabudu. Ibada inahusisha mahusiano mengi:

- Mungu huwaalika waabudu, hupokea ibada, na huwaongoza viongozi wa ibada wanapohudumu mbele za watu.
- Viongozi wa ibada huongoza waumini katika ibada, kusikiliza sauti ya Mungu, na kushiriki kama waabudu.
- Waumini humwabudu Mungu, husikiliza Neno la Mungu, na kuzungumza wao kwa wao katika ibada.




**Jinsi ya Kuepuka Ibada Kama Onyesho la Utendaji [70]**

1. Imba nyimbo ambazo watu wanajua au wanaweza kujifunza kwa urahisi. Ziimbe katika tuni inayoeleweka kwa kanisa. Tumia nyimbo mpya kwa kiasi.
2. Imba na ushangilie uweza, utukufu, na wokovu wa Mungu. Tumikia waumini wako. Wajaze kwa Neno la Mungu. Usiimbe nyimbo zenye maneno mabaya au theolojia dhaifu.
3. Weka taa juu. Punguza kuongea sana. Usiruhusu vitanzi/taa/vielelezo viwe njia yako ya ubunifu kwa gharama ya ukuu wa injili.
4. Badili uongozi wako wa ibada na nyimbo unazochagua zifae watu wengi wa kanisa lako. Ongoza kwa upendo wa kichungaji.
5. Elekeza kwa Yesu. Usijivutie upande wako.

**Sifa za Kiongozi wa Ibada**

Bila kujali cheo chako, kama kiongozi wa ibada unafanya kazi ya kichungaji. Ikiwa wewe ni mchungaji, tayari unaelewa hili. Ikiwa wewe ni kiongozi wa kawaida, lazima uelewe kwamba jukumu lako linakuweka katika nafasi ya uongozi wa kiroho.

Katika kuchagua kiongozi wa ibada, lazima tuzingatie sifa za kiroho, si tu sifa za uimbaji au za kibinafsi. Mitume walipochagua mashemasi kuwatunza wajane wa Kiyunani, walitafuta wanaume wenye sifa nzuri, waliojaa Roho na hekima (Matendo 6:3). Sifa za kimaadili, za kiroho, na za kiadili zilikuwa muhimu sana.

---

[70] Imetolewa kutoka kwa Jamie Brown, "Are We Headed For A Crash? Reflections on the Current State of Evangelical Worship." Inapatikana hapa https://worthilymagnify.com/2014/05/19/crash/ July 22, 2020.

Katika baadhi ya makanisa, uchaguzi wa viongozi wa nyimbo, wanamuziki, na majukumu mengine ya uongozi hutegemea umaarufu. Ikiwa mashemasi waliohudumu kwenye meza walichaguliwa kwa sifa zao za kiroho, hakika viongozi wa ibada wanapaswa kuchaguliwa kwa sifa za kiroho.

Ikiwa unaongoza ibada katika kanisa lako (kama mchungaji, mwanamuziki, au kiongozi mwingine katika ibada), unapaswa kutafuta kukuza sifa zinazofanya kuwa kiongozi bora wa ibada.

- **Upambanuzi wa kiroho. "**Je, ninaweza kupambanua uongozi wa Roho Mtakatifu?"
- **Unyeti**. "Je, nina wepesi wa kujua mahitaji ya waumini? Je, ninachagua nyimbo na maandiko yanayozungumzia mahitaji hayo?
- **Ushirikiano.** "Je, ninatumikia kwa ufanisi kwenye timu? Je, ninashirikiana na mchungaji anaponiuliza nibadilishe wimbo wa kufunga? Je, ninakubali mahitaji ya timu nzima?"
- **Maarifa.** "Je, ninakua katika ujuzi wangu wa Neno la Mungu? Je, ninalifanya Neno la Mungu kuwa jambo kuu katika ibada?"
- **Hekima**. "Je, ninakua katika hekima ya kuelewa na kutatua mizozo kuhusu ibada? Je, ninajiweka nidhamu ili kuwa mwepesi wa kusikiliza na si mwepesi wa kusema? (Yakobo 1:19).
- **Subira**. "Je, nina subira waumini wanapochelewa kuitikia mpango wangu wa ibada?"
- **Unyenyekevu**. "Je, niko tayari kuimba wimbo unaozungumzia mahitaji ya waumini walio na mafunzo kidogo? Je, niko tayari kuhubiri kwa mtindo rahisi zaidi unaokidhi mahitaji ya washirika wasio na elimu katika kanisa langu? Je, ninaongoza kwa unyenyekevu, au ninajiona kuwa bora kuliko kanisa ambalo Mungu ameniweka?" Kama kiongozi wa ibada, ubunifu wako lazima upate nafasi katika wajibu wako wa kichungaji. Wajibu wako wa kwanza ni kuwahudumia watu.
- **Ubunifu.** "Je, ninatafuta njia za kufanya ibada iwe na maana? Je, ninaepuka kuangukia katika muundo unaojirudia ambapo kila ibada ni sawa?"
- **Nidhamu**. "Je, nawajibika kudhibiti ubunifu wangu ili usisababishe kuchanganyikiwa katika ibada? Je, najiepusha kufanya kila ibada iwe mpya sana kiasi kwamba watu watashindwa kuongeza umakini kwa Mungu?"

- **Ubora.** "Je, ninatoa kile kilicho bora kila wiki? Je! ninaendelea kukua kama kiongozi wa ibada?"[71]

### Hatua Muhimu katika Kuongoza Ibada

Kiongozi hawezi kuwalazimisha watu kuabudu; hata hivyo, kiongozi anaweza kufanya iwe rahisi kwa waumini kuongeza umakini kwa ibada.

#### *Kuongoza kwa mfano*

Mojawapo ya mapendeleo ya kuongoza katika ibada ni fursa ya kuabudu pamoja na waumini. Kiongozi lazima aabudu huku akiongoza washirika katika ibada.

Kwa bahati mbaya, ibada inaweza kuwa changamoto kwa kiongozi wa ibada. Tunaweza kuwa na shughuli nyingi sana za kuongoza ibada hadi tukashindwa kuabudu! Ikiwa wewe ni kiongozi wa muziki, unaweza kujikuta ukijaribu kuabudu huku ukiwa na mawazo kama vile:

- "Mpiga gitaa amechelewa. Natumaini atafika hapa kwa wakati kwa ajili ya wimbo maalum!"
- "Watu hawakuimba vizuri kwenye wimbo wa kwanza. Je, wimbo huo ni mgumu sana kwa kanisa letu?"
- "Ninahisi kama tunaimba polepole sana. Je, niharakishe ubeti unaofuata?"

Ikiwa wewe ni mchungaji, unaweza kujikuta ukijaribu kuabudu huku ukifikiri:

- "Tumepungukiwa na watu 10 ikilinganishwa na wiki iliopita. Wako wapi?"
- "Je, nimalize mahubiri kwa kuwaalika watu madhabahuni?"
- "Wimbo huo hauendani na mahubiri yangu! Ninawezaje kuhamia kutoka wimbo kuhusu mbinguni hadi kwenye mahubiri yangu kuhusu Hukumu?"

Hatupaswi kuruhusu uendeshaji wa ibada kuchukua nafasi ya ibada katika maisha yetu. Tunapoongoza ibada, lazima tuabudu. Hii inahamasisha ibada kwa waumini. Msemaji mmoja alisema, "Kama viongozi wa ibada hatuko kama **mbwa wa wachungaji** wanaouma visigino vya waumini kuwalazimisha waende kwenye mwelekeo tunaoitaka. Sisi ni **waabudu** tunaowaalika waumini kwenda pamoja nasi katika uwepo wa Mungu." Waumini hawaabudu wakati kiongozi anawaambia waabudu; wao huabudu wakati kiongozi anaabudu. Kiongozi wa ibada hungoza kwa mfano.

---

[71] Ubora haumaanishi kuwa viongozi waliofunzwa kitaalamu pekee ndio wanaweza kuongoza ibada. Harold Best anafafanua ubora kama "mchakato wa kuwa bora kuliko nilivyokuwa hapo awali." Kwa kuwa ibada ni sadaka yetu kwa Mungu, tunaendelea kutafuta kuwa bora kuliko tulivyokuwa. Harold Best, *Music through the Eyes of Faith* (San Francisco: Harper Books, 1993), 108

***Kuongoza kwa kutia moyo***

Susanna alikuwa macho mpaka saa 3:00 asubuhi akimhudumia mtoto mgonjwa. Baada ya masaa matatu ya usingizi, aliamka kuandaa kifungua kinywa na kujitayarisha kwa ajili ya kanisa. Alifika kanisani akiwa amechoka kutokana na kukosa usingizi, akiwa amevunjika moyo kwa sababu alimkemea mwanawe vikali aliposahau kuweka kitu cha kuchezea, na akiwa amepwaya kiroho kwa sababu alikuwa na muda mchache peke yake na Mungu wiki hii.

Mchungaji Joel anataka kuona ushiriki zaidi katika ibada. Baada ya wimbo wa kwanza, anaingia kwenye mimbari, "Mna nini nyinyi watu? Tupo katika uwepo wa Mungu. Tunamwabudu Mfalme, na baadhi yenu mnaonekana kama mngependelea kuwa nyumbani mmelala! mnapaswa kuwa na aibu. Jiunge katika ibada!"

Nia ya Mchungaji Joel ni njema. Anataka waumini wake wawe washiriki kikamilifu katika ibada, lakini Susanna anasikia nini? "Mimi ni mtu aliyeshindwa kama mama; Nilikuwa mkali sana kwa mwanangu. Nimefeli kama Mkristo; Nilikosa ibada zangu binafsi jana. Nimeshindwa hata kuhudhuria kanisani; Mungu anakasirika kwa sababu sikuimba." Kwa kutumia hatia kama kichochezi, Mchungaji Joel amefanya ibada kuwa ngumu zaidi kwa Susanna.

Kama viongozi wa ibada, tunapaswa kuhimiza ibada; tunapaswa kuwa kielelezo cha ibada katika maisha yetu wenyewe; kisha tun aweza kuacha matokeo mikoni mwa Mungu. Ni neema ya Mungu inayofanya ibada iwezekane; ni neema ya Mungu inayotia nguvu ibada ya kweli; ni neema ya Mungu inayovuta moyo wa mwabudu.

Tunapaswa kuhimiza ibada kwa maneno yenye matumaini, lakini hatupaswi kujaribu kuwahadaa waabudu kwa hatia au kwa kujaribu kuchochea hisia kwa njia isiyo sahihi. Lengo letu ni kuwaelekeza waabudu kwa Mungu. Yeye ndiye anayeleta hamasa ya ibada; ibada haitegemei mbinu zetu za uhamasishaji au udanganyifu wa kihisia. Sisi kama viongozi wa ibada hatuhitaji kufanya kazi ya Mungu!

Sehemu hii ilianza na hadithi ya Susanna. Tumalizie na hadithi ya kweli ya kiongozi mnyenyekevu na mwenye kutia moyo. Daudi alijitahidi kuwahamasisha vijana kushiriki katika ibada. Aligundua kuwa walikuwa wakijikita zaidi kutuma ujumbe wa maandishi kuliko kushiriki katika ibada. Baadhi ya viongozi wangeweza kuanza ibada na kitu kama hiki: "vijana, tuko hapa kuabudu. Wekeni mbali simu hizo na mzingatie ibada. mnamkosea Mungu heshima!"

Daudi alifanya jambo tofauti sana. Mpiga gitaa alipokuwa akipiga wimbo wa utulivu wa ibada, Daudi alisema kwa upole, "Tunapokuja katika uwepo wa Mungu, najua usingependelea kumvuruga jirani yako katika kuabudu kwake. Hebu wote tuweke simu zetu pembeni na kusikiliza sauti ya Mungu asubuhi ya leo." Kila mtu ndani ya kanisa aliweka simu yake. Daudi kwa unyenyekevu alifundisha ujana wake kuabudu.

**Kuongoza au Kuigiza?**

Sikiliza ushuhuda wa kiongozi wa kisasa wa ibada:

"Nikiwa mwanafunzi wa mwaka wa kwanza, nilitembelea kanisa karibu na chuo kikuu changu; yake… mwanga mkali na muziki wenye sauti kubwa [zilikuwa] za kusisimua. Kiongozi wa ibada alikuwa na nywele za mtindo, jeans na gitaa la gharama kubwa. Mwanzoni mwa ibada, niliona kipaza sauti kisichotumika kimefungwa kwenye kiuno chake. 'Hiyo inaweza kuwa na kusudi gani?' nilijiuliza, kisha nikainua mikono yangu na kuzama katika nyimbo hizo.

"Sauti hiyo ilikuwa nzuri sana, kikundi cha sifa kilikuwa bora, na muziki ulipangwa kwa umakini kuongoza wimbo hadi mwisho. Kiongozi alipoimba maneno ya mwisho napiga magoti, najitoa kwako kikamilifu. Ni wakati huo ndipo nilitambua madhumuni ya kipaza sauti kisichotumiwa. Iliwekwa kwenye urefu sahihi ili kiongozi aweze kuimba na kupiga gitaa akiwa amepiga magoti. Sitaki kuhukumu nia ya kanisa hili, lakini sikuweza kujizuia kuhisi kuwa yalikuwa ni maigizo kuitikia wakati huu wa kihisia, ambao ulionekana wazi kuwa ulipangwa mapema."[72]

Mfano huu unatoka kwenye ibada ya kisasa, lakini tunaweza pia kutumia mifano kutoka kwa ibada ya kitamaduni. Tatizo la kuigiza haliishii tu kwa mtindo mmoja wa kuabudu. Bila kujali mtindo wetu wa muziki au nia zetu za dhati, tunaweza kulichukulia kanisa kama vibaraka ambao tunawaongoza ili wawe na hisia Fulani maalumu.

Je, hisia katika ibada ni mbaya? Hapana; tunaona mifano mingi ya kibiblia ya athari za kihisia za ibada. Je, ni makosa kujaribu kuhamasisha mwitikio wa kihisia? Hapana; mawasiliano mazuri hugusa akili na hisia zote. Hata hivyo, tusipokuwa waangalifu, tunaweza kufanya kazi ya kuunda athari fulani ya kihisia, mbali na kazi ya Roho Mtakatifu.

Je, tunawezaje kutofautisha kati ya uongozi wa ibada na maigizo? Maigizo huja wakati mwitikio wa kanisa unategemea ufanisi wa matendo ya viongozi badala ya nguvu za Roho Mtakatifu. Labda hatuwezi kamwe kutofautisha kikamilifu kati ya kuongoza na kuigiza, lakini kuna baadhi ya ishara zinazopendekeza kuwa tunaweza kuwa tunafanya maigizo.

1. **Tuko katika hatari ya kuigiza kuabudu tunapochanganya hisia na ibada**. Tunaanza kufikiri kuwa ni jukumu letu kutengeneza muamko wa kihisia. Baadhi hata ya viongozi wa ibada wamesema, "Fanya hivyo hadi iwe halisi. Tengeneza hisia hadi watu wahisi ukweli. Hii inachukuliwa kwamba kazi yetu ni kutumia hisia kuunda ibada. Viongozi wa ibada huongoza ibada; hatuumbi ibada.

2. **Tuko katika hatari ya kuigiza ibada tunapodhania kuwa hali ya hisia kubwa inahitajika kwa ajili ya mabadiliko ya moyo**. Mungu anaweza kufanya kazi

[72] Joel Wentz, "Confessions of a Former Worship Leader." Inapatikana kupitia https://relevantmagazine.com/life5/1301-confessions-of-a-former-worship-leader/ July 22, 2020.

katika ibada ya kanisa iliyojaa hisia, lakini pia anaweza kufanya kazi katika nyakati tulivu nyumbani. Tuko katika hatari ya kujaribu kuliigizia kanisa ikiwa tunaamini kwamba ni kupitia jitihada zetu tu ndipo Mungu anaweza kuleta mabadiliko katika mioyo ya wale tunaowatumikia.

3. **Tuko katika hatari ya kuigiza ibada tunapolinganisha tendo fulani la kimwili na ibada**. Wakati fulani kiongozi anataka watu waitikie, kwa hiyo anasema, "Ikiwa unampenda Yesu, utainua mikono yako." Bila shaka, inawezekana kabisa kwamba mtu fulani kanisani ambaye hampendi Yesu kikweli atanyosha mikono yake! Au, mtu fulani katika kanisa ambaye anampenda Yesu anaweza asiinue mikono yake. Ibada hailinganishwi na tendo fulani la kimwili. Kupiga makofi tunapoimba hakuthibitishi kwamba tunaabudu zaidi ya kukaa kwa utulivu wakati wa maombi kunaonyesha kwamba tunaomba. Mungu pekee ndiye anayeona moyo wa mwabudu. "**Viongozi wa ibada wanapofanya vitendo vya nje kuwa kipimo kikuu cha tabia ya ndani, wanakanyaga kwenye ardhi hatari.**"[73]

4. **Tuko katika hatari ya kufanya maigizo ibadani tunapojaribu kuiga kile ambacho Mungu amefanya wakati mwingine au mahali pengine.** Hatupaswi kudhani kwamba kwa sababu Mungu alibariki wimbo fulani wiki iliyopita, ni lazima abariki wimbo huohuo wiki hii. Mungu anapofanya kazi, anafanya kazi kwa njia yake mwenyewe. Viongozi wa kuabudu lazima wamwachie Mungu uhuru kuja kama apendavyo. Hakuna kichocheo cha maajabu ambacho huunda majibu ya kiroho katika kila hali.

5. **Tuko hatarini kuigiza ibada tunapopima huduma yetu kwa uwezo wetu wa kupata mwitikio kutoka kwa watu**. Mzungumzaji yeyote wa hadhara au mwanamuziki anapenda kupata mwitikio kutoka kwa wasikilizaji; hiyo ni kawaida. Lakini tunapopima ufanisi wa huduma yetu kwa miitikio hii, tuko katika hatari ya kutegemea ujuzi wetu badala ya kutegemea Roho Mtakatifu.

Mada hii ni ngumu. Mara nyingi, maneno yale yale yanayosemwa katika hali mbili tofauti huwakilisha motisha tofauti sana. Kwa upande mmoja, tusipokuwa waangalifu tunaweza kuanza kuigiza ibada. Kwa upande mwingine, ikiwa tuna hofi sana na hisia hatuwezi kutoa uongozi hata kidogo!

Kwa sababu hii, hatupaswi kuwa wepesi kuhukumu uongozi wa ibada wa mtu mwingine lakini wepesi kutathmini uongozi wetu wenyewe. Ni lazima tumwombe Mungu atuonyeshe nia zetu katika kuongoza. Ni lazima tuwe waangalifu kuongoza katika ibada bila kuwaigizia waabudu kwa mwitikio fulani ambao tunatamani.

---

[73] Warren Wiersbe, *Real Worship* (Grand Rapids: Baker Books, 2000), 215

**Maswali ya Kivitendo**

***Je, tunaanzaje Ibada?***

Mfano mbaya:

*Saa 4:00, ni wakati wa kuanza ibada. Mchungaji anajaribu kumtafuta kiongozi wa wimbo. Wanawake watatu wanashiriki mapishi. Wanaume wanne wanazungumza juu ya ukosefu wa mvua kwa mazao. Je, tunahamaje kutoka kwa shughuli hizi zote hadi kwenye ibada?*

Moja ya majukumu muhimu ya kiongozi wa ibada ni ufunguzi wa ibada. Je, tunawaalikaje watu wa Mungu katika uwepo wa Mungu?

- **Baadhi ya makanisa huanza na muda wa ukimya**. Kiongozi anaanza kwa urahisi, "Jiunge nasi katika muda wa maombi ya utulivu tunapoingia katika uwepo wa Mungu."
- **Baadhi ya makanisa huanza na muziki "Wito wa Kuabudu.**" Huu unaweza kuimbwa na kwaya au mtu binafsi, au inaweza kuwa kwaya ya kanisa. Katika baadhi ya makanisa, mchungaji atatangulia mbele na kuanza kuimba ubeti kama, "Nitaingia malangoni mwake nikiwa na shukrani moyoni mwangu…."
- **Baadhi ya makanisa huanza na mstari wa Maandiko,** mara nyingi hutolewa kutoka kitabu cha Zaburi.

  > Njoni, tumwimbie BWANA; tumfanyie shangwe mwamba wa wokovu wetu! Tuje mbele zake kwa shukrani; tumfanyie shangwe kwa zaburi (Zaburi 95:1-2).

  Zaburi zinazowaalika waabudu katika uwepo wa Mungu ni pamoja na Zaburi 15, Zaburi 66:1-4, Zaburi 96:1-4, Zaburi 100, Zaburi 105:1-3, Zaburi 107:1-3, Zaburi 149:1-2 na Zaburi 150.

***Je, matangazo ni ibada?***

Mchungaji mmoja wa Hispania aliuliza, "Matangazo yanafaa wapi katika ibada? Tunajaribu kuzingatia ibada na uwepo wa Mungu katika kanisa letu. Tuna Ibada nzuri kisha tunamalizia na orodha ndefu ya matangazo ya kuchosha. Hii inaathiri moyo wa ibada. Je, tunafanyaje matangazo kuwa sehemu ya ibada?"

Bila kujali ni wapi tunaweka matangazo, yanaweza kuharibu ibada. Ni mara chache sana matangazo kuwa ibada; badala yake yanaingilia ibada. Unaweza kufanya nini? Hakuna jibu kamili, lakini mapendekezo machache yanaweza kusaidia:

- Inapowezekana, chapisha matangazo badala ya kuyasoma kwa sauti. Inapolazimika kutoa matangazo ya umma, yafanye mafupi.
- Tumia projekta ya juu kuonyesha matangazo kabla ya ibada kuanza.

- Makanisa mengine yana matangazo, muda wa maombi, na kisha ibada huanza. Kuna kanisa moja ambalo huanza ibada saa 4:00. Kanisa hili hufanya matangazo saa 3:50. Mchungaji alisema, "Hii inatimiza mambo mawili. Kwanza, inahimiza watu waje mapema kwa sababu hawatasikia matangazo ikiwa hawapo hapa kufikia 9:50. Pili, inaturuhusu kuzingatia ibada kwa umakini tangu maneno ya mwanzo ya ibada."
- Usiruhusu matangazo yakatize roho ya ibada. Badala yake, chukulia matangazo kama sehemu ya kufanikisha huduma ya kanisa, toa matangazo, na endelea mbele. Tunapotambua kwamba shughuli za kanisa (maombi ya pamoja, huduma za kijamii, matukio ya nje, na miradi ya kanisa) ni sehemu ya ibada, matangazo ya shughuli hizi ni sehemu ya ibada ya kanisa. Kama vile baba anavyoweza kumalizia ibada ya familia kwa kukumbusha familia juu ya mipango ya wiki, mchungaji anaweza kumaliza ibada kwa kukumbusha kanisa juu ya shughuli za wiki. Matangazo kuhusu shughuli za kanisa hutukumbusha kwamba sisi ni familia; ushirika wa familia ni kipengele muhimu cha ibada.

**Hatari za Ibada: "Tunafanya Hivi Kwa Sababu ..."**

Bibi harusi mpya alikuwa akipika nyama kwa ajili ya chakula cha jioni cha Jumapili. Kabla ya kuweka nyama kwenye jiko la umeme, alikata kwa uangalifu sehemu ya mwisho ya nyama na kuiweka kwenye sufuria ndogo. Mume wake akamuuliza, "Kwa nini unafanya hivyo?"

"Hivyo ndivyo unavyotakiwa kupika nyama ya nguruwe. Mama yangu daima alikata sehemu ya mwisho ya nyama kabla ya kupika. Nadhani inasaidia ladha." Bibi-arusi mpya akaanza kujiuliza, "Kukata kipande cha nyama inaongezaje ladha yake?" Alimwita mama yake kuuliza, "Kwa nini unakata sehemu moja ya mwisho ya nyama?"

Mama yake alisema, "Kwa sababu bibi yako, mama yangu, kila mara alikata sehemu moja ya mwisho ya nyama kabla ya kupika. Lazima iongeze ladha. Hebu tumuulize yeye."

Bibi arusi alimuita bibi yake mwenye umri mkubwa. Bibi hakupika tena, lakini alijibu swali lao. "Ndio, ninakumbuka kwa nini nilikata sehemu ya mwisho ya nyama. Mimi na babu yako tulipooana, hatukuweza kumudu sufuria nyingi za kupikia. Sufuria yangu pekee ya kuchoma nyama ilikuwa ndogo. Nyama ya nguruwe isingetosha kwenye sufuria yangu isipokuwa niikate sehemu moja!"

Kwa miaka 50 mtoto wake na kisha mjukuu wake walikuwa wameendeleza "desturi" ambayo haikuwa na maana yoyote. Hawajawahi kuuliza, "Kwa nini?"

Kama viongozi wa ibada, wakati mwingine tunafanya mambo bila kuzingatia "Kwa nini?"

Sababu za kanisa kufanya mambo kwa njia maalum:

1. **Makanisa ya zamani yalifanya hivyo**. Kuna thamani katika mila. Ikiwa makanisa ya zamani yalifanya jambo fulani, hatupaswi kulitupa nje bila kuuliza, "Kwa nini walifanya hivyo?" Tunaweza kupata sababu nzuri ya kuhifadhi mapokeo; lakini ikiwa

"makanisa ya zamani walifanya hivyo" ndiyo sababu *pekee* tu, hakika inaweza isiwe sababu ya kutosha.

2. **Makanisa makubwa hufanya hivyo.** Kuna umuhimu wa kujifunza kutoka kwa wengine. Ikiwa jambo linafanya kazi vizuri katika makanisa mengine, tunapaswa kuuliza, "Je, jambo hilo lina manufaa kwetu? Kwa nini wanafanya hivyo?" Tunaweza kugundua kwamba kuna sababu nzuri ya kuiga desturi ya ibada; lakini ikiwa "makanisa makubwa yanafanya hivyo" ndiyo sababu *pekee* tu, hakika inaweza isiwe msaada kwa hali yetu.

3. **Watu wanapenda.** Kuna faida ya kuwa na ibada inayohamasisha ushiriki wa watu. Hakuna kitu katika Maandiko kinachosema, "Ibada yako inapaswa kuwa ya kuchosha!" Tunaweza kugundua kwamba wimbo unaopendwa na watu wetu ni wa kweli na ni wa kuabudu. kama ndivyo, hiyo ni nzuri; lakini ikiwa watu wanapenda wimbo unaofundisha mafundisho ya uwongo, hatupaswi kuuimba.

4. **Inaturuhusu kumwabudu Mungu katika roho na kweli**. Hii ndiyo sababu kuu ya kile tunachofanya. Katika kupanga ibada na kuongoza ibada, tunapaswa kuuliza, "Je, wimbo huu unatusaidia kumwabudu Mungu vyema zaidi? Je, utaratibu huu wa ibada unatupeleka katika uwepo wa Mungu? Je, mwaliko utakuwa njia bora zaidi ya kuitikia mahubiri haya, au tumalizie kwa wimbo wa sifa? Je, tunamwabuduje Mungu katika roho na kweli wiki hii?"

## Hitimisho: Tunaposhindwa katika ibada

Kanisa liliimba wimbo wa ufunguzi kwa shauku ndogo. Kwaya ilikuwa imefanya mazoezi, lakini waliimba vibaya asubuhi hiyo. Mwimbishaji alisahau maneno. Mpiga kinanda alicheza noti zisizo sahihi. Mahubiri ya mchungaji hayakuonekana kugusa watu. Ibada ilikuwa janga. Je, imewahi kukutokea? Unafanya nini unaposhindwa kuongoza ibada?

### (1) Kumbuka, ibada zote ni mazoezi.

Ibada yetu ni mazoezi ya ibada ya mbinguni. Sisi ni watu wasio wakamilifu, na ibada yetu itakuwa isiyokamilika sikuzote. "Tumeitwa kutoa kilicho bora katika ibada, na sio kutoa kilicho kamilika."[74]

### (2) Wiki Ijayo Inakuja.

Usijiuzulu Jumatatu. Subiri hadi Jumanne ili kutathmini Ibada. Jifunze kutokana na makosa na uendelee mbele. Katika ibada iliyoelezwa hapo juu, wimbo wa ufunguzi haukufahamika kwa waumini wa kawaida. Kiongozi alidhani wanaujua wimbo huo; lakini sivyo. Aliandika maandishi katika wimbo wake, "Fundisha kwaya wimbo huu kabla ya mkutano kuuimba

---

[74] Nukuu hii na mapendekezo katika sehemu hii yanatokwa kwa Franklin Segler na Randall Bradley, *Christian Worship* (Nashville: B&H Publishing, 2006), 274-275.

tena.” Jifunze kutokana na makosa yako, tafuta msaada wa Mungu, na umruhusu Mungu afanye kazi kupitia wewe Jumapili ijayo.

**(3) Kumbuka, kuabudu ni neema.**

Viongozi wengi wa ibada ni wapenda ukamilifu; hatutosheki. Ibada haihitaji ukamilifu; kuabudu ni neema. Mungu hufanya kazi hata kwa kushindwa kwetu ili afikie malengo yake. Hivi ndivyo inavyopaswa kuwa! Tunapotambua kwamba ni Mungu anayetuwezesha kuabudu, tunaletwa mahali pa unyenyekevu na utii.

**(4) Ikiwa tumejitolea kwa uwezo wetu wote, hatujashindwa.**

Jumapili hiyo, kiongozi wa ibada alitoka nje ya kanisa akiwa amekata tamaa. Alipokuwa akiondoka kwenye jengo hilo, Timotheo alikuwa akimngoja. Timotheo alikuwa mwenye aibu na sio mzungumzaji, lakini asubuhi hiyo alisema, “Uliimba wimbo unasema ‘Yesu Ananipenda’ alijitoa dhabihu kwa ajili yangu.” (Ndiyo, kiongozi wa ibada alijua wimbo alioimba - alikuwa ameharibu!) Lakini Timotheo aliendelea, "Nilihitaji kusikia wimbo huo. Wiki hii daktari aliniambia kuwa nina saratani; Nilihitaji kukumbushwa kwamba Yesu ananipenda.”

Ikiwa tumejitolea kwa uwezo wetu wote, hatujashindwa. Mungu anafanya kazi kupitia jitihada zetu dhaifu za kusema Neno lake kwa watu tunaowatumikia.

► Majadiliano ya kikundi. Angalia "Mapitio ya Somo la 8." Je, kuna hoja zozote ambazo hukubaliani nazo? Ni hoja gani unahisi ni muhimu zaidi kwa matumizi yako ya haraka?

## Mapitio ya Somo la 8

(1) Je, tunajiandaa vipi kwa ibada?

- Maandalizi kwa ajili ya ibada huanza na kujiandaa kwa kiongozi wa ibada kwa kutumia muda wake kwenye Neno.
- Utaratibu wa kupanga husaidia kutoa muundo kwa huduma ya ibada.
- Mada kwenye ibada husaidia kuwasilisha ujumbe muhimu.
- Uwiano hukakikisha ibada yetu huzungumzia injili yote kwa kanisa zima.
    - Ibada yenye uwiano huonesha ukuu wa Mungu na uwepo wa Mungu kwetu.
    - Ibada yenye uwiano ni ya pamoja na binafsi.
    - Ibada yenye uwiano hujumuisha yale yanayofahamika nay ale yasiyofahamika.
- Kupanga kwa ajili ya ibada kunapaswa kujumuisha timu ya viongozi wote wa kanisa.
- Kupanga kwa ajili ya ibada inapaswa kuangalia muda mrefu.
- Tunaweza kupanga bila shinikizo kwa sababu ibada haituhusu; ni kuhusu Mungu.

(2) Ni nini muhimu katika kuongoza ibada?

- Msikilizaji muhimu zaidi katika ibada ni Mungu.
- Kanisa, viongozi wa ibada, na Mungu wote hushirikiana katika ibada. Viongozi hawafanyi ibada kwa wasikilizaji.
- Kiongozi wa ibada lazima aabudu. Huongoza kwa mfano.
- Kiongozi wa ibada anapaswa kuwa mwenye kutia moyo, si kuhukumu.
- Kiongozi wa ibada lazima aongoze, sio kuigiza.
- Matangazo yanapaswa kushughulikiwa kwa njia isiyoleta usumbufu iwezekanavyo.
- Baada ya kupanga ibada, tunapaswa kumwachia Mungu aingie katika huduma zetu kwa njia anayochagua kuja.

## Somo la 8 Mazoezi

(1) Katika Somo la 6 na 7, ulichagua nyimbo na maandiko juu ya mada tano tofauti. Panga ibada kulingana na kila moja ya mada tano. Kuwa na maelezo ya kina iwezekanavyo katika kupanga ibada ya umoja, ikijumuisha nyimbo za kutaniko, maandiko, mada ya mahubiri na maandishi, pamoja na vitu vingine vyovyote vinavyofaa kwa ibada yako. Tumia muhtasari mmoja au zaidi uliotolewa katika Kiambatisho A kwa mradi huu.

(2) Mwanzoni mwa somo linalofuata, utafanya mtihani kulingana na somo hili. Jifunze maswali ya mtihani kwa uangalifu katika maandalizi.

## Jaribio Somo la 8

(1) Orodhesha sehemu kuu mbili katika muundo wa ibada unaozingatia mahubiri.

(2) Orodhesha sehemu kuu nne katika muundo wa ibada kulingana na shughuli za watu wa Mungu katika ibada.

(3) Orodhesha sehemu kuu tatu katika muundo wa ibada kulingana na Zaburi ya 95.

(4) Ni mambo gani matatu tunapaswa kukumbuka kuhusu ibada yenye uwiano?

(5) Katika mfano wa kibiblia wa ibada, nani ni hadhira ya ibada yetu?

(6) Orodhesha sifa tatu za kiongozi bora wa ibada.

(7) Ni dalili gani tatu zinazoonyesha kwamba tunaweza kuwa tunafanya maigizo ya ibada?

(8) Andika 2 Mambo ya Nyakati 5:13-14 kutoka kwenye kumbukumbu.

# Somo la 9
# Maswali Mengine

## Malengo ya somo

Mwisho wa somo hili, mwanafunzi anapaswa:

(1) Kutambua umuhimu wa kuwa mwaminifu kwa maandiko huku akiheshimu tofauti za kitamaduni katika kuabudu.

(2) Kutathmini ibada kuhusiana na maandiko na utamaduni.

(3) Kuelewa changamoto mahususi za kutathmini mtindo wa muziki.

(4) Kutumia kanuni za Warumi 14 katika ibada.

(5) Kuthamini umuhimu wa kuwashirikisha watoto na vijana katika ibada.

(6) Jihadharini na kusisitiza hisia kupita kiasi au kupuuza hisia katika ibada.

## Matayarisho kwa somo hili

*Kariri 1 Wakorintho 14:15-17.*

## Utangulizi

Warren Wiersbe aliandika kuhusu uzoefu wake katika kanisa ambalo lilishindwa kuelewa ibada:

> "Hakikisha unarudi kwa ibada ya jioni," alisema kiongozi wa ibada, akiwa na sauti na tabasamu la mtangazaji wa mchezo wa runinga. "Tutakuwa na wakati mzuri wakufurahia."
>
> Wakati wa saa za mchana jumapili, nilijiuliza kauli hiyo ilimaanisha nini. "Tutakuwa na wakati mzuri wakufurahia" kauli hii inaeleweka katika mwaliko wa sherehe ya kuzaliwa, lakini inahusianaje na kikundi cha waamini Wa Kikristo waliokusanyika kumwabudu Bwana wa utukufu? Musa na watu wa Israeli hawakuwa na wakati wa kujifurahisha walipokusanyika kwenye Mlima Sinai….
>
> Yohana alipitia mambo makuu yenye kustaajabisha akiwa katika Kisiwa cha Patmo, lakini si rahisi kusema kwamba alikuwa katika wakati wa furaha.[75]

Katika masomo haya, tumeona kwamba ibada ni zaidi ya wakati wa kufurahisha, zaidi ya ibada fulani, na zaidi ya shughuli ya Jumapili asubuhi. Kuabudu ni kumpa Mungu utukufu

---

[75] Warren Wiersbe, *Real Worship* (Grand Rapids: Baker Books, 2000), 169-170

unaomstahili. Kwenye karatasi, hii ni rahisi; katika maisha halisi, inaweza kuwa changamoto. Katika somo hili, tutaangalia maswali yanayohusiana na ibada. Unapojifunza maswali haya, kumbuka kwamba swali kuu sio, "Ninapenda nini?" Swali kuu la kuabudu ni “Mungu anapenda nini? Ni nini kinachomletea heshima na utukufu?”

## Ibada na Utamaduni

► Jadili mtindo wa Ibada wa kanisa lako. Ni vipengele vipi vya ibada yako vimeamriwa katika maandiko na ni vipengele vipi vinavyoamuliwa na utamaduni?

*“Suala gumu zaidi kwa ibada katika nchi yangu ni umuhimu wa kitamaduni. Makanisa mengi yanaingiza mtindo wa ibada kutoka nje - iwe ni ya kisasa au ya kitamaduni. Watu wetu huchukua mtindo kutoka nchi za magharibi kwa sababu tu wanataka kuwa wa kisasa, lakini si ibada ya ‘kitamaduni’ wala ya ‘kisasa’ inayowagusa watu kwa sababu zote mbili ni za kigeni. Je, tunaabuduje kwa njia inayomheshimu Mungu na inayozungumza na ulimwengu ambao tunahudumu?”*

### Utamaduni au Biblia?

Bibi-arusi na bwana harusi walikuwa wanatoka tamaduni mbili tofauti sana. Katika sherehe ya harusi, vyakula vinavyotolewa hutoka katika utamaduni wa bibi arusi. Sahani moja ilipopitishwa, bwana harusi aliuliza, “Ni nini hicho?” Bibi-arusi akamwambia, "Katika nchi yangu, hii ni kitamu." Alijibu akiwa amekunja uso, "Katika nchi yangu, hii ni chukizo!" Tofauti za kitamaduni zinaweza kuwa changamoto.

Sisi sote tunasukumwa na utamaduni wetu. Sababu ya baadhi ya Wakristo kula na uma badala ya vijiti si kwa sababu uma ni wa kibiblia zaidi au wa ufanisi zaidi. Wanakula kwa uma kwa sababu walikulia katika utamaduni wa kutumia uma. Marafiki wao Wakristo katika sehemu nyinginezo za ulimwengu huona vijiti vya kulia kuwa muhimu zaidi kuliko uma.

Ibada yetu inaathiriwa na utamaduni wetu. Mambo mengi ya ibada yetu ni suala la utamaduni. Mtu ambaye alikulia katika kanisa lenye utamaduni wa Marekani anaweza kupenda sauti ya kinanda kanisani. Kuwa na kinanda kanisani sio kibiblia Zaidi kuliko gitaa; ni sehemu ya utamaduni.

Nchini Lesotho, kanisa linaimba kwa kuita na kuitikia kati ya kiongozi na waumini. Katika mtindo huu, kiongozi huimba sentensi na kisha waumini huimba sentensi inayofuata. Mtindo huo mzuri wa uimbaji huenda usisike kamwe katika kanisa la Marekani. Ikiwa muongozji wa muziki katika kanisa la Marekani angejaribu, waumini wangeweza kuchanganyikiwa. Uimbaji wa umoja wa *kuita/kuitikia* ni suala la kitamaduni, si kanuni ya kibiblia.

Kuna maswali matatu ambayo tunapaswa kuuliza tunapochunguza mtindo wa kuabudu:

1. Je, tunachanganya utamaduni na Maandiko?
2. Je, utamaduni wetu unapingana na Maandiko?
3. Je, ibada yetu inawezaje kuzungumza kwa ufanisi zaidi na watu katika utamaduni ambao Mungu ametuweka?

### ***Je, tunachanganya utamaduni na Maandiko?***

Swali hili ni muhimu tunapotathmini uzoefu wa ibada ambao ni tofauti na wetu wenyewe. Katika hali hii, lazima tuhakikishe hatuchanganyi utamaduni na Maandiko. Ni rahisi kwetu kusoma maadili yetu ya kitamaduni katika Maandiko na kisha kusisitiza kwamba kila mtu mwingine asome Biblia kwa njia hiyo hiyo. Tunaelekea kudhani kwamba njia yetu ni njia ya kibiblia.

Mtu anaweza kusema, "kinanda aina ya organi ni chombo sahihi cha muziki kanisani. Gitaa hazina nafasi katika ibada." Hata hivyo, katika sehemu nyingi za dunia, kinanda cha organi hakitumiki, wakati gitaa linalobebeka ni muhimu sana katika uimbaji. Hakuna mtu anaweza kukataa kwamba makanisa ya nyumbani katika karne ya pili yalitumia vinanda vya bomba! Mtu anaweza kupenda vinanda vya bomba, lakini hawapaswi kuchanganya mapendeleo yao ya kitamaduni na kanuni za kibiblia.

Paul Bradshaw, mwanahistoria wa ibada, ameonyesha kwamba hata katika karne mbili za kwanza za kanisa, kulikuwa na aina mbalimbali za ibada. Kanisa lilipoenea, haikuonyesha kwamba ibada ilibaki vile vile katika kila mpangilio.[76]

Je, ni matokeo yanayofaa ya swali hili? Tunapotathimini mitindo ya kuabudu ya wengine au kuitikia mawazo mapya kutoka ndani ya makanisa yetu wenyewe, hatupaswi kuchanganya utamaduni na Maandiko. Hatupaswi kukataa wazo kwa sababu tu linapingana na matakwa yetu ya kitamaduni. Ikiwa desturi ya kuabudu haipingani na kanuni za kibiblia, basi **tunapaswa kuwaruhusu wengine waabudu kwa jinsi wanavyopenda.**

Hii haimaanishi kwamba kila mtindo wa ibada ni sahihi kwa kila kanisa. Kiongozi wa ibada mwenye busara ataongoza kwa mtindo ambao unafaa watu ambao yeye anawahudumu.

#### **Kujipima**

Je, kuna mazoea ya kuabudu ambayo umeyakataa kwa sababu ya upendeleo wako wa kitamaduni, na si kwa sababu ya kanuni za kibiblia? Ikiwa ndivyo, je, uko tayari kuruhusu waumini wengine kuwa na uhuru wa kuabudu kwa njia yao, mradi tu haikiuki Maandiko?

### ***Je, utamaduni wetu unapingana na Maandiko?***

Swali hili ni muhimu tunapojaribiwa kutetea desturi ya ibada kwa sababu tu ni ya kawaida katika utamaduni wetu. Ikiwa tunagundua kwamba kile ambacho ni cha kawaida katika utamaduni wetu kinapingana na Maandiko, **ni lazima tutii Maandiko badala ya matarajio ya utamaduni wetu.**

Wanamatengenezo walikabiliana na suala hili walipofanya mabadiliko makubwa sana kwenye ibada. Utamaduni wa zama za kati ulisema, "watu wa kawaida hawapaswi kusoma

---

[76] Paul Bradshaw, "The Search for the Origins of Christian Worship" in Robert Webber, *Twenty Centuries of Christian Worship* (Nashville: Star Song Publishing, 1994), 4

Biblia; hawawezi kuelewa." Wycliffe, Huss, Luther, na Wanamatengenezo wengine walikuja kutambua kwamba Maandiko yalikuwa kwa ajili ya watu wote. Utamaduni wao wa zama za kati ulipingana na mafundisho ya Maandiko. Wanamatengenezo walihatarisha maisha yao ili kukabiliana na utamaduni wao na ukweli wa Maandiko.

Utamaduni ukipingana na Maandiko, ni lazima tuondoe utamaduni wetu! Neno la Mungu ndilo mamlaka yetu ya mwisho; hatuwezi kuhatarisha uaminifu kwa Maandiko ili kupatana na ulimwengu unaotuzunguka. Muhtasari wa Warumi 12:2 unasema, "Wala msiifuatishe namna ya dunia hii, bali mgeuzwe kwa kufanya upya nia zenu."[77] Hatuwezi kuruhusu ulimwengu utusukume katika umbo lake.

**Kujipima**

Je, kuna maeneo ambayo ibada yako inapingana na kanuni za Maandiko?

### *Je, ibada yetu inawezaje kuzungumza kwa ufanisi zaidi na watu katika utamaduni ambao Mungu ametuweka?*

Swali hili ni muhimu kwa ajili ya kuufikia ulimwengu wetu kwa injili. Ikiwa tunataka kugusa ulimwengu unaotuzunguka kwa injili, ibada yetu lazima izungumze katika lugha wanayoelewa.

Yohana Wesley alikabiliana na swali hili alipoanza kuhubiri nje. Kama vijana wenzake wa Kianglikana, mwanzoni Yohana aliamini kwamba kanisani ndio mahali pekee pazuri pa kuhubiri. Chini ya ushawishi wa George Whitefield, Yohana alianza kuelewa kwamba amri kuu ilimtaka ahubiri nje ya kanisa.[78] Yohana alilazimika kujiuliza, "Ninawezaje kuhubiri injili kwa ufanisi zaidi kwa wachimbaji migodi ya makaa ambao kamwe hawataingia kanisani isipokuwa kwa ajili ya harusi na mazishi?" Jibu lilikuwa kuhubiri nje.

Mnamo Aprili 2, 1739, Yohana alienda nje ya mji na kuhubiria watu wapatao 3,000 waliokusanyika uwanjani. Hii ilianzisha huduma ambayo ingebadilisha ulimwengu wa watu wanaozungumza Kiingereza wa karne ya 18.

Yohana alikuwa ameyapinga mahubiri ya nje kwa nguvu sana kiasi kwamba wakati fulani alisema, "ningefikiri kwamba kuokoa nafsi ni dhambi kama isingefayika kanisani." Alipogundua kuwa chuki zake za kitamaduni zilikuwa kizuizi kwa injili, Yohana alikuwa tayari kubadilisha mazoea yake. Vijana wenzake wakianglikana walikataa badiliko hili. Ndani ya mwezi mmoja baada ya kuanza kuhubiri nje, askofu mmoja alimwambia Yohana kwamba hakubaliwi tena kuhubiri katika makanisa ya Kianglikana. Kuwa tayari kubadilisha utamaduni wako kunaweza kugharimu sana; ilimgharimu Yohana heshima ya wengi wa Waanglikana wenzake. Wito wa Yesu wa kuwa nuru na chumvi ni kipaumbele cha juu kuliko faragha wa kibinafsi.

---

[77] E. H. Peterson, *The Message* (Colorado Springs: NavPress, 2002)

[78] Hii inaelekeza kwa Swali la 2 - "Je, utamaduni wetu unapingana na maandiko?"

Michael Cosper anapendekeza maswali matatu ya kuelewa uhusiano kati ya ibada yetu na utamaduni unaotuzunguka.[79]

**(1) Nani yupo hapa?**

Swali hili linatazama waamini wetu; "ni nani hushiriki ibada zetu?" mara nyingine tunakuwa na wasiwasi sana kuhusu kuwafikia watu ulimwenguni kiasi kwamba tunashindwa kuwahudumia waumini wa kanisa. Ibada yetu inakuwa si halisi tunapojaribu kuwa mtu ambaye sio. Kwa kuwa ibada inapaswa kuhudumia waumini, ni lazima tujiulize, "Ni nani yupo hapa? Mungu amemweka nani katika kanisa letu?"

**(2) Nani alikuwa hapa?**

Swali hili linaangalia urithi wetu. Kama waamini, tuna urithi unaorudi hadi kanisa la kwanza na kuenea kote ulimwenguni.

Hii ina maana kwamba tutafanya jitihada za kutambulisha nyimbo kuu za zamani kwa kizazi chetu. Ina maana kwamba tutawaunganisha watu leo na historia ya kanisa. Vijana Wakristo wanapaswa kufahamu kwamba wao ni sehemu ya urithi ambao ulianza muda mrefu kabla ya sisi kuzaliwa na utaendelea muda mrefu hata baada ya sisi kuondoka. Sisi ni sehemu ya kanisa zima linaloundwa na waumini kutoka vizazi vyote.

Urithi wetu wa ibada unarudi nyuma hadi Pentekoste, unarudi kwenye ufunuo wa Mungu kwa Musa katika Mlima Sinai, na hatimaye unarudi kwenye ufunuo wa Mungu kwa Adamu na Hawa katika bustani ya Edeni. Ibada yetu inapaswa kuadhimisha historia hiyo. Tunapoimba "Ngome Imara Ni Mungu Wetu," tunajiunga na ibada ya Mageuzi. Tunapokariri Imani ya Mitume, tunajiunga na ibada ya karne ya pili. Katika ibada tunauliza, "Ni nani aliyekuwa hapa kabla yetu?"

**(3) Nani anapaswa kuwa hapa?**

Swali hili linaangalia jamii yetu. Tunapouliza, "Ni watu gani wanaopaswa kuwa sehemu ya kanisa letu," tunauliza maswali kama vile:

- Je, tunajaribu kumfikia nani kupitia injili?
- Iwapo jamii yetu ingekuja kanisani, ibada yetu ingeonekanaje?[80]
- Tunawezaje kuwa waaminifu kwa ujumbe wetu tunapoabudu kwa njia inayozungumza na watu tunaojaribu kuwafikia?

---

[79] Michael Cosper, *Rhythms of Grace: How the Church's Worship Tells the Story of the Gospel* (Wheaton: Crossway Books, 2013), 176-179

[80] John Wesley alikabili suala hili. Waanglikana walitambua kwamba ibada iliyohudhuriwa na wachimba migodi ya makaa ya mawe, makahaba waongofu na wenye maduka wasiojua kusoma na kuandika ingekuwa tofauti sana na ibada rasmi ya Waanglikana wa tabaka la juu. Mapadre wengi waliamua kuwa hawakuwa tayari kuruhusu ibada yao kuingiliwa na tabaka za chini. Hii ilisababisha kuundwa kwa jamii za Methodist.

Maswali haya ni magumu katika maisha halisi kuliko kwenye karatasi! Angalia matukio manne. Kila kanisa limekabiliana na changamoto ya kuzungumza na jamii.

### *Kanisa A: Kanisa ambalo lilishindwa kuuliza, "Ni nani yuko hapa?"*

Kanisa A liko katika jamii ya wastaafu. Umri wa wastani katika jamii ni miaka 70, na wastani wa umri katika kanisa ni miaka 70. Miaka miwili iliyopita, mchungaji wao aliamua kufikia familia za vijana. Katika kipindi cha miezi miwili, alibadilisha kinanda, kwaya, na nyimbo na gitaa, timu ya sifa, na skrini ya juu.

Kwa bahati mbaya, mchungaji alisahau kuuliza, "Ni nani yuko hapa?" Kwa sababu hiyo, kanisa la wazee 100 limeshuka hadi kuwa kanisa la wazee 35 wanaoimba muziki ambao hawapendi, kuangalia skrini ambayo hawapendi, na kunung'unika kuhusu gitaa kubwa.

Je, Kanisa A linapaswa kuwafikia watu nje? Kabisa! Lakini watu wanaoweza kuwafikia kwa ufanisi zaidi ni wazee wasio na kanisa katika jamii yao ya wastaafu. Kwa kuwapuuza watu ambao tayari wako kanisani, wanashindwa kuabudu kwa njia inayozungumza na kanisa lenyewe au na jamii inayowazunguka. Kanisa A lilishindwa kuuliza, "Ni nani yupo hapa?"

### *Kanisa B: Kanisa ambalo lilishindwa kuuliza, "Nani alikuwa hapa?"*

Kanisa B lipoo katika mji unakuwa kwa kasi wenye familia nyingi za vijana. Kanisa hilo linazungumza lugha ya jamii yao; ibada yao ni ya kusisimua na yenye shauku.

Kanisa B lina shauku ya uinjilisti. Kwa bahati mbaya, kanisa hilo halijauliza, "Ni Nani alikuwepo hapa?" Kanisa B limesahau urithi wake kama kanisa lililohubiri ujumbe wa moyo safi na maisha ya Kikristo ya ushindi. Mchungaji anaepuka kuhubiri mafundisho kwa sababu anafikiri, "Watu hawataki kusikia mafundisho; wanataka mahubiri ya vitendo." Kiongozi wa sifa na muziki anaepuka nyimbo zenye kina kibiblia kwa sababu anafikiri, "Watu hawapendi nyimbo zenye maneno magumu; wanapenda nyimbo rahisi." Kwa hiyo, kanisa limelea kizazi cha "wapagani waliobatizwa."[81]

Kanisa B linaongezeka kwa idadi, lakini wahirika wachache wanakua katika utauwa. Watu wengi huhudhuria kwa sababu ni kanisa la kuburudisha ambalo linahitaji kujitolea kidogo. Kwa sababu Kanisa B halijui urithi wake, waongofu wengi hivi karibuni wanageukia makanisa mengine ambayo hutoa burudani bora zaidi. Kanisa B lilishindwa kuuliza, "Nani alikuwa hapa?"

### *Kanisa C: Kanisa ambalo lilishindwa kuuliza, "Nani anapaswa kuwa hapa?"*

Kanisa C lilianzishwa karibu miaka 100 iliyopita katika jamii ndogo ya vijijini. Ibada, mahubiri, na muziki viliwasiliana na watu walioishi katika mji huo. Katika miaka ya kati, jamii imebadilika kabisa. Kanisa C sasa limezungukwa na jiji la ndani, lakini ibada yake bado imeundwa kuvutia watu wa tabaka la kati la vijijini.

---

[81] Neno la Mark Dever kwa wanaojiita Wakristo ambao hawana msingi wa kibiblia.

Cha kusikitisha ni kwamba, watu wengi wanaoishi karibu na Kanisa C hulipita kanisa kila wiki bila kujua kwamba kanisa lina majibu ya njaa yao kuu. Kanisa C lina ujumbe ambao jamii yake inahitaji, lakini haliwasiliani kwa uwazi na jamii. Kama Kanisa C lingeweza kuabudu kwa njia inayowasiliana na Mungu na kwa ulimwengu wenye mahitaji, lingeweza kubadilisha jamii yake. Badala yake, Kanisa C linakufa kwa sababu lilishindwa kuuliza, "Ni nani anayepaswa kuwa hapa?"

***Kanisa D: Kanisa linalozungumza na jamii***

Kanisa D limeweza kuwa na sifa nyingi za makanisa matatu yaliyotangulia. jamii imebadilika sana tangu kanisa lilipoanzishwa miaka 40 iliyopita. Tofauti na makanisa mengine katika utafiti huu, Kanisa D limejifunza kuwasiliana vyema na jamii yake.

Watendakazi wa wachungaji walipogundua kuwa waongofu wengi wachanga hawaelewi mafundisho yanaliyohubiriwa siku ya Jumapili, walianzisha vikundi vya ufuasi ili kuwaleta waumini wapya kwenye ukomavu. Kiongozi wa muziki alipogundua kuwa muziki huo hauzungumzi na watu wengi katika jamii yao, alianza kujumuisha nyimbo ambazo ni za kweli kimafundisho na zenye kuvutia kimuziki.

Kanisa lilipokua, walipanda makanisa katika miji jirani na kuruhusu makanisa haya kuendana na mahitaji ya jamii zao. Makanisa haya yanachungwa na vijana waliokuwa sehemu ya Kanisa D. Kila kanisa ni tofauti, lakini kila kanisa lina uaminifu kwa injili. Kanisa D linasitawi kwa sababu lilijifunza kuuliza "Ni nani aliye hapa, nani alikuwa hapa, na ni nani anayepaswa kuwa hapa?" limejifunza kusema ukweli wa Biblia kwa jamii ambayo Mungu aliliweka ndani yake.

**Kujipima**

Je, ibada yako inazungumza na watu wanaohudhuria kanisa lako? Je, ibada yako inaakisi urithi wa kanisa la Kikristo? Je, ibada yako inazungumza na wale ambao Mungu anataka kuwafikia kupitia kanisa lako?

**Vipi kuhusu Muziki?**

Wanamuziki wa makanisa katika sehemu nyingi za dunia wanakabiliwa na changamoto ya kupata nyimbo zinazofaa kibiblia na zinazozingatia utamaduni. Tunatafuta muziki unaozungumza lugha ya moyoni kwa jamii tunayotaka kufikia. Muziki wa kigeni unaweza usiwe na umuhimu wa kitamaduni, na baadhi ya nyimbo za kitamaduni zinaweza zisiwe za kibiblia. Je, tunachaguaje muziki ambao utaendana na Maandiko na unaozingatia utamaduni ambao tunachunga? Hapa kuna majibu kutoka kwa wachungaji ambao wanakabiliwa na suala hili:

*Linapokuja suala la kuchagua nyimbo za kanisa, mtu hahitaji kuchagua kati ya kuwa mwaminifu kulingana na biblia na kuwa mwangalifu kiutamaduni. Kwa kuwa "mwaminifu kulingana naa biblia" natafuta nyimbo ambazo ni za kweli na zilizo wazi. Kwa kuwa*

*"mwangalifu kiutamaduni" ninatafuta nyimbo ambazo ni rahisi kuimba na kushirikisha kanisa.*

*Uaminifu wa Kibiblia unachukua kipaumbele, lakini hatuhitaji kuchagua kati yao. Ikiwa lengo la kuimba ni mawasiliano, je, si ni vema kuchagua lugha ya muziki inayolingana na utamaduni [mazingira] ya kanisa letu? Tungekuwa wapumbavu tukifikiri kwamba hisia za kitamaduni hazifai, na hatutakuwa na maana ikiwa nyimbo zetu si za kweli au zisizo wazi.*

(Murray Campbell, mchungaji huko Melbourne, Australia)

*Katika mafunzo ya wachungaji wa Kiafrika, tunawahimiza watafute nyimbo zilizojaa zaidi maandiko, zinazomlenga Mungu, zinazoongozwa na injili, zinazojenga, na za kuimba ambazo wanaweza kupata, za zamani na mpya, na kuziachia! Katika utamaduni wowote, watu wa Mungu wanahitaji nyimbo ambazo zitawafundisha kuishi na kufa kwa ajili ya Kristo.*

(Tim Cantrell, mwalimu huko Johannesburg, Afrika Kusini)

*Msururu wa nyimbo thabiti za kitheolojia, zinazofaa kimuktadha katika jamii ya Kihindi ni ndogo sana. Nyimbo nyingi ambazo zina theolojia nzuri zimetafsiriwa kutoka kwenye nyimbo za zamani za Magharibi au nyimbo za kuabudu za kisasa. Ingawa maneno yanaweza kuwa ya uaminifu, muziki huo si wa kiasili, na wenyeji wanaona ni vigumu kuuimba. Pia, nyimbo kama hizo zinathibitisha tu tuhuma za watu kwamba Ukristo ni dini ya Magharibi.*

*Kwa upande mwingine, nyimbo za Kihindi ambazo zina muktadha wa muziki mara nyingi hazina uzito wa teolojia, zinajirudiarudia, na hazina Maandiko. Mara nyingine nyimbo hutumia tuni zinazotumiwa katika mahekalu. Tunaepuka aina zote hizi za nyimbo.*

*Jambo la kwanza ninaloangalia wakati wa kuchagua nyimbo ni utimilifu wake wa mafundisho. Ikiwa wimbo hauna msingi thabiti wa kitheolojia, hatutauimba, licha ya muktadha wake. Ikiwa maneno ni mazuri lakini wimbo sio wa Kihindi, hatutauimba. Tunachagua nyimbo zenye tuni za Kihindi na maneno ya uaminifu. Kwa kweli, hakuna nyimbo nyingi ambazo ziko katika kitengo hiki, lakini tunaunda mtindo wetu polepole.*

(Harshit Singh, Mchungaji huko Lucknow, India)

Kama vile kuna lugha ya moyo ya maongezi ambayo mtu huzungumza kwa kawaida zaidi na anahisi kwa undani zaidi, kuna lugha ya muziki ya moyo ambayo inazungumza na mtu kwa undani zaidi.

Fikiria kuhusu mmishonari anayeshindwa kujifunza lugha ya watu anakohudumu. Anaweza kusema (kwa lugha yake mwenyewe), "Niko hapa kuwaletea injili. Huwezi kuelewa ninachosema, lakini endelea kunisikiliza. Hatimaye, mtaelewa ninachosema, nanyi mtajua habari njema." Bila shaka hapana hautaweza kujua habari jema! Vivyo hivyo, tunapokosa

kutumia lugha ya kimuziki wa utamaduni fulani, tunafanya habari njema kuwa ngumu zaidi kueleweka.[82]

Kwa kusikitisha, kama Mchungaji Singh alivyoandika, katika baadhi ya tamaduni kuna nyimbo chache zenye msingi wa kibiblia zinazotumia lugha ya muziki isiyo ya Magharibi. Hii mara nyingi huwaacha makanisa yakiwa na chaguo mbili: nyimbo zenye nguvu za kibiblia zenye tuni zinazosikika kigeni au nyimbo zenye udhaifu wa kibiblia zenye tuni zinazolingana na muktadha wa muziki. Ikiwa tunataka kutumia muziki kujenga kanisa kote ulimwenguni, tunapaswa kutafuta muziki ambao ni wa kweli kwa Maandiko na ambao unazungumza katika lugha ya muziki ya moyo ya watu. Ninaamini kwamba Mungu anataka kuwaita waandishi wa nyimbo wacha Mungu katika kila utamaduni.

Ikiwa unahudumu katika utamaduni ambapo kuna nyimbo chache za ibada zenye ubora, unaweza kuhamasisha muziki mpya. Hili linaweza kuhitaji ushirikiano kati ya watu wawili; mtu wa kuandika au kutafsiri maandishi bora na mtu wa kuandika muziki. Waandishi wachache wakubwa wa nyimbo waliandika nyimbo zao wenyewe. Tafuta mwanamuziki wa Kikristo aliyejitolea na uwafanye waandike tuni za nyimbo zinazozungumza ukweli wa kibiblia. Kwa kufanya hivi, unaweza kuimba ujumbe wa kibiblia katika lugha ya muziki inayowasiliana na ulimwengu wako.

Ni lazima kila wakati tufikirie Swali la 2 hapo juu: "Je, utamaduni wetu unapingana na Maandiko?" Ikiwa utamaduni wa muziki unapingana na Maandiko, hatupaswi kuutumia. Hata hivyo, wakati hakuna kanuni ya kibiblia inayohusika, tunapaswa kutafuta kuongoza ibada katika lugha ya muziki ya waabudu.

Alipokuwa akiabudu katika kanisa la baba yake, kijana mmoja aliyejitayarisha kwa ajili ya huduma alitambua kwamba watu wachache walielewa nyimbo walizokuwa wakiimba. Badala ya kuabudu, walionyesha uelewa mdogo wa kweli walizokuwa wakiimba. Kijana huyo alipolalamika kuhusu jambo hilo, baba yake alijibu, "Ona kama unaweza kufanya vyema zaidi." Kijana Isaac Watts alikubali changamoto ya baba yake.

Watu wanaozungumza Kiingereza wanaimba nyimbo za Isaac Watts leo kwa sababu mchungaji kijana aliazimia kuandika nyimbo zinazowasilisha ujumbe wa Biblia katika lugha ambayo watu wanaelewa.[83] Katika kizazi chetu, tunahitaji waandishi wa nyimbo ambazo zinazungumza ukweli wa kibiblia katika lugha inayogusa mioyo ya ulimwengu wa wasiozungumza kiingereza.

---

[82] Mfano huu umechukuliwa kutoka kwa Ronald Allen na Gordon Borror, *Worship: Rediscovering the Missing Jewel* (Colorado Springs: Multnomah Publishers, 1982), 168.

[83] "Furaha kwa Ulimwengu," "Ninapochunguza Msalaba wa Ajabu," na "Ee Mungu, Msaada Wetu Katika Zama Zilizopita" ni nyimbo tatu kati ya 750 zilizoandikwa na Isaac Watts.

## Baadhi ya Mawazo Ya Kufunga Kuhusu Mtindo wa Muziki

Kwakuwa muziki ni sehemu muhimu katika maisha, wengi wetu tuna Imani kubwa kuhusu muziki. Majadaliano yoyote kuhusu mtindo wa muziki katika ibada yanaweza kupelekea migogoro.

Wale wanaoamini kwamba mtindo fulani wa muziki haufai husema, "mtindo fulani pekee wa muziki unaweza kutumika katika ibada." Ingawa, Maandiko hayajatoa mwongozo maalumu kuhusu mtindo wa muziki.

Wale wanaoamini kwamba mitindo ya muziki haifungamani na upande wowote wa kimaadili husema, "Tafuta muziki ambao watu wanapenda na uuimbe. Mtindo haujalishi; imba unachopenda." Hata hivyo, Maandiko yanaweka wazi kwamba ni lazima tuepuke chochote kinachotupeleka kwenye tabia ya kimwili. Kwa sababu ya maana fulani ya kitamaduni na kihisia, muziki fulani haufai kwa ibada.

Akiandika kuhusu uchaguzi wa muziki, Scott Aniol aligawanya mjadala wake katika sehemu mbili:[84]

1. **Maandishi: suala sahihi na lisilo sahihi.** Bila kujali mtindo wa muziki, ikiwa maneno hayazungumzi ukweli waziwazi haufai kwa ibada. Hili ni suala la sahihi na lisilo sahihi. Kuna nyimbo nyingi zinazotumia mitindo ya muziki wa kitamaduni ambazo zina maneno ambayo hayafundishi ukweli wa kibiblia; haya hayafai kwa ibada. Kuna nyimbo nyingi zinazotumia mitindo ya kisasa ya muziki ambayo ina maneno ambayo hayafundishi ukweli wa Biblia; haya hayafai kwa ibada.
2. **Mtindo wa muziki: suala lisilo wazi.** Kwa kuwa Maandiko hayasemi waziwazi kuhusu mtindo wa muziki, tunapaswa kufuata kanuni za Warumi 14. Tunapaswa kuepuka muziki unaotiliwa shaka kwa sababu ya muingiliano wake wa kitamaduni. Hata hivyo, hatupaswi kuwahukumu wengine ambao dhamiri yao inawaongoza katika mwelekeo tofauti wa muziki.

### Kujipima

Je, kuna maeneo ya kitamaduni katika ibada yako ambayo yanapunguza uwezo wako wa kufikia ulimwengu wako kwa injili? Je, uko tayari kusalimisha mapendeleo yako kwa ajili ya kuufikia ulimwengu wako na injili?

### Vipi kuhusu Kupiga makofi?

Vipi kuhusu kupiga makofi ibadani? Je, ni sahihi au sio sahihi? Kupiga makofi hutokea katika miktadha miwili, ikiwa na maana mbili tofauti kabisa.

---

[84] Scott Aniol, *Worship in Song* (Winona Lake, IN: BMH Books, 2009), 135-140

### *Kupiga makofi kama sehemu ya ibada*

Makanisa mengi hupiga makofi kama sehemu ya kuimba; kupiga makofi ni sehemu ya ibada ya kanisa. Hii ni sehemu ya kipengele cha kimwili cha ibada kinachoelezwa katika Maandiko. "Enyi watu wote, pigeni makofi, Mpigieni Mungu kelele kwa Sauti ya shangwe!" (Zaburi 47:1) waabudu wa kiyahudi walikuwa wenye shauku. Ibada ya kiyahudi ilijumuisha aina mbalimbali za vifaa vya muziki, kuinua mikono, na kupiga makofi.

Ikiwa kupiga makofi ni sehemu ya ibada yako, kiongozi wa ibada lazima ahakikishe kwamba inafaa kwa wimbo unaoimbwa. Kupiga makofi wakati wa wimbo wa maombi hakuleti ujumbe. Kupiga makofi wakati wa wimbo wa sifa za shangwe kunafaa. Swali kwa kiongozi sio kila wakati, "Je, kupiga makofi ni sawa au sio sawa?" Swali bora zaidi linaweza kuwa, "Je, kupiga makofi kunafaa kwa wimbo huu na katika hatua hii ya ibada yetu?"

### *Makofi kwa kuitikia ibada*

Suala gumu zaidi ni kupiga makofi *kwa kuitikia* wimbo maalum. Hakuna kiashiria katika Maandiko kwamba waabudu Wayahudi au Wakristo walipiga makofi katika kuitikia ibada.

Baadhi ya tamaduni leo ni wepesi wa kupongeza kama kuonyesha shukrani. Katika tamaduni hizi, ni kawaida kutoa sifa kwa Mungu kwa kupiga makofi. Tamaduni nyingine kupiga makofi kunahusiana hasa na kuthamini utendaji mzuri. Katika tamaduni hizi, kupiga makofi kwa mwitikio wa kwaya au mwanamuziki kunaweza kuunda mazingira ya tamasha, badala ya ibada.

Kwa kuwa Maandiko hayazungumzii suala hili moja kwa moja, tunapaswa kuepuka kauli kamilifu. Ikiwa makofi ni itikio la kawaida la shangwe linalomsifu Mungu, huenda likawa tendo la ibada. Makofi yakitangazwa, "Mtu huyu amefanya vyema kwa ajili ya kufurahia kwetu," huenda ikapunguza ibada.

Kanisa na mwanamuziki wanapaswa kuangalia msukumo wa kupiga makofi. Watu katika ibada wanapaswa kujiuliza, "Kwa nini ninapiga makofi? Je, makofi yangu yanachochewa na sifa kwa Mungu, au makofi yangu yanachochewa na sifa kwa mwimbaji?"

Mwanamuziki anapaswa kuuliza, "Kwa nini waumini wanapiga makofi? Je, wimbo wangu ulichochea tendo la shangwe la kumsifu Mungu, au wimbo wangu ulivuta fikira zao kwenye ustadi wangu wa kuimba? Je, niliongoza katika kuabudu?" Kama viongozi wa ibada tunapaswa kuwa waangalifu kwamba huduma yetu iwe inamuelekea Mungu, na si kwa uwezo wetu.

### Kujipima

Ikiwa kanisa lako linapiga makofi wakati wa ibada, je, kweli kwamba makofi hayo huelezea sifa kwa Mungu au ni huelezea sifa kwa mwimbaji?

## Warumi 14 na Mitindo ya Kuabudu

► Soma Warumi 14:1-23.

Warumi 14 inatoa miongozo muhimu kwa mambo yenye kutiliwa shaka ambayo Maandiko hayasemi waziwazi. Paulo anahutubia wale ambao hawakubaliani kuhusu kula nyama au kuadhimisha siku maalum. Anatoa kanuni zifuatazo.

**(1) Usiwahukumu wengine kuhusu mambo yenye kutiliwa shaka (Warumi 14:1-13).**

Katika maeneo ambayo Maandiko hayasemi waziwazi, ni lazima turuhusu uhuru wa dhamiri kwa wale ambao hawakubaliani nasi. Hatupaswi kuwa dhahiri zaidi kuliko Maandiko yenyewe!

**(2) Usiwafanye wanyonge wajikwae (Warumi 14:13-15).**

Paulo alitambua kwamba mwamini ambaye hajakomaa anaweza kudhuriwa na uhuru unaotumiwa na mwamini aliyekomaa zaidi. Katika hali hiyo, sheria ya upendo inatutaka tuweke kikomo uhuru wetu kwa niaba ya wanyonge. Usimwangamize yeye ambaye Kristo alikufa kwa ajili ya uhuru wako.

Kauli ya Paulo ni kielelezo chenye nguvu kwa maeneo yote ya tabia ya Kikristo; "Kwa hiyo, chakula kikimkwaza ndugu yangu, hakika sitakula nyama hata milele, nisije nikamkwaza ndugu yangu" (1 Wakorintho 8:13).

**(3) Tenda kwa imani, na sio mashaka (Warumi 14:23).**

Hii ni kanuni muhimu kwa vijana Wakristo. "Kila tendo lisilotoka katika imani ni dhambi." Hatupaswi kamwe kukiuka dhamiri yetu ili kumpendeza mtu mwingine. "Aliye na shaka, kama akila, amehukumiwa kuwa ana hatia, kwa maana hakula kwa Imani."

Zinapotumika kwenye mitindo ya kuabudu, kanuni hizi hutuonya:

1. **Usiwahukumu wale wanaotumia mtindo ambao wewe hujapendezwa nao.** Ikiwa Maandiko hayasemi kwa uwazi, lazima usiwe mwepesi kuhukumu.

2. **Usitumie muziki ambao unaweza kumuudhi mwamini mpya.** Ikiwa mwamini anatoka katika mtindo wa maisha ambamo mitindo fulani ya muziki inahusishwa na mwenendo mpotovu, mtindo huo hauwezi *kamwe* kuwa wa manufaa kwa mwamini huyo. Upendo kwa ndugu Mkristo unapaswa kukuchochea uepuke jambo lolote linaloweza kuzuia ukuzi wake wa kiroho.

3. **Usitumie uhuru wakati dhamiri yako ina mashaka.** Haupaswi kujaribu mistari. Kumpenda Mungu kunapaswa kukuchochea uepuke jambo lolote linaloleta shaka katika dhamiri yako mwenyewe.

## Kuwashirikisha Watoto na Vijana katika Ibada.

*"Tunawezaje kuwashirikisha watoto na vijana katika ibada? Je, tuwaweke katika ibada tofauti hadi wawe na umri wa kutosha kuelewa ibada ya watu wazima? Je, tunawahimizaje watoto na vijana kuabudu kweli?"*

Makanisa mengi hutenganisha watoto, vijana, na watu wazima katika ibada. Kuna sababu mbili za hili: wasiwasi kwamba watoto wadogo watasumbua watu wazima kwenye ibada na wasiwasi kwamba watoto na vijana hawataelewa kile kinachotokea katika huduma ya ibada.

Hakuna kitu katika Maandiko kinachokataza ibada za tofauti kwa vijana na watoto. Hata hivyo, kuna angalau mambo matatu ambayo yanapaswa kuzingatiwa:

1. **Katika Maandiko, ibada ilikuwa ya vizazi.** Maandiko hayapendekezi kwamba watoto na vijana walitendewa tofauti katika ibada. Katika ibada ya Hekaluni, familia ilibaki pamoja kwa ajili ya ibada ya dhabihu. Hakuna mahali katika Agano Jipya panapopendekeza kwamba kanisa la kwanza lilitenganisha watoto au vijana wakati wa ibada.

2. **Ibada kati ya vizazi mbalimbali inaunganisha Mwili wa Kristo.** Kama vile kutoa huduma tofauti katika ibada ya kisasa na ibada ya kitamaduni kunaweza kudhoofisha umoja wa Mwili, vivyo hivyo kutoa huduma tofauti kwa watoto na vijana kunaweza kupunguza ufahamu wao wa kuwa sehemu ya familia ya kanisa. Kwa upande mwingine, watoto na vijana wanapojumuishwa katika ibada ya familia ya kanisa, kila mtu anaelewa kwamba wao ni sehemu ya thamani ya Mwili wa Kristo (1 Timotheo 4:12)**.**

3. **Kupitia ibada ya vizazi, imani hupitishwa kwa kizazi kijacho.** Tunajifunza kuabudu kwa kuabudu. Isipokuwa imepangwa kwa uangalifu, ibada ya watoto inaweza kuwa ni wakati wa kuburudisha watoto ili wasiingiliane na ibada ya watu wazima. Tukifanya hivi, ni lini watoto watajifunza kuabudu?

### Vijana na Watoto kama Sehemu ya Huduma ya Ibada ya Pamoja

Vijana na watoto mara nyingi wanaweza kushiriki katika ibada ya pamoja inayozungumza na kila kizazi. Hii inaweza kuhusisha mahubiri mafupi ya watoto juu ya mada sawa na mahubiri makuu.

Tunapodhani kwamba watoto hawawezi kuelewa ukweli wa kina, tunashindwa kuwapa sifa za kutosha kuhusu kupambanua kiroho. Ni Roho Mtakatifu ambaye huangazia nuru yake kwa kila msikilizaji, mtu mzima au mtoto (1 Wakorintho 2:10). Hata katika ibada ya watu wazima, Roho Mtakatifu anaweza kusema ukweli kwa mioyo yao michanga. Kujumuisha watoto katika ibada ya watu wazima inatuhitaji kuwafundisha kuhusu ibada. Tunaweza kuelezea ibada kwa watoto. Tunaweza kufafanua maneno magumu katika usomaji wa Maandiko na nyimbo. Hata watu wazima wakati mwingine wanahitaji maneno hayo kufafanuliwa! Kwa kuwapa watoto nafasi katika ibada, tunawaruhusu wakue kama waabudu pamoja na mwili wote.

**Ibada Tofauti kwa Vijana na Watoto[85]**

Makanisa mengi hutoa ibada tofauti kwa vijana na watoto. Ibada hizi zinapaswa kuwa ibada, sio burudani. Ikiwa watoto na vijana hawatajifunza kuabudu, hawatakua na kufikia ukomavu wa kiroho. Kama vile mtoto hasitawishi afya ya kimwili kwa kula peremende, mtoto hatasitawisha afya ya kiroho kwa kula vyakula visivyofaa vya kiroho.

Ikiwa kanisa linatoa ibada tofauti za watu wazima na vijana/watoto, lazima tuhakikishe kwamba ibada hiyo ni ibada ya kweli. Ibada ya vijana na watoto inapaswa kujumuisha usomaji wa Maandiko. Kwa watoto, vielelezo vya kuvutia vinaweza kuimarisha ukweli wa Maandiko.

Ibada inapaswa kujumuisha mahubiri au somo la Biblia linalotumia Neno la Mungu kwa mahitaji ya vijana na watoto. Biblia yenyewe inapaswa kushikwa kwa upendo mikononi mwa mwalimu. Watoto na vijana hujifunza kuheshimu na kutumia Neno la Mungu kwa kulitazama likitumiwa na watu wazima wanaowaheshimu.

Ibada inapaswa kujumuisha nyimbo zinazozungumza ukweli wa kibiblia. Inapaswa kujumuisha muda wa maombezi, sifa na maombi. Inapaswa kujumuisha sadaka inayoruhusu watoto kuleta zawadi zao kwa Mungu. Vipengele vyote vya ibada vinapaswa kujumuishwa katika ibada ya watoto au vijana.

**Kufundisha Watoto Kuomba: "Mkono wa Maombi"**

**Kidole gumba** kinatukumbusha kuwaombea walio karibu nasi (familia).

**Kidole cha kuashiria** kinatukumbusha kuwaombea wale wanaoelekeza watu kwa Yesu (wachungaji, waalimu, na wamisionari).

**Kidole cha kati** ndicho kirefu zaidi. Hii inatukumbusha kuwaombea viongozi wa nchi, shule, kanisa na nyumba zetu.

**Kidole cha nne** ni dhaifu zaidi. Onyesha hili kwa kujaribu kuinua kidole cha nne pekee. Hii inatukumbusha kuwaombea wale walio dhaifu na wanaomhitaji Yesu.

**Kidole cha tano** ni kidogo zaidi. Hii inakukumbusha kujiombea mwenyewe.

Kuinua **mkono mzima** kunatukumbusha kumsifu Mungu.

Mkono huu wa maombi unaweza kuwa muundo wa maombi unaoinua kiwango cha maombi cha waabudu wachanga.

[85] Sehemu hii inatumia nyenzo kutoka kwa Bi. Christina Black, Profesa wa Elimu katika Hobe Sound Bible College

**Muhtasari**

Ikiwa tunataka kuona watoto wetu wakikua na kuwa waumini waliokomaa, ni lazima tuwaandalie chakula cha kiroho. Iwe katika ibada ya umoja au katika ibada tofauti, ni lazima tuwaongoze watoto wetu kwenye ibada.

**Kujipima**

Iwe una ibada tofauti kwa watoto na vijana au ibada ya umoja kwa kanisa zima, je unawafundisha watoto wako na vijana kuabudu?

## Hisia Katika Ibada

*"Watu katika nchi yetu wana hisia nyingi sana, na ibada yetu mara nyingi huonyesha maisha yetu ya kihisia moyoni. Muziki wetu wa kuabudu kwa kawaida huwa wa haraka, wenye sauti kubwa na wenye mdundo. Inaturuhusu kushiriki na kueleza hisia. Hata hivyo, ninaogopa kuwa muziki ni hisia* ***tu****. Sijui ikiwa muziki wetu unachangia ibada ya kweli."*

Ibada ya kweli ni kuabudu katika roho na kweli. Ibada ya kweli inahusisha hisia, lakini ni zaidi ya hisia. Kuna makosa mawili yanayohusiana na hisia katika ibada ambayo yanaweza kutupoteza.

**(1) Kosa la kukataa hisia katika ibada.**

Baadhi ya waabudu hukana hisia katika ibada. Wanaona kuabudu kuwa ni kukutana na Mungu kiakili; wanashindwa kutambua kipengele cha hisia cha kukutana na Mungu. Ibada ya kweli inazungumza na hisia. Huduma yetu ya kuabudu inapaswa kuwapa waabudu fursa ya kueleza mwitikio wao wa kihisia kwa ufunuo wa Mungu juu yake mwenyewe.

> "Kuimba ni njia ambayo watu wa Mungu hushika Neno lake na kupatanisha hisia zao na shauku zao sawa na Neno la Mungu."
>
> - Kutoka kwa Jonathan Leeman

**(2) Kosa la kusisitiza zaidi hisia katika ibada.**

Hatari iliyo kinyume ni kosa la kuzungumza tu na hisia katika ibada. Ibada inayozungumza na hisia huku ikipuuza akili inakiuka 1 Wakorintho 14:15; "Imekuwaje, basi? Nitaomba kwa roho, tena nitaomba kwa akili pia; mtaimba kwa roho, tena nitaimba kwa akili pia." Kipengele chochote cha ibada kinaweza kuangukia kwenye jaribu hili: mahubiri ya ajabu ambayo yako kinyume na Maandiko; muziki wa hisia unaoshindwa kusema ukweli wa Biblia; mazoea ya ibada yanayokengeusha hisia za waabudu. Ibada inayozungumza tu na hisia sio ibada ya kweli.

**Ibada ya Kweli: Ibada katika Roho na Kweli**

Mfano wa kibiblia wa ibada huheshimu umuhimu wa hisia huku tukitathmini kwa makini ukweli wa kile tunachohubiri na kuimba. Kwa sababu muziki ni chombo cha hisia, ni lazima tuwe waangalifu hasa ili kutathmini ukweli wa kile tunachoimba. Hata hivyo, muziki ukitumiwa ifaavyo unaweza kuwa wenye matokeo hasa katika kueleza ukweli unaozungumza na akili na hisia pia.

Yohana Wesley alithamini hisia katika ibada. Alielezea moya ya kutaniko moja "Waliokufa kama mawe - tulivu kabisa, na wasiojali kabisa." Aliamini kwamba kukutana na ukweli kunapaswa kuhamasisha mwitikio wa kihisia. Wakati huohuo, alikuwa mwepesi kukosoa maelezo ya kihisia ambayo yaliondoa ibada ya kweli.

Wesley alionya dhidi ya hisia iliyokithiri; kukataa hisia au kuruhusu hisia kututawala. "Je, kuna ulazima wowote wa kuingia katika hali ya kupita kiasi au nyingine? Je, tusiongoze njia ya kati na kujiweka mbali vya kutosha na roho ya upotovu na shauku bila kukataa karama ya Mungu na kuacha mapendeleo makuu ya watoto Wake?"[86] Huu ni mfano mzuri kwetu leo: kuheshimu umuhimu wa hisia katika ibada, huku tukiepuka kupita kiasi na kukengeusha fikira zetu kutoka kwa Mungu na kweli yake.

### *Hisia na Ukweli: Uzoefu wa Mkristo Mmoja* [87]

"Kwa asili, mimi ni mtu mwenye hisia. Muziki unaweza kuwa na ushawishi mkubwa juu ya hisia zangu. Nilijifunza somo miaka michache iliyopita kuhusu kuweka imani nyingi katika mwitikio wangu ya kihisia.

"Nilipokuwa nikisikiliza wimbo wenye sauti nzuri, niliguswa moyo sana. Wimbo ulipokuwa kwenye mabadiliko muhimu ya sauti, nilijikuta nikilia. Kufikia mwisho wa wimbo, nilihisi kana kwamba nilikuwa na uzoefu wa kina wa kiroho.

"Hata hivyo, niliposikiliza mara ya pili, niligundua jambo fulani lenye kushtua: wimbo huu haukuwa ukimuabudu Mungu wa Biblia. Wimbo huo ulikuwa ukiimba sifa kwa mungu wa ibada ya uwongo. Maneno katika badiliko hilo la sauti yalikuwa ni uzushi.

"Siku hiyo nilijifunza kwamba hisia zangu zinaweza kudanganywa kwa urahisi, hasa muziki. Hiyo haimaanishi kuwa kila mwitikio wa kihisia kwa muziki ni batili, lakini inamaanisha kwamba lazima nitathmini maudhui ya nyimbo. Ni lazima 'nizijaribu roho' ili kuhakikisha kwamba zinatoka kwa Mungu."

### Kujipima

Je, ibada yako inazungumza na akili na hisia? Je, uko makini kutathmini kile unachoimba na kufundisha ili kuhakikisha kwamba ni sahihi kwa Maandiko?

## Hatari za Ibada: Kudharau Ibada

Somo hili lilianza na onyo la Warren Wiersbe dhidi ya kuchukulia ibada kama wakati wa kufurahisha.[88] Alionya kwamba tunapodhani ibada ni kuhusu kujifurahisha badala ya kumtafuta Mungu katika ibada zetu, tunaidharau. "Makanisa bado yanatumia neno *ibada* lakini maana yake imebadilika. Mara nyingi *ibada* ni neno tu ambalo watu hutumia kutoa

[86] John Wesley, Mahubiri ya John Wesley, "Ushahidi wa Roho"
[87] Barua kutoka kwa Dk Andrew Graham. Mei 29, 2014.
[88] Nukuu katika sehemu hii zimechukuliwa kutoka Warren Wiersbe, *Real Worship* (Grand Rapids: Baker Books, 2000), 169-174.

heshima ya kidini kwa chochote walichopanga waumini kufanya, bila kujali ikiwa Mungu ndiye kitovu cha mkutano huo. Je, hii hutokeaje?

### Tunahama Kutoka Patakatifu Kwenda Kwenye Ukumbi wa Michezo

Ibada inaweza kutokea popote. Wakristo wameabudu katika mapango wakijificha kutokana na watesi au moto kwenye kambi zao wakati wa mapumziko ya kanisa. Wakristo wameabudu katika nyumba za kibinafsi au majengo yenye mapambo. Wakristo wameabudu wakiwa wamelala hospitalini, wakisafiri kwa ndege, au wanapofanya kazi. Ibada inaweza kutokea mahali popote, lakini ibada nyingi za ushirika hufanyika katika jengo la aina fulani. “Waumini wa kanisa lazima wakutane mahali fulani, na ‘mahali fulani’ patakuwa patakatifu au ukumbi wa michezo.”

Tofauti ni ipi? Patakatifu “ni mahali ambapo watu hukusanyika kumwabudu na kumtukuza Bwana wao.” ukumbi wa michezo ni mahali ambapo watu hukusanyika kutazama maonyesho. Je, jengo lako la kanisa ni ukumbi wa michezo au patakatifu?

### Tunahama Kutoka Kanisa hadi Kwa Wasikilizaji

“Kanisa la Kikristo hukusanyika ili kumwabudu Yesu Kristo na kumtukuza Yeye. Wasikilizaji hukusanyika ili kuona na kusikia onyesho. Kanisa linaelekezwa kwa Mungu; waikilizaji wanaelekeza umakini kwa mtendaji. Kanisa linaundwa na washirika; wasikilizaji wanaundwa na watazamaji. Je, unaongoza kanisa au wasikilizaji?

### Tunahama Kutoka Kwenye Huduma hadi kwenye Maoanyesho

“Tunahudumu kimsingi ili **kueleza** ukweli wa Mungu; tunafanya onyesho ili **kuvutia** watu kwa uwezo wetu. Mhudumu anajua kwamba Mungu anatazama na kwamba kibali chake ndicho cha maana; mwonyeshaji anatafuta makofi ya watazamaji." Huduma inaweza kuwa onyesho kwa njia nyingi tofauti: mwanamuziki anayefanya onyesho kwa ajili ya burudani ya wasikilizaji, kikundi cha sifa kinachotafuta mwitikio fulani wa kihisia, au mhubiri anayepima mahubiri yake kulingana na jinsiwatu wanavyoitikia. Je, unahudumu au unafanya maonyesho?

## Hitimisho: Ushuhuda wa Mmisionari - Warumi 14 katika vitendo

“Nilijifunza somo muhimu kuhusu kuhukumu wengine kwa sababu ya mtindo wao wa kuabudu nilipohudhuria semina ya uongozi na rafiki mmisionari na wachungaji wanane wa Ufilipino.[89]

“Tuliingia kwenye kituo kikubwa cha mkutano na tukapata viti vyetu juu kwenye mabehewa. Skrini kubwa na vipaza sauti vilikuwa vinaning'inia kwenye dari. Kiongozi wa ibada alikuwa mwanamke Mfilipino akiwa na timu ya sifa nyuma yake. Walikuwa wakipiga makofi na

[89] Ushuhuda kutoka kwa Mchungaji David Black, mmisionari wa zamani nchini Ufilipino.

kuongoza umati wenye msisimko kwa wimbo wa ‘Ndiyo, Bwana, Ndiyo!’ ulionekana kuwa umechangamka sana kwa ladha yangu.

“Muziki wenye kurudia-rudia, uimbaji wenye sauti kubwa, na harakati za mwili vilinipa wasiwasi sana. Tulikuwa tumewapa changamoto wachungaji wetu wa Ufilipino kuwa viongozi watakatifu, na sasa tulikuwa tunawaleta katika aina hii ya ibada! Mmoja wa wachungaji wa Ufilipino, kiongozi wa kiroho sana, alikuwa amesimama ameinamisha kichwa chake. Alikuwa akiomba kimya kimya na kutokuwa sehemu ya ibada.

“Nilipata shida, ‘Tunafanya nini?’ Baadaye, nilimwona mchungaji huyohuyo akipiga makofi na kuimba kwa moyo wake wote. Uso wake ulikuwa uking'aa, na alionekana kushikwa na ibada.

“Jioni hiyo, tulishirikishana kile tulichojifunza kuhusu uongozi katika mkutano huo. Wakati wa mazungumzo, nilimuuliza kiongozi huyu wa Ufilipino nini kilifanyika kubadili tabia yake. ‘Kwa nini ulitoka katika kutoshiriki hadi kuabudu ghafla na kufurahia uimbaji?’

"Jibu lake lilikuwa na nguvu. 'Nilitatizwa na muziki. Lakini nilipokuwa nikiomba, Mungu alinionyesha kwamba kiongozi wa ibada na watu katika kutaniko hili walikuwa wanamwabudu Mungu kwa mioyo yao yote. Walikuwa wakimpa Mungu kilicho bora zaidi kulingana na wanavyojua. Bwana akasema, “Je, unaweza kuwaacha kwangu? Je, unaweza kuniabudu bila kuwahukumu wengine?”

“Mchungaji huyu alianza kumwabudu Mungu kwa moyo wake wote kama kawaida kuliko kuwahukumu wale walio karibu naye. Je, hii ilibadilisha mtazamo wa kuabudu wa mchungaji huyu? Hapana; aliporudi kanisani kwake, hakuiga mtindo wa kuabudu aliouona mwisho wa juma hilo.

“Akiwa kama kiongozi katika makanisa yetu, mwanamume huyu mara nyingi aliwahimiza wachungaji wenzake kuruhusu uhuru katika ibada bila kuwalaghai washirika. Aliwahimiza wachungaji wenzake kusawazisha kanuni mbili:

1. Fuata kwa uangalifu kanuni za kibiblia za ibada katika kanisa lako.
2. Epuka kukosoa mitindo ya kuabudu ya makanisa mengine.”

## Mapitio ya Somo la 9

(1) Ibada na Utamaduni

- Tunapotathimini mitindo ya kuabudu, hatupaswi kuchanganya utamaduni na Maandiko.
- Utamaduni wetu unapopingana na Maandiko, ni lazima tutii amri za Maandiko badala ya matarajio ya utamaduni.
- Ili kufikia ulimwengu kwa injili, tunapaswa kuuliza jinsi ibada yetu inaweza kuzungumza kwa ufanisi zaidi katika utamaduni wetu.

(2) Maswali matatu yanatusaidia kuelewa uhusiano kati ya ibada ya kanisa la mahali na utamaduni unaozunguka:

- ***Nani yuko hapa?*** Inaangalia waamini ambao ni sehemu ya kanisa.
- ***Nani alikuwa hapa?*** Inaangalia urithi wa kanisa.
- ***Nani anapaswa kuwa hapa?*** Inaangalia jamii tunayoitwa kufikia.

(3) Kwa sababu muziki ni muhimu sana kwa utambulisho wetu wa kitamaduni, makanisa yanapaswa kuchagua muziki unaoaminika kibiblia na unaozingatia utamaduni.

(4) Ikiwa kupiga makofi ni sehemu ya ibada, tunapaswa kuuliza, "Je, kupiga makofi kunafaa kwa wimbo huu na jambo hili katika ibada yetu?"

(5) Ikiwa kupiga makofi ni kuitikia wimbo maalum, tunapaswa kuuliza, "Je, makofi yangu yanachochewa na sifa kwa Mungu au sifa kwa mwimbaji?"

(6) Ikiwa tutawaweka watoto na vijana katika ibada ya watu wazima, tunapaswa kupanga ibada ambayo itazungumza na vizazi vyote.

(7) Ikiwa tuna ibada tofauti kwa watoto na vijana, tunapaswa kuhakikisha kuwa ibada ni ibada, sio burudani.

(8) Hatupaswi kusisitiza kupita kiasi au kukataa hisia katika ibada.

## Somo la 9 Mazoezi

(1) Somo hili lilijumuisha maswali kadhaa ya " Kujipima". Andika jibu la ukurasa mmoja kwa mojawapo ya maswali haya. Jibu lako lazima lijumuishe sehemu mbili:

- Tathmini ya kile unachofanya hivi sasa katika ibada.
- Pendekezo la mabadiliko ambayo yatafanya ibada yako kuwa muhimu zaidi kitamaduni bila kuhama kutoka kwa kanuni za kibiblia za ibada.

(2) Mwanzoni mwa somo linalofuata, utafanya Jaribio kulingana na somo hili. Jifunze maswali ya mtihani kwa uangalifu katika maandalizi.

**Jaribio Somo la 9**

(1) Je, tunapaswa kuitikiaje mazoea ya kuabudu ambayo yanachukiza mapendeleo yetu ya kitamaduni lakini hayapingani na kanuni za kibiblia?

(2) Je, tunapaswa kuitikiaje mazoea ya kuabudu ambayo yanakubalika katika utamaduni wetu, lakini yanapingana na maandiko?

(3) Ni maswali gani matatu tunapaswa kuuliza ili kuelewa uhusiano kati ya ibada ya kanisa letu na utamaduni unaotuzunguka?

(4) Kutoka Warumi 14, orodhesha kanuni tatu zinazohusiana na ibada.

(5) Orodhesha mambo matatu ya kuzingatia kwa ibada ya vizazi.

(6) Taja makosa mawili yanayohusiana na hisia katika ibada.

(7) Andika 1 Wakorintho 14:15-17 kutoka kwenye kumbukumbu.

# Somo la 10
# Mtindo wa Maisha wa Kuabudu

## Malengo Ya Somo

Mwisho wa somo hili, mwanafunzi anapaswa:

(1) Kutambua uhusiano kati ya ibada ya ushirika na mtindo wa maisha wa kuabudu.
(2) Kuelewa kwamba mtindo wa maisha wa kuabudu hubadilisha maadili ya mtu.
(3) Kutafuta kuishi kwa utukufu wa Mungu.
(4) Kujitolea kwa mtindo wa maisha wa kuabudu unaofundishwa katika Warumi 12:2.
(5) Kutaja theolojia ya kuabudu yenye msingi wa kibiblia.

## Matayarisho kwa somo hili

*Kariri 1 Wakorintho 10:31.*

## Utangulizi

Katika mwaka huohuo, taifa moja la Kiafrika latokea kwenye orodha mbili: "Idadi kubwa zaidi ya Wakristo katika Afrika" na "Taifa lenye ufisadi mwingi zaidi barani Afrika."

Mchungaji wa mojawapo ya makanisa makubwa zaidi barani Asia apatikana na hatia ya kuiba mamilioni ya dola.

Kiongozi wa kanisa kuu la Marekani ajiuzulu baada ya kukiri kutokuwa mwaminifu katika ndoa.

Tatizo ni nini? Kuna sababu nyingi katika hali hizi, lakini jambo moja ni la kawaida kwa wote: Ibada ya Jumapili haiathiri maisha ya Jumatatu. Jumapili inachukuliwa kuwa "ibada" - hisia na shauku. Jumatatu inachukuliwa kuwa "maisha halisi"- mazoea ya biashara yasiyo ya kimaadili na kujiridhisha. Kwa watu wengi, shughuli za ibada hazileti mabadiliko ya maisha.

► Jadili jinsi ibada inavyoathiri maisha yako ya kila siku. Je, biashara yako inaendeshwa tofauti tofauti kwa sababu ya ibada yako? Je, mahusiano ya familia yako yanaboreshwa kwa sababu ya ibada yako? Maadili yako? Siasa zako? Mazoea yako ya kifedha? Je, unaishi maisha ya mtidno wa ibada?

## Ibada: Zaidi ya Jumapili

Tatizo lililoelezewa katika utangulizi wa somo hili si geni. Amosi alizungumza na watu walioleta dhabihu na kufuata taratibu za Hekalu, lakini walishindwa kuishi maisha ya kumcha Mungu (Amosi 5:21-24). Yeremia alihubiri kwa watu waliopaza sauti "Hekalu, Hekalu," lakini hawakujua uhalisia wa uwepo wa Mungu (Yeremia 7:4). Yesu alieleza wale

walioshika kila undani wa sheria, ambao walitoa zaka kwa vitu vidogo zaidi, na ambao walikuwa waaminifu katika maombi, utunzaji wa Sabato na taratibu nyingine za ibada, lakini mioyo yao ilikuwa michafu (Mathayo 23:23). Watu hawa walidai kuwa waabudu, lakini ibada yao ilikuwa ya uwongo. Ibada ya kweli huathiri maisha yote.

Paulo aliwaandikia waumini ambao walikabili suala la nyama iliyotolewa kwa sanamu. Baada ya kushughulikia tatizo hili, Paulo alihitimisha, "Basi, mlapo, au mnywapo, au mtendapo neno lo lote, fanyeni yote kwa utukufu wa Mungu" (1 Wakorintho 10:31). Ingawa Paulo alikuwa akizungumzia suala la nyama iliyotolewa kwa sanamu, kanuni hiyo inatumika katika nyanja zote za maisha. Ikiwa tunaabudu kweli, maisha yetu ya kila siku yataishi kwa utukufu wa Mungu.

> "Kiongozi wa kuabudu anapaswa kuwa mtu wa mfano wa ibada katika nyanja zote za maisha; ambaye humfuata Mungu kwa kila kitu; ambaye huongoza kanisa katika mtindo wa maisha wa kuabudu."
>
> - Imetolewa na Stephen Miller

Moja ya ufafanuzi wa kuabudu ni "…mwitikio wa yote tuliyonayo kwa yote ambayo Mungu alivyo."[90] Ufafanuzi huu unaonyesha kwamba ibada itahusisha nyanja zote za maisha. Kuna kanuni mbili ambazo lazima ziwekwe kwa usawa wakati wa kufafanua ibada.

**Ibada ya Pamoja: Ibada siku ya Jumapili**

Ibada ya pamoja inarejelea mkusanyiko wa kundi la kanisa. Mkutano huu unaweza kutokea katika jengo la kanisa, katika nyumba, au katika mazingira mengine. Mpangilio sio muhimu, lakini wakati uliotengwa kwa ajili ya ibada ya pamoja ni muhimu. Wakristo wamepewa fursa na wajibu wa kukusanyika kwa ajili ya ibada ya pamoja (Waebrania 10:25).

**Kuabudu kama Mtindo wa Maisha: Kuabudu Katika Maisha Yote**

Katika Bustani ya Edeni, kama ungewauliza Adam na Hawa, "Mnaabudu lini?" wangejibu, "Tunaabudu daima. Maisha yetu yote ni ibada." Hii ni ibada kama mtindo wa maisha.

Kuabudu ni mkutano wa pamoja wa waumini na maisha yanayoishi kwa utukufu wa Mungu. Askofu wa karne ya pili Iraeneus wa Lyons alisema, "Utukufu wa Mungu ni mwanadamu, aliye hai kabisa." Huu sio ubinadamu unaozingatia mwanadamu; ni utambuzi wa Mungu kwamba kusudi kuu la mwanadamu ni kuishi kwa utukufu kwa Mungu. Hii ndiyo ibada ya kweli.

Kama Wakristo, tunatoa kila kitu maisha yetu, hata mambo ya kawaida, kwa Mungu. Ibada sio Jumapili tu. Kazi zetu, michezo, na kazi zetu za kawaida hufanywa kwa utukufu wa Mungu. Warumi 12:1 inaonyesha kwamba ibada inahusisha kutoa miili yetu

> "Kutoa maisha yetu katika kumtumikia Mungu kila siku ni wito wetu wa maisha yote. Ibada ya Jumapili asubuhi ni mwendelezo wa wito huo."
>
> - Barry Liesch

[90] Warren Wiersbe, *Real Worship.* (Grand Rapids: Baker Books, 2000), 21

kuwa dhabihu iliyo hai; hii ni ibada yetu ya kiroho. Mtazamo wa kibiblia kuhus ibada ni kwamba ibada sio kutaniko la kila wiki tu; ni kutoa maisha yetu yote kwa Mungu.

**Mtazamo wa kibiblia wa ibada unajumuisha ibada ya pamoja na maisha ya kila siku.** Vipengele vyote viwili ni muhimu. Ikiwa tunasahau kwamba ibada inahusisha maisha ya kila siku, tunaweza kuhudhuria ibada bila kuona matokeo yoyote katika maisha yetu yote. Hii inatupelekea kushiriki katika ibada ya pamoja huku tukishindwa kuishi katika utii wa kila siku kwa Mungu.

Hata hivyo, ikiwa tunasisitiza tu "ibada ni ya maisha yote," tunasahau umuhimu wa wakati wa kawaida uliotengwa kwa ajili ya ibada ilyojikita. Kushiriki katika ibada ya ushirika hutukumbusha uwakili wa Mungu wa maisha.

Kanuni hii ya uwakili inaonekana katika zaka na Sabato. Uwakili wa Kikristo unamaanisha kwamba pesa zetu zote ni za Mungu; imani yetu katika kanuni hiyo inaonekana kwa zaka yetu. Mtazamo wa Kikristo wa wakati unamaanisha kwamba maisha yote ni ya Mungu; tunadhihirisha hilo kwa kutenga siku moja kwa juma kuabudu na kupumzika. Vivyo hivyo, sehemu zote za maisha yetu ni sehemu ya ibada; tunaonyesha hilo kwa kukusanyika pamoja na waamini wenzetu kwa ajili ya ibada ya pamoja.

Bob Kauflin alionyesha uhusiano kati ya ibada ya ushirika na ibada kama mtindo wa maisha:

> Jumapili inaweza kuwa kilele cha wiki yetu, lakini sio kilele pekee. Wakati wa wiki, tunaishi maisha ya ibada tunapopenda familia zetu, kupinga majaribu, kusema kwa ujasiri kwa ajili ya watu wanaodhulumiwa, kusimama dhidi ya uovu, na kutangaza injili. Katika mambo yote hayo, sisi ni **kanisa linaloabudu lililotawanyika**.
>
> Lakini tunachoka katika vita vyetu dhidi ya ulimwengu, mwili wetu, na shetani na tunahitaji kuimarishwa na kutiwa moyo na Neno la Mungu na uangalizi wa watakatifu wengine. Tunataka kushirikiana na wale ambao Mungu ametuunganisha nao kupitia damu ya Mwanawe. Kwa hiyo, tunakutana ili kuwa **kanisa linaloabudu lililokusanyika.**[91]

[91] Bob Kauflin, *Worship Matters* (Wheaton: Crossway Books, 2008), 210

## Ibada: Kuishi kwa Utukufu wa Mungu

### Ibada huonyesha maadili yetu

Tumeumbwa kwa ajili ya ibada. Sisi sote tunaabudu kitu au mtu fulani. Tunaabudu kile tunachothamini zaidi. Ibada husema, "Hii ndiyo inayo nafasi ya kwanza katika maisha yangu."

> "Kila mtu ana madhabahu. Na kila madhabahu ina kiti cha enzi. Basi unajuaje unachokiabudu? Ni rahisi: fuata mkondo wa muda wako, mapenzi yako, nguvu zako, pesa zako, na utii wako. Mwishoni mwa njia hiyo utapata kiti cha enzi, na chochote, au yeyote yule, aliye kwenye kiti hicho cha enzi ndiye aliye na thamani kuu kwako. Kwenye kiti hicho cha enzi. is what you worship."
>
> \- Louie Giglio

Watu wengi huabudu pesa, kazi, cheo, mahusiano, au mmbo yanafurahisha. Mambo hayo huchukua nafasi ya kwanza katika maisha yao. Unajuaje unachoabudu? Angalia maisha yako. Ni nini kinachopata nguvu zaidi, muda, na pesa? Hilo ndilo uliloamua ni la thamani zaidi kwako; hicho ndicho unachokiabudu.[92]

Mungu pekee ndiye anayestahili kuabudiwa; vitu vingine vinafuata. Mtindo wa maisha wa kuabudu humtanguliza Mungu katika kila jambo. Waabudu wa kweli wamemweka Mungu kwenye kiti cha enzi cha maisha yao; Ana thamani ya juu zaidi. Hiyo inamaanisha kwamba kwa waabudu wa kweli, kila sehemu ya maisha yao inaishi kwa utukufu wa Mungu.

### Ibada ya Kweli Hubadili Maadili Yetu

Katika Isaya 6, tunaona kwamba ibada ya kweli inabadilisha. Ibada sio tu inaonyesha maadili yetu, pia inabadilisha maadili yetu.

Kuabudu, kwa Mungu au sanamu, kunabadilisha jinsi tulivyo. Zaburi 115:8 inaonyesha kwamba kuabudu sanamu hutubadilisha na kuwa mbaya. "Wazifanyao watafanana nazo, kila mmoja anayezitumainia." Waabudu masanamu wanakuwa kama masanamu yao. Wale wanaoabudu pesa wanazidi kuwa wenye tamaa; wale wanaoabudu anasa wanazidi kuwa watumwa wa starehe; wale wanaoabudu umaarufu wanazidi kuwa wabinafsi. Tunakuwa kama chochote tunachoabudu.

> Ibada sio tu kitu tunachofanya; ibada inatufanyia kitu sisi.

Vivyo hivyo, wale wanaomwabudu Mungu wanazidi kuwa kama yeye. "lakini sisi sote, kwa uso usiotiwa utaji, tukiurudisha utukufu wa Bwana, kama vile katika kioo, tunabadilishwa tufanane na mfano uo huo, toka utukufu hata utukufu" (2 Wakorintho 3:18). Katika ibada, tunabadilishwa kuwa mfano wake.

---

[92] Imetolewa kutoka kwa Louie Giglio, *The Air I Breathe: Worship as a Way of Life.* (Sisters, OR: Multnomah Publishers, 2003).

Tunapoabudu, maadili yetu yanabadilishwa. Kama waabudu, lazima tuulize, "Je, ibada inabadilisha maisha yangu?"

**Kuishi kwa Utukufu wa Mungu Kunahusisha Maisha Yote**

Ibada kama mtindo wa maisha humaanisha kwamba maisha yote unaishi kwa utukufu wa Mungu. Wakristo wengi hugawanya maisha yao katika nyanja mbili zilizotenganishwa: takatifu (Jumapili) na ya kidunia (Jumatatu-Jumamosi). Wanaishi kama "Wakristo wa Jumapili." Wanahudhuria kanisani na kukiri imani ya Kikristo, lakini ibada ya Jumapili haina matokeo kwenye biashara ya Jumatatu, maisha ya familia ya Jumatano, au burudani ya Jumamosi.

Neno *la kidunia* linamaanisha maisha katika ulimwengu huu. Mkristo ameitwa kuishi maisha ya ulimwengu huu kwa utukufu wa Mungu. Mkristo anatakiwa kuishi siku ya Jumatatu kwa njia inayoonesha matokeo ya ibada ya Jumapili. Mwishoni mwa ibada, lazima tujiulize, "Nitafanya nini kesho ili kuweka ibada ya leo katika vitendo?" Haya ni maisha yanayoishi kwa utukufu wa Mungu.

**Je! Kuishi kwa Utukufu wa Mungu Kunaonekanaje?**

Kuishi kwa utukufu wa Mungu kunamaanisha kwamba maisha yote yanatawaliwa na shauku kwa ajili ya Mungu. Inamaanisha kumpenda Mungu kiasi kwamba furaha yetu ndiyo inayompendeza. Mtu mmoja alisema kwamba kumpenda mtu kunamaanisha kuwa na wasiwasi naye. "Unampenda mtu (au kitu) ambacho unakifikiria juu yake wakati haufikirii juu ya kitu kingine chochote."

Vivyo hivyo, Louie Giglio anapendekeza kwamba "tunajua kile kilicho kikuu katika nafsi zetu kwa kile kinachotoka vinywani vyetu."[93] Tunazungumza kile ambacho ni cha thamani zaidi kwetu.

Hiyo inaweza kuonekana kuwa rahisi kupita kiasi, lakini fikiria. Je, watu wanaopenda pesa wanazungumzia nini? Pesa. Wanatukuza pesa. Mshabiki wa michezo anazungumza nini? Michezo. Anaitukuza timu anayopenda ya michezo.

Je, hiyo inamaanisha kwamba Mkristo anapaswa kuzungumza kuhusu Biblia katika kila hali? Hapana; ina maana tu kwamba kila jambo tunalozungumzia litamtukuza Mungu. Tunapofanya uamuzi wa kibiashara, hatuwezi kuwaambia wenzetu, "Uamuzi huu lazima umtukuze Mungu," lakini utukufu wa Mungu utaathiri uamuzi wetu. Tunapolazimika kumrudi mtoto , huenda tusianze mazungumzo kwa kusema, "Mwanangu, nataka adhabu hii imtukuze Mungu,' lakini tutajiuliza, Je, nidhamu hii




[93] Louie Giglio, "Zaburi 16" katika Matt Redman na Friends, *Inside, Out Worship* (Ventura: Regal Books, 2005), 78

itampendeza Mungu au ninafurahisha hasira yangu tu? Je, hivi ndivyo Baba yangu wa mbinguni angenirudi mimi?"

Tukiwa Wakristo, tunafanya kila uamuzi katika nuru ya utukufu wa Mungu. Ibada kama mtindo wa maisha kunamaanisha kwamba Mungu na utukufu wake ndio kiini cha kila kitu tunachofanya.

Katika somo la awali, tuliona kwamba bila neema, ibada ya pamoja inakuwa ya kisheria, ambapo tunajiuliza "Je, tunawezaje kuabudu kwa njia ambayo inapata kibali cha Mungu?" Vivyo hivyo, bila neema, mtindo wa maisha wa ibada unakuwa mzigo wa kisheria, ambapo tunajiuliza "Je, ikiwa uamuzi huu sio njia bora ya kumtukuza Mungu? Nikiharibu, je, Mungu atakasirika?"

Tofauti na ibada ya kisheria, kuabudu katika nuru ya neema ya Mungu kunakuwa ni heshima ajabu. Ibada ya pamoja kwa nuru ya neema ya Mungu ni fursa ya kusherehekea Mungu ni nani na amefanya nini. Vivyo hivyo, mtindo wa maisha wa kuabudu (unapoishi katika nuru ya neema ya Mungu) ni fursa ya kumtukuza Mungu katika maisha ya kila siku.

Uamuzi wa kibiashara wa Jumatatu si juhudi isiyo na furaha ya kutii sheria ya Mungu; ni fursa ya furaha ya kumtukuza Mungu na maadili yanayolingana na tabia yake. Kumrudi mtoto si kitu cha kuhuzunisha kinachofanywa tu ili tusimkosee Mungu; ni fursa ya furaha ya kuiga tabia ya upendo ya Mungu kwa mtoto wako. Neema inabadilisha mtindo wa maisha wa ibada.

## Kuabudu kama Mtindo wa Maisha: Mfano wa Kibiblia

Katika Warumi 12:1, Mkristo anaitwa kujitoa mwenyewe kama dhabihu iliyo hai, takatifu na ya kumpendeza Mungu. Hii ndiyo ibada yetu ya kiroho. Warumi 12:2 inaonyesha jinsi dhabihu hii itakavyotolewa. Andiko hili ni muhimu sana kwa kuelewa ibada kama mtindo wa maisha.

Baada ya sura 11 ambamo Paulo anaweka msingi wa kitheolojia kwa maisha ya Kikristo, anahamia kwenye vitendo. Kwa kuwa tumehesabiwa haki kwa neema (Warumi 1-11), tunapaswa kuishi kwa namna fulani (Warumi 12-16). Sura hizi zinatoa kielelezo cha mtindo wa maisha wa kuabudu.

### Mtazamo Hasi katika Mtindo wa Maisha wa Ibada

Paulo anaanza kwa amri hasi: "Msiifuatishe namna ya dunia hii." Hatupaswi kuishi kwa kufuata kawaida za ulimwengu huu. Hatuwezi kujisalimisha kwa ulimwengu huu na ufalme wa mbinguni pia; hatuwezi kumwabudu Mungu na roho wa wakati huu.

J.B. Philips alitafsiri agizo la Paulo, "Usiruhusu ulimwengu unaokuzunguka ukufinyange katika mfumo wake." Wakati udongo unapowekwa kwenye umbo lake, haraka unachukua umbo hilo. Ulimwengu unataka kuwafinyanga Wakristo ili wachukue umbo lake. Ulimwengu unataka kutulazimisha tukubaliane na matakwa yake. Badala yake, tunapaswa kuishi maisha ya ibada, kukataa ushawishi wa ulimwengu huu.

Kishawishi hiki ni hatari sana kwa sababu tunaweza kubadilika bila hata kufahamu umbo hilo. Samaki wanaoishi ndani ya maji hawafikirii, "Haya ni maji." Ni ulimwengu anamoishi tu. Mdudu anayetambaa kwenye uchafu hafikirii, "Huu ni uchafu." Ni ulimwengu anamoishi tu. Tusipokuwa waangalifu, Mkristo anayeishi katika ulimwengu ulioanguka hatafikiri, "Huu ni ulimwengu ulioanguka." Itakuwa tu ulimwengu anaoishi.

Hii ndiyo sababu ibada ya pamoja ni muhimu. Mwandishi wa Waebrania alionya kwamba hatupaswi kupuuza kukutana pamoja. Kwa nini? Kwa sababu hivi ndivyo tunavyotimiza amri hizi zingine:

- "Na tukaribie wenye moyo wa kweli, kwa utimilifu wa Imani…" (Waebrania 10:22)
- "Na mlishike sana ungamo la tumaini letu, lisigeuke…" (Waebrania 10:23)
- "Tukaangaliane sisi kwa sisi na kuhimizana katika upendo na kazi nzuri…" (Waebrania 10:24)

Katika ibada, tunakumbushwa kwamba sisi si wa ulimwengu huu. Huko Babeli, akiwa amejitenga na Hekalu, hakuweza kushiriki katika ibada ya pamoja ya watu wake, Danieli aliomba mara tatu kwa siku, madirisha yake yakiwa yamefunguliwa kuelekea Yerusalemu (Danieli 6:10). Ibada ilimtia nguvu Danieli dhidi ya kugeuzwa na ulimwengu wa Babeli. Alipokabili Yerusalemu, Danieli alikumbushwa, "Mimi si mwenyeji wa Babeli; Mimi ni raia wa Yerusalemu. simsujudu Marduk; Ninamtumikia Yehova."[94]

Mtindo wa maisha wa ibada unamaanisha kwamba tunakataa kufinyangwa katika umbo la ulimwengu wetu. Hii ni zaidi ya kushinda majaribu fulani. Ni zaidi ya kuzingatia sheria fulani. Ni zaidi ya mtindo fulani wa mavazi, kanuni za tabia, au utamaduni wa kidini. Ni njia nzima ya kufikiria na kuishi. Inamaanisha kutathmini kila kitu kulingana na ufalme wa Mungu.

Kama Wakristo, hatuweza kamwe kufaa kwa urahisi katika utamaduni unaotuzunguka. Baada ya darasa nchini China kuhusu Mahubiri ya Mlimani, mwanafunzi mmoja alisema, "Nchini China, ni vigumu kuishi kama Yesu alivyofundisha." Mwalimu akajibu, "Usishangae. Hata Marekani, pia ni vigumu kuishi kama Yesu alivyofundisha." Haijalishi utamaduni ni upi, mtindo wa maisha wa ibada utapingana na roho ya ulimwengu huu.

### Mtazamo Chanya katika Mtindo wa Maisha wa Ibada

Kufuatia amri hiyo hasi, Warumi 12 inaendelea na maagizo chanya: "bali mgeuzwe kwa kufanywa upya nia zenu."

Kinyume cha kufuata namna ya dunia hii sio tu kuwa tofauti au kusisitiza utu wako mwenyewe. Badala yake, ni kubadilishwa mpaka utakapojua mapenzi ya Mungu. Wakristo wengine wamefuata mtindo wa maisha tofauti na tamaduni zao, lakini hawajageuzwa kuendana na mapenzi ya Mungu. Badala yake, wametumia mtazamo fulani wa kisiasa,

---

[94] Imefafanuliwa kutoka kwa Tim Keep, Misheni za Methodisti ya Biblia. Mahubiri ya kanisa dogo katika Hobe Sound Bible College, Novemba 2013.

kijamii, au mavazi kwa ajili ya mustakabali wa dunia hii. Hawajabadilishwa kwa kufanywa upya nia zao.

J.B. Phillips alitafsiri, "Usiruhusu ulimwengu unaokuzunguka ukufinyange katika mfumo wake" (hasi), "bali acha Mungu akufanye upya ili mtazamo wako wote wa akili ubadilishwe" (chanya). Sehemu iliyobaki ya kitabu cha Warumi inaonyesha jinsi nia iliyogeuzwa itaonekana.

- Warumi 12: Muumini aliyebadilishwa hutumia karama zake za kiroho kuwatumikia wengine.
- Warumi 13: Muumini aliyebadilishwa anaheshimu mamlaka ya kiraia.
- Waroma 14: Mwamini aliyebadilishwa anaheshimu imani ya waamini wenzake.

Mtindo wa maisha wa kuabudu ni zaidi ya tabia; ibada inabadilisha njia yetu yote ya kufikiri. Fikiria matokeo ya mtindo wa maisha wa ibada:

- Je, bara la Afrika litakuwaje ikiwa wafanyabiashara na wanasiasa Wakristo watabadilishwa katika mitazamo yao kuhusu pesa na mamlaka?
- Je! Makanisa ya Asia yatakuwaje ikiwa viongozi watajiona kama mawakili wa pesa za Mungu?
- Je! Ndoa huko Amerika itakuwaje ikiwa Wakristo wanaona uzinzi kupitia macho ya Mungu, badala ya macho ya Hollywood?

Mtindo wa maisha wa ibada hubadilisha mawazo ya mwamini; akili iliyobadilishwa itaonekana katika maisha yaliyobadilishwa; maisha yaliyobadilishwa yatabadilisha jamii. Mtindo wa maisha wa ibada hatimaye utabadilisha ulimwengu wetu.

### Hatari za Ibada: Kuabudu bila Utiifu

Mitume walionya dhidi ya ibada bila utii. Watu wa siku za Yeremia waliamini kwamba Hekalu lingewalinda kutoka katika utumwa wa Babeli. Yeremia alijibu, "Msitumainie maneno ya uongo, mkisema, Hekalu la BWANA, Hekalu la BWANA, Hekalu la BWANA ndiyo haya.'" (Yeremia 7:4) Badala yake,

> **Mkitengeneza** kabisa njia zenu na matendo yenu;
>
> **Kama** mkihukumu hukumu ya haki kati ya mtu na jirani yake;
>
> **Kama** hamwonei mgeni, wala yatima, wala mjane, wala kumwaga damu isiyo na hatia mahali hapa, wala kuifuata miungu mingine kwa hasara yenu mwenyewe:
>
> **Ndipo** nitakapowakilisha mahali hapa, katika nchi hii niliyowapa baba zenu, toke zamani hata milele (Yeremia 7:5-7).

Watu wa Israeli waliamini wangeweza kubadilisha ibada kwa utii. Manabii walihubiri kwamba ibada bila utii haina maana.

Katika baadhi ya mila, utii unabadilishwa na ibada ya liturujia. Vipengele vya ibada vipo. Nyimbo zinasema ukweli. Maandiko yanasomwa na kuhubiriwa. Maombi yanaombewa. Hata hivyo, hakuna utii kwa Neno la Mungu. Maisha hayabadilishwi. Hii ni ibada ya liturujia, sio ibada.

Katika baadhi ya mila, utii hubadilishwa na mwitikio wa kihisia. Lengo la ibada ni kuzalisha hisia fulani. Muziki huchochea hisia. Mahubiri huongoza kwenye mwaliko au muda wa kujitoa kwa Mungu. Hata hivyo, ibada hiyo haifuati maisha ya utii na kujitoa kwa Mungu. Hii ni hisia, sio ibada.

Ibada katika Hekalu ilisherehekea agano la Israeli na Mungu na kuwakumbusha Israeli wajibu wao wa agano. Katika kanisa la kwanza, ibada iliadhimisha agano jipya lililotolewa kupitia kifo cha Yesu na kuwakumbusha Wakristo wajibu wao wa kuishi maisha matakatifu. Ibada ambayo haina matokeo ya utii ni ya uwongo.

Ibada ya kweli humbadilisha mwenye kuabudu. Katika kipindi hiki chote, tumeona kwamba watu wanaoabudu kikweli hubadilishwa. Lengo la kozi hii si tu kwamba utakuwa bora zaidi katika kupanga na kuongoza huduma za ibada, lakini kwamba utakuwa mwabudu ambaye anabadilishwa na ibada. Kisha utaliongoza kanisa lako katika ibada inayombadilisha kila mshirika wa kanisa.

## Hitimisho: Ushuhuda wa Mchungaji

Ibada ya kweli ina matokeo gani? Msikilize mchungaji wa kanisa la Uhispania.

“Mnamo 1991, hali ya kiroho ya kanisa letu ilikuwa katika hali ya chini zaidi. Uasherati ulikuwa umenasa baadhi ya washirika wetu. Tulipowaadhibu washirika walioanguka, kanisa liligawanyika. Hatimaye, katika hali ya kuvunjika kiroho na kihisia, mwongofu mpya alipendekeza kwamba tufunge na kuomba siku nzima ya Jumapili. Tulifanya hivi na Mungu akaanza kutembea kati yetu.

“Wiki chache baadaye, tulianza kambi yetu ya kila mwaka. Mgawanyiko fulani kanisani ulikuepo. Mwinjilisti alipoanza mahubiri yake Jumatano usiku, alihisi kwamba Mungu alimtaka aimbe ‘Jinsi Ulivyo Mkuu.’

“Alipokuwa akiimba wimbo huu, utukufu wa Mungu ulishuka juu ya umati wenye njaa. Wengine waliitikia kwa sifa; wengine walianza kumtafuta Mungu madhabahuni. Mwanamke aliyekuwa mzizi wa migogoro kanisani alitokwa na machozi. Akiwa amesimama mbele ya watu 400, alikiri, ‘Mimi ni mwanamke nisiye na furaha zaidi kwa sababu nimemkosea Mungu na kanisa lake kwa kuhifadhi chuki moyoni mwangu. Ninamwomba Bwana anisamehe, na nawasihi ninyi kama kanisa mnisamehe.’

"Maneno hayo yalipotoka midomoni mwake, wengine walipatanishwa. Jioni hiyo, Mungu alirudisha umoja katika kanisa letu. Watu wa Mungu walipojinyenyekeza katika maombi na

kufunga, na kama mtumishi wa Mungu alivyokuwa mtiifu kwa uongozi wa Roho Mtakatifu, tuliletwa katika uwepo wa Mungu. Dhambi iliungamwa; umoja ulirejeshwa. Haya ndiyo dmatokeo ya ibada ya kweli."[95]

### Mapitio ya Somo la 10

(1) Ibada ya pamoja hufanyika Jumapili; mtindo wa maisha wa ibada hutokea katika maisha ya kila siku. Zote mbili ni muhimu kwa mtazamo wa kibiblia wa ibada.

(2) Ibada ya kweli inaonyesha kile tunachothamini hasa.

(3) Ibada ya kweli hubadilisha kile tunachothamini.

(4) Mtindo wa maisha wa kuabudu unamaanisha kuishi kwa utukufu wa Mungu. Hii ina maana kwamba Mungu atakuwa kitovu cha maisha yote.

(5) Mfano wa kibiblia wa mtindo wa maisha wa kuabudu unaonekana katika Warumi 12:2. Inajumuisha

- Kipengele Hasi: "Msiifuatishe namna ya dunia hii."
- Kipengele chanya: "Mgeuzwe kwa kufanywa upya nia zenu."

### Jaribio Somo la 10

(1) Andika karatasi ya kurasa 3-4 yenye kichwa "Theolojia Yangu ya Ibada." Karatasi hii inapaswa kuonyesha jinsi ibada inavyoegemezwa kwenye kanuni za Maandiko. Karatasi inapaswa kuwa ya kibiblia na ya vitendo.

(2) Hubiri mahubiri kuhusu ibada ya kweli yanayotegemea Yohana 4:23-24.

(3) Kumaliza mradi wako wa somo: Andika taarifa ya ukurasa mmoja kwa kiongozi wa darasa ambayo inajumlisha kile umejifunza kutoka katika "Safari yako ya Siku 30 ya Ibada." Wala huhitaji kugeuza karatasi yako.

(4) Kwa jaribio lako la mwisho, andika 1 Wakorintho 10:31 toka kwenye kumbukumbu.

[95] Ushuhuda wa Mchungaji Sidney Grant, Hope International Missions

# Kiambatanisho A
# Muhtasari wa Kupanga Huduma ya Ibada

| Muhtasari wa Ibada Ulioundwa Kuzunguka Mahubiri | | |
|---|---|---|
| **Kusudi** | **Shughuli za ibada** | **Mpango wa Wiki** |
| Kuhubiri Ukweli wa Neno | • Nyimbo<br>• Maandiko<br>• Mahubiri | |
| Kuitikia Ukweli wa Neno | • Mwaliko<br>• Sadaka<br>• Wimbo wa Kufunga<br>• Baraka (Maandiko) | |

| Muhtasari wa Ibada Ukitegemea Zaburi ya 95 | | |
|---|---|---|
| **Mfano wa Kibiblia** | **Shughuli za Ibada** | **Mpango wa Wiki** |
| Ingia kwa Shukrani za Furaha | • Wito wa kuabudu<br>• Wimbo wa Kusifu | |
| Endelea na Ibada yenye kicho | • Nyimbo za Kujitolea<br>• Maombi | |
| Sikia Sauti ya Mungu | • Usomaji wa Maandiko<br>• Mahubiri | |

| Muhtasari wa Ibada Unaotegemea Shughuli za Watu wa Mungu Katika Ibada | | |
|---|---|---|
| **Harakati** | **Shughuli za Ibada** | **Mpango wa Wiki** |
| Watu wa Mungu Wakusanyika | Sifa<br>• Wito wa Ibada<br>• Nyimbo za Sifa<br>Ukiri<br>• Maombi | |
| Watu wa Mungu Husikia Neno | • Usomaji wa Maandiko<br>• Mahubiri | |
| Watu wa Mungu huitikia Neno | • Wimbo wa Kuitikia Neno<br>• Maombi<br>• Sadaka | |
| Watu wa Mungu Wanatumwa Nje | • Wimbo wa Kufunga<br>• Baraka (Maandiko) | |

| Muhtasari wa Ibada Unaoonyesha Mazungumzo kati ya Mungu na Watu Wake (Isaya 6) | | |
|---|---|---|
| **Kitendo** | **Shughuli za Ibada** | **Mpango Wa Wiki** |
| Mungu Anajifunua | • Wito wa Kuabudu (kutoka kwa Maandiko) | |
| Watu Hujibu kwa Sifa na Kukiri | • Sifa: Nyimbo<br>• Maombi | |
| Mungu Husema na Watu Wake | • Usomaji wa Maandiko<br>• Mahubiri | |
| Watu Huitikia kwa Kujitolea | • Wimbo wa Mwaliko<br>• Sadaka | |
| Mungu Anawatuma Watu Wake | • Baraka | |

# Kiambatanisho B
# Fomu ya Tathmini ya Wimbo

| **Kichwa cha Wimbo:** | | | |
|---|---|---|---|
| | **Dhaifu** | **Wastani** | **Bora** |
| Je, maandiko haya ni ya kweli kwa mujibu wa mafundisho ya imani? | | | |
| Je, maneno ya wimbo yana muktadha wa kikristo | | | |
| Je, watu waliokusanyika kuabudu wataelewa ujumbe wa wimbo? | | | |
| Je, mtindo wa muziki unalingana na maneno? | | | |
| Je, tuni ya wimbo ni rahisi kwa wanaoabudu kuimba? | | | |

# Vyanzo na Rejea Zinazopendekezwa


### Somo la 1

Ili kujifunza zaidi kuhusu maana ya ibada, tafadhali tazama nyenzo zifuatazo:

**Vitabu:**

Jeremiah, David. *Worship*. CA: Turning Point Outreach, 1995. (Tazama Masomo 1-2.)

Reimers, Gary. *The Glory Due His Name*. Greenville: Bob Jones University Press, 2009.

Segler, Franklin M. and Randall Bradley. *Christian Worship: Its Theology and Practice*. Nashville: B&H Publishing, 2006. (Tazama Sura ya 3.)

**Rasilimali za Mtandao:**

"The Language of Worship: Seven Minute Seminary." (Lugha ya Kuabudu: Seminari ya Dakika Saba) https://www.youtube.com/watch?v=RqDCG_-cbrg

"Sin and Worship in Romans: Seven Minute Seminary." (Dhambi na Ibada katika Warumi: Seminari ya Dakika Saba) https://www.youtube.com/watch?v=6RyrW3aO0UI

### Somo la 3

Ili kujifunza zaidi kuhusu ibada katika Biblia, tafadhali tazama nyenzo zifuatazo.

Peterson, David. *Engaging with God: A Biblical Theology of Worship*. Downers Grove: InterVarsity Press, 1992.

Ross, Allen P. *Recalling the Hope of Glory: Biblical Worship from the Garden to the New Creation*. Grand Rapids: Kregel Publications, 2006.

Webber, Robert. *The Biblical Foundations of Worship*. Nashville: Star Song Publishing Group, 1993.

### Somo la 5

Ili kujifunza zaidi kuhusu historia ya ibada, tafadhali tazama nyenzo zifuatazo.

Segler, Franklin M. and Randall Bradley. *Christian Worship: Its Theology and Practice*. Nashville: B&H Publishing, 2006. (Tazama Sura ya 3.)

Webber, Robert. *Rediscovering the Missing Jewel: A Study in Worship Through the Centuries*. Peabody: Hendrickson Publishers, 1997.

Webber, Robert. *Twenty Centuries of Christian Worship*. Nashville: Star Song Publishing Group, 1994.

**Somo la 6**

Ili kujifunza zaidi kuhusu muziki katika ibada, tafadhali tazama nyenzo zifuatazo.

Hustad, Donald. *Jubilate II: Church Music in Worship and Renewal*. Carol Stream: Hope Publishing, 1993.

Janvier, George. *Leading the Church in Music and Worship*. Nigeria: Africa Christian Textbooks, 2003.

Lloyd-Jones, D. Martyn. *Singing to the Lord*. Wales: Bryntirion Press, 2003.

Wolf, Garen. *Church Music Matters*. Salem: Schmul Publishing, 2005.

**Somo la 7**

Kujifunza zaidi kuhusu maandiko na maombi katika ibada, tafadhali tazama nyenzo zifuatazo.

Bounds, E. M. *Power through Prayer*. (Matoleo mengi yanapatikana.)

Drury, Keith. *The Wonder of Worship: Why We Worship the Way We Do*. Fishers: Wesleyan Publishing House, 2002.

Duewel, Wesley. *Mighty Prevailing Prayer*. Grand Rapids: Zondervan, 2013.

Murray, Andrew. *With Christ in the School of Prayer*. (Matoleo mengi yanapatikana.)

**Somo la 9**

Stauffer, S. Anita, ed. "The Nairobi Statement on Worship and Culture," in *Christian Worship: Unity in Cultural Diversity*. Geneva: Lutheran World Federation, 1996.

Witvliet, John D. "An Open and Discerning Approach to Culture." Video lecture. At http://worship.calvin.edu/resources/resource-library/an-open-and-discerning-approach-toculture

# Kumbukumbu za Mazoezi

Jina la Mwanafunzi ________________________________________

Kwenye jedwali hapa chini, andika herufi za mwanzo za majina yako wakati kila zoezi imekamilika. Majaribio huchukuliwa kuwa yamekamilka ikiwa mwanafunzi anapata alama ya 70% au zaidi. Kazi zote lazima zikamilishwe kwa mafanikio ili kupokea cheti kutoka kwa Shepherds Global Classroom.

| Somo | Jaribio | Zoezi | | |
|---|---|---|---|---|
| 1 | | | | |
| 2 | | | | |
| 3 | | | | |
| 4 | | | | |
| 5 | | | | |
| 6 | | | | |
| 7 | | | | |
| 8 | | | | |
| 9 | | | | |
| 10 | | | | |

Ombi la Cheti cha Kukamilika kwa Darasa la Kimataifa la Shepherds linaweza kukamilishwa kwenye ukurasa wetu wa tovuti kwa www.shepherdsglobal.org. Vyeti vitatumwa kidijitali kutoka kwa rais wa SGC hadi kwa wakufunzi na wawezeshaji wanaokamilisha ombi kwa niaba ya wanafunzi wao.